# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

### Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 22 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Katibu!!

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 244

**Malipo ya Wenyeviti wa Mitaa na Madiwani**

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI** aliuliza:-

Wenyeviti wa Mitaa, Madiwani, Wabunge na Rais huchaguliwa na watu wanaoishi katika eneo la mipaka yake na wote hawa wanafanya kazi ya kuwahudumia wananchi katika maeneo yao.

Je, Serikali imeridhika na malipo wanayopata Wenyeviti wa Mitaa pamoja na Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji katika kusimamia shughuli za maendeleo. Majukumu yanayotekelezwa na viongozi hao ni utekelezaji wa dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi ambapo mipango yote na usimamizi yanafanywa katika ngazi za msingi za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiboresha maslahi ya Waheshimiwa Madiwani kadri uchumi wa nchi unavyoruhusu. Kwa mfano posho ya Madiwani ilipandishwa mwaka 2015 kutoka shilingi 120,000 hadi shilingi 350,000 kwa mwezi. Kwa vipindi tofauti hususani Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilipokutana na Waheshimiwa Madiwani katika mkutano wa

*ALAT* hoja hii imekuwa ikijitokeza. Hata hivyo Serikali inalifanyia kazi jambo hili kulingana na mwenendo wa Kifedha wa nchi na jambo hili litakapokamilika utekelezaji wake utafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa hulipwa posho kutokana na asilimia 20 ya makusanyo ya ndani inayopaswa kurejeshwa kwenye ngazi ya msingi katika kata na vijiji. Kila Halmashauri imetakiwa kuhakikisha fedha hizo zinapalekwa kwenye vijiji kwa ajili ya shughuli za utawala ikiwemo kulipa posho na shughuli za maendeleo. Aidha, Halmashauri zimetakiwa kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ili kujenga uwezo wa kulipa posho hizo kupitia makusanyo yanayofanyika.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Serikali kwa maana ya TAMISEMI wametoa muongozo katika makusanyo yale ya Halmashauri kwa maana ya kwamba asilimia 60 zinapaswa kwenda kwenye maendeleo, asilimia 20 zinapaswa kwenda kwenye kata, asilimia 10 zinapaswa kwenda kwa vijana na wakina mama, kwa hiyo Halmashauri inabakia na asilimia 10 peke yake ambayo ndiyo sasa ilipe mishahara na kuendesha Halmashauri. Je, kutokana na hali hiyo ni kwanini sasa hawa Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wasilipwe moja kwa moja kutoka Serikali Kuu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ukiwaangalia hao Madiwani pamoja na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa wanayo majukumu mengi na makubwa kwa hiyo hata wakati mwingine wanashindwa kutekeleza majukumu yao kutokana na tabu walizonazo hasa hasa za usafiri. Je, Serikali sasa imejiandaaje kuhakikisha kwamba nao inawawezesha kupata usafiri ili waweze kutekeleza majuku yao ya kila siku? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kwamba kwanini sasa hawa Wenyeviti wasilipwe moja kwa moja kutoka Serikali Kuu na msingi umesema kwamba kwa sababu kulikuwa na suala zima la mgawanyo wa zile fedha kwamba asilimia 60 ziende katika maendeleo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipowasilisha bajeti yetu mwaka Mheshimiwa Waziri alitoa ufafanuzi hapa kwa kina kwamba hili limeonekana kwa sababu lilikuwa hoja ya msingi ya Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana tumetoa maelekezo. Mheshimiwa Waziri alizungumza wazi hapa kwamba fedha hizi sasa zitagawanyika tofauti, kwamba kwa baadhi ya Halmashauri hasa zile ambazo uwezo wake ni mdogo, sasa asilimia 60 zitakwenda katika matumizi haya mengine na asilimia 40 itakwenda katika maendeleo, huu ndio ufafanuzi kulingana na bajeti ya mwaka huu tuliyoipitisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata hivyo, lengo letu kubwa katika dhana ya ugatuaji wa madaraka ni kutafuta jinsi ya kufanya katika kuongeza nguvu za Halmashauri za kuweza kukusanya mapato. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mathayo tutaendelea kulisimamia hilo, lakini kubwa na la msingi ni jinsi ya kufanya katika kukusanya vizuri mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja ya pili, kuhusu vyombo vya usafiri; ni kweli, tukiangalia viongozi wetu wana changamoto kubwa ya usafiri, kwa sababu kama Madiwani wanafanya kazi kubwa, lakini hili naomba tulichukue sisi Serikali kwa sababu ni jambo ambalo naona ni la msingi hapo baadaye kwa kupitia Halmashauri zetu ni kwa jinsi gani tutafanya kupitia mifuko mbalimbali ili aangalau kuwezesha Waheshimiwa Madiwani waweze kupata vyombo vya usafiri. Hata hivyo jambo hili tutashirikishana vizuri kupitia katika Serikali zetu za Mitaa.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kama ilivyoulizwa katika swali la msingi, baadhi ya Madiwani wanaruhusiwa kuingia katika vikao vya Halmashauri husika lakini baadhi ya Wakurugenzi imekuwa vigumu kwao kuwaruhusu, na mfano mzuri ni Mheshimiwa Stella Allex Ikupa ambaye anapaswa kuingia katika Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Ilala, lakini mpaka leo hii imekuwa vigumu kuhudhuria vikao hivyo.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri unatoa kauli gani ili aweze kuingia katika Baraza hilo na kuwatendea haki watu wenye ulemavu katika kuhakikisha kwamba masuala yao yanaingizwa katika bajeti husika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii nadhani kwamba imeshakwisha, kwa hiyo kama kuna ukakasi wa aina yoyote ofisi yetu italifanyia kazi; lengo kubwa ni kwamba mtu aliyepewa dhamana katika eneo hilo aweze kushiriki vizuri hasa lile kundi analoliwakilisha, kundi la walemavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maftaha Nachuma. Mheshimiwa....

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Selasini.

**MWENYEKITI:** Selasini amechangia mara nyingi sana. Mheshimiwa...

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Nassari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna watu ambao wanasaidia kazi za uongozi kwenye nchi hii nafikiri hata kuliko sisi Waheshimiwa Wabunge na wamekuwa msaada mkubwa

sana kwetu kwenye kutekeleza majukumu yetu kwenye majimbo na kwenye Halmashauri zetu ni viongozi wa Serikali za Mitaa kwa maana ya Wenyeviti wa Vijiji, lakini ambao wanafanya kazi kubwa zaidi ni Madiwani kwenye Halmashauri zetu. Hata hivyo ukweli ni kwamba unapoangalia maslahi ambayo hawa watu wamekuwa wakiyapata ni madogo sana na mara nyingine Serikali inaamua ku-*temper* nayo kwa makusudi kabisa hata kuingilia ule utendaji wa ndani wa Halmashauri wa moja kwa moja inapokuja suala la matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kila wakati tumekuwa tukihoji kwenye Bunge hili kwamba ni lini Serikali inakwenda kuboresha maslahi ya Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Madiwani ili nao waweze kuishi kama viongozi na waonekane kwamba kweli kazi wanayoifanya inathaminika kwenye Taifa? Kila siku Serikali inasema...

**MWENYEKITI:** Inatosha, swali limetosha Mheshimiwa.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, Serikali naomba iji-*commit* kabisa kwamba ni lini watakwenda kuboresha kabisa haya maslahi ya wenyeviti wa vijiji pamoja na Madiwani na waache kusema tutaliangalia, tutaliangalia...........

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa inatosha.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** ......ni lini *exactly? When?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali tunatambua viongozi hawa wa ngazi za chini, Wenyeviti wa Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani wanafanya kazi kubwa sana katika nchi hii, maendeleo yote yanasimamiwa na wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni kweli pia kwamba maslahi ya watumishi mbalimbali wa umma pia watumishi wa kisiasa kila mmoja anasema hayatoshi, tuongeze. Hata

Wabunge wanasema hivyo, walimu wanasema hivyo na wote wanasema tuongeze. Hili litawezekana endapo uchumi wa nchi utatengemaa. Katika mazingira ya sasa, kinachowezekana na ambacho sisi tunaona kinapaswa kufanywa na Serikali kwa ngazi hizi za chini ni ile asilimia 20 tunayoipeleka kwa ajili ya kuendesha ofisi, lakini pia huwa kuna posho ambayo inapatikana. Asilimia 20 ya kiasi cha shilingi bilioni moja au Halmashauri zingine zinakusanya makusanyo ya ndani mpaka shilingi bilioni 50 si hela kidogo zikigawanywa vizuri

Kwa hiyo mimi niseme tu kwamba tunatambua mchango wa viongozi hawa wakati ambapo uchumi utatengemaa tunaweza tukaongeza lakini kwa sasa utaratibu ndiyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wake kama tulivyosema, 40% zitakwenda kwenye miradi wa maendeleo kwenye fedha ile ya *own source,* lakini 10% kwa mikopo kwa ajili ya wanawake na vijana na 20% itakwenda kwa ngazi za chini na hiyo 30% itatumika katika kuendesha Halmashauri. Hii ndiyo hesabu mpya ambayo tumeiweka baada ya bajeti yetu tuliyoisoma hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, swali linaulizwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga lianelekezwa kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 245

**Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Itilima**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ni mpya na haina Hospitali ya Wilaya.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo ili wananchi wa Wilaya hiyo waweze kupata huduma za afya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa jumla ya ekari 30 zimepatikana kwa gharama ya shilingi milioni 30 ili kupata eneo la ujenzi wa hospitali ya Wilaya. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 159.6 kutoka mapato ya ndani na shilingi milioni arobaini na tano kutokana na ruzuku ya maendeleo *(CDG)* kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri imetenga kiasi cha shilingi milioni 371.16 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wagonjwa wa *nje (OPD).* Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 169.9 zinatokana na mapato ya ndani na shilingi milioni 201.2 ni fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu *(CDG).*

**MHE. NJALU D. SILANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante na ahsante kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu ya Itilima kwa mwaka wa fedha 2017/2018 tulikaa na kupitisha katika bajeti makadirio ya shilingi bilioni 1.6 na kipaumbele chetu tukaweka shilingi milioni 650 iwe ndiyo sehemu ya ujenzi wa hospitali hiyo. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni kigezo gani kilichotumika kutoka kwenye shilingi milioni 600 na kurudi shilingi milioni 179?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Halmashauri yetu ya Itilima ina changamoto nyingi katika maeneo yetu, na tayari Halmashauri yangu kushirikiana na wananchi eneo tumeshalipata na tayari tumeshafyatua tofali zaidi ya 15,000 na hivi sasa tumekuwa tukitegemea mapato ya ndani yataweza kusaidia kusukuma uendeshaji wa jengo

hilo pamoja ikiwa na zina ahadi ya Mheshimiwa Rais? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hoja inayozungumzwa na Mheshimiwa Njalu ni hoja ya msingi, na jambo hili Mheshimiwa Njalu alilizungumza mara kadhaa wakati tulipokuwa tukibadilishana mawazo, lakini jambo hili tulivyokuwa tukilifuatilia ilikuwa ni kuhusu mchakato na ilipofika *decision* ya mwisho, juzi nilikuwa naongea na Mkurugenzi wa Itilima kwamba nini kilijiri mpaka imefikia hapo; imeonekana kwamba baada ya kikao kile cha mwisho cha Baraza la Madiwani kulikuwa na makubaliano kutokana na fedha iliyotengwa kwamba milioni 169 iliekezwe katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ndiyo manaa Serikali Kuu ikaongeza shilingi milioni 200 na zaidi. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge anajua kwamba haja ya suala zima la Hospitali ya Wilaya sisi kupitia Ofisi yetu hata katika *commitment* tuliyoweka kwa ajili ya eneo lako la Itilima ukiangalia katika maeneo ambayo tunakwenda kuboresha vituo vya afya Itilima nako tutapeleka takribani shilingi milioni 700 Mungu akijaalia kwa lengo tu kubwa la kuhakikisha kwamba wananchi wa Itilima wanapata hospitali.

Kwa hiyo, jambo hili ni la msingi na sisi Serikali tunalichukulia kwa uzito wake mkubwa sana. Jukumu letu kubwa ni kuwasaidia wananchi wako wa Itilima ambao Mheshimiwa Mbunge unawapigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuongeza fedha katika kuhakikisha kwamba ujenzi huu ambao unaendelea katika maeneo mbalimbali, kama tulivyosema katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2017/2018 katika fedha zile za *CDG* tumeziweka katika mafungu ambayo yatamalizia miradi mbalimbali ambayo ime-*stuck* katika sekta ya afya na sekta ya elimu. Jukumu letu kubwa ni kuweza kuongeza nguvu za wananchi ili hii miradi iliyoanza iweze kumalizika, kwa hiyo, Mheshimiwa Njalu naomba uwe na imani kwamba

Serikali yako iko nawe kuhakikisha kwamba maendeleo katika jimbo lako ambalo ni jimbo jipya yanaweza kufanikiwa kama ilivyokusudiwa.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Matatizo yaliyopo huko Itilima yapo pia katika Halmashauri mpya ya Wilaya ya Itigi. Wananchi wa Itigi wanaitegemea sana Hospitali ya *Mission* ya Mtakatifu Gaspari hawana hospitali ya wilaya. Je, Sasa Serikali iko tayari kusaidia Halmashauri ya Itigi kujenga nayo hospitali ya Wilaya ili iondokane na gaharama kubwa wanazotumia wananchi wake ambao ni wapiga kura wetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Itigi kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kuna changamoto, lakini mara nyingi ndugu zangu nilikuwa nikisema hapa kwamba hili suala la ujenzi wa hospitali, ujenzi wa vituo vya afya mara nyingi michakato hii inaanza kule *site* chini. Hata hivyo niseme kwamba kwa kesi ya Itigi Mheshimiwa unakumbuka kwamba umeuliza swali hili mara kadhaa na ndiyo maana kutokana kwamba umeliuliza swali hili mara kadhaa, hata Serikali sisi kupitia ofisi yetu iliona lazima iipe kipaumbele Itigi kwa sababu hakuna Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokwenda kutembelea pale Itigi tulikuta kituo cha afya ambacho hali yake si shwari, tukasema tunaanza na hapa. Ndiyo maana muda si mrefu ujao tutakwenda kujenga *centre* ya upasuaji kubwa sana na kujenga wodi zingine. Lengo kubwa ni kukiboresha kile Kituo cha Afya cha Itigi angalau kiweze kutoa huduma ambayo inalingana lingana japo na hospitali ili wananchi wa Jimo lako waweze kupata huduma vizuri.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Kama ambavyo Halmashauri ya Itilima ilivyokuwa na tatizo la Hospitali ya Wilaya, Wilaya ya Liwale ni Wilaya ya zamani sana na lile jengo lake la Hospitali ya Wilaya limeshachakaa na limezidiwa uwezo. Kwa kutambua hilo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Liwale imetenga eneo kama hekari 50 hivi kwaili ya mradi wa hospitali mpya ya Wilaya ya Liwale. Je, Serikali ipo tayari kutuunga mkono katika mradi huu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu tulikuwa wote *site* siku ile Liwale na mvua ilikuwa kidogo inanyesha na tumefika Hospitali yake ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao Liwale pale wana hospitali ya Wilaya, lakini ni hospitali ya muda mrefu sana. Kama wazo hilo zuri lilivyo ambapo mnafikiria kujenga hospitali mpya Serikali haitoshindwa kuungana nanyi, lakini hayo mawazo lazima yaanze kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana kwa kuona umuhimu wa Serikali Mheshimiwa Rais alipita kule kutoa ahadi, na kwa sababu hiyo katika kile Kituo cha Afya cha Kibutuka kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais, tutakifanyia ukarabati mkubwa Kituo cha Afya cha Kibutuka kwa kujenga *theater* pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa ni kwamba kina mama wanaopatikana katika eneo lile waweze kupata huduma. Kwa hiyo, Serikali itakuwa tayari kushirikiana na mipango mizuri ya pale.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea Waheshimiwa Swali Namba 146 linaulizwa na Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga na linaelekezwa kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 246

## Ajali za Bodaboda Nchini

**MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB** aliuliza:-

Kumezuka wimbi kubwa sana lenye kutisha la ajali za bodaboda nchini kiasi cha kufanya hospitali zetu kupungukiwa na uwezo wa kuwahudumia waathirika wote wa ajali hizo.

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Taifa sababu za kutokea kwa wingi kwa ajali hizo?

(b) Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na utitiri wa ajali hizo bila kuathiri ajira hiyo ya bodaboda?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mbunge wa Chonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pikipiki za matairi mawili (Bodaboda) na za matatu (Bajaj) zilianza kutumika kubeba abiria mwaka 2008 Tanzania Bara na mwaka 2009 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia vyombo hivyo vitumike kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria. Sababu kubwa za kutokea kwa ajali zinazohusisha bodaboda na bajaj ni uzembe wa baadhi ya waendesha pikipiki na bajaji kutokufuata Sheria na Kanuni za Usalama Barabarani kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikijibu hapa Bungeni, Serikali inatambua biashara hiyo inayofanywa na pikipiki za kubeba abiria na inathamini mchango huo katika kutoa ajira katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na ajali nyingi zinazosababishwa na bodaboda, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua dhidi ya waendesha pikipiki ambao hawazingatii Sheria ya Usalama Barabarani na kanuni zake pamoja na masharti ya leseni za usafirishaji. Aidha, Jeshi la Polisi limekuwa likitoa mafunzo kwa waendesha bodaboda juu ya matumizi bora ya barabara.

**MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Swali la kwanza naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, yeye mwenyewe amekiri hapo kwamba ajali hizi zinasababishwa na uzembe na wahusika kutofuata sheria. Lakini pamoja na kuelewa hivyo bado ajali zinaendelea kutokea na bahati mbaya sana ni kwamba ajali hizi zinawahusu nguvu kazi vijana wadogo sana wa Taifa letu.

Je, Serikali inafikiria njia gani nyingine ya kuwabana hawa kuhakikisha kwamba suala hili halitokei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali lingine, Mheshimiwa Waziri hamuoni kwamba inawezekana hawa vijana mbali na uzembe wanapata hizi leseni kwa njia ya rushwa? Kwamba wanafanya kazi hii bila ya ujuzi lakini ukiwafuata unakuta kwamba leseni wanazo. Je, Serikali itahakikisha vipi kwamba hawa vijana wote wanapata leseni kwa njia inayostahili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa *concern* yake kwa sababu ni kweli jambo hili linagharimu maisha ya vijana wenzetu. Lakini niseme tu njia mbadala ambayo tumekuwa tukisisitiza ni kila familia na kila rika na kila vijiwe vya bodaboda kuchukulia kwamba jambo hili wana wajibu nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili si la Serikali peke yake kwa sababu Serikali imeweka taratibu zote hizi. Lakini

ambacho huwa kinatokea kwa vijana wenzetu hawa anaweza akawepo mmoja anayemiliki leseni au anayemiliki pikipiki kwa taratibu zote, lakini anavyotoka na anavyokuwa kituoni, wanatokea wengine kirafiki wanapeana unakuta yeye hata mafunzo ya kuendesha bodaboda hiyo amejifunza ziku hiyo hiyo mpaka saa 4 asubuhi na inapofika mchana anabeba abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa sababu abiria anayepanda hamuulizi kwanza leseni yako iko wapi yeye anaona tu yuko na chombo mambo haya yanajitokeza. Na ndio maana tunapoona hayo yamejitokeza tunachukua hatua kali. Lakini msisitizo tunaofanya na tunapotoa mafunzo, tunaelekeza kila mmoja atambue kwamba hiki ni chombo cha moto na ukikiuka utaratibu wa matumizi yake una hatari ya kupata majeraha ama kupoteza maisha wewe mwenyewe pamoja na wale uliowabeba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuhusu taratibu za leseni, kwa kiwango kikubwa tunafanya hivo. Sasa hivi kwenye kila Mikoa tumeelekeza taratibu za namna ya kuweza kupunguza hata athari za ajali zinapokuwa zimetokea kwa vijana wetu hawa kwa kuzingatia mahitaji yanayotakiwa katika matumizi ya vyombo hivyo vya moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nimewaelekeza hata wale viongozi wa vijiwe hivi vya bodaboda kuchukua wajibu wa kiuongozi kuelekezana kwamba hili jambo ni jambo linaloua, lakini vilevile wazingatie matumizi bora ya mahitaji ambayo yanatolewa katika uendeshaji wa vifaa hivo vya moto.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ajali hizi za wanaoendesha vyombo vya moto ni nyingi sana hapa nchini, je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kila anayehitaji leseni anakuwa na bima ya afya ili waweze kurahisisha matibabu?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mchemba kwa *concern* hiyo ya vijana wetu, tumelipokea kama Serikali na tunaendelea kuongea na wenzetu wa Wizara ya Afya. Lakini kubwa si kwa anayehitaji leseni, tunaongelea kwa wale ambao wanafanya ile shughuli yenyewe. Kwa sababu kwenye leseni kuna kuwepo na vitu vya aina mbili, kuna yule anayemiliki na kuna wale wanaoendesha ambao ndio wamekuwa wakipata zaidi ajali kuliko wale wanaomiliki bodaboda zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na viongozi wa vijiwe hivi tumeendelea kuwaelekeza kwamba wahakikishe katika makundi yale wanatambuana wale wanaohusika na akiongezeka ambaye hayuko kwenye kijiwe chao na hawajui kuhusu leseni zao, nao wachukue wajibu huo kwa sababu kwa kweli ni jambo ambalo linatoa ajira, lakini limekuwa likitugharimu sana maisha ya vijana wetu hawa wanapofanya kazi hizo.

Na. 247

**Tatizo Kubwa la Riba Zinazotolewa na Benki Nchini**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza:-

Lengo la Serikali ni kusaidia sekta binafsi hasa wajasiriamali wadogo ili waweze kujiajiri, lakini tatizo kubwa la wajasiriamali hao katika sekta ya binafsi Tanzania ni tozo kubwa ya riba inayotolewa na benki hapa nchini kuwa kubwa kuliko nchi yoyote Afrika Mashariki.

(a) Licha ya Tanzania kuwa na benki nyingi zaidi kuliko nchi zote Kusini na Mashariki mwa Afrika, je, kwa nini wingi huo bado haujaleta unafuu katika tozo ya riba?

(b) Je, kwa nini Serikali isiweke ukomo wa riba kisheria kwa benki hizi ili kumsaidia mjasiriamali wa sekta binafsi Tanzania kama ilivyofanya nchi ya Kenya?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya sekta ya fedha ya mwaka 1991 yalisababisha Serikali kujitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa shughuli za kibenki nchini ili kuruhusu mfumo wa soko huria, hususan nguvu ya soko kuamua viwango vya riba za mikopo, riba za amana na gharama zingine za huduma za kibenki. Viwango vvya riba za mikopo hupangwa kwa kuzingatia gharama za upatikanaji wa fedha, gharama za uendeshaji, gharama ya bima, sifa za mkopaji na hatari ya mkopaji kutolipa mkopo pamoja na kasi ya mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya uhitaji na utoaji wa mikopo *(demand and supply theory)* si kigezo pekee kinachoweza kupunguza viwango vya riba hapa nchini. Hatari ya kutolipa mkopo ni kigezo kikubwa kinachotumiwa na benki kupanga viwango vya riba za mikopo hususan kwa wajasiriamali wadogo. Uzoefu uliopo sasa unaonesha kuwa benki zinapendelea kukopesha wajasiriamali waliojiunga katika vikundi kuliko mjasiriamali mmoja mmoja ili kupunguza kiwango cha mikopo isiyolipika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanzidata ya mikopo *(credit reference bureau)* ina umuhimu mkubwa katika kuwatambua wakopaji kwa kuwa huhifadhi historia na sifa za wakopaji. Kwa sehemu kubwa, historia na sifa za wafanyabiashara wakubwa zinapatikana kutoka kwenye kanzidata ya mikopo. Hivyo basi wafanyabishara wakubwa wanaaminika na kupata mikopo kwa riba nafuu ikilinganishwa na wajasiliamali wadogo kwa sababu taarifa na sifa zao zinapatikana kirahisi.

Kwa kuwa wajasiriamali walio wengi taarifa zao hazipo kwenye kanzidata ya mikopo, ni vigumu benki

kuwatambua, kuwaamini na kuwapa mikopo kwa riba nafuu. Pia kiwango cha mikopo mibovu kwa wajasiliamali wadogo ni kikubwa ikilinganishwa na makundi mengine.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Taasisi za Fedha ya mwaka 1991 iliyotungwa kwa kuzingatia misingi ya mfumo wa soko huria, Benki Kuu imepewa jukumu na mamlaka ya kusimamia na kuzichukulia hatua taasisi za fedha zinazoendesha shughuli zao kwa hasara. Kutoa maelekezo kwa benki kutumia viwango fulani vya riba, kutaifanya Benki Kuu kukosa nguvu na mamlaka ya kuzichukulia benki hatua endapo zitapata hasara kwa kutumia riba ambayo Benki Kuu imeelekeza. Hivyo basi, Serikali haina mamlaka ya kuweka ukomo wa riba au riba elekezi itakayotumiwa na benki katika kutoa mikopo kwa wajasiliamali.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mikopo isiyolipika *(non performing loans)* imekuwa kwa kikubwa sana tangu miaka 1990, na sababu kubwa ni mbili, ya kwanza ni mazingira magumu ya biashara na ya pili ni riba kuwa juu.

Swali, ni kwanini, Serikali haioni haja ya kuwasaidia wafanyabiashara kwa kuwapa riba yenye mikopo nafuu kama njia ya *stimulus package?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa muda mrefu Serikali yetu imekuwa ikijinadi kuwa yenyewe ni Serikali ya Kijamaa, na misingi na Sera ya Serikali ya Kijamaa ni pamoja na kuwa ukomo wa riba. Je, ni lini Serikali itaweka ukomo wa riba kama ambavyo nchi ya kibepari ya Kenya imeweka ukomo wa riba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa haipendezi hilo neno lako la mwisho la nchi ya kibepari, sema tu nchi ya Kenya. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kutokana na mfumo wa

mwaka 1991 na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, Benki Kuu au Serikali haiwezi kutoa mwelekeo au ukomo wa riba kwa ajili ya benki na taasisi za kifedha. Nchi yetu ni nchi huru inayofuata *liberalization of the economy* na hilo haliwezi kufanyika kwa sababu nimesema ni sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, nchi ya Kenya iliweka ukomo huo lakini imeingia katika matatizo makubwa ya kiuchumi kwa benki na taasisi za kifedha. Hivyo nchi yetu kama nchi huru inayofuata *liberalization of the economy* hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu ni sheria iliyopanga hivyo.

**MHE. DEO K. SANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kupitia Wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji juu ya wajasiriamali wakiwemo wa Makambako juu ya Soko la Kimataifa, nini kauli ya Serikali? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nini kauli ya Serikali kwa wajasiriamali wa Makambako?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Serikali ilitoa kauli wakati tunapitisha bajeti ya Wizara ya Ulinzi na kuhusu wafanyabiashara wajasiriamali wa soko la Makambako naomba kumwambia Mheshimiwa Sanga kwamba Serikali sasa inafanya uhakiki wa mwisho, itakapokuwa imekamilisha kufanya uhakiki huo Serikali itaanza kuwalipa wajasiriamali na wananchi wote ambao wanastahili kulipwa fidia katika maeneo mbalimbali yaliyotwaliwa na Serikali.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016 mikopo ya benki kwenda kwenye sekta binafsi imeporomoko kuliko wakati mwingine wowote katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Fedha inachukua hatua gani madhubuti ya kuhakikisha kwamba wajasiliamali na hasa viwanda na wafanyabiashara wanaendelea kupata mikopo benki kwa kuboresha hali ya uchumi wa nchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba hali ya uchumi wa Taifa letu bado iko imara na iko vizuri na si kwamba kutokupewa mikopo kwa sekta binafsi kunaashiria kuporomoka kwa uchumi, hilo naomba niliweke vizuri hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwambie kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Benki Kuu imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuhakikisha mikopo hii kwa sekta binafsi inaendelea kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba, benki zetu zimekaa vizuri sasa katika kuhakikisha zinadhibiti mikopo chechefu ambayo imekuwa ikizisumbua miaka mingi iliyopika. Kwa hiyo ni usimamizi madhubuti uliowekwa na Benki Kuu kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, na tunaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba kabla ya benki na taasisi za kifedha hazijatoa mikopo wahakikishe mtu wanaempa mikopo ni nani na ana uhakika gani wa kurejesha mikopo ambayo ipo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na riba kubwa inayotozwa kwa wafanyabiashara wadogo lakini pia wafanyabiashara wadogo wanachangamoto kubwa ya tozo za ada na ushuru katika makundi haya ya bodaboda, mama ntilie na wauza mbogamboga. Na kwa kuwa Serikali yetu kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliahidi Itazitazama upya tozo hizi ambazo ni kikwazo kwa wafanyabiashara wadogo, sasa ni lini Serikali yetu itatazama upya tozo hizi ili wafanyabiashara wadogo waweze kupunguziwa mzigo mkubwa katika uendeshaji wa biashara yao?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, ni lini mtaziangalia tozo hizo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Bunge lako Tukufu limeona kupitia Wizara ya Kilimo kuna tozo ambazo zimependekezwa nyingi tu kuondolewa, ambazo serikali iliahidi kuziondoa. Na nyingine ambazo haziko chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko kwenye mchakato wa kuandaa *Tax Measures* na *Finance Act, 2017,* hivyo tuvute subra, yote haya ambayo Serikali yetu iliahidi yote yatatekelezwa.

**MWENYEKITI:** Tuvute subra Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Swali namba 248 linaulizwa na Mheshimiwa Mashimba Mashahuri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi na linaelekezwa kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Na. 248

**Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI** aliuliza:-

Serikali imekamilisha mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Mji wa Ngudu na vijiji vilivyo karibu na Mji huo Wilayani Kwimba, mradi huu unatoa maji ya uhakika kuliko miradi ya visima vifupi ambavyo ni vya msimu, lakini Mji Mdogo wa Malampaka na vijiji vingine vya karibu kama Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyabubinza na Mwang'horoli ambavyo vipo karibu na Mji wa Ngudu havijaunganishwa kwenye mradi huo.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunganisha Mji Mdogo wa Malampka na vijiji vya Jihu, Bukigi, Muhida, Lali, Nyababinza na Mwang'horoli katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetekeleza mradi wa maji safi kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Mji wa Ngudu na vijiji vilivyopo kandokando ya bomba linalopeleka maji katika Mji wa Ngudu. Vijiji hivyo ni Runele, Ngatuli, Nyang'onge, Damhi na Chibuji. Mradi huu ulihusu ulazaji wa bomba kilomita 25 na sehemu nyingine ya bomba lilitumika bomba la zamani la mradi wa visima uliojengwa miaka ya 70. Bomba hilo ni la kipenyo cha inchi nane na kulingana na usanifu halitoshi kupeleka maji kwenda Malampaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji inatekeleza miradi ya maji Malampaka, Sayusayu, Mwasayi, Njiapanda na Sangamwalugesha, ambapo miradi hii imekamillika na wananchi wanapata maji.

Aidha, miradi ya maji ya Lalagomandang'ombe na Jija inaendelea kujengwa na ujenzi umefikia asilimia 50. Serikali pia imekamilisha usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa miradi ya maji ya Mwabulimbu, Mwamanenge, na Badi ambao utahudumia vijiji vitatu vya Muhiba, Jihu na Badi yenyewe. Ujenzi wa miradi hii utafanyika katika awamu ya pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda kwenye Miji ya Sumve, Malampka na Mallya. Hadi sasa taratibu za kumpata mtaalamu mshauri atayefanya usanifu wa mradi huo zianendelea. Hivyo, baadhi ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vitajumuishwa katika mradi huo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi huo.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nishukuru pia kwa majibu mazuri ya

Mheshimiwa Waziri lakini nataka kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali pia ilitenga kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kufanya usanifu na ushauri kwa mradi huu wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwa miji hiyo mitatu. Mwaka huu pia wameweka kama shilingi bilioni mbili kama alivyosema. Je, Serikali inatuhakikishiaje sisi wananchi wa Maswa Magharibi, kwamba kazi hii sasa itafanyika mwaka huu na mradi uweze kuanza mwakani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa miradi mingi ya visima vifupi alivyovitaja Mheshimiwa Waziri inakauka wakati wakiangazi kikali, mwezi wa nane, wa tisa na wa kumi. Je, Serikali haioni sasa kutupatia maji kutoka vyanzo vya kudumu kama mabwawa makubwa pamoja na miradi kama hii ya kutoa maji Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Ndaki kwa sababu kwanza ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji, lakini pia amekuwa ni Mheshimiwa ambaye tunaongea naye sana, anakuja ofisini kufuatilia suala la maji katika jimbo lake na nilishawahi kutembelea katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza ni kwamba katika bajeti ya mwaka 2016/2017 tumetenga shilingi bilioni moja na mwaka huu haujaisha, hela hiyo ndio iliyotufanya tuanze kufanya usanifu wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda kupeleka Malampaka, na kuna kazi kubwa ambayo imeshafanyika, na ni matarajio yetu kwamba baada ya kukamilisha uzanifu tunaanza sasa kutangaza, na fedha hiyo tutaangalia utaratibu ili iweze kuanza kutumika katika mradi huu tukishapata wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya utaratibu, kama nilivyokwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeona tuwatumie *KASHWASA.* Wale *KASHWASA* wana utaalamu

mkubwa wameshatekeleza mradi mkubwa, kwa hiyo kutakuwa na wepesi kidogo kwa kushirikiana na halmashauri yako tuhakikishe kwamba mradi huu unatekelezwa kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la visima vifupi, ni kweli kabisa maeneo mengi tumechimba visima vifupi lakini hivi vinapata maji kipindi cha mvua na muda kidogo wa miezi michache baada ya mvua. Kutokana na hilo basi sasa hivi tunafanya utaratibu, kama ulivyopendekeza mwenyewe, kuangalia sehemu inayofaa kuchimba mabwawa tunahakikisha kwa kushirikiana na halmashauri tunasanifu na tunachimba mabwawa yaweze kutunza maji kama ambavyo bwawa lile la Maswa linatunza maji na kulisha vijiji 11 pamoja na mji wa Maswa, lakini pia na kutumia vyanzo vya kudumu kama bomba la *KASHWASA* kama tunavyotaka kufanya sasa hivi ili kuachana na visima vifupi.

**MWENYEKITI:** Ahsante, acha tuone yanayofanana na hali halisi ya Maswa. Swali la msingi linahusu Maswa, Mheshimiwa Stansalus Nyongo Mbunge wa Maswa Mashariki.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nashukuru sana kwa kujali hilo.

Ningependa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa maji kwamba kuna mradi ule mwingine wa Ziwa Victoria unaopita hadi maeneo ya Kolandoto kwenda Wilaya ya Kishapu. Nilishawahi kuuliza siku za nyuma kwamba kuna vijiji vya Mwamashindike, Mwabalatulu, Mwakidiga, Lalago hadi Budekwa viko karibu na eneo la Kishapu. Je nini kauli ya Serikali kwa maeneo hayo kupata maji kutoka ule mradi wa Kolandoto kuja maeneo hayo? Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Katika utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka Kishapu tulichokifanya ni kwamba maeneo yote ambayo lile bomba limepita tumetoa matoleo ya kupeleka kwenye vile vijiji ambavyo vipo ndani

ya kilometa 12 kila upande. Sasa tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi, kwamba sasa wanapopanga mipango yao ya kupeleka maji kwenye vijiji vyao pale ndipo patakapokuwa chanzo cha kuchukulia maji. Kwa hiyo, mipango ya halmashauri na vipaumbele vyao tumeshawazogezea sasa kwenye lile bomba kubwa. Lakini pia tutaweza kuendelea na bajeti ya Serikali maeneo yale mengine kulingana na bajeti ambayo mmeipitisha hivi karibuni. Tukipata fedha hizo basi tutaendelea nasi kusaidiana na Halmashauri kupeleka maji maeneo mengi jinsi itakavyokuwa inawezekana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea swali namba 249 linaulizwa kwa Wizara hiyo hiyo Wizara ya Maji na Umwagiliaji na linaulizwa na Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto Mbunge wa Kigoma Mjini.

Na.249

**Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji Katika Delta ya Mto Luiche**

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO** aliuliza:-

Mwezi Juni, 2015 Serikali ya Falme ya Kuwait kupitia Wakfu ya Kuwait iliijulisha Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kuwa wapo tayari kufadhili mradi wa kilimo cha umwagiliaji katika Delta ya Mto Luiche.

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa mradi huo ili kuongeza uzalishaji wa chakula nchini, kujenga viwanda vidogo vya mazao ya kilimo na kuondoa umaskini kwa wakazi wa Manispaa ya Kigoma Ujiji Mkoani Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Ruyagwa Zitto, Mbunge wa Jimbo la Kigoma Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kilimo cha umwagiliaji unaopendekezwa katika Bonde la Mto Luiche, Manispaa ya Kigoma Ujiji una wastani wa eneo la hekta 3,000 linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mazao ya mpunga, mahindi na mbogamboga. Mnamo mwaka 2015 Serikali iliwasilisha ombi kwa Serikali ya Falme ya Kuwait kuhusu uendelezaji wa mradi huo ambapo Serikali ya Falme ya Kuwait ilikubali kwa masharti ya kupewa taarifa ya upembuzi yakinifu *(feasibility study report)* na maoni kutoka kwa nchi zinazotumia maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hii, Serikali ilifanya upembuzi yakinifu wa awali mwaka 2015. Hivi sasa Serikali ipo katika hatua ya manunuzi ya mtaalamu mshauri kwa ajili ya kazi ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Kazi hii ikikamilika Serikali itawasilisha taarifa ya kina ya kiwango cha maji kinachohitajika kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwemo kilimo cha umwagiliaji.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia hatua hii kuna juhudi kubwa ambazo zimefanywa na ninapenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watu wa Tume ya Umwagiliaji kuweza kuhakikisha kwamba tunafikia hatua hii. Lakini kumekuwa na tabia ya miradi ambayo tayari inakubaliwa na wafadhili lakini hatua za kuchukua mpaka kupata hiyo miradi inakuwa ni ya muda mrefu sana mfano wa mradi huu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali tu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali. Kwa hiyo, kwa mfano mradi huu toka mwaka 2015 tumepewa haya masharti na sasa hivi ndiyo kwanza tunakwenda kwenye hatua za manunuzi ya mtalaamu mwelekezi.

Sasa Waziri anaweza kutufahamisha hatua hizi za kukamilisha *detailed design* na hii *feasibility study* zitakamilika lini ili kuweza kuona mradi wenyewe utaanza kutekelezwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kwa upande wa Serikali ni hatua gani zitachukuliwa katika kuhakikisha kwamba miradi ambayo tunakuwa tumeahidiwa na imeshakubalika tunapunguza muda ambao tunauchukua kuikamilisha ili hii miradi isiende nchi nyingine? Kwa sababu sasa hivi miradi mingi inaenda Kenya na Mozambique kwa sababu ya kuchelewa kwetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa umeeleweka. Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Injinia Isack Kamwele majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ameonesha *concern* yake kwamba wafadhili wanatoa fedha lakini pengine taratibu zinachukua muda mrefu. Nikuhakikishie Mheshimiwa Kabwe kwamba ni utaratibu wa kawaida, kunapokuwa na mradi ni lazima ufanye *feasibility study* ili uweze kuonesha *economic viability* ya mradi ule na huwezi ku-*rush,* lazima uende uweze kupata taarifa za uhakika zinazotakiwa. Baada ya hapo unaingia kwenye hatua nyingine sasa ya *detailed design*. Information hii tunayoifanya Mheshimiwa Mbunge kama haikukaa vizuri haiwezi kupitishwa kule tunakopeleka. Kwa hiyo, tunachokifanya ni utaratibu wa kawaida kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, Serikali inaitaka hiyo fedha, haiwezi kuiacha na ndiyo maana Hazina wanaendelea kufanya mawasiliano na hii Falme ya Kuwait ili kuhakikisha kwamba wanaendelea kututunzia hiyo fedha na taarifa tayari zipo. Sasa hivi tunafanya manunuzi ya kumpata mtaalamu mshauri na huyo ndiye atakaye-*define,* kwa sababu tunapoweka ile *proposal* ya kwa wale ma-*consultant* ndipo tunawapa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kutokana na *complexity* ya ile *site* tunaweza tukasema mfanye kwa miezi sita wakasema haitawezekana tukafanye miezi nane kulingana na hali yenyewe ya eneo wanalofanyia kazi. Hatuwezi kutoa muda kwa sasa, ngoja kwanza tusaini mikataba ya *consultant* ambayo itaonyesha *period*

watakayotumia na wao ndio watakaotushauri muda tutakaouanza suala la ujenzi; baada ya hapo Mheshimiwa Mbunge tutakupa taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante hebu tuone jirani yako hapo atasema nini, Mheshimiwa Nsanzugwanko kwako.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Huu mradi wa umwagiliaji wa Mto Luiche umefanana sana na mradi wa umwagiliaji wa Bonde la Titye na Bonde la Rungwe Mpya. Sasa ningependa kujua, miradi yote hii miwili kwa kweli inasuasua sana, imeshaanza lakini uendelezaji wake wa kujenga mifereji umekwama sana. Nilitaka kujua ni lini sasa Wizara hii itaangalia *scheme* hizo mbili ambazo zimeshaanza kufanya kazi lakini shida imekuwa ni mifereji ya kupeleka maji kwa wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Nsanzugwanko kuhusiana na miradi miwili kwenye jimbo lake ambayo anadai kwamba ilishaanza kufanyiwa kazi lakini kuna mambo ambayo hayajakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba katika ziara nilizozifanya kwenye maeneo mengi ya umwagiliaji ni kweli kabisa hoja ya Mheshimiwa Nsanzugwanko, kwamba unakuta miradi kwenye vyanzo yale mabanio yameshajengwa, mifereji mikubwa imejengwa lakini midogo ya kusambaza maji kupeleka kwenye mashamba bado. Hata hivyo kuna miradi mingine ambayo imesanifiwa vizuri na imejengwa vyanzo vya maji kutokana na uharibifu wa mazingira vimekauka na ile miradi haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndio maana sasa Serikali ya Japan imetusaidia fedha na mshauri ameanza kufanya kazi, ili kupitia miradi yote hii tuweze kubaini changamoto na aweze kuainisha zile hekta 1,000,000 tulizoahidi kuzijenga katika hiki kipindi cha miaka mitano. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba timu iliyopo itafika mpaka kwako ili kubaini changamoto gani imefanya hiyo miradi

isikamilike, kuna shida gani baada ya hapo tunaweka fedha kuhakikisha tunakamilisha ili wananchi waweze kulima na tuwe na uhakika wa chakula.

**MWENYEKITI:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, swali namba 250 linaelekezwa Wizara ya Kilimo na Mifugo na linaulizwa na Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 250

**Dawa za Kilimo na Mifugo Kutokukidhi Vigezo**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo la uagizaji wa dawa za kilimo na mifugo ndani ya nchi zisizokidhi vigezo na bei ya dawa hizo zinaongezeka siku hadi siku na kufanya wakulima na wafugaji wadogo kukosa maendeleo.

(a)Je, Serikali inachukua hatua gani za kuhakiki dawa hizo kabla hazijaingia nchini?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kudhibiti bei hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassin Chikambo, lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa ubora na usalama wa dawa na viwatilivu vinavyoingia nchini na ambavyo vipo katika soko unafanywa na Mamlaka mbalimbali za Serikali kama vile Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* kwa upande wa dawa za mifugo na Taasisi ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kitropiki *(TFRI)* kwa upande wa viuatilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu hili Mamlaka hizo zina mifumo ya udhibiti katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili wa dawa zinazoingia nchini; dawa zote na viuatilifu vinavyoingia nchini zinatakiwa kwanza ziwe zimesajiliwa na mamlaka hizo ili kujihakikishia ubora, usalama na ufanisi kabla hazijaingia katika soko la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa viwanda vinavyotengeneza dawa; ukaguzi huu hufanywa na mamlaka hizo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa vinazingatia viwango vya uzalishaji bora wa dawa *(good manufacturing practice).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa kufuatilia dawa katika soko *(post marketing surveillance)* hufanyika ili kuhakikisha kuwa dawa zilizopo katika soko zinaendelea kuwa na ubora ule ule kama wakati ziliposajiliwa. Sampuli mbalimbali za dawa huwa zinachuliwa katika soko na kupelekwa maabara kwa ajili ya kuzipima kwa minajili ya kudhibiti na kuthibitisha ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa bei za dawa na viuatilifu zinapangwa na nguvu ya soko lakini Serikali imeondoa ushuru wa forodha na *VAT* ili kumpunguzia mkulima mzigo wa bei. Aidha, Serikali inaendelea kuzipitia tozo na ada mbalimbali katika sekta ya kilimo na ikionekana inafaa ziondolewe ili kuongeza unafuu kwa mkulima.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilipenda niseme kama ifuatavyo:-

Suala la uingizaji wa dawa za kilimo zisizokidhi vigezo limekuwa sugu katika nchi yetu. Hata hivyo Mheshimiwa Waziri ameeleza mamlaka mbalimbali ambazo zinahusika katika kuhakiki hizo dawa na uingizaji. Nilipenda kujua ni hatua zipi zimekuwa zikichuliwa kwa makampuni hayo ambayo

yamekuwa yakileta dawa ambazo hazikizi vigezo; hasa kwa sabau zinaleta mzigo mkubwa kwa wakulima wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali inaendelea kupitia tozo mbalimbali katika sekta ya kilimo ili kuona uwezekano wa kuziondoa tozo hizo. Nilipenda kujua kwamba zoezi hilo la kupitia hizo tozo ambazo zimekuwa mzigo kwa wakulima wetu litaanza lini ili kuleta unafuu kwa wakulima wetu? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na uingizwaji wa dawa ambazo hazikidhi viwango ni kweli kabisa kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna changamoto hiyo. Hata hivyo Serikali imeendelea kudhibiti na kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha tatizo hilo linamalizika ili kuhakikisha kwamba wakulima wetu hawaathiriwi na viuatilifu ambavyo si salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya hatua ambazo tunazichukua ni kwamba pale tunapogundua, kwamba Kampuni fulani imeingiza dawa ambayo si sahihi, mara nyingi Kampuni ile inafutiwa leseni, lakini vile vile kama ni maduka tunayafunga, lakini tayari vile vile kuna kesi nyingi ambazo ziko Mahakamani kwa watu na Makampuni ambao wamebainika kuvunja taratibu za Kisheria kuhusiana na viuatilifu pamoja na dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2016 tulifanikiwa kukamata viuatilifu lita 14,600 ikiwa ni sehemu ya ufuatiliaji wa kawaida wa kuhakikisha kwamba wakulima wetu wanapata viuatilifu na dawa salama. Ifahamike tu kwamba viuatilifu vingi ambavyo vinaingia ambavyo havikidhi viwango vingi vinatoka nje na hiviingizwi kwa utaratibu wa njia rasmi, zinapitia katika uchochoro, katika *panya roads.* Kwa hiyo, mara nyingi wahalifu kila wakati wanagundua njia mpya ya kuhakikisha kwamba wanakwepa mkono wa Sheria lakini Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba kila wakati yule ambae anahusika anachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na tozo, nafikiri Mheshimiwa Mbunge amekuwepo, kwa sababu sasa tunaendelea na mjadala wa Wizara yetu, kwamba tayari Wizara imependekeza kufuta tozo 108, tozo ambazo tunahakika zikifutwa zitamsaidia sana mkulima, mfugaji na mvuvi wa Tanzania katika kuendelea kunufaika na kilimo, ufugaji na uvuvi wao. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aendelee kufuatilia kwa sababu tayari tumeishaondoa hizo tozo, lakini Wizara inaendelea kuongea na Wizara zingine ambazo zinasimamia baadhi ya tozo ili tuendelee kuziondoa au kuzipunguza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Maswali mawili ya nyongeza Mheshimiwa Chegeni na Mheshimiwa Maige.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa viuatilifu hivi kwa kweli imekuwa ni hasara kubwa sana kwa wakulima, na kwa kuwa wakulima wa Jimbo la Bariadi na Jimbo la Busega katika msimu huu wamelima sana zao la mahindi lakini limeshambuliwa na funza, kitu ambacho kimesababisha watapata uhaba wa chakula, je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi ili watu hao wanaoingiza viatilifu ambavyo havifai na viko chini ya viwango wanadhibitiwa na wanapewa adhabu kali?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali; kama Mheshimiwa Mbunge anawafahamu watu au makampuni ambao wameingiza viuatilifu ambavyo haviko katika ubora unaotakiwa kisheria tutawachukulia hatua. Hata leo hii hii akinipa *list* yao tutaanza kufanyia kazi na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuwafungia na kuwaondolea leseni ya kuagiza na kuuza viuatilifu lakini vile vile kuwapeleka Mahakamani kwa sababu ni kinyume cha Sheria kuuza dawa na viuatilifu ambavyo havina ubora.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri unisikilize vizuri. Msimu

uliopita wa mwaka juzi, wakulima wa pamba wote wa Kanda ya Ziwa walilazimishwa kutumia dawa ya kuua wadudu inayoitwa Ninja. Dawa hiyo ilikuwa inasambazwa na Bodi ya Pamba na haikusaidia kabisa na pamba iliharibika kabisa kwa sababu haikuwa na ubora. Niliuliza swali hapa Bungeni nikaahidiwa na Serikali kwamba, na yenyewe imethibitisha kwamba suala hilo ni kosa la uhujumu uchumi, kwa hivyo, wahusika watapelekwa mahakamani na wakulima watalipwa fidia ya gharama waliyotumia kununua ile dawa.

**MWENYEKITI:** Swali sasa.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua kwamba Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa hilo jibu ambalo Serikali iliniambia hapa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba iligundulika kwamba ilitokea matatizo makubwa kwa wakulima wa pamba waliotumia kiuatilifu ambacho kilikuwa kinatiliwa shaka kuhusu ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na uchunguzi kubaini ni nini hasa kilitokea, kwa sababu tayari kuna mvutano kuhusu je, suala lilikuwa ni ubora wa dawa, namna ya matumizi, namna ya matunzo au ni suala la wakulima wenyewe walivyotumia ile dawa. Kwa hiyo, Serikali bado inaendelea na uchunguzi, lakini pale itakapobainika kwamba ni kweli kabisa kwamba suala ni kuhusu ubora sheria zitachukua mkondo wake. Kama nilivyosema, itakuwa ni pamoja na kuwafungia na kuwachukulia hatua wale wote ambao wamehusika. Vile vile ikibainika kwamba kampuni ambazo zili-*supply* hiyo dawa kwa Bodi ya Pamba wao watawajibika moja kwa moja katika kuhakikisha kwamba wakulima wanalipwa fidia. Hata hivyo kama nilivyosema suala hili bado linachunguzwa, tufahamu hasa kiini kwa sababu bado kuna mvutano kuhusu sababu hasa yenyewe iliyosababisha tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, lakini kamilisheni uchunguzi, haiwezekani mkaendelea miaka mitatu mnachunguza tu. *(Makofi)*

Tunaendelea Waheshimiwa swali linalofuata 251 linaulizwa na Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega Mbunge wa Mkuranga na linaelekezwa kwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 251

**Fidia Kwa Wananchi Waliowekewa Alama 'X' - Mkuranga**

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ipo tayari kuwalipa fidia wananchi waliowekewa alama za 'X' kwenye nyumba zao katika Barabara ya Mkuranga kwenda Kisiju?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Hamis Ulega, Mbunge wa Mkuranga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, eneo la hifadhi ya barabara kwa barabara kuu na barabara za mikoa limeongezeka kutoka mita 22.5 zilizotajwa katika Sheria ya Barabara ya mwaka 1967 hadi mita 30 kila upande kutoka katikati ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mkuranga hadi Kisiju yenye urefu wa kilometa 46 ni miongoni mwa barabara za mikoa zilizopo chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*. Katika kutimiza matakwa ya Sheria ya Barabaa ya mwaka 2007 Wakala wa Barabara Tanzania ulifanya zoezi la utambuzi wa mali zilizopo ndani ya hifadhi

ya barabara kuu na barabara za mikoa nchini nzima ikiwemo Barabara ya Mkuranga hadi Kisiju. Lengo la kuweka alama ya 'X' ni kuwajulisha na kuwatahadharisha wananchi juu ya ongezeko la eneo la hifadhi ya barabara ili wasifanye maendeleo mapya kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya nyumba zilizowekwa alama 'X' kuna ambazo zimo katika hifadhi ya barabara ya mita 22.5 kila upande wa barabara ambapo wamiliki wake walipewa *notice* ya kuziondoa bila kulipwa fidia kwa kuwa walivamia eneo la hifadhi ya barabara. Kwa zile ambazo zimo kati ya mita 22.5 hadi 30 kila upande wamiliki wake wanastahili kulipwa fidia. Kwa sasa wananchi hawa hawatakiwi kufanya maendelezo yoyote katika maeneo hayo ingawa hawalazimiki kuomba wala kuondoa mali zao mpaka hapo Serikali itakapolihitaji eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Aidha, kabla Serikali haijatwaa eneo hilo uthamini utafanyika na wananchi wanaostahili kulipwa fidia watalipwa.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa ni wa muda mrefu sasa, wao wenyewe wameridhi kutoka kwa wazazi wao ambao wameshafariki, na wao wenyewe miongoni mwao wanaelekea kuwa watu wazima sasa, ni lini Serikali itawalipa haki zao wananchi hawa, ilimradi wale warithi wao wasisumbuke kama ambavyo wao sasa hivi wanavyoishi, wakiwa hawaelewi ni lini watalipwa pesa zao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu la swali la msingi, ni kwamba wananchi hao waliowekewa alama 'X' hawatakiwa kufanya maendelezo, lakini hawatakiwi kubomoa nyumba zao, wataendelea kuzitumia mpaka pale Serikali itakapokuja kuyatwaa maeneo hayo kwa ajili ya upanuzi au ujenzi wa barabara.

Kwa sasa kwa wale ambao wako ndani ya mita 22.5 wanatakiwa wabomoe na waondoke wakajenge sehemu nyingine. Wale ambao wako kati ya mita 22.5 na mita 30 wanaendelea kuyatumia maeneo yao mpaka pale Serikali itakapolitaka hilo eneo, na ndipo uthamini utafanyika na fidia watalipwa. Tumetoa hizo alama 'X' barabara zote Tanzania nzima, sidhani kama ni sahihi kwamba wewe uliyewekewa alama ya kijani ya 'X' ulipwe fidia nchi nzima hata bajeti yote tukiitumia kulipa fidia haitatosha. Kwa hiyo, tutakuwa tunalipa pale tu ambapo sasa tunataka kuanza kulitumia hilo eneo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gama halafu Mheshimiwa Kikwembe. Hawa wanatosha.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa wananchi wa Mkuranga na Kisiju pale Songea Mjini na sisi tuna tatizo hilo hilo la 'X'. Barabara ya *Mtwara Corridor* ambayo inapita Songea Mjini inafanya mchepuko katika eneo la Ruhilaseko kuelekea Masigira, Msamala, Mkuzo na Luhuwiko. Eneo hili wananchi wamewekewa 'X' kwa muda mrefu lakini hawajalipwa fidia yao na wala barabara haijaanza kujengwa. Sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, je wananchi hawa ambao wana alama za 'X' za muda mrefu ni lini watalipwa fidia zao ili barabara ianze kujengwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ni lini mtaanza kujenga hiyo barabara?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jibu la haraka kwa swali lake ni kwamba tutalipa fidia mara pale barabara hiyo au barabara ile ya mchepuko tutakapoanza kuijenga. Katika fedha tutakazozitenga kwa ajili ya kujenga barabara ile ya mchepuko zitahusisha vilevile na fedha za fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu niongeze kidogo kuhusu eneo analoliongelea, kwa bahati nzuri ule mchepuko

ni lazima ujengwe haraka kutokana na mazingira ya mji wa Songea yalivyo, na hivyo nimhakikishie tu kwamba malipo haya hayatachelewa sana kwa sababu ujenzi wa barabara ile ya mchepuko hautachelewa sana kushughulikiwa.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, katika majibu yake ya msingi amesema kwamba watalipwa pale maeneo watakapoyahitaji, lakini tukiangalia kuna maendeleo yanayoenda kufanywa sasa hivi, kwa mfano katika barabara yangu ya Kibaoni, Usevya, Mbede, Majimoto, Mamba, Kasansa mpaka Mfinga ambako tutatekeleza *REA III.* Ni lini wananchi hawa wenye alama za 'X' za kijani mtawalipa pesa zao ili waweze kufaya marekebisho ya nyumba zao waweze kuweka umeme wa *REA?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu katika swali la msingi la Mheshimiwa Ulega, ni kwamba kila tunapotaka kuanza kujenga barabara fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara zinaunganishwa vile vile na fedha za kulipa fidia katika maeneo ambayo tunatarajia kuyajenga.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Pudenciana Kikwembe na wananchi wa Kavuu kwamba tutawalipa fidia wale wanaostahili kulipwa fidia mara tutakapopata fedha za kuanza kujenga barabara husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, swali 252 linaulizwa na Mheshimiwa Munira Mustafa Khatibu Mbunge wa Viti Maalum na linaelekezwa kwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Na. 252

**Kufuta Tozo na Gharama za Vifaa vya Kujifungulia na Upasuaji**

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta tozo na gharama za vifaa vya kujifungulia na upasuaji kama ilivyofuta za matibabu ya wazee na wagonjwa wa kisukari?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Mheshimiwa Kigwangalla majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatibu, Mbunge wa Viti Malaam kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaeleza kuwa huduma za kina mama wajawazito katika vituo vya ngazi zote zinapaswa kutolewa bila malipo. Serikali haijawahi kuweka tozo na gharama za vifaa vya kujifungulia na wala vya upasuaji. Huduma hizo zinatolewa katika ngazi zote katika vituo vya umma vya kutolea huduma kwa gharama za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha sera hii inatekelezwa kwa vitendo, Wizara inahakikisha akina mama wanakuwa na vifaa muhimu vya kujifungulia, ambapo vifuko maalum vyenye vifaa vya kujifungulia *(delivery packs)* kwa wanawake 500,000 vitasambazwa nchi nzima kulingana na uhitaji. Kwa wastani nchini Tanzania jumla ya akina mama 1,900,000 wanajifungua kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa tusaidiane kusimamia utekelezaji wa sera tulizokubaliana katika maeneo yetu kwa kuhakikisha huduma hizi za akina mama zinapatikana kwa gharama za Serikali ili azma ya Serikali ya kuhakikisha akina mama wajawazito wanapata huduma nzuri na lengo la kupunguza vifo vya Mama na watoto hapa nchini lifikiwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nipende kumuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini inaonesha kwamba kila mwaka akina mama zaidi ya 400 wanapoteza maisha kutokana na vifo vinavyosababishwa na kujifungua. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza vifo hivi 400 kwa mwaka vinavyojitokeza wakati wa kujifungua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, ni kwa nini vituo vya huduma ya upasuaji katika Tanzania yetu ni vichache hasa ukizingatia maeneo ya vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu, kwa Mheshimiwa Munira, na unamuona alivyo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze kwa hali aliyo nayo na nimtakie kila la kheri yeye na mwanaye na niwahakikishie kwamba watamaliza safari yao salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujibu maswali yake naomba niyajibu kwa pamoja tu kwamba tuna mkakati gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati tuliyonayo ni mingi na kwa kiasi kikubwa Serikali kwa sasa imewekeza nguvu zake zote kwenye huduma zijulikanazo kitaalamu kama *Comprehensive Emergency Obstetric and Neonatal Care (CEmONC).* Hizi ni *package* ya *medical interventions* ambazo zinahusisha kufanya upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni, kumsaidia mama kwa kutumia njia za *manual,* lakini kumsaidia mama wakati wa kujifungua kama mtoto amekwama kwenye njia, pia kumuongezea damu mama mjamzito wakati wa kujifungua ama baada ya kujifungua, vile vile huduma za kutoa dawa ambazo zinajulikana kama *urotonic* ambazo zinasaidia ku-*contract* ile *placenta* wakati wa kujifungua ili kupunguza damu nyingi kupotea kwa mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile huduma za dawa zinazopunguza magonjwa ya kifafa cha mimba, magonjwa kama *eclampsia*, *pre-eclampsia*, *gestational hypertension* na magonjwa yote yanayohusiana na akina mama wajawazito. Sasa hii *package* inapaswa kutolewa kwenye vituo vya afya nchini, inaitwa *CEmONC.* Huduma hizi kwa kweli zilikuwa za kiwango cha chini sana. Katika vituo vya afya takribani 484 tulivyo navyo nchini vinavyomilikiwa na Serikali tulikuwa na vituo 113 tu vinavyotoa huduma hizi; lakini kwa mujibu wa sera vituo vyote vingepaswa kutoa huduma hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ndiyo maana katika bajeti iliyopita hata kwenye bajeti hii tumejikita zaidi kwenye kuongeza idadi ya vituo ambavyo vitaweza kutoa huduma za *CEmONC,* na pia mkakati wetu umeendana sambamba na kuhakikisha hizo dawa nilizozisema kama oxytocin na *magnesium sulphate* zinapatika kwenye vituo vyote, hiyo ndiyo mikakati tuliyonayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** ahsante, Waheshimiwa Wabunge hili la akina mama hili eeh sasa, Mheshimiwa Mlata, Mheshimiwa Msabaha na Mheshimiwa Khadija, inatosha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Serikali kuweka mikakati mizuri ya kuhakikisha

inapunguza vifo vya akina mama, nilikuwa naomba; wewe unatambua sasa hivi kuna Watanzania wengi walioko vijijini na mitaani wanaoteseka, wanaoumwa na kuugua maradhi yanayotibika lakini wamekosa fedha za kutibiwa hospitali mpaka wanagundulika na vyombo kama televisheni au redio au waandishi kwa sababu ya kukosa pesa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia watu hawa? Kwa mfano kuna kijana mmoja anaitwa John ambaye ana maradhi makubwa ya moyo amegundulika na *Clouds Television,* je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wagonjwa hawa? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza nivipongeze vyombo vya habari na Watanzania wote ambao wamekuwa katika nyakati tofauti wakichangia gharama za huduma kwa Watanzania wenzetu ambao wanakuwa wamekosa uwezo wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niseme tu kwamba Serikali ina utaratibu wa kutoa misamaha kwa kila Mtanzania ambaye atashindwa kumudu gharama za huduma ya afya kwa sababu huduma za afya ni haki ya msingi ya kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nitoe rai, kama kuna Mtanzania ametozwa gharama ambazo hawezi kuzimudu, kuna utaratibu wa kufuata kueleza hali yake kwamba hana uwezo wa kumudu gharama hizo kupitia kwa Maafisa Ustawi wa Jamii waliopo kwenye Halmashauri zote na kwenye hospitali zote. Afisa Ustawi wa Jamii akifanya uchunguzi na akathibitisha kwamba kwa kweli Mtanzania huyu mwenzetu ameshindwa kumudu gharama za matibabu alizopewa basi Afisa Ustawi wa Jamii ata-*write-off* msamaha, ataandika msamaha kwenye fomu zake na Mtanzania huyu atapata huduma hizo bure bila gharama yoyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ni watu sasa wauelewa utaratibu huu na sisi Waheshimiwa Wabunge tuwaeleweshe Watanzania wenzetu, wanahabari pia wawaeleweshe Watanzania wenzetu, wala hakuna sababu ya kwenda kuchangishana kwenye vyombo vya habari ili ukapate huduma kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa sababu kama huduma hiyo ipo na huna uwezo wa kulipa muone Afisa Ustawi wa Jamii utapewa msamaha na utatibiwa bure hapo hapo Muhimbili.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sambamba na kuokoa tatizo la akina mama katika uzazi salama bado akina mama hao wamekuwa wamachinga wa kubeba vifaa mbalimbali wakati wa kwenda kujifungua. Je, kama Serikali mnatambua tatizo hili ni lini Serikali mnahakikisha mnatenga bajeti ya kutosha katika hospitali zote za akina mama na akina mama wakifika kule kujifungua wapate huduma salama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri jibu lako la msingi lina majibu hayo turudi hapo hapo.

**NAIBU WAZIRI WA WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kwanza nimesema kwenye jibu la msingi kwamba kuanzia mwaka wa fedha unaoendelea sasa hivi tuliweka bajeti ya kununua *delivery packs* ambayo itakuwa ina vifaa vyote vya kujifungulia kuanzia *mackintosh* kuja *catgut* na vitu vingine vyote vinavyopaswa kujifungulia, nguo zile za kujifungulia, *sterile gown* kwa ajili ya kumsaidia mama wakati wa kujifungua, na tutawagawia akina mama laki tano. Lakini pia kwenye bajeti ya mwaka huu tunavyo vifaa vingine *(delivery packs)* milioni moja, kwa hivyo katika akina mama 1,900,000 ambao wanajifungua kila mwaka tutakuwa tuna vifaa vinavyokaribia 1,500,000, lakini sio wote ambao watahitaji vifaa hivyo. Kwa hiyo, tutavigawa kwa watu ambao wana mahitaji kwa hivyo ni jambo ambalo tumekwisha kulitazama.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Serikali imekuwa ikitoa huduma bure kwa wagonjwa wa kisukari, kifua kikuu pamoja na UKIMWI, je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuanza kutoa huduma bure kwa wagonjwa wa saratani ili kuwapunguzia wananchi gharama hiyo?

**MWENYEKITI**: Eeeh, goli limehama eeh! Haya Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za saratani kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 nchini Tanzania ni bure katika ngazi zote na kwa maana hiyo kila mgonjwa wa saratani atapata huduma zote anazohitaji bure *(free of charge)* wala hakuna gharama yoyote ile, kwa hiyo sio kwamba tutaanza lini tayari sera inasema hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila kama mgonjwa haijajulikana kwamba ana saratani wakati anafanyiwa uchunguzi, haijathibitika kwamba ana saratani anaweza akachajiwa vipimo na vitu vingine lakini kuanzia pale atakapogundulika kwamba ana saratani atapata huduma zote bure.

**MWENYEKITI:** ahsante, Waheshimiwa tunaendelea muda sio rafiki swali 253 linaulizwa na Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi Mbunge wa Igalula na linaelekezwa kwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia.

Na. 253

**Usajili wa Shule Mpya**

**MHE. MUSA R. NTIMIZI** aliuliza:-

Serikali inahamasisha upatikanaji wa elimu kwa maana ya ujenzi wa shule nyingi zaidi karibu na makazi ya

wananchi wetu yaani *satellite schools* na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani wameitikia wito na viongozi tumezichangia sana.

Je, ni kwa nini Serikali haizisajili shule hizo na kupeleka walimu?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia *Engineer* Stella Manyanya.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musa Rashid Ntimizi, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzishwa kwa *satellite schools* au shule shikizi ni kuwezesha watoto wadogo wa darasa la kwanza mpaka la tatu ambao hawana uwezo wa kutembea umbali mrefu kufuata shule mama kusoma karibu na makazi yao. Sababu nyingine za kuanzishwa shule hizi zinajumuisha kuwepo vituo vya msimu vya wavuvi, wafugaji wanaohamahama na kuwepo mazingira yanayosababisha maafa kama mafuriko na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za shule hizo kutosajiliwa na kupangiwa walimu ni kuwa ni za muda mfupi ambazo ziko chini ya shule mama husika. Kwa mfano, ikianzishwa kwa sababu ya mafuriko, mafuriko yakiisha na shule hiyo itakuwa imekufa. Vilevile shule hizi hazikidhi vigezo vya kusajiliwa ambavyo ni uwepo wa ofisi ya mwalimu mkuu, mwalimu mkuu msaidizi, ofisi za walimu, vyoo, vyumba vya madarasa, maktaba na *store.*

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nazungumzia shule hizi ambazo tunazijenga kutokana na

umbali wa shule mama. Kuna maeneo ni zaidi ya kilometa 20 watoto wanatembea, hata hawa kuanzia darasa la nne mpaka darasa la saba wanatembea zaidi ya kilometa 20 kwenda na kilometa 20 kurudi, tunasababisha wasichana kukatisha masomo yao kutokana na kupata mimba, lakini pia tunasababisha wavulana kuona hakuna umuhimu wa kwenda kusoma kwa sababu ya umbali wa shule hizi.

Je, kwa nini sasa Serikali haioni umuhimu wa kutumia kigezo hicho kuzisajili shule hizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili Mheshimiwa Waziri amesema moja ya sababu ya vigezo vinavyoweza kufanya shule hizo zisisajiliwe ni kutokuwa na ofisi za Walimu Wakuu na kadhalika kama alivyovitaja. Baadhi ya shule zetu nyingi hizo tunazoziita za *satellite* zimeshajengwa kwa asilimia zaidi ya 80 zimekamilika lakini bado hazisajiliwi. Wakaguzi wakija wanatoa kila siku sababu mpya. Kwa nini shule hizi ambazo zimetimiza zaidi ya 80% ya vigezo zisijaliwe? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Asante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi, muda.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lengo la Serikali kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanaotakiwa kusoma wanasoma, kwa hiyo shule hizi zinapoanzishwa ni vema kukawa na ushirikishwaji vizuri. Kwa mfano kuanzisha shule katika maeneo ambayo yanatambulika rasmi, kama ni vijiji ni vijiji rasmi isiwe ni yale maeneo ambayo watu wanaenda labda pengine kwa shughuli za kilimo za msimu tu halafu wakasema kwamba wanaanzisha shule kwa sababu shule inatakiwa iwe endelevu.

Sasa kama kuna shule ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa kamati za shule zinatambua na kwa jinsi ambavyo wananchi walioko huko ni wengi wa kutosha na kuna hiyo miundombinu ya kutosha na bado haijasajiliwa, basi mimi

nashauri wafuate tataribu na mimi nitakuwa tayari kusaidia kama hizo shule zinakidhi vigezo husika.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Pamoja na jitihada za Serikali kudhibiti taasisi ambazo zinatoa elimu na mafunzo ambazo hazijakidhi vigezo kwa maana ya kusajiliwa bado kuna taasisi ambazo zinaendelea kufanya hivyo, kwa mfano ni Chuo kimoja ambacho kinaitwa *Dodoma College of Business Management* ambacho kiko hapa Dodoma.

**MWENYEKITI:** Swali, swali, Mheshimiwa.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niombe au niseme Mheshimiwa Waziri anaweza kufuatilia na kujiridhisha kuona kwamba Chuo hiki cha *Dodoma College of Business Management* hakijasajiliwa? Kwa sababu kinasababisha hasara kwa watoto, kwa miaka minne mfululizo chuo hiki kimekuwa kikitoa vyeti ambavyo havitambuliwi na *NACTE* wala *VETA* yuko tayari kufuatilia na kujiridhisha?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema kwamba ni marufuku Chuo ambacho hakijasajiliwa rasmi kuanza kutoa mafunzo na kuanza kukusanya ada kwa wazazi kiasi cha kusababisha usumbufu baadaye. Vilevile kwa hicho chuo ambacho unakizungumzia nitaomba nipate taarifa ili tuweze kukifuatilia.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Kwa sababu katika Wilaya ya Mkalama ziko shule shikizi ndio hizo *satellite schools* za Ilangida, Songambele, Ilama pamoja na Mkola

ambazo zinafanya kazi lakini hazijasajiliwa. Na TAMISEMI tuliona udahili au uandikishaji unakuwa ni wa kiasi kidogo kwa sababu wanafunzi wengine wadogo wanashindwa kwenda mbali.

Je, Waziri yuko tayari kuingilia suala hili na kuhakikisha shule hizo nne zimesajiliwa, ambapo zimeshajengwa na miundombinu ipo kwa asilimia 80 kama alivyosema muuliza swali?

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kama nilivyosema hapo awali kama shule inakidhi vigezo na inastahili kupata usajili basi ni suala la kuwasiliana tuweze kufanya hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge tumekula sana muda wetu na nianze na matangazo.

Tangazo la wageni naona liliendа kufanyiwa marekebisho halijarejea ikirejea ntatangaza wageni wetu. Hata hivyo tuna wageni wa Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa Mheshimiwa Lubeleje ambao wamekuja kuona mambo ya shughuli za maji, wageni wa kutoka Mpwapwa wako wapi, haya karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, basi nimeipata sasa ya wageni wetu waliopo Bungeni asubuhi hii. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ukiondoa niliyemtaja, tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Joshua Nassari kutoka Jimboni kwake Arumeru Mashariki ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru Mashariki wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Willy Njau, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni mbalimbali Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuja kutembelea Bunge. Tunao wageni waliotembelea Bunge letu kwa ajili ya mafunzo nao

ni wanafunzi 62 wa Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)* mko wapi, enhee! Wamekuja kwa mafunzo karibuni sana sana.

Tunao pia wanafunzi 70 wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo mko wapi wanafunzi wa Hombolo, aah, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa William Ngeleja anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge matokeo ya mechi zilizochezwa siku ya Jumamosi juzi tarehe 20, Mei kati ya *Bunge Sports Club* na *NSSF*. Kwa upande wa mpira wa miguu *(football)* timu ya *Bunge Sports Club* ilishinda kwa magori matatu, na wenzetu *NSSF* walifunga magoli, eeh! *(Kicheko)*

Mimi nasoma ilivyoandikwa lakini inanishtua na *NSSF* walifunga magoli manne eeh! Kwa hiyo, tuiweke sahihi. Mpira wa pete *(netball) Bunge Queens* walishinda kwa magoli 26 na *NSSF* walipata magoli saba. Tunawapa pongezi wachezaji wetu wote na wananchi waliofika kuangalia michezo hii siku ya Jumamosi. Hayo ndio matangazo, nadhani ni hayo tu Waheshimiwa Wabunge, nawashukuruni. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mwongozo wa Spika! Mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara, uniruhusu basi nikae. Hata sijakaa unasema Mwongozo, sasa nitaanza saa ngapi kuandika?

Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Rhoda...

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mussa Mbarouk.

**MWENYEKITI:** Bado sijaja huko. Mheshimiwa Mussa. Tunaanza na Mheshimiwa Mussa Abdallah.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Ni Mussa Mbarouk, sio Mussa Abdallah.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kwa jambo lililotokea mapema hapa Bungeni. Wakati Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla akijibu swali namba 252 lililoulizwa na Mheshimiwa Munira Mustapha, likafuatiwa na swali la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, aliyetaka kujua ni lini Serikali itatoa matibabu bure kwa wagonjwa wa saratani? Mheshimiwa Naibu Waziri alijibu kuwa sera iliyopo ni kwamba maradhi ya saratani yanatibiwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka mwongozo wako, tumekuwa tukishuhudia katika hospitali ya *Ocean Road* na hospitali nyingine kwamba wagonjwa wa saratani ama hawatibiwi bure au dawa zao ni ghali sana. Sasa nataka maelezo ya kina kusudi nielewe. Naomba Mwongozo wako ili Mheshimiwa Naibu Waziri atufafanulie, ni kweli saratani inatibiwa bure au watu wanalipia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Na mimi nasimama kwa Kanuni ya 69(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekuwa likijadili changamoto mbalimbali zinazolikumba Taifa hili. Mkononi hapa nina risiti zaidi ya 300 za michango inayochangishwa na baadhi wa Watendaji wa Serikali kuhusiana na michango ya mwenge wakiwepo walimu, wafanyabiashara na wafanyakazi wa kada mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni malalamiko ya muda mrefu sana. Walimu pamoja na wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika kwamba michango hii wanalazimishwa. Kibaya zaidi Serikali iliwahi kutoa tamko kwamba michango hii ni hiari. Tulipofikia sasa hivi ni kwamba mikoa mbalimbali...

**MWENYEKITI:** Usilihutubie Bunge, sema tu unachotaka kusema.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba wafanyabiashara hawa, wafanyakazi pamoja na walimu kwa kuendelea kulazimishwa kuchangia Mwenge wakati Mwenge ni hiari; haoni kwamba tunaendelea kuwatesa na kuwanyanyasa watu hawa kwenye Taifa lao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mwongozo wako, jambo hili aidha, Serikali itoe tamko kwa sababu imekuwa ikitoa tamko na tamko hili halitekelezwi. Naomba kutoa hoja ili Bunge lako Tukufu lijadili hoja hii ili sasa wafanyabiashara hawa na Walimu wapate ahueni ya kutokuendelea kunyanyaswa na Serikali yao.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba Mwongozo wako kwa kutumia Kanuni ya 68(7) na jambo hili limetokea leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa hapo nje, nimeangalia magazeti na hasa gazeti la Mtanzania ambalo linaelezea matumizi ya fedha iliyochangwa kwenye rambirambi kule kwenye Shule ya Msingi Lucky Vincent, kwamba fedha zile kwanza inaonekana madaktari wamelipwa kama posho, wale ambao wamepelekewa watoto kupata matibabu. Lakini la pili, inaonekana zinaenda kujenga hospitali badala ya kupelewa waathirika kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha kwa kweli Bunge linahusika kwa sababu sisi tulikatwa posho hapa kwa maana ya kutoa rambirambi au misaada kwa wahusika. Imekuwa ni tabia ambayo inajirudia mara kwa mara kwamba fedha

inachangwa kwa ajili ya rambirambi, Serikali inaipangia matumizi mengine, kitu ambacho kwa kweli kinatukwaza sana, hasa mimi mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako, kama tutakuwa tunachangishana fedha hapa halafu wanaenda kufanya matumizi yao, kulipana posho na vitu vingine, ni afadhali kila chama humu ndani au kada fulani tuchangie wenyewe, tukabidhi kwa wahusika kuliko hii tabia ambayo inayoendelea.

Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako, hivi ni sahihi kweli fedha inachangwa kwa ajili ya rambirambi halafu inabadilishwa matumizi juu kwa juu bila hata wahusika kupelekewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako katika jambo hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pascal Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) juu ya jambo lililotokea leo mapema. Wakati swali namba 248 la Mheshimiwa Ndaki na la 249 la Mheshimiwa Zitto ulisema kwamba unawapa maswali ya nyongeza wale ambao ni Majimbo ya jirani ambapo ulimpa ndugu yangu hapa Mheshimiwa Nsanzugwanko kwa swali la Zitto, lakini pia la Maswa ukampa wa Jimbo la jirani, Mheshimiwa Nyongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijue kwamba huo utaratibu ndiyo utakaotumika kuanzia leo na kuendelea au umetumia kwa leo tu. Pia nataka tujue tu kwamba kwa yeyote atakaye... *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ni mmoja tu bwana! Mheshimiwa, *sorry!* Ni swali moja tu.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ndiyo hilo tu, nataka nijue kama ndiyo utaratibu

kila atakayekalia kiti hicho atafanya hivyo, kama busara ulizotumia leo au ndiyo itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba Mwongozo wako kuhusu hilo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kila siku ya Mwenyezi Mungu ina changamoto zake. *(Makofi/Kicheko)*

Nawashukuru sana kwa maombi yenu ya Mwongozo. Nianze na hili la Mheshimiwa Pascal Haonga. Ni kweli, busara ya kiti ikizingatia Kanuni ya swali la msingi na anayetaka kuuliza swali la nyongeza.

Swali la nyongeza kama tunavyofahamu sote lazima litokane na swali la msingi na sababu yake; moja ni kwamba, aliyeuliza swali anataka afahamu kile anachokiuliza kutoka kwa Serikali. Majibu ya Serikali na vyombo vyake huwa wanalifanyia kazi ya kina kumjibu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo anakotoka.

Sasa Mbunge aliyeuliza swali la msingi ana fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, lakini unamtegemea yeye atajielekeza zaidi kwa jibu alilopewa na Waziri aliyeulizwa swali. Asiporidhika na majibu hayo, utaratibu wetu wa Kanuni upo wazi kwamba anaweza akasimama akaomba Mwongozo na akasema swali lake halijajibiwa kikamilifu, ndiyo *scheme* iliyopo kwenye Kanuni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa wauliza maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Ndaki aliuliza swali la msingi na ndiyo nikasema, anayeuliza swali la msingi, hebu tuone muuliza swali huyo kama atafanana na huyo aliyemwuliza Waziri hali halisi ya eneo hilo. Hivyo hivyo kwa upande wa Mheshimiwa Zitto Kabwe, jirani yake wa Mkoa wa Kigoma ambaye anayaelewa vizuri maswali ya Lwiche na maeneo mengine, ndiyo maana nilitoa nafasi hiyo na ndiyo maana umeona hata majibu ya Serikali yanaelekea katika kutosheleza kiu ya Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali la nyongeza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, siyo kwamba itaendelea hivyo, inategemea. Uzoefu wangu wa Kanuni ndiyo hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda tu niwashauri, bado mna safari ndefu; miezi miwili na nusu au mitatu; Kanuni hizi wengi wenu mtazifahamu tu. Hata mimi nilipoanza kazi ya kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nilizisoma. Nanyi mtayaelewa tu. Siyo lazima uende mpaka Chuo Kikuu kuja kufahamu Kanuni hizi. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Waitara, kwanza humu Bungeni sisi hatuendeshwi na magazeti. Kwa heshimia zote, Mheshimiwa Waitara, kwanza kwa mila na desturi za Kiafrika, ukishatoa mchango wako wa rambirambi unawaachia familia hiyo au chombo kile ambacho hayo yanakwisha. Sijatoa Mwongozo, lakini kwa maoni yangu, tusiendeleze mambo haya. Serikali ipo na Bunge hili lipo, uongozi wa Bunge upo, unategemea mrejesho kwa michango ya Wabunge ili na siku za usoni mtakapokuja kuombwa kufanya hivyo muwe na ule uhiari na mwitikio ule wa haraka. Kuanza kuleta tuhuma kwamba hazijaenda huko, nasema kidogo ni tatizo.

Mheshimiwa Waitara, kwa Mwongozo wangu, hilo halijatokea Bungeni, umesoma huko kwenye magazeti yako, nami nakuacha liishie huko, lakini umeelewa *sentiments* za Kiti. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Rhoda Kunchela, nakushukuru sana. Napenda sana hizo risiti zako, furushi hilo la risiti mkalichukue tupewe tutaikabidhi Serikali tuone. Kanuni ya 69 ambayo ulisimama na kuomba, umeisoma vizuri, lakini Waheshimiwa Wabunge mjue tu kwamba haiishii tu kwa Mheshimiwa Mbunge kutaka atoe hoja yake. Kanuni ya 69(2) inasema hivi: "Kama Spika atakuwa na maoni kwamba kuwasilishwa kwa hoja hiyo ni kinyume cha uendeshaji bora wa shughuli za Bunge, atakataa kuitoa ili iamuliwe."

Sasa katika Kanuni hii ulianza vizuri kuelezea tu hisia yako halafu kama ungeruhusiwa ndiyo ungeweza ukaitoa

hoja yako halafu iungwe mkono kama itaungwa mkono halafu nipime.

Kwa kupima tu moja kwa moja kwa maelezo uliyoyatoa Mwongozo wangu naamini kabisa kwa mujibu wa Kanuni ndogo ya pili kuruhusu uitoe hoja hiyo kwa mazingira haya tuliyonayo, kwa taarifa ya upande mmoja, tutakuwa hatulitendei Bunge haki, kwa sababu hawayaelewi hayo unayoyasema. Kwa maana hiyo, naamua kwamba haitakuwa matumizi bora ya uendeshaji wa shughuli za Bunge, kuruhusu hoja yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mussa Abdallah, nimechanganya jina?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk, sio Abdallah.

**MWENYEKITI:** Ooh, Mheshimiwa Mbarouk! Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Yakhe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, umesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kama wengine, kutokana na majibu ya nyongeza ya Serikali yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Wewe kwanza hukuuliza swali la nyongeza na hata kama ungeuliza swali la nyongeza, Mwongozo wangu ni hivi, kwa mujibu wa Kanuni na maelekezo ya Spika kwa masuala haya, mwenye swali la msingi, Mheshimiwa Munira yeye ndio alipaswa sasa aoneshe kutokuridhishwa kwake au la na majibu ya Serikali.

Muuliza swali la nyongeza hawezi akadai kwamba hakujibiwa kikamilifu swali hilo, maana mwenye swali karidhika. Wewe ulikuwa unauliza swali la nyongeza ambalo hata Serikali ilikupatia majibu. Mara nyingi inakuwa hivyo kwa maswali ya jumla haya, kwa sababu maswali ya nyongeza ni *impromptu,* hutegemei sana kujibiwa kikamilifu, labda Waziri awe anajua sana eneo hilo, lakini atakupatia majibu ya juu juu tu.

Kwa hili, kwa sababu nilivyomwelewa sana Mheshimiwa Naibu Waziri na yeye, Serikali ipo alilielezea kwamba kwa hali ya kawaida, mgonjwa anayegundulika kwamba ana saratani, iwe na aina yoyote ile, hakuna malipo yoyote. Hatua ya kwanza ya uchunguzi, lazima agharamie. Akishagundulika kwamba ana tatizo hilo, ndiyo Serikali ina *stepin* kubeba gharama hizo.

Sasa wewe hukuuliza swali la nyongeza, unataka tu ushereheshe Bunge kwa kupewa majibu ya ziada na Serikali ambayo mimi naamini kama unataka kueleweshwa vizuri Mheshimiwa Mbarouk, Waziri yupo atakuelimisha. Kama *concern* yako ni kwamba bei ya dawa za magonjwa ya saratani ziko juu, sasa Serikali ndiyo imesema, yenyewe ndiyo inabeba kupitia kodi za wananchi kugharamia dawa hizi. Sasa tatizo liko wapi? Kama hukuridhika, Serikali ipo. Huo ndiyo Mwongozo wangu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo imetosha. Ahsanteni sana. Tunaendelea, Katibu.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea kwa uwiano wetu huo huo. Naanza na Mheshimiwa David Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Susanne Maselle na Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoijadili Wizara ya Kilimo tunajadili wakulima namba moja, wafugaji pamoja na wavuvi. Chama cha Mapinduzi (CCM) ndiyo chama pekee ambacho kwenye bendera yake kuna nembo ya jembe na nyundo. Jembe linamwakilisha mkulima ambae ndiyo leo tunamjadili hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamechangia humu ndani. Wizara ya Kilimo ambayo ndiyo uti wa mgongo wa hili Taifa, Serikali kwenye bajeti zake wamepeleka asilimia tatu za miradi ya maendeleo ya kilimo. Asilimia tatu ambao wako kule ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba katika kila shilingi 100/= Serikali imepeleka shilingi 3/= kwa ajili ya kumwezesha mkulima ambaye yupo kwenye bendera ya Chama cha Mapinduzi, mkulima mnyonge. Tanzania ukizungumzia mnyonge, tunamzungumzia mkulima, hatumzungumzi mtu yeyote. Mkulima ndio tunajadili kwamba ndio mnyonge. Mpaka kwenye Chama cha Mapinduzi, ndiyo tulitumia kama silaha ya kumuondolea mkoloni, mnyonge mkulima, asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magazeti baada ya kusoma hotuba, yalipongeza sana hotuba yakaisifu kwa kuondoa tozo, lakini hizi tozo hatujazijadili kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imeondoa tozo, kwa mfano, tozo 80 kwenye mazao ya biashara, kwenye tumbaku wameondoa tozo kumi, kwenye Kahawa wameondoa tozo 17, kwenye sukari tozo 16, kwenye pamba tozo mbili, kwenye korosho tozo mbili na kwenye chai tozo moja. Sasa nataka tujadili tozo moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia tozo za sukari 16, zote kwenye kitabu zinamhusu mnunuzi na wala siyo mkulima moja kwa moja. Tozo zinamsaidia mtu wa kati, siyo mkulima wa kawaida wa chini. Tozo hazijadili kuhusu miundombinu ambayo wakulima wanahitaji. Wanahitaji soko la uhakika, wanahitaji miundombinu kwa maana ya umwagiliaji na

wanahitaji mbolea. Hayo ndiyo mambo ambayo Wizara ya Kilimo ingekwenda kujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye tozo ya pamba, yenyewe inasema, wameondoa pale tozo mbili; ukija kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri anasema kwa mfano, kuna tozo ya kituo cha kununulia pamba katika ngazi ya Halmashauri ambayo Wizara ya Kilimo mpaka sasa hivi inasema tozo hii Wizara itawasiliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji wa suala hili. Maana yake mpaka sasa hivi Wizara haijawasiliana na TAMISEMI. Tulitegemea nini hapa? Tulitegemea kwamba Wizara wanapokuja hapa, hili suala liwe limeshakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo ya pili inasema tozo ya maendeleo ya elimu kwenye pamba inayotoza kwa kiwango cha shilingi 10/= kwa kilo katika Halmashauri ya Meatu, Halmashauri moja, wao Meatu waliweka hii tozo ili wachangie elimu wapate mapato ya ndani. Wizara ya Kilimo inasema, Wizara itawasiliana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya utekelezaji. Maana yake bado hawajatekeleza, lakini ilivyoandikwa ni kama jambo limekwisha, hiyo ni kwenye tozo ya pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija tozo ya korosho; tozo mbili zote zinahusu wanunuzi wa korosho. Hapo utaona tu kwamba tozo zinazoondolewa; gharama za magunia na kamba shilingi 56/=. Ni nani anahitaji hayo magunia na kamba? Ni mkulima wa kawaida? Ni yule anayenunua, anayepeleka huko mbele. Ada ya Leseni ya kununua korosho kwa kiwango cha dola 1000, siyo mkulima hapa. Wakulima wa korosho wanataka wahakikishiwe kwamba yale madawa kwa ajili ya mbolea pamoja na korosho ndiyo yanayotakiwa na ndicho ambacho tumekuwa tukikijadili hapa. Hapa ukiangalia, ni mtu wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa ni kwamba tumesaidia watu, wale *middle men* kwa maana wafanyabiashara badala ya wakulima wa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye tozo ya tumbaku, ni hivyo hivyo. Kati ya tozo kumi ni tozo mbili tu ndizo zinawahusu wakulima wa kawaida moja kwa moja. Ukienda kwenye tozo za kahawa kati ya 17 ni tozo mbili peke yake ndizo zinazohusu wakulima moja kwa moja. Sasa tunapojadili tozo, tujadili kwa kuwasaidia wakulima wa chini na ndiyo maana siku zote tumekuwa tukisema kwamba hapa Serikali ingekuja ingejadili uhakika wa mbolea kwa wakulima wa kawaida, uhakika wa masoko kwa wakulima wetu, miundombinu ya umwagiliaji kwa mwaka mzima. Hayo ndio mambo ambayo tungesema kwamba tunamyanyua mkulima wa kawaida tunampeleka juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo sukari ni kwamba baada ya kuona ime-*mess up* na hata ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha uagizaji wa mwaka huu, sukari inaonekana mazao yameongezeka kweli kweli kuliko mwaka 2016. Kwa hali halisi kwenye soko la humu humu ndani ni kwamba hali ya sukari ni mbaya kuliko hata ile ya mwaka uliokuwa umepita. Sasa ukipitia hizi takwimu, zinaji-*contradict*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo mambo ambayo tunayahitaji hapa tuyajadili. Ukijadili takwimu kwa *spin,* magazeti yakakusifu lakini ulichokiandika ndani hakitekelezeki na wala hakitamgusa mwananchi wa kawaida na ndicho ambacho mimi baada ya kukisoma hivyo, ndiyo maana ukienda hata kwenye hotuba ya Kamati, Kamati imeeleza vizuri, kilimo siyo moja ya vipaumbele vya Serikali. Maoni ya Kamati ndiyo maoni ya Bunge zima maana yake Bunge tunaiambia Serikali kwamba kilimo mnachokifanya ni sawa sawa na kazi bure, haya ni maoni ya Bunge yaani Kamati ni Bunge, ndicho tunachokijadilia hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji majibu juu ya haya masuala. Moja, tunahitazi ufafanuzi juu ya tozo moja baada ya nyingine, hizi ambazo zimeandikwa. Kwenye Kamati hizi hazikupelekwa, zimeletwa tu hapa ndani ya Bunge na ndiyo maana tunahitaji ufafanuzi juu ya hili jambo. Jambo lingine tunahitaji uhakika kwamba hawa wakulima ambao

tumekuwa tukiwajadili kila mwaka iliwemo kule Momba, mwaka 2016 Serikali imeshindwa kununua chakula na tishio la njaa la mwaka 2016 ndilo ambalo sasa mwaka huu lilitakiwa tunapokuja katika mwaka huu mpya wa fedha, tishio lililokuwa linaoneka mwaka wa fedha uliopita lilitakiwa mwaka huu sasa Wizara ije na bajeti ambayo tutasema kwamba tutanunua chakula ambacho kitaweza kusaidia nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze tu, usalama wa Taifa siyo kuwa na bunduki nyingi. Usalama wa Taifa ni kuwa na chakula. Ukiwa na bunduki na mabomu, lakini mwisho wa siku watu wako wakiwa na njaa, hiyo vita huwezi kushinda. Ukisikia Marekani wanakwambia kwamba tuna uwezo wa kupigana vita tatu ama nne kwa wakati mmoja, ama mpaka vita sita, siyo kwamba kwa sababu wana mabomu ama wana teknolojia, wana uhakika wa kuweza ku-*feed* wanajeshi wao wakaendeleza mapambano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi uhakika wenyewe wa chakula ndani ya hili Taifa haupo, lakini ukiangalia mazingira yaani *geographically position* ya nchi yetu, ipo vizuri kabisa. Kwa maana, ukiangalia kama ni maziwa, yapo ya kutosha, kama ni mito ipo ya kutosha; lakini mwisho wa siku ni kwamba, miradi ya umwagiliaji haifanyi kazi vile inavyotakiwa. Miradi ambayo ilikuwa imeanziswa na Serikali, leo wananchi ndio wamekuwa wakilalamika.

Mheshimiwa Mewnyekiti, mwisho wa siku ni kwamba miradi hii ambayo ilikuwa imeanzishwa kwa mfano, miradi ya umwagiliaji badala ya kuwasaidia wananchi wa chini wa kawaida, sasa ile miradi anakuja mwekezaji mmoja anaambiwa sasa wewe huu mradi wa maji ndiyo utakaotumia. Kwamba anakuja mwekezaji, ameshaona miundombinu pale ya Serikali, anaambiwa ninyi mtatumia huu mradi na wananchi wa kawaida hawapewi ile namna ya kutumia yale maji kwa ajili ya kilimo cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo nilitaka kabisa lazima Serikali inapokuja itoe ufafanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, tuelezwe, unapotaka kununua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wetu ndio huo Mheshimiwa Silinde, tunakushukuru kwa mchango wako, Mheshimiwa Susanne Maselle atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Mariam Ditopile ajiandae.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** nakushukuru Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sijaanza kuchangia napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuilinda familia yangu, hasa baba yangu ambaye alikuwa anaumwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nipongeze hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ambayo imesheheni vitu vingi sana na vya muhimu ambapo Serikali kama itavichukua na kuvifanyia kazi, basi sekta hii itafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu uvuvi. Kanda ya Ziwa katika sekta hii ina umuhimu sana hususan Mkoa wa Mwanza, maeneo ya Buchosa, Magu, Kwimba na Ilemela wanategemea sana uvuvi, lakini Serikali naona kama haitilii umuhimu sana hii sekta. Kwa sababu gani nasema hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wamekuwa wakinyanyaswa sana kwa kunyang'anywa nyavu zao. Siyo kwamba nabariki watumie nyavu ambazo hazifai, la hasha! Mwaka 2016 nilizungumza nilivyokuwa nachangia kwamba Serikali inatakiwa itoe elimu jinsi ya kutumia hizi nyavu, ni nyavu gani wavuvi wanatakiwa watumie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza na Waheshimiwa Wabunge wengi sana walizungumza kwamba

ni kwa nini maduka bado yapo ambayo yanauza; na viwanda vinatengeneza nyavu hizo? Wavuvi hawa wamekuwa wakinunua kwa kutumia pesa, matokeo yake, wananyang'anywa, zinachomwa na wanajikuta wanaingia katika umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Februari kulikuwa na mgomo wa wavuvi na Serikali ikasema kabisa kwamba inaunga mkono mgomo huo. Sasa mimi nikashangaa ni kwa nini Serikali iunge mkono badala ya kutatua tatizo? Maana yake ni kwamba inaunga mkono tuwe na watu ambao hawana kipato na mtu asipokuwa na kipato matokeo yake anakuwa anafikiria mawazo mabaya ambayo yanapelekea hata kujiingiza katika vitendo vibaya ambavyo siyo vizuri kwa jamii. Kwa mfano, tunaweza tukatengeneza watu ambao ni vibaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningetaka tu Serikali na Mheshimiwa Waziri anapokuja atuambie ni mkakati gani walionao wa kuweza kutatua hili tatizo ili wananchi wetu waweze kufanya hii shughuli wakiwa na amani na kusiwe na ile tabia ya Serikali na wavuvi kuviziana. N kama vile wanaviziana kwamba wakitumia hizo nyavu na wenyewe wanakuja kuwanyang'anya ni kama kuviziana. Sasa tukitoa elimu, tutakuwa tumewasaidia sana watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu kilimo, Mkoa wa Mwanza una eneo kubwa, takribani asilimia 53 ambalo limzungukwa na Ziwa Victoria. Hii inatoa nafasi kubwa kwa kilimo cha umwagiliaji, lakini mpaka sasa sijaona hatua yoyote ambayo imechukuliwa ili tuwe na kilimo cha umwagiliaji katika Mkoa Mwanza. Wakulima wengi wamekuwa wakitegemea kilimo ambacho ni cha majira, lakini majira yakibadilika, wanashindwa kulima. Kama kwa sasa, kumekuwa na ukame, tungekuwa na kilimo cha umwagiliaji wananchi wetu wangeweza kulima bila kutegemea majira ambayo yanakuwa yanawaangusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona chakula kimekosekana na wananchi wanapolalamika, kwa mfano

Mheshimiwa Rais alikuja, nafikiri ilikuwa ni Shinyanga, watu wakamwabia kwamba wana njaa na akawaambia hawezi kuwapikia. Wanaposema kwamba wana njaa, siyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Muda wetu ndiyo huo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ally Saleh, atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile na Mheshimiwa Ester Mmasi ajiandae.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeanza kuwa na wasiwasi, msemaji wa mwisho naona kama hazikutimia dakika kumi, nina wasiwasi na mimi dakika kumi zangu zitatimia?

**MWENYEKITI:** Ni tano.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Tano! *Okay,* sawa. Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Wenyewe wametuandikia hapa, dakika tano.

Waheshimiwa Wabunge, mimi sipangi muda, ninyi ndio mnakubaliana.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Sawa, nakubali, kwa sababu inavyoonesha mwenyewe hakujua kama kapewa dakika tano. Haya, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchangiaji wangu utakuwa na *theme* kwamba nchi hii inahitaji mabadiliko ya fikra kwa sababu hapa tulipo tumegota. Kama kilimo tunakipa asilimia chinjo kila mwaka, kama kilimo kinapata asilimia tatu tu katika maendeleo, wakati huo tunasema tunataka

maendeleo ya kilimo na maendeleo ya kilimo haya tunataka yaungane na viwanda, nafikiri tunahitaji fikra mpya. Hapa tulipo tumegota. Miaka 53 ya nchi hii haiwezekani tusiweze kujilisha au kusimamia wakulima wetu. Nafikiri tumegota na tunataka mabadiliko ya fikra katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo hivi sasa, nchi hii ina ardhi ya kutosha, ina maziwa ya kutosha, ina mito ya kutosha, ina ukanda wa bahari wa kutosha, lakini ni kitu gani tunajitosheleza? Je, tunajitosheleza kwa chakula? Tunajitosheleza kwa uvuvi? Tunajitosheleza kwa mazao ya nyama au maziwa? Sifikiri katika yote hayo kama tunaweza kuyatimiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisema hivi mara nyingi tunakuwa tunalaumiwa, lakini nafirikiri badala ya kwenda mbele kwa kilimo tunarudi nyuma. Kwa sababu baada ya miaka 53 haiwezekani kwa mfano, Kenya ambao sisi tunawapita kwa idadi ya ng'ombe kwa zaidi ya mara mbili ya mifugo wana maziwa ya kutosha sisi hatuna au nchi nyingine nyingi ambazo tunapakana nazo. Kwa hiyo, katika utewekezaji wetu wa kilimo, tumeshindwa kupima muda, fursa na rasilimali zetu. Kwa sababu hiyo, ninaamini kwamba tunahitaji fikra mpya, hapa tulipo, tumegota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tulipo hivi sasa, nchi hii, kwa mujibu wa Ripoti ya Benki ya Dunia ni kwamba tuna ekari ambazo ni *arable* na ambazo zinalimika ni milioni 13,500,000; tuna ukanda wa bahari wenye maili 1,400; tuna eneo la mikoko ambalo lina hekta za mraba 115,000 lakini kwa mfano kwenye bahari mpaka hivi leo hatujaweza kuvuna rasilimali za bahari na wanaokuja kuwekeza tunawakamata, tunawashitaki na tunawanyang'anya vyombo vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaalamu ambao hautaki tena kuvumbua; nchi za Philipines Cambordia, Malaysia na nyingine zinatumia mikoko ambao sisi tunaihifadhi tu, lakini kina kitu kinaitwa *mud crab farming,* yaani ufugaji wa kaa katika mikoko ambao una utajiri

mkubwa sana, lakini bado hatujautumia. Naamini tumegota katika fikra na tunataka tupate mapinduzi ya fikra. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nashangaa katika nchi hii ambayo asilimia 52 ni misitu. Tuna eneo la maji ambalo linaweza kuzalishwa kwa kilimo ni zaidi ya hekta za mraba 61,500; lakini haielekei kama kuna *connectivity* baina ya Serikali yenyewe na Wizara kwa Wizara, kwa sababu kama kuna *connectivity* ingekuwa hadi hivi leo isingewezekana rasilimali zote tulizonazo tusiweze kuzitumia vya kutosha. Nafikiri tunataka fikra mpya, sasa hivi Serikali inaonekana kama imeshindwa katika eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje katika *leather industry.* Tanzania ni ya tatu kwa ng'ombe Afrika; ni ya 11 kwa ng'ombe duniani. Ina asilimia ya ng'ombe asilimia 1.67 ya dunia. Tumefaidika nini katika *leather Industry?* Kama hatuna *leather Industry,* ina maana hakuna maana ya kufuga ng'ombe maana hatupati maziwa ya kutosha, hatuna viwanda vya maziwa, ngozi yetu hatuitumii vya kutosha. Kwa hiyo, haina maana ya kufuga. Nafikiri tumegota, tunataka fikra mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye mazao ya chakula, tumebaki katika yale yale ambayo ni *traditional;* na vile vile mazao ya biashara ambayo ni *traditional.* Sasa hivi sisi tunajifunza, tuna hali ya hewa nzuri sana au ya kila namna; ipo joto kidogo, baridi kidogo, ipo ya mchanga kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mazao mapya ambayo tunaweza kuyavumbua, tumeingia kwenye *vanilla* kidogo kwa Kilimanjaro na Kagera. Hivi sasa bei ya *vanilla* ni dola 500 kwa kilo moja. Sisi kama nchi tumehiza vipi zao hili? Kuna mazao kama zafarani *(saffron)* ambayo kilo moja ni dola 4,000. Tumefunguka vipi kama nchi? Nafikiri tumegota na tunataka mapinduzi ya fikra. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna masoko yamejifungua chungu nzima. Tuna Vietnam wamekuja

kuingia mkataba na sisi, tuna Wachina, tuna Waturuki; tumefikiria vipi juu ya mazao? India peke yake inaweza kumeza kwa siku 15 mazao yote ya choroko ya Tanzania, kunde zote za Tanzania. Tumewafunza vipi watu wetu kutumia soko hilo? Tunataka mabadiliko ya fikra, tunafikiri CCM mmegota kimawazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii pia hatuoni upya wa mambo ambayo tunayafanya. Walisema kwamba walitaka wamtue mwanamke ndoo, walisema wanataka wamnyang'anye mkulima kijembe cha...

**WABUNGE FULANI:** Cha mkono mkono.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Cha mkono, lakini kwa miaka kadhaa hivi leo bado ni *tradition farming.* Niambieni nchi hii, wapi kuna shamba la kilimo la kisasa la mwekezaji ambaye analima kwa maelfu ya heka kuitoa nchi hii katika njaa? Nafikiri mmegota na inabidi tupate mabadiliko ya fikra. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri kuna haja kubwa ya mabadiliko. Kwa fikra zangu, nadhani sasa hivi irudisheni agenda kwa wananchi, mwaambie wananchi kwamba katika kilimo, mifugo na uvuvi, mmeshindwa; ili baada ya bajeti hii turudi tena kwa wananchi tujadili jambo hili. Kwa sababu nafikiri kunahitajika mapinduzi ya fikra na fikra hamwezi tena kuitoa ninyi kwa sababu mmeshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Ditopile na kama nilivyosema, Mheshimiwa Ester Mmasi ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba nitangulize shukrani zangu kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na kuweza kusimama hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumpongeza Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kutimiza ahadi yake. Alisema kipindi cha kampeni, yeye akiahidi anatekeleza. Kwa Wana-Dodoma ametuletea Makao Makuu na kweli Serikali imeshahamia. Kipindi cha kampeni wananchi waliilalamikia *CDA* kwamba amethubutu, ameivunja mamlaka ya ustawishaji. Sisi tunamwambia tuko naye bega kwa bega, tunasema uungwana ni vitendo asubirie 2020, Dodoma tuko naye pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza tu ni kwamba Serikali tunaomba sasa muda muafaka umefika wa kuleta muswada wa Sheria ya Makao Makuu. Leo hii tunajadili Wizara nyeti, tunajadili maisha robo tatu ya Watanzania. Kwa mujibu wa hotuba yako Mheshimiwa Waziri, umesema kwamba sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, imeajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge, *everybody is entitled to his/ her opinion,* lakini lazima tuseme ukweli. Wao wanaosema tumeganda wakati Sudan inategemea chakula kutoka Tanzania, Kenya wanategemea mahindi kutoka Tanzania, Uganda wanategemea mahindi kutoka Tanzania na mazao mengine! India wanategemea chorosho, choroko, dengu, mbaazi zote zinatoka Tanzania. La msingi ni kwamba tunatakiwa tuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii naomba niwaambie, Waziri wa Fedha na Naibu Waziri, naomba mnisikilize. Mipango yenu ni kwamba tunataka kupeleka nchi kwenye uchumi wa viwanda, tunataka kuwa na uchumi wa kati, tuwekeze kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Kilimo, mifugo na uvuvi ni afya, kilimo, mifugo na uvuvi ni ajira, itampunguzia kaka yangu Antony Mavunde adha aliyokuwa nayo. Kilimo, mifugo na uvuvi ni fedha na uchumi, kilimo, mifugo na uvuvi ni amani. Tukiwa na njaa tutaweza kuwa na amani?

Kwa hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, ukipeleka hela kwenye kilimo, mambo yako yote, mpango wa maendeleo utafanikiwa kwa asilimia 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi, lawama nyingi sana zimemwendea Mheshimiwa Waziri. Namfahamu Mheshimiwa Waziri. Nimeshalima naye, ni mkulima mzuri sana. Tena bahati nzuri analimia hapa hapa katika Mkoa wetu wa Dodoma. Mheshimiwa Waziri amekua kama mtoto wa mfugaji, kazaliwa kwenye jamii ya ufugaji, anatoka Kanda ya Ziwa, anaelewa uvuvi. Ukikaa na Mheshimiwa Waziri, maono aliyokuwanayo kwa Wizara yake ni makubwa, lakini hana fedha, atafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nieleze umuhimu wa utafiti, sayansi na teknolojia katika kilimo. Kwa Kiingereza tunasema, *science and technology innovation in agriculture.* Tunasikitika, bajeti ya ugani iko wapi? Bajeti ya utafiti ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma kitabu chote, leo hii nchi yetu ina watu takriban milioni 50, baada ya miaka 10 tutakuwa na watu zaidi ya milioni 65. Hakuna mpango mkakati wa kutuvusha kutupeleka huko na yote Mheshimiwa Waziri siyo kosa lake; huna utafiti, uta-*project* vipi? Utapangaje mipango yako vizuri kama hujafanya utafiti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote, niwaambieni, dunia nzima kati ya watafiti wanaoheshimika ni Tanzania. Kigoma Watanzania walifanya utafiti wa mbegu ya michikichi ambayo Malyasia ndio wanatumia. Leo hii niwaambieni, kuna Mtanzania mmoja alikuwa Serikalini, amefyatuliwa risasi juu, amechukuliwa na *Bill Gates Foundation* Marekani kama mtafiti na aliombwa abaki kule afundishe masomo ya kilimo, lakini amechukua uzalendo wake, amerudi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa utafiti naomba niwaambieni Serikali, leo hii mjiulize kwenye uvuvi, Ziwa Victoria sisi ndio wenye sehemu kubwa, lakini ukienda kwenye *statistics* za dunia, Uganda imetupita, yenyewe ni ya sita katika uvuvi wa Ziwa Victoria. Sisi ni wa nane, kwa nini? Leo hii tujiulize Bukoba kahawa mwaka 1978, miaka 30 na kitu iliyopita walikuwa wanazalisha zaidi ya tani 140,000, lakini leo kwenye kitabu mmeona, tuna-*project* kuvuna tani 47,000

kwa sababu hatujafanya tafiti ya kuendeleza hizi kahawa. Miche imekuwa mikuu, haizalishi, imekuwa *dormant.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu niwaeleze umuhimu wa *science and technology innovation.* Leo hii tunafurahi hapa kusema kwamba tunalisha *East and Central Africa,* lakini tusipojipanga vizuri, tunu hii tuliyopewa na Mwenyezi Mungu tutaikosa, Malawi wamejipanga kwenye pamba. Malawi ni nchi ndogo, lakini leo hii inaenda kutupita kwenye uzalishaji wa pamba kwa sababu ya tafiti na kujipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuongelea suala la mbegu. Tumejaribu sana kuendeleza kilimo. Nashukuru Serikali ilijaribu kutoa matrekta, lakini hebu tuweke azimio, Mheshimiwa Waziri, kaa chini. Vituo unavyo, mahitaji unayajua, sitaki kuzungumzia sana yaliyokuwemo humu. Hebu tusonge mbele, tuwafunge watu midogo. Tuweke azimio kwamba Serikali ihakikishe kila mkulima anapata mbegu bora. Wakulima wetu wamekuwa wanatumia nafaka. Nendeni mkasome muone tofauti ya mbegu na nafaka *(seed and grain).* Mkulima analima heka yake moja, akivuna mahindi, yale yale aliyoyavuna, anahifadhi anaifanya mbegu. Siyo mbegu! Atajikuta alivuna mawili atabaki na moja. Kwa hiyo, tuweke azimio, uwezo huo tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba kuzungumzia Mkoa wangu wa Dodoma. Mkoa wa Dodoma unafanya *tremendous* kwenye kilimo, ingawa watu wanajua kwamba ni kame. Msimu wa mwaka 2013/2014 Tanzania iliuza tani 860,000 China, kati ya hizo tani 300,000 ufuta umetokea hapa Dodoma. Tuna maonyesho ya Nane Nane. Pale inaonekana mazao yote yanawezekana. Kwani ile ardhi ya Nane Nane ni ya wapi? Ni Arusha? Siyo ya Dodoma! Lakini humu sijaona Mheshimiwa Waziri. Nina vijana wengi na kila siku nawapigia kelele waingie kwenye kilimo. Hebu tuhamishe basi ile Nane Nane tuipeleke Chamwino, tuipeleke Kondoa, tuipeleke Chubi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ally Saleh kauliza kuhusu shamba kubwa, twende Chubi kwa Mheshimiwa Kijaji ukaone shamba kubwa za hizo heka unazosema na mwekezaji ujifunze. Tembea, *no research, no right to speak. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naongea kwa sababu niko *field,* najua raha ya kilimo, najua machungu ya kilimo, najua mafanikio na ninajua tukiweka nguvu kidogo, tutafika mbali. Nataka sana vijana. Vijana wanataka *red market,* wanataka mitaji, hatuna sehemu ya kuwapeleka zaidi ya kilimo. Tuwekeze jamani! Leo hii haiwezekani, nchi ya Egypt ina *River Nile* peke yake*. Source* ya *River Nile* ni *Lake Victoria.* Kale ka-*Nile* kanatokana na *Lake Victoria* wanakatumia, wanafanikiwa vibaya mno! Sisi wenye Ziwa Victoria, wenye Ruvu na mito kibao hatuongei, kwa nini tunashindwa kutumia hizi fursa? Tumeona mwenyewe Mheshimiwa Waziri umeshasema hii ndiyo sekta ambayo inaleta pesa kuliko zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nigusie kwenye uvuvi katika Ziwa Victoria, kuna samaki anaitwa sangara. Sangara jamani...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililie kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako mzuri. Endelea kuhamasisha kwenye kilimo na Serikali itakusaidia. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, nami niweze kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbele kwenye mada zangu, kwanza kabisa kwa unyenyekevu mkubwa na kwa nia njema kabisa, naomba niwapongeze viongozi wetu, Mheshimiwa Waziri na Naibu wake namwona anatabasamu kwa sababu anafahamu ninafahamu jitihada

zake, ninafahamu kiu yako kuona vijana wa nchi hii wanashiriki rasmi kwenye sekta ya kilimo. Nawapongeza sana, vijana wanawapongeza sana. Pia wanasema kwamba, asiyejua kushukuru huyo ni mnyang'anyi. Mimi siwezi kuwa mnyang'anyi kwenye Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, ninanukumbuka nilikuja hapa Dodoma nikawafuata pale Wizarani, ninyi mlinipa kibali cha kuweza ku-*organize* vijana wote nchini Tanzania, wakaja tukapanga mipango. Siyo hivyo tu, mlinisimamia na mimi nikafanikisha azma yangu ya kuanzisha vikundi vya ushirika katika nchi ya Tanzania. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mnafahamu nimeanzisha Ushirika wa Vijana Wahitimu, nimeanzisha kule Buchosa, Geita, Bukombe, siyo hivyo tu, nimeanzisha Kigoma ambapo huko pia nimetafuta shamba ekari 1,000, Mto Malagarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, wamenisaidia nimeanzisha ushirika Songea, Dodoma, nimeanzisha ushirika wa vijana *graduates* Mkoa wa Dar es Salaam, lakini Mheshimiwa Waziri naomba tu kukwambia kwamba, vijana wale bado wanakusikiliza, wamekupa macho yao yote na matumaini yao kwako. Ninaomba kwa moyo wa unyenyekevu kabisa, usiwaache vijana wale. Uliwapa matumaini makubwa, uliwasimamia na ukasema utawaongoza. Ninakuomba usimame mstari wa mbele uongoze Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika mawasilisho ya Wizara ya Viwanda tuliona kabisa mpango wa Serikali katika kufufua viwanda. Najiuliza kule Mkulazi ambapo mnasema tutazalisha tani 200,000 za sukari, hatuoni kwamba huu mradi utahitaji *outgrowers* kwa maana kwamba utahitaji malighafi kutoka nje ya *Mkulazi project*! Tunawaandaaje vijana hawa?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, shamba la Mbigiri, mmesema mtazalisha miwa tani 30,000 kwa mwaka, mmewaandaaje vijana hawa? Ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 31(v) umesema moja ya

mikakati katika Wizara ni kuona kwamba vijana wanashiriki kwenye sekta ya kilimo kikamilifu.

Mheshimiwa Waziri najiuliza leo, tukiwa katika mawasalisho ya bajeti zenu huu mwaka wa fedha unaoisha Juni, 30 tuliona mipango mingi, nikauliza hawa vijana watashirikije? Mkasema kwamba atapewa hati za kimila ili waweze kukopesheka katika mabenki. Najiuliza tukiangalia fungu la maendeleo, tumetenga shilingi bilioni 101, lakini zimeenda asilimia tatu tu. Fedha za kawaida tulitenga shilingi bilioni 109, tunaona zimeenda shilingi bilioni 62 sawa na asilimia 54. Ninajiuliza, kwa nini *vote three* matumizi ya kawaida yanakuwa ni makubwa, lakini fungu la maendeleo linakuwa hamna kitu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza leo, katika hii shilingi bilioni 150 mliyoitenga *this year,* mtatupa shilingi ngapi vijana hawa waweze kupatiwa hati za kimila na waweze kukopesheka kwenye mabenki? Mheshimiwa Waziri unafahamu na umekuwa ukituhutubia hapa kwamba *NMB* wametenga shilingi bilioni 500 katika kusaidia vijana, lakini wewe ni shahidi, nimezunguka *NMB* wananijua, kama wapo waniangalie, *CRDB* wananijua, nimezunguka na vijana wa Taifa hili hakuna wanakokopesheka. Hiki ni nini?

Mheshimiwa Waziri, ona huruma kwa vijana wako. Unafahamu vijana wanavyokulilia, umepokea simu za mchana na usiku, tibu kilio cha Watanzania, tibu kiu ya vijana hawa waweze kushiriki kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Waziri unaelewa, wamekuja vijana, mara ngapi wanakupigia simu? Vijana wako tayari wanataka kulima. Siyo hivyo tu, *CRDB*, *Agribusiness Loans Unit,* nimekwenda pale wananijua. Nime-*mark time several times;* nimefanya vikao na Makatibu Wakuu, wananijua, wako hapa waulize. Nimeongea nao usiku na mchana, vijana hawasaidiki katika nchi hii.

Mheshimiwa Waziri unafahamu Benki ya Kilimo, tulitenga shilingi bilioni 60 lakini ombi la Dar es Salaam tu

lilikuwepo bilioni 55. Ni nini hiki? Tukiwa wadogo tulisoma hadithi za Abunuasi, leo mimi na utu uzima wangu ukiniambia nisome kitabu cha Abunuasi siwezi kusoma. Mheshimiwa Waziri ninakuomba uangalie, Taifa linakutegemea.

Mheshimiwa Waziri, siyo hivyo tu, *TIB*, *Women's Bank* tumeona, *Women's Bank* sasa hivi ina-*run the second with high growth rate in NPL; you know it!* Mheshimwia Waziri unafahamu. Benki hii tuliambiwa kutakuwa na dirisha la akina mama waweze kukopesheka na waingie kwenye kilimo. Hamna kitu! *TIB the same, it is running the third with higher NPL growth rate* ambayo ina asilimia 52 *Women's Bank* na hii *TIB* ina asilimia 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifungwa vinywa hapa na Mheshimiwa Waziri wa Afya akatuambia kwamba *CAG* atafanya kazi atuletee ripoti. Waheshimiwa Wabunge wenzangu na akina mama wa Bunge hili, ninaombeni tusikae kimya, tuisemee Benki ya Wanawake. Wanawake wanatutegemea sisi tuwasemee. Tunajiuliza leo kama Benki ya Kilimo ilikuwa ina-*operate under Central Bank guidelines*, ilitakiwa iwe na Bodi. Benki hii inakuwa *Head* wa *Risk Manager,* kuna *board members,* watu hawa wamewajibishwa lini? Benki za Taifa hili zinakufa, wamama waende wapi? Vijana waende wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu. Tumeona mambo makubwa ambayo yametukatisha tama. Vijana hawa wanahangaika. Mmeongea kwenye Sera ya Ajira, lakini hakuna tumaini tena. Ninaowasemea hapa ni watoto wa maskini, pengine hatuwajui. Watoto wa maskini ni wale ambao tunapoenda kule kula nyama kwenye minada, ni wale watoto ambao wanakinga makombo yetu kwenye beseni, wanaenda nyumbani wanapika. Siamini kama kuna mtoto wa maskini ambaye anachungwa na mbwa kwenye nyumba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa maskini ni wale ambao tunapopeleka watoto wetu China, wanabeba

mabegi, wanaenda *airport* wanawapungia watoto wa matajiri mikono. Hawa ndio watoto wa masikini ninaowasemea katika Bunge hili. Mheshimiwa Waziri tuna imani nawe, ukiamua inawezekana. Wizara yako ikiamua vijana wetu watashiriki rasmi kwenye Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu asilimia 75 ya wananchi wa Taifa hili ni wakulima, usiwaache; lakini asilimia 65 za ajira za uhakika zinapatikana kwenye Sekta ya Kilimo. Vijana wamenituma niwasemee. Vijana wamenituma nipaze sauti zao kwa niaba yao. Nakuomba kabisa utakapokuja kuhitimisha hapa, utuambie una mpango gani kwa vijana hawa waweze kushiriki kwenye *project* ya Mbigiri - Morogoro, utuambie vijana hawa watashiriki vipi kwenye *National Milling* ambayo umesema inafufuliwa hapa Dodoma. Malighafi hizi, vijana wana nguvu za kutoa malighafi kwenda kwenye viwanda hivi. Nakuomba uwashirikishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliongea habari ya *AGOA*, kuondolewa vikwazo vya kimasoko kwa nchi ya Marekani kupitia mlango wa *SADC.* Najiuliza, ni nani aliyeweza kufaidika kwenye mlango huu wa *AGOA*? Wanatoka Wahindi nchi ya India wanakuja Tanzania wananunua *cashew nut* yetu, wanapitia kwenye mradi huu wa *AGOA,* Watanzania tumebaki watazamaji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linasikitika, linahuzunika, tusaidie Mheshimiwa Tizeba una uwezo. Mheshimiwa Olenasha mna uwezo na mna nguvu; na ninajua mna *passion* ya kweli katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha popote alipo na mama Ashatu Kijaji, tunawaomba kabisa kwa moyo wa dhati na unyenyekevu, Taifa linawaangalia. Toeni hela wasaidieni akina Mheshimiwa Olenasha wafanye kazi. Toeni hela Mheshimiwa Tizeba aweze kufanya kazi, Taifa linawaangalia. Ninaomba kwa moyo wa dhati na unyenyekevu, Bunge hili lisikie sauti ya vijana wa Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nisiendelee sana, pengine ninaweza nikafika sehemu nyingine. Naomba niishie hapo, naunga mkono hoja asilimia mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mmasi nakushauri sasa uende ukanywe maji. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru, kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na watendaji wao wote kwa kazi nzuri waliyoifanya. Naomba niende moja kwa moja kwenye kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu kwa watu wote; siyo hata kwa asilimia kiasi gani, ni kwa watu wote. Asilimia 75 inatoa ajira, asilimia 100 yote inatoa chakula, inatoa malighafi kwenye viwanda na inachangia pato la Taifa kwa 28%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wote kwa pamoja kama tulivyoonesha toka juzi kwamba sekta hii ni sekta muhimu na tuombe Serikali ione umuhimu wake kwa kujali kuiongezea bajeti, hata kama siyo mwaka huu, basi miaka inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia utaona kilimo kinashuka, hakipandi. Ndiyo maana umaskini wa watu unaongezeka ndugu zangu. Mwaka 2011 kilimo kilikua kwa 3.5%, mwaka 2016 kilimo kilikua kwa 1.7%. Angalieni kutoka 3.5% mpaka 1.7% na bado tunategemea kuondoa umaskini wa Tanzania itakuwa ni kazi ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kilimo kimechangia 28% katika pato la Taifa. Bajeti ya kilimo kwa mwaka 2011 ilikuwa 7.8% ya bajeti ya Serikali. Mwaka 2016 bajeti ya kilimo imepangiwa 4.9%. Kwa hiyo, muone uhusiano kati ya ukuaji wa kilimo na jinsi bajeti inavyotolewa. Kwa hiyo, naomba Waziri aone na Serikali nzima ione kwamba namna pekee ya kukuza sekta hii ni kuiongezea bajeti yake

na kujielekeza kwenye changamoto ambazo zinakabili sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kuona kwamba, namna moja ya kukabiliana na changamoto ni kuwa na ununuzi wa pamoja wa pembejeo na hususan mbolea. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumeisaidia sana, lakini naomba sana mbolea hii ifike kwa wakulima na wapate manufaa ya ununuzi wa pamoja, isiishie hapa katikati kwa sababu kuna hatari ya manufaa haya kwenda kwa wafanyabiashara badala ya wakulima na hivyo isiwe na *impact* kwenye kilimo chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niongelee kwa muda uliobaki juu ya mifugo. Mimi ni mtoto wa wafugaji, lakini vilevile wafugaji ambao wanalima. Kwa hiyo, sina sababu ya kupendelea upande mmoja, ila ninaomba Waheshimiwa Wabunge na Serikali tuone kwamba mifugo ni mali ya watu mmoja mmoja, lakini ni rasilimali ya Taifa. Mifugo kweli ni mali ya mtu mmoja mmoja lakini ni rasilimali ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hifadhi zimepangiwa maeneo na yanajulikana. Kilimo kinajulikana kwa sababu mazao yako shambani, lakini mpaka leo maeneo ya wafugaji hayajulikani, wao wanahangaika nchi nzima. Ninaomba sana, mipango na matumizi ya ardhi ndiyo namna pekee ya kuondoa migogoro na hifadhi na wakulima na watumiaji wengine na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kwa maisha yao wafugaji wanategemea mifugo hiyo, kunapokuwa hakuna majani wanatafuta. Mipaka ya hifadhi wakati mwingine haijulikani, kwa hiyo, ng'ombe wanaingizwa kwenye hifadhi labda kwa bahati mbaya, siyo kwa sababu watu wanataka kuvunja sheria. Kwa hiyo, wanapokutwa ng'ombe kule, wanapokamatwa na wanapoadhibiwa wafugaji, wakiamua kwamba ng'ombe warudi, ni lazima warudi wamepungua. Hii ni sawa na ni haki jamani? Naomba tuwasaidie wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, kunapokuwa na ukame, kwanza bei ya mifugo inashuka, lakini na ng'ombe wanahitaji maji na mito itakuwa kwenye hifadhi. Tunafanya nini? Badala ya kungojea kuwaadhibu wafugaji, naomba tujielekeze katika namna ya kuweza kutatua matatizo yao kwa kuwa na mabwawa na miundombinu ambayo itasaidia wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili kwamba vilevile kunapokuwa na migogoro, wafugaji wanapoenda Mahakamani, pamoja na kwamba watu watalia kwamba kuna rushwa, lakini wanaposhinda basi, ama wale wanaoshindwa, wakate rufaa, lakini wasiamue kuwatesa wafugaji kwa kuwanyima ng'ombe wao au kuwauza. Hata sasa hivi, najua hifadhi zina sheria kali, lakini tuone hali yenyewe ya nchi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tuone kilio cha wafugaji; wafugaji ni Watanzania, wana rasilimali ya Taifa, wanalinda mali ya Taifa kwa sababu Tanzania ni ya tatu katika ufugaji Afrika. Manufaa ya wafugaji hayaonekani, siyo kwa sababu tu ndugu zangu wanahamahama au wanachunga badala ya kufuga, ni kwa sababu, wanahitaji elimu, wanahitaji miundombinu na kuzijua sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye alama au chapa ya ng'ombe. Naelewa kwamba ufuatiliaji wa mifugo *(traceability)* ni muhimu sana, lakini naomba tuwaelimishe wafugaji. Vilevile unapoandikisha ng'ombe wako Gairo, kama hakuna maji, hivi watabakije pale? Lazima wahame, kwa hiyo, wafugaji wanaona mkiwachapa ng'ombe, ni kwamba sasa mnawa-*condemn* wale ng'ombe kufa yatakapotokea matatizo ya ufugaji, kama ukame au magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana, wakati tunachapa ng'ombe, ili *traceability* iwe rahisi, tuhakikishe na miundombinu ipo; ili wananchi waone manufaa. Wafugaji nao waelewe kwamba ng'ombe wanavyoweza kufuatiliwa, soko la dunia inakuwa rahisi

kulipata. Kama hakuna namna ya kufuatilia, Soko la Dunia linakuwa na wasiwasi. Kwa hali ilivyo sasa hivi, tunakazania kuchapa ng'ombe, lakini hatukazanii kuunda miondombinu kuweza kuwasaidia wafugaji na changamoto ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo juu ya uvuvi na Mheshimiwa Waziri anatoka kule kwenye uvuvi. Jamani ni Tanzania tu ambapo uvuvi haramu umeenea. Ninaomba tuchukue hatua ambazo zinatakiwa ili huu uvuvi haramu uweze kwisha. Wavuvi vilevile waelimishwe waone umuhimu wa kutumia nyenzo zile ambazo zinatakiwa katika uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaiangalia sekta hii vizuri, Tanzania itaondokana na umaskini na itafika kwenye uchumi wa kati na uchumi wa viwanda. Bila kilimo kutengemaa, viwanda havitawezekana nawaambia. Wafanyakazi wa viwandani watakuwa wanakula nini kama hakuna kilimo nchi hii? Tutakuwa tunaagiza nje. Malighafi zitatoka kule, kama hakuna kilimo, viwanda vitakuwaje imara? Kama viwanda vya Tanzania havitahusishwa na kilimo, maana yake tutakuwa hatuna utengamavu kwa sababu, tunachotaka tuwe na uchumi ambao unapanda kupitia kuongeza thamani ya mazao ambayo Watanzania wengi ndio wanayategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nilikuwa nafikiri nitachelewa kutoka Dar es Salaam, nimewahi. Naomba Wabunge wote tuone umuhimu wa kilimo, ufugaji na uvuvi kusudi nchi yetu iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wafugaji waangaliwe kwa macho ya huruma badala ya kuwafunga au kuchukua ng'ombe zao na bila kuona kwamba pengine siyo makusudi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua**.**

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Ahsante sana...

**MWENYEKITI:** Ngoja Mheshimiwa

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana...

**MWENYEKITI:** Ngoja kidogo Mheshimiwa.

Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Abdallah Bulembo wajiandae.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo. Pia nielekeze mchango wangu kwenye eneo la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema lolote, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwatetea na kuwasimamia wakulima. Ni kweli kwamba kilimo kinachukua nafasi kubwa ya Watanzania, lakini pia ni kweli kwamba tunaendelea kuimarisha mifumo ya kutetea haki na maslahi ya wakulima kadiri siku zinavyozidi kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli pia kwamba kuna umuhimu mkubwa wa Wizara ya Fedha kuangalia uwezekano wa kutoa fedha za kutosha kwa Wizara hii. Ukiangalia ukurasa wa 25 wa hotuba ya Waziri, unaonesha wazi kwamba fedha zinazotolewa ni kidogo sana hadi kufika Mei mwaka huu. Haitawezekana kutekeleza mipango na mikakati ya Wizara hii ambayo inabeba msingi wa uchumi wa nchi yetu kama fedha zinazotolewa hazitoshi mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kufikiria utaratibu mpya wa utoaji wa pembejeo za ruzuku kwa 100% kwa wakulima. Hili ni jambo kubwa sana na ni jambo ambalo linaweza likachochea maendeleo katika sekta ya kilimo, hususan sisi tunaotegemea kilimo cha korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie utaratibu wa namna ambavyo mazao mchanganyiko yanaweza kununuliwa mwaka huu. Katika msimu uliopita wa mazao mchanganyiko kwa upande wa Mikoa ya Kusini, nazungumzia mbaazi na choroko, bei ya kilo moja ilikuwa shilingi 400 hadi shilingi 600. Ukweli ni kwamba bei hii haitoshelezi na haifanani na gharama za uzalishaji wa mazao haya kwa kilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninapozungumza tayari wanunuzi wa choroko wameshafika kwa wakulima na wanaanza kununua choroko kwa shilingi 900; hii bado ni bei ya chini sana. Tunaiomba Serikali iangalie uwezekano wa kusimamia uuzaji na ununuzi wa mazao haya ili kuwafanya wakulima wetu waweze kuona mazao yao yana tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa na Serikali kwamba wametafuta soko nchi za India, Vietnam na nchi nyingine ambazo wanatumia mazao haya kwa wingi, lakini hali halisi ya ununuzi wa mazao haya haiendani na kauli ya Serikali. Tunaomba sana, jambo hili liweze kusimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kidogo kuhusiana na suala la kilimo cha korosho pamoja na suala la ununuzi na uuzaji wa zao hili. Naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa waliyofanya ya kuondoa tozo katika zao hili, kupunguza baadhi ya tozo. Tozo hizi baada ya kupungua zinapandisha bei, lakini zinatoa matumaini zaidi kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo katika zao la korosho zinawagusa kabisa wakulima. Zinawagusa na wanaziona zina tija kubwa, lakini yapo mambo ambayo Serikali inapaswa kuyatilia mkazo zaidi. Tunashukuru mwaka 2015/2016 ulifanyika ubadhirifu na Serikali katika mwezi huu inaendelea na imepiga hatua kubwa kuhakikisha kwamba wale waliofanya ubadhirifu katika tasnia hii ya korosho wanachukuliwa hatua kwa kuondolewa kwenye uongozi. Hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali, katika msimu wa 2016/2017 korosho zimenunuliwa kwa bei nzuri na wale waliofanya ubadhirifu mpaka sasa hivi tunavyozungumza kesi yao iko mahakamani. Haya ni mambo ya msingi yanayoendana kabisa na kasi ya Serikali ya kutetea maslahi ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo la kujiuliza, kuna ambao walifanya ubadhirifu mwaka 2015/2016 na kuna ambao wamefanya ubadhirifu mwaka 2016/2017 na mpaka sasa tunapozungumza wakulima wa korosho wanadai fedha zao hata kwa msimu huu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa korosho 2016/2017 katika Wilaya ya Masasi peke yake wakulima wanadai zaidi ya shilingi bilioni 1.5. Umefika wakati sasa wa Serikali kuhakikisha wakulima hawa wanalipwa. Serikali inaweza kuangalia uwezekano wa kutumia hata fedha ambazo zilikuwa ni michango yao wakulima, fedha ambazo zimewekwa katika Mfuko wa Pembejeo. Je, Serikali haiwezi kutumia fedha hizi kuwalipa wakulima wakati wanaendelea na utaratibu mwingine wa fedha hizi kurudishwa? Kwa sababu hali ya wakulima wetu ni mbaya na wakulima wanaendelea kudai, na sisi tumechoka na huu mzigo wa kuwasemea kila siku wakulima kwa mambo ambayo hayatatuliwi. Fedha zao zinatakiwa zipelekwe, walipwe kwa sababu korosho hizi zimeshauzwa, fedha zimekwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kero imezidi kuwa kubwa. Tunaomba Serikali itoe tamko na Waziri anapofanya majumuisho atuambie na asiposema nitashika shilingi kuhakikisha kwamba Waziri anaeleza *commitment* ya Serikali katika jambo hili. Korosho za wananchi bado hazijalipwa katika msimu uliopita, Serikali inaendelea na huo utaratibu, lakini ituambie ni lini jambo hili litakwisha? Wananchi wameuza korosho toka mwaka 2016 mwezi Oktoba, wengine mwezi Novemba. Kwa hiyo, Serikali ituambie inafanya nini katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la ushirika. Tunalo tatizo na Serikali ina jukumu kubwa sana la kuimarisha ushirika. Sekta ya Ushirika kwanza inakabiliwa na rasilimali watu ambayo haina weledi wa kutosha wa kusimamia ushirika. Serikali tunaomba iliangalie hili kuanzia katika vyama vya msingi mpaka katika Chama Kikuu cha Ushirika ili kuwa na watu wenye weledi wa kutosha wa kusimamia hasa yanapofika masuala ya fedha za wananchi. Kwa hiyo, Serikali iliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo lingine la ziada. Tunao watendaji wa Serikali, tunao watumishi ambao wana maslahi ndani ya mfumo wa ushirika na wana maslahi ndani ya biashara, hususan biashara ya korosho. Tumeeleza mambo haya kwa muda mrefu na Serikali baadhi ya mambo inaendelea kuyafanyia kazi; lakini tunaeleza wazi hatutakuwa tena tayari kuendelea kufanya kazi na watumishi ambao kwa namna moja ama nyingine wana maslahi ndani ya mfumo wa ununuzi na uuzaji wa korosho. Kwa kweli hawawezi kusimamia mfumo huu kwa kutetea maslahi ya wakulima wetu. Tunaomba Serikali iendelee kuchukua hatua na iwaondoe wale wote ambao kwa namna moja ama nyingine wanashiriki katika biashara ya korosho na kushindwa kuwasimamia wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na hayo ya kuzungumza. Naunga mkono hoja ya Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Daktari, ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba niipongeze Serikali kwa namna ya pekee ambavyo imekuwa ikitenda kazi na kutekeleza ahadi mbalimbali zilizoko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi katika Jimbo la Nsimbo 97% ni wakulima, 3% ni watumishi ambao ni kada upande wa walimu na huduma ya afya. Kwa maana hii ni kwamba, Wilaya hii inagusa sana Jimbo la Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Nsimbo 55% ya mapato ya ndani yanatokana na zao la Tumbaku, lakini tumekuwa na changamoto na nimshukuru Waziri kuna tozo amezipunguza hapa, lakini katika hizi tozo kumi, tozo nne zinagusa wakulima, tozo sita zinagusa makampuni.

Sasa Mheshimiwa Waziri, hizi tozo zinazogusa makampuni kwa tani 60,000 ambazo haya makampuni wanatarajia kununua, ukichukua *average cost per ton* na hiki alichokipunguza *is very minor.* Hai-*promote* katika wakulima kupata bei nzuri kwa haya makampuni kununua Tumbaku; kutoka 4,000 mpaka 2,000 na hizi 4,000 nyingine alizofuta. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie tena, libakie la wakulima, la makampuni liondoke kwa sababu hai-*promote* kwenye bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, wakati wa Mkutano wa Wadau wa Tumbaku, Morogoro, mwaka 2016 Desemba, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba suala la bei na kuna sheria ambazo zitakuja, tutaweza kuzibadilisha hapa ndani. Sasa tutaomba wakati wa majumuisho atuambie ni lini zinakuja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na malalamiko sana kwa upande wa wakulima kuhusiana na ukaguzi unaofanywa na *COASCO.* Hii *COASCO* iangaliwe, kwa sababu ukiangalia tija yao katika ukaguzi wa vitabu vya mahesabu vya vyama vya msingi bado kuna mahali wanapita wanatoa Hati Safi lakini badaye unakuta kuna ufujaji wa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri angalia *WETCU* Tabora. Waziri Mkuu kafanya ziara, ameibua, kasimamisha watendaji na Bodi, lakini rudi nyuma kwenye ripoti za

*COASCO.* Kwa hiyo, *COASCO* iangaliwe kama uongozi ubadilishwe, mfumo na utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoangalia zao la Tumbaku tuangalie na mazingira. Ni zao ambalo linahitaji sana miti. Mmetoa mabanio kidogo ya kisasa, lakini pia makampuni yanaenda yanashusha kiwango cha kununua. Ukiangalia katika hotuba ya Waziri, mwaka wa fedha 2015/2016 kwa tumbaku ni 60,691 na takwimu hiyo hiyo ikaenda 2016/2017, lakini 2017/2018 itakuwa 55,900. Kwa hiyo, kiwango kinashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa watu masikini ambao ni wakulima waliozoea kulima tumbaku, wanahitaji zao mbadala. Kwa nini tunahitaji zao mbadala? Tayari nchi imeamua kuwa ya viwanda. Tatizo kwenye tumbaku limeshaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Wizara, ile *mapping* ya mazao nchi nzima kwa kila Wilaya yanastawi mazao gani? Tuweze kugawiwa tuwape wananchi wetu wapate mazao mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tuna *demand* ya viwanda. *General Tyre* sasa hivi *raw materials* anatoa wapi? Bakhresa anatengeneza *juice, raw materials* nyingi inatoka nje ya nchi, kwa nini yasitoke humu humu? Kuna maeneo mengine watu hawana uelewa kwamba hapa ninaweza nikalima zao gani kwa sababu tangu mkoloni mtu amezaliwa, tangu mababu analima mazao hayo na watu wanaendelea hivyo hivyo. Kwa hiyo, Wizara kwa kupitia Halmashauri zetu, itoe hizo takwimu na sisi wanasiasa, Wabunge na Madiwani tusaidie kuelimisha wananchi. Hii itasaidia viwanda vipya vinavyokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vya zamani vinavyohitaji *raw materials* na wengi wananunua kutoka nje na matokeo yake pesa nyingi ya kigeni tunazitumia kuagiza malighafi kwa ajili ya viwanda badala ya kwamba tuwekeze kwenye kilimo zaidi, tupunguze pesa ya kigeni kwenda nje ili

*balance of payment* iendelee kuwa *positive* na ndiyo uchumi ambavyo unaenda unakua.

*Mheshimiwa* Mwenyekiti, tuna suala limezungumziwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, kuhusu utafiti, mambo ya *research,* nami niungane mkono nao. Mwaka 2016 tumepitisha hapa Bungeni *The Tanzania Agriculture Research Institute Act, 2016* na tumepitisha *The Tanzania Fishers Research Institute Act, 2016.* Kuna Bodi zinatakiwa ziundwe kwenye hizi *institutes,* je, mpaka sasa hivi zimekwishaundwa na kazi zimeanza? Kwa sababu inawezekana zile nyadhifa za Rais bado hajakumbushwa kuweza kuteua.

*Mheshimiwa* Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri utatupa mrejesho wa hizi sheria mbili tulizopitisha na hizi Bodi kama zimeanza kazi na faida yake ni ipi? Kwa sababu tunajua, moja ya majukumu ya Bodi kama *Agriculture Research Institute,* ni kuishauri Serikali katika *national policies, laws* na *regulations* mbalimbali kwenye mambo ya Kilimo. Sasa badala ya kukaa tunalalamika hapa mambo ya *research* na sheria tumeshatunga, ni suala ambapo mnatakiwa Wizara sasa ndiyo mkimbie badala ya kutembea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna suala la pembejeo. Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini mvua zinawahi kuanzia mwezi wa kumi. Serikali ijaribu kuangalia kwamba pembejeo hizi zije kwa wakati, na pia ruzuku iwepo. Serikali imekuwa na jitihada kubwa sana tangu Uhuru. Nilikuwa naangalia *Hansard* swali la mwaka 1963 liloulizwa na Marehemu Philipo Mbogo, kwamba ni lini Serikali italeta matrekta na majibu ya Serikali, ilikuwa kwamba kwa kupitia *Agriculture Credit Agency* watapeleka matrekta Mpanda *by that time.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mikakati hii tangu baada ya Uhuru ya kunyanyua kilimo, tukaja Benki ya *CRDB* hatukuifanyia vizuri, matokeo yake Benki ya *CRDB* imekuwa benki ya kibiashara badala ya kusadia vyama vya ushirika na wakulima. Sasa hivi tuna *Tanzania Agriculture Development Bank*. Mtaji ni mdogo, wakulima wetu kule

kwenye vyama vya msingi wanakopa kwenye benki ya biashara, wanatozwa riba kubwa, lakini benki mahususi ambayo imeanzishwa kwa ajili ya kilimo, bado haiwasaidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo, kama ilivyokufa *CRDB* imekuwa benki ya kibiashara isije na hii Benki ya Maendeleo ya Kilimo na yenyewe ikaangukia vile. Kuna uwiano kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kuna ile kitu inaitwa *MUVI* (Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini). Wakulima wanafundishwa, wanapewa mbegu bora, Kwa Nsimbo lini watakuja? Mawasiliano kati ya Wizara ya Viwanda na Kilimo yako wapi?

Pia katika tafiti tuangalie, tunaenda kwenye nchi ya viwanda, kuna *writeup* ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli wakati akichukua *Doctorate* alifanya *writeup* kwa kuangalia utomvu kwenye mabibo ya korosho jinsi gani yanaweza kutumika katika kuondoa kutu. Kwa hiyo, ni moja ya vitu ambavyo tunaweza tukaviangalia na vikatusaidia katika nchi yetu kuweze kuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kuhusu umwagiliaji. Tunaishi kwa kudra za Mwenyenzi Mungu, tunategemea mvua. Mikoa kati hapa mwaka huu imekosa mvua. Sisi kule tumebahatika, kwa nini tusiende kwenye umwagiliaji? Tunatumia maji kwa ajili ya kunywa. Maji ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Mto Malagarasi. Kwa nini tusiende kwenye kilimo cha umwagiliaji? Tunavyoleta maji huku kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya *domestic,* kwa nini tusitengeneze na mabwawa yakatumika kwa umwagiliaji? Nile inalisha huko Ethiopia na Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Unatukumbusha mengi na ninatabua *record,* baba yako Marehemu alikuwa Mbunge kijana sana wakati ule.

Tunaendelea na Mheshimiwa Abdallah Bulembo atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia kwenye Wizara hii nyeti.

Awali ya yote, kwanza nawapongeza Serikali kwa kuondoa tozo zile ambazo zilikuwa ni usumbufu sana kwa wananchi wetu hasa wakulima. Nawapongeza sana kuwa Serikali sikivu na kuweza kutuondolea hiyo kero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianzie kwenye mifugo. Kuna sehemu moja inaitwa Nkenge, Misenyi kule kuna *blocks*. Zile *blocks* kuna watu wamezikodisha lakini hawana mifugo. Ajenda hii ni ya muda mrefu, tangu alipokuwa Mheshimiwa Mbunge Mshama, amekuja Kamala na mimi leo naichangia ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Serikali ni nini? Serikali inajua, kwamba wafugaji wa eneo lile sio wale ambao wana asili ya maeneo yale. Watu wamechukua ma-*block* wanakaa Dar es Salaam na popote wanapokaa, watu kutoka nje wanaingiza mle mifugo wanakodisha. Wananchi wa eneo la Misenyi hawana mahali pa kufugia, wanatangatanga na mifugo yao. Wasukuma walioko huko wanafukuzwa, wanafanya nini, sasa Serikali ituambie, suala hili limekuwa la muda mrefu. Mheshimiwa Waziri wakati anakuja hapa hebu, aje na majibu mazuri ili usituamishie kwenye taratibu zile nyingine za kutaka kujua kwa nini mpaka leo Serikali inakuwa na kigugumizi katika eneo hili la Misenyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wana haki yao katika nchi yao, lakini unafanyaje kumpa *block* mtu mfanyabiashara? Je, vigezo vyenu ni vipi vya kugawa hizi *blocks* wakati mnawapa watu? Kila mwenye hela ndio anapewa, lakini hana mifugo. Watu wanateseka, wanaangaika, watu wa maliasili wanakamata ng'ombe za Watanzania, zinakwenda kwenye shida, lakini wale watu maeneo yapo. Serikali haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tunaomba majibu sahihi ili angalau tuwaambie wananchi wetu kule kwamba haki yao ya kufuga inafananaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihamie kwenye eneo la uvuvi. Wavuvi hasa nchi nzima sasa, wamekuwa wakichomewa nyavu zao, wakinyang'anywa, wakikamatwa wakisumbuliwa, sisi wavuvi tunafuata maji yalipo, lakini nyavu zinauzwa madukani na viwandani. Sasa Serikali pamoja na kwamba inakusanya kodi kutoka kwenye nyavu, ni lini italeta sheria humu Bungeni kwamba labda hizo nyavu zisitengenezwe? Kwa sababu mimi ni mvuvi, nimeshanunua nyavu, nimepeleka majini, kesho nakamatwa mimi na mali yangu. Anayepata hasara ni mtu huyu mlalahoi. Sasa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inawajali wanyonge. Wanyonge hawa wa kuvua, lini haki yao itapatikana? Kule anayewauzia, anawapa risiti. Kwa nini, hamnyang'anyi mkafuata mwenye duka aliyemwuzia akarudisha gharama yake basi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi kwa kweli ni shida. Mheshimiwa Waziri atuambie, ni lini wanaleta sheria ya hao wanaosabisha kuuza halafu wananchi wanaonunua ndio wanakuwa na hatima ya kunyanganywa mali zao, kufilisika, kupata taabu na kuchomewa mitumbwi? Ni shida sana. Kwa hiyo, naomba viongozi wa Wizara ya Kilimo na Serikali yangu tuleteeni majibu mazuri ambayo yatawapa imani wavuvi kule walipo baharini na ziwani ili wawe na amani na kazi yao kwa sababu ndiyo maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la ajira, ambalo pia ni eneo la Kilimo. Katika utaratibu, tunapenda viwanda, tunapenda uwekezaji, na kadhalika. Nataka kuuliza swali moja, nina mtu anaomba nimtaje kabisa, nita-*declare interest*. Kuna mtu anaitwa Vedic yuko kwenye Kampuni inaitwa *Alpha Group.* Mtu huyu mwaka 1997 sisi wavuvi wa Kanda ya Ziwa tutakumbuka, alikuja kama mhasibu kwenye kiwanda kinaitwa *TFP (Tanzania Fish Process)* pale Mwanza kama mhasibu. Kibali chake cha kuishi alikuwa na kibali *Class B*. Leo ni miaka 20 anaitwa *Manager Group.* Hivi akija mtu

kama mhasibu mpaka akafikia umeneja, Watanzania wangapi wanakosa kazi kwenye eneo hilo? Huyu mtu analindwa kwa *style* gani? Kibaya zaidi mtu huyu amezidi kuongeza wafanyakazi wa nje akiwaleta kama watalaam wa samaki, lakini watu hao leo tukienda pale Kipawa wanauza samaki. Yaani yupo pale anapokea hela ameingia kama mhasibu. Ukienda pale Kilwa wanavua mpaka pweza. Mtu amekuja kama mhasibu ni mtu wa nje, anazuia Watanzania kufanya kazi ambazo ana uwezo nazo, anavua samaki pale, anavua mpaka pweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka pale, shuka kule Tunduru anauza, Kilwa Kivinje anauza, *Mtwara Supermarket* wanauza, Lindi, Songea, sasa hivi ajira mnazilindaje jamani? Ninyi watu wa Kilimo na Mifugo, inawezekanaje akaja mtu miaka 20 anapewa kibali huyo huyo? Kile alichokuja kufanya, haijawahi kupatikana Watanzania wenye sifa hizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema mimi ni mfanyabiashara wa samaki, namjua, wala sisemi kwa bahati mbaya. Anayetaka kunijibu aje nimpe majibu, ninayo. Mtu huyu ameondoa Watanzania wote kwenye ajira, analeta ndugu zake, wanawaingiza mle kama wataalam samaki, kazi wanayofanya sasa, wako mtaani. Lini Mhindi akaenda kuchukua pweza baharini? Amepita wapi? Vibali *(permit)* hivi nani anatoa? Tunawalindaje Watanzania wetu waliosoma ambao wazawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme, Serikali yangu naomba inisamehe katika hili, lazima niseme. Huyu mtu anaitwa Vedic katika nchi hii, yeye ni nani? Mpaka anaingia kwenye siasa, naye anachagua watu wanaotakiwa kuwa viongozi katika nchi hii. Kwa kibali kipi? Naomba Mheshimiwa Waziri aje na maelezo hapa, huyu Vedic ana kibali cha aina gani katika nchi hii? Kwa nini vibali watu wanavyokuja navyo hawavifanyii kazi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu kama RK ana miaka 20 nchini. Tangu alivyokuja Vedic, RK akaja, wakienda ukaguzi, wanafungiwa kabatini. Nchi ipo, kwa nini? Hawa

Watanzania mnawasaidiaje? Raslimali ni zetu lakini mnasema wawekezaji waje, hamwendi kuwakagua na ninyi ndio maliasili pale. Ndiyo wazee wa uvuvi mko hapa. Kwa nini hamwasaidii Watanzania wenzenu? Viwanda hivi si viko chini yenu? Kwani hamna haki ya kuuliza? Sisi tunawapa *data*, wataalam wenu kule kama wame-*associate* na wale, nao mwende mwambie. Haiwezekani, haiwezekani mtu miaka 20 amekuja mhasibu, leo ni *Group Manager*, haiwekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda pale Mafia, nimekaa Mafia Kilindoni. Pale Vedic, miaka hiyo, mpaka leo, hapana! haki ya Watanzania lazima ipatikane. Haki ya Watanzania kama Wizara ya Mifugo, ninyi ndio mmekalia; tutaleta na maswali mengine humu ndani. Mheshimiwa Waziri bila kunipa maelezo ya kina, sijawahi kushika shilingi, lakini leo niko na wewe. Lazima unipe majibu ya kina. Inakuwaje mtu mmoja anakuja kama mvuvi, leo anataka na kwenye siasa atupangie nani achaguliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya wafugaji na wakulima, nina swali na ninaomba kutoa maelezo kidogo. Hivi suala hili vipi? Hawa watu wetu wanaouana kila siku, wakulima na wafugaji, Serikali mmejipangaje? Leo tunaliongelea kwenye kilimo, lakini kwa mawazo yangu kidogo naomba nitoe ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili linaihusu ardhi, kwa sababu lazima ardhi apange maeneo ili watu wasiuane. Eneo hili linahusu maliasili, leo ng'ombe wako kule, wanafukuzwa, wanachinjwa, wanauzwa shilingi 5,000. Suala hili linahusu sheria, linahusu maji, lazima kuwe na visima na malambo ya watu ambako watu watawapeleka ng'ombe, linahusu TAMISEMI, Mheshimiwa Waziri atuambie, lini mnakuja na ajenda ya kuwanusuru wananchi wetu kufa. Watu kuuana kwa kugombania maeneo ya malisho ya uchungaji. Lini mnakuja natafasiri kamili hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua suala hili ni mtambuka hamwezi kulifanya ninyi, lakini ninyi kama Serikali lini mtakaa kuleta majibu kuwaokoa Watanzania hawa.

Hawa watu wanaouana ni Watanzania, tuna haki ya kuwalinda, tuna haki ya kuwahudumia, lakini tukisema leo, wewe Bwana Mifugo utasema mimi sina ardhi, utasema sina maji. Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri atuambie, Serikali mtuambie lini mnaenda kukaa pamoja mkakutana mkaleta majibu ya yanayofanana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sixtus Mapunda na Mheshimiwa Subrina Sungura, ajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi name nichangie kwenye uti wa mgongo wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Awali ya yote nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, muda wote nilipokuwa nauliza maswali ya msingi na ya nyongeza kuhusu kero zinazowakabili wakulima wa kahawa kwenye tozo nyingi zisizoeleweka, leo wamelijibu hili kwa kuondoa tozo 17. Tulipokuwa tunapigania zile tozo zitoke kwenye 26 na 27, tulitambua kwamba kati ya vitu vinavyomkwaza mkulima wa kahawa kule chini, ni bei ndogo iliyosababishwa na tozo nyingi zilizokuwa katikati ya mchakato, yaani kutoka kwa mkulima mpaka unafika juu kwa mnunuzi mnadani na nje ya mnada. Sasa mmelifanya hili jambo kubwa sana na kuna wachache watabeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba kwenye hili Serikali mmefanya jambo zuri na ongezeni moja lingine. Kwa sababu mmeziondoa zile 17, msiache hewani, wekeni na bei ya kiwango cha chini cha ununuzi wa kahawa. Kwa sababu

kwenye tafiti zetu tunajua, hizo dola zote zilizopungua zimeondoa gharama za uendeshaji, uzalishaji na gharama za usafiri na kitu kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tumsaidie mkulima kule chini tufanye kama tulivyofanya kwa mahindi mwaka 2016, tukasema mtu asinunue mahindi ya mkulima mpaka awe na shilingi 500 kwa kilo ndiyo yanunuliwe. Kwenye kahawa, korosho, tumbaku na kwenye pamba tunaweza tukafanya hivyo hivyo. Tukifanya haya ninayoyasema, ule wasiwasi aliokuwa nao ndugu yangu Mheshimiwa Silinde utakuwa umeondoka. Kwa kweli tutakuwa tumemsaidia mkulima, ila tunafahamu gharama zilizokuwa katikati ya mchakato zilikuwa zina-*trickle down* zinafika zinamsumbua mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala lingine kuhusu ukuaji wa kilimo na Tanzania ya viwanda. Tutaongea hapa siku zote kuanzia asubuhi mpaka jioni, tusipo-*link* hizi sekta mbili; sekta ya kilimo na sekta ya viwanda, mambo yote mawili hayataweza kwenda. Kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema tunataka tumsaidie mkulima aliyelima nyanya zake zikaoza pale Dumila kabla hajafika kwenye soko, anahitaji katikati kitu kinaitwa *processed Industry* ili kwanza kuongeza *value* ya zile nyanya zake, lakini kuzitunza ili zisiweze kuharibika. Pale anahitaji awe na kiwanda. Utaongelea korosho, *the same*, utakwenda kwenye mahindi, tutazalisha mahindi ya kutosha, lakini tusipoyaongezea ubora wa kutosha tutapata tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakuna maendeleo ya viwanda kwenye Taifa la Tanzania bila kuwa na maendeleo ya kilimo, vyote vinakwenda pamoja. Utakwenda kuongelea habari za ufugaji, utaongelea masuala ya ngozi hapa, mimi mpaka nashangaa. Hivi kweli tunashindwa ku-*intervene* tukapata kiwanda kimoja hata kwa mkopo kwa ajili ya ku-*process* bidhaa zinazotokana na ngozi, halafu wafugaji wetu wakawa na ahueni kwenye maisha yao? Kweli hili linashindikana.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Taarifa Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumtaarifu Mheshimiwa Mapunda kwamba Mwanza pale tulikuwa na kiwanda kikubwa sana kinaitwa *Mwanza Tanneries* na kiwanda kile mpaka kinauzwa kilikuwa na mashine zote, lakini sasa hivi ni *godown* ya mkandarasi. Naomba uendelee. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unasemaje kuhusiana na taarifa hiyo?

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana Mheshimiwa Kanyasu. Kimsingi hiyo taarifa ana-*compliment* kwa ninachokiongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachohitaji, *we need a serious government intervetion* kwenye vitu kama hivi. Kama kiwanda kilikuwepo, vilikuwepo vingi, sitaki kurudi nyuma. Nilichotaka nikiseme hapa kwa nia njema, tukitaka tutoke tuisaidie Sekta ya Kilimo, tunahitaji *a serious intervetion* kwenye kuwekeza kwenye kilimo. Kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, lazima tuichore tena ramani ya kilimo ya nchi yetu *including* watalaam wa *research,* wafanye tafiti. Ukiangalia Morogoro, ina sifa kubwa ya *alluvial soil*. *Alluvial soil* ni udongo wenye rutuba na Mkoa wa Morogoro tukiungalia unapata mvua bila matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa mvua, bado una mito mikubwa inayoweza kufanya Morogoro peke yake ikafanya Tanzania isife njaa. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu Serikali hapa haija-*invest* kwa huyu mkulima, inadhani mkulima anajua. Mkulima hajui. Hapa lazima tumwambie mkulima cha kufanya, namna ya kufanya na namna gani tutatoka hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mvua zilizopita zimetuletea mafuriko lakini mafuriko yale kwa wenzetu ni neema. Hebu tujiulize tungeweka mabwawa ya kuyaelekeza yale maji ya mafuriko kipindi hiki ambacho wakulima hawawezi kulima na wakilima mvua zinazidi mazao yanaharibika, tungeyateka yale maji tungeweka katika maeneo ya mabwawa, kipindi cha mwezi wa Sita, wa Saba ambapo mvua hakuna, maji yale yale ambayo yalitukwaza sasa yatumike kwenye kilimo. Vitu kama hivi vinahitaji tu kuelekezwa, Serikali elekezeni tu kila kitu kitafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine mnaongea *irrigation, irrigation, irrigation,* kuna njia rahisi sana za kuifanya Tanzania iwe ya umwagiliaji. Tuna utaratibu tumeuweka hakuna shule ya sekondari, shule ya msingi itakayojengwa bila choo, tunashusha tu *circular,* hakuna shule yoyote ya msingi na sekondari itakayojengwa bila kuwa na miundombinu ya kuvuna maji ya mvua. Ukivuna maji ya mvua *from day one* mtoto akiwa shule ya msingi anajifunza umwagiliaji kutokana na maji ya mvua. Sasa sijui tumelogwa, hata sijui tufanyeje lakini ninachoweza kusema hapa kwa kweli Serikali inahitaji *serious intervention* kwenye hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine huwezi ukakuza sekta ya kilimo bila kuwa na uhakika wa matumizi bora ya ardhi. Douglass Jerrold katika andiko lake la *"A land of Plenty"* alitumia methali moja ya kilatini, alisema *"Cujus est solum, ejus est usque ad coelum"* akimaanisha *"He who owns the soil or land owns up to the sky"* kwamba matumizi bora ya ardhi ni utajiri mkubwa kuliko kitu kingine chochote. Nchi yetu tumebarikiwa kuwa na ardhi bora, kinachotusumbua sisi kila siku tunadhani tunaanza upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuulize swali moja Mheshimiwa Waziri anaikumbuka Kapunga *Rice Project? Project* ambayo ilikuwa kuwa ya *irrigation scheme,* iliandaliwa kwa ajili ya kuwasaidia watu, ukifika pale kwa sababu maji yapo, mkulima ana uhakika wa kuvuna. Nenda

pale Morogoro kuna ile *Dakawa Rice Project* nayo ni *irrigation system* nzuri, kama Serikali ilishawekeza watu wananufaika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuichore ramani ya Tanzania kwa maeneo sita au saba ya kuanzia kama tulivyofanya Dakawa, tufanye vilevile Kilombero, tufanye hivyo kwa Mheshimiwa Mwamoto kwenye lile Bonde la Mto Ruaha wanalima vitunguu vizuri sana kule, wawekewe utaratibu uleule wa *irrigation* haya mambo yote yatakwisha tutakuwa hatuna matatizo na twende maeneo ya Rungwe kule kuna mifumo mizuri ya kilimo kuanzia Januari mpaka Disemba. Tusipofanya *a serious intervention* kwenye kilimo hatutatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza nikashauri ili twende vizuri, tunataka tuwasaidie wakulima, wakulima tukiwaacha na hekari moja moja hatutafanikiwa. Jambo la kufanya, wale wote ambao wanalima kwenye eneo linaloelekeana tufanye *mechanization of agriculture.* Kama mtu ana hekari mbili kijiji kizima mna jumla ya hekari 10,000, hizi hekari 10,000 zote zinakuwa *communal* tuna-*inject* pale trekta na taaluma, kwa hiyo, kila mwenye hekari yake moja ana-*offer labour* kwenye ardhi yake ili tupate tija kwa sababu hatuna uwezo wa kila mmoja kuwa na trekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ndivyo kilimo kilivyokuwa duniani kote, hatuwezi tukaendelea na hii asilimia 65 hapa tunajidanganya. Asilimia 65 ya hekari moja moja tunalima nini? Mimi hapa nimepata magunia mawili, mwingine matatu halafu tunajiita wakulima, *we are not...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Silanga.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inachukua asilimia 80 ya Watanzania yaani ukiangalia wakulima, wafugaji na wavuvi ni *almost* asilimia 80, asilimia 20 ndiyo ya Watanzania wanaofanya shughuli nyingine. Sekta hii isipoangaliwa kwa umakini wa hali ya juu ni dhahiri kabisa kwamba tunaweza tukaliingiza Taifa kwenye mgongano wa wenyewe kwa wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana, nchi hii imejaliwa maeneo mazuri, ardhi nzuri, mito, bahari, mabonde, milima na kila kitu na asilimia kubwa ya ardhi bado iko vijijini na wakulima na wafugaji wengi bado wapo vijijini, ni tatizo gani linalotushinda kama nchi kuweka sera nzuri zitakazohakikisha kwamba Taifa haliingii kwenye migogoro? Tuna *Land Use Planning,* tumejipanga kila kitu, kwa nini watu wanagombana, shida iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kuna sababu za kijiografia zinazopelekea watu wanahama na mifugo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Kuna maeneo ambayo kwa mvua jinsi ilivyonyesha mwaka huu mifugo haiwezi ku-*survive* mafuriko lazima watahama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Tumeona nchi nzima mvua inanyesha lakini Dodoma hii kuna maeneo kabisa mvua haikufika *automatically* lazima wakazi wa maeneo hayo ama wafugaji wa maeneo hayo ku-*shift* kutoka hapa kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati gani mfugaji huyu atakwenda kuomba kibali cha kuhakikisha kwamba anahama na mifugo yake na wakati mifugo wale wanatakiwa ile ili wasife na njaa? Kwa hiyo, tunapoweka sera, sheria na sheria ndogo lakini lazima tuhakikishe mabadiliko ya kijiografia ambayo yanaweza yakapelekea watu wetu waweze kuhama yanazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la uvuvi. Mkoa wa Kigoma tuna Ziwa Tanganyika na lina samaki wa aina nyingi sana lakini samaki wale kwa kweli hawavuliwi ipasavyo. Tuna dagaa wazuri ambao

wanapelekwa Uingereza, Marekani, Malaysia na sehemu zingine lakini bado wanavunwa kwa kiasi kidogo sana. Tunaomba kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia vijana wetu na wavuvi wanaotoka Ziwa Tanganyika waweze kuvua uvuvi wenye tija na kulisha nchi lakini pia na kulisha nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kwa wavuvi wetu katika Ziwa Tanganyika wanatekwa na maharamia kutoka Congo na wengine kutoka Burundi wakiingia kule wananyang'anywa nyavu zao, pesa, mashine na kadhalika. Hali hii inawarudisha vijana wengi nyuma na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi kwa kuhofia usalama wao. Serikali inawa-*guarantee* vipi vijana hawa ambao wana-*risk* kwenda kutafuta maisha katika ziwa lenye kina kirefu kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa ufanisi mkubwa na kuweza kuchangia uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia bado kodi kwa wavuvi ni kubwa. Nilikuwa na-*discuss* na Mheshimiwa hapa wa Ukerewe, wavuvi wanatozwa kodi kubwa sana za uvuvi, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza kodi hizi? Kwa sababu mvuvi anapokwenda kuvua kwanza kuna mawili, aidha, arudi salama ama asirudi salama. Kwa hiyo, pamoja na kuchukua *risk* yote hii kwa nini tunawatoza tozo kubwa na ni za kero? Mna mkakati gani wa kuhakikisha kwamba tunapunguza kodi za kero kwa wavuvi wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkoa wa Kigoma tunalima, tuna zao la mchikichi. Kwa taarifa ya *research* zilizofanyika hivi karibuni, zao la mchikichi linatumika katika kuzalisha bidhaa mbalimbali katika nchi ya *Europe* kwa asilimia 80. *Chocolate* hizi zinazotengenezwa ili ziweze kuganda na ziweze ku-*survive* zinatumia zao la mchikichi, lakini hakuna utaratibu wowote unaowekwa kuhakikisha kwamba unafanyika utafiti wa kutosha na zao hili liweze kulimwa kwa umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Njalu Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Aisharose Matembe dakika tano na Mheshimiwa Mussa Ntimizi dakika tano.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya wakulima na mimi nikiwa kama mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Serikali, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wataalam, kazi yao inaonekana. Kwa miaka miwili tumeona bei za mazao yetu zikiongezeka. Pamoja na hilo, ziko changamoto ambazo tunahitaji wazitatue kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la tozo kwenye mazao yetu, zile tozo zinazopunguzwa moja kwa moja zinaongeza thamani ya bei ya mkulima. Nimepata tabu kidogo Waheshimiwa Wabunge wanasema inamsaidiaje mkulima. Ni suala la kujiuliza kwa sababu mfanyabiashara siku zote yeye hapati hasara, gharama zote anampelekea mkulima. Kwa hiyo, tunapojaribu kuchangia kwenye suala la kilimo tuwe makini sana pale tunapoishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana unakuta kwenye zao la pamba kuna *VAT* na asilimia 70 ya wakulima wanaotarajiwa kuwezesha viwanda na vitu vingine wanatokana na kilimo. Sasa utaona asilimia 70 hii ya wakulima wote wanapelekewa *VAT* na akipelekewa *VAT automatically* ile *VAT* itakwenda kumpunguzia mkulima, kwa hiyo, utaona bei zinakuwa chini. Ndiyo maana unakuta mazao mengi wakulima wanakuwa wanayakimbiakimbia kuyatekeleza, wanaibua wao wakulima wenyewe kwa maarifa yao lakini yakishaibuliwa inakuja kodi mbele yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana Serikali mambo haya ya msingi tuyaangalie, huwezi kuweka *VAT* kwenye pamba. Mashudu kwani mfanyabiashara mdogo

yule ambaye angenunua yale mashudu kwa ajili ya vifaranga vya kuku na vitu vingine vingeendelea kufanyika umeshamwekea kodi hataweza kununua na hivyo bei ya pamba haitapanda katika maeneo yale. Kwa hiyo, utakuta bei zinaendelea kushuka kwa sababu hatuwezi ku-*control* masoko haya tunatarajia kutoka nchi za nje. Kwa hiyo, naomba suala hili la mazao hususani zao la pamba mwangalie sana kodi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema ametoa kodi kwenye pamba, Mwenge sio kodi, ni makubaliano kati ya *DC* na *ginneries* husika. Suala la msingi hapa ni kwamba toeni *VAT* kwenye suala hili ili bei za wakulima ziendelee kuongezeka na zikitolewa tutapata fedha nyingi za kigeni lakini tutapata ajira nyingi na viwanda vitaendelea kufanya kazi katika eneo letu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la mbegu. Kwenye suala hili la mbegu watafiti wetu wanaendelea kutafiti vizuri tu kwa muda mrefu lakini ukijiuliza, mfano, nataka nizungumzie suala la pamba, kuna mbegu ya *UK91* imeshapitwa na wakati. Ndiyo maana siku zingine Wabunge tunauliza kwa nini mbegu hazijaota, hii ni kwa sababu zimeshapitwa na wakati na watafiti na wataalam wanalifahamu hili hata mfumo wa kuzipitisha hakuna, zinakuwepo tu ili mradi lakini *GOT* yake ni kidogo asilimia 32 inayosababisha hata bei zenyewe za pamba zisipande. Kuna hii *UK08* ikisimamiwa vizuri, ikizalishwa vizuri katika maeneo husika tuna uhakika tutazalisha *GOT* asilimia 40 ambayo itakuwa ni *average* kubwa sana na tutapata fedha nyingi za kigeni katika maeneo yetu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mifuko ambayo ilianzishwa ya *CDTF* ilikuwa na wadau watatu, Serikali, wakulima pamoja na wafanyabiashara wenye mfuko husika. Kwa muda mrefu sana fedha hii imekuwa ikitumika nje ya utaratibu badala ya kumnufaisha mkulima anakuwa anafanya *double payment,* amechangia kwa mwaka huu na mwaka unaokuja anaambiwa kuchangia halafu mwisho wa siku hapati pembejeo. Namwomba sana Mheshimiwa

Waziri kwa mwaka huu ambao tunaumalizia maeneo mengi yameathirika sana kwa sababu ya pembejeo hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mfumo huu ulivyoanzishwa kulitengenezwa kitu kinaitwa *pass book* kwamba mkulima alikuwa anaweka benki yake, benki hii akienda kuchukua dawa ina maana apewe bure lakini matokeo yake mkulima huyu amekuwa akitozwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri hii pembejeo ya mwaka huu awatangazie wakulima na wananchi wa Tanzania nzima hususan mikoa inayolima pamba kwa sababu ni pesa zao walizozichanga, hakuna sababu ya mtu anakuja anasema anafanya kilimo cha mkataba na kilimo cha mkataba hiki tayari pembejeo zile alishachangia mwananchi. Kwa hiyo, hizo anatakiwa apewe bure ili aweze kujiendesha kwa msimu unaokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niombe kwenye suala zima linalohusiana na suala la kilimo cha mkataba tungetafuta jina lingine, sio kilimo mkataba. Hii ni kwa sababu unaposema mkataba unapomaliza mkulima atakwambia nataka niuze bei hii na sisi hatupangi bei, tunategemea mataifa makubwa yanavyopanga bei ndiyo tunashusha gharama zetu na kadhalika ndiyo tunapata bei sahihi. Kwa hiyo, naomba litafutwe jina lingine, dhana ni nzuri ambayo itaweza kuboresha na kuleta tija kubwa katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona ukurasa wa 34 wamesema wastani wa uzalishaji umeongezeka kutoka 728 kwa hekta kwenda 925. Napata tabu kwa sababu mwaka jana takwimu walizotuletea walisema kwamba takribani hekari milioni moja za pamba zimelimwa. Kwa takwimu hii ukiizidisha tungepata milioni 328, matokeo yake kwa mwaka jana tumepata milioni 120 tu. Kwa hiyo, utaona hizi takwimu ni za kukaa na kujifungia na kubumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana suala hili hasa la utafiti litiliwe mkazo na waangalie ni jinsi gani itakayoweza kusaidia. Haya mambo tunayazungumza

sana, wakulima wanayazungumza lakini tuna tatizo la wataalam kwa maana ya Maafisa Kilimo, hatujui wanawajibika kwa nani, nalo hili ni tatizo kubwa. Kwa hiyo, tunamwomba Waziri aweze kukaa na kujua mamlaka haya husika, huyu mtu anawajibika wapi, bodi yupo peke yake, atazunguka na pikipiki yake katika Wilaya nzima lakini pale kwenye Serikali kwa maana ya TAMISEMI kuna Afisa Ugani kila Kijiji, Kata na kila maeneo lakini hawa watu hawawajibiki, wanawajibika kwa nani? Mwisho wa siku inapotokea sasa Halmashauri imetengeneza mapato ndiyo watu wa kwanza kuingia kwenda kutoza kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili ni tatizo na lazima tuliangalie kwa mapana Waheshimiwa Wabunge tujaribu kusaidia kwamba mifuko yetu hii na bodi zinazoundwa hizi ziweze kufanya kazi yake vizuri lakini ziweze kuisaidia Serikali. Waziri kwenye suala zima la Bodi ya Pamba sasa hivi ni mwaka wa tatu Bodi ya Pamba haina *Board Members* wake ndiyo maana tunakosa mambo mengi maeneo yetu kwa sababu hakuna ushauri. Mnakutana na wataalam wale wale mkirudi hakuna jambo jipya litakaloendelea kupatikanika katika maeneo yetu. Naomba hilo nalo Mheshimiwa Waziri ajaribu kuliangalia, hii bodi itatengenezwa lini na vitu gani vifanyike ili mambo yaende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nimpongeze Mkurugenzi Mtunga na Waziri kwa sababu mmeendelea kutengeneza mfumo mzuri wa bei. Nina imani na mwaka huu bei zetu zinaweza zikawa nzuri. Ombi kubwa kwa Serikali toeni hizi kodi na wananchi watajiendesha wao wenyewe. Haya mambo tunazungumza, leo tuna asilimia tatu tu ya kilimo lakini mwananchi huyu anaendelea tu kuhangaika kule lakini bado hatujataka kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba sana hasa kwenye suala zima la mbegu tunajua kule Simiyu, wameanzisha na Meatu ni jambo jema na maeneo mengine tujipange kuhakikisha tunaweka utaratibu mzuri. Vilevile wako wakulima wazuri tu ambao wanaweza wakafanya

kazi hiyo kwa kuwaelimisha wengine. Nashauri angalau kila kijiji kuwe na wakulima wawili ambao watakuwa ni sehemu ya mfano, watu watafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwenye suala la la mbegu za mahindi wakati zinakuja watu walikuwa wanalalamika lakini sasa baada ya kuona uzuri wa mbegu zinavyozalisha watu wanaenda kununua wenyewe tofauti na kutumia nguvu kubwa na fedha nyingi. Nina imani wakulima wa kanda zetu kule wakishajua jambo wao wenyewe hujiongoza. Unaweza ukasema wakati mwingine hata kilimo wanaweza wakawa wanakwamisha, wanawapa matumaini makubwa, matokeo yake hata mbegu hawaleti. Kwa hiyo, tufike mahali tusiwe tunatoa matumaini kwa wananchi wetu ambapo wanatarajia kwamba kuna kitu fulani kinakuja, pembejeo inakuja mwezi wa Nne au wa Tano kitu ambacho inakuwa muda wake umeshaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Aisharose Matembe na Mheshimiwa Ntimizi dakika tano tano na Mheshimiwa Ngwali ajiandae.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na afya njema na hatimaye kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nampongeza Rais wangu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mawaziri wote kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Taifa hili na kuhakikisha maendeleo ya haraka na yenye tija yanapatikana kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha mapinduzi kwenye uchumi wa viwanda yanapatikana na hii itafanikiwa tu iwapo tutakuwa na mikakati thabiti ya kilimo chenye tija. Asilimia 80 ya wakazi wa Mkoa wa Singida wanajishughulisha na kilimo, hulima mazao ya mahindi, uwele, mtama, viazi vitamu na muhogo kama mazao ya chakula. Pia hulima mazao ya biashara kama alizeti, vitunguu, pamba, karanga pamoja na choroko lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na pembejeo zisizokuwa na viwango, bei kubwa za pembejeo za zana za kilimo, ruzuku ndogo inayotolewa na Serikali, uhaba wa wataalam na mashamba darasa pamoja na uhaba wa mitaji na mikopo kwa wakulima. Hii inawakatisha tamaa sana vijana na wanawake ambao wengi wana hamasa kubwa ya kujikita katika kilimo cha kisasa lakini hukimbilia mijini ambapo hudhani ndiko kuna maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mkoa wa Singida unakabiliwa na uhaba mkubwa sana wa Maafisa Ugani ambao ni watu muhimu sana katika kilimo na hasa kwa wale wananchi waliopo maeneo ya vijijini. Ukiangalia tu Wilaya ya Iramba, wapo Maafisa Ugani 79 lakini mahitaji ni 324, Wilaya ya Singida Vijijini mahitaji ya Maafisa Ugani ni 188 lakini waliopo ni 45 tu, Wilaya ya Mkalama mahitaji ni 185 lakini waliopo ni 38. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya uwepo wa Maafisa Ugani hao wachache, bado wanakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi kama pikipiki na hivyo kushindwa kuwafikia wananchi waliopo maeneo ya vijijini. Ni vema sasa Serikali ikaangalia jambo hili kwa kina kwa kuongeza Maafisa Ugani wa kutosha katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee masikitiko yangu juu ya mgao mdogo wa ruzuku ya pembejeo kwa Mkoa wa Singida. Kwa msimu wa mwaka uliopita, 2016/2017, Serikali

iliweza kutupatia tani 20 tu za mbegu za mpunga, tani 20 za mbegu za mahindi na tani 100 ya mbolea ya kukuzia ambayo ni sawa na asilimia 0.29 ya mbolea kwa mahitaji ya mkoa mzima. Kiwango hiki ni kidogo sana, mahitaji yetu ni kuanzia tani 33,000 mpaka 44,000 kwa mkoa mzima. Singida tumekuwa tukiachwa nyuma kwa kila jambo. Wakati ufike sasa wauangalie Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida ni miongoni mwa mikoa inayolima mazao ya mafuta. Kwa Mkoa wa Pwani ni nazi, kwa Mkoa wa Kigoma ni mawese na Mikoa ya Singida na Dodoma ni alizeti. Hata hivyo, Serikali haijalitilia mkazo zao hili na haijalitaja kama ni zao la kimkakati, hata Mpango wa *ASPD II* haujatilia mkazo kabisa zao hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msimu uliopita takribani tani 58,000 ziliuzwa nchini Kongo ambazo ziliingiza zaidi ya shilingi bilioni sita. Iwapo zao hili litatiliwa mkazo uzalishaji utaweza kuongezeka lakini pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Musa Ntimizi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngwali.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hata hizi dakika tano. Kwanza kabisa, kwa haraka haraka, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri kwa namna wanavyoshughulikia zao la tumbaku katika Mkoa wetu wa Tabora. Zao la tumbaku lilikuwa na changamoto nyingi sana, tumekuwa tunalalamika sana, lakini sasa tunakoelekea zao la tumbaku litamnufaisha mkulima wetu wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze kwa hizi tozo ambazo zimepunguzwa katika zao letu la tumbaku. Baadhi ya watu wanasema hizi tozo hazimsaidii mkulima, lakini tozo hizi zimemgusa mkulima, zimemgusa mnunuzi, mwisho wa

siku inagusa bei ya mkulima. Nina uhakika kabisa tunakokwenda, bei ya tumbaku itakuwa inamnufaisha mkulima wetu kwa sababu tozo nyingi zitakuwa zimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba watusaidie kitu kimoja, tuna *grades* za tumbaku kama 67, hatujamsikia Mheshimiwa Waziri akilizungumzia hili kwa mapana ili kuondoa *grades* zilizopo kumsaidia mkulima wetu wa tumbaku auze katika *grades* ambazo zitamsaidia mkulima wetu wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, naomba nigusie pia suala la mbolea kwenye tumbaku na mahindi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa wazo la *bulk procurement,* itasaidia sana. Ilikuwa vichekesho, mbolea ya kupandia ilikuwa inakuja wakati wa kukuzia, mbolea ya kukuzia ilikuwa inakuja wakati tunavuna. Kwa hiyo, ilikuwa haitusaidii sisi kama wakulima wa mazao ya tumbaku na mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kidogo nimwombe Mheshimiwa Waziri anieleze, asali ni zao linalofahamika au halifahamiki na Serikali yetu? Kwa sababu nimejaribu kupitia kitabu chake sijakuta sehemu hata moja ameizungumzia asali, asali ni zao ambalo linasaidia kipato cha mkulima katika maeneo yetu. Igalula na Urambo tunarina asali nyingi sana na ni asali bora kabisa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze ana mkakati gani na wakulima wa asali ambao hawajatengenezewa mazingira yoyote ya kufanya asali yao iweze kuwasaidia kuongeza kipato. Vilevile Mheshimiwa Waziri, asali hii ikisimamiwa vizuri inaweza ikaongeza pato la nchi. Naomba Mheshimiwa Waziri aniambie kama anafahamu kuna sehemu wanarina asali na asali hii inaweza kusaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie wafugaji kwa haraka haraka. Sisi katika Jimbo la Igalula tuna

wakulima na wafugaji lakini hata siku moja hujawahi kusikia tuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Ninachotaka nishauri, wafugaji wetu tusiwaone kwamba ni tatizo katika maeneo yote ya nchi, wafugaji wetu wana haki kama watu wengine katika nchi hii. Bahati mbaya sana hatujawa na mkakati mzuri wa kuwasaidia wafugaji wetu, hatujawatengenezea mazingira ya kufugia, maeneo ya kwenda kufugia, leo lazima tutamlaumu mfugaji kwamba ni mkorofi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna maeneo mengi ya *reserve* lakini labda tufanye tathmini, hayo maeneo yanastahili kuendelea kuwa *reserve* mpaka sasa? Maeneo mengi ya *reserve* watu wa maliasili wamekuwa wakiyatumia kama maeneo ya kupatia kipato. Wafugaji wetu wakienda kule wanakamatwa, wanatozwa faini kubwa bila sababu lakini ukiangalia Serikali haijatenga mazingira mazuri ya kumwezesha mfugaji huyu akafuga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niulize, hivi mkata mkaa na mfugaji wa ng'ombe, nani anaharibu sana mazingira? Inaonekana sana mfugaji akipeleka mifugo kwenye maeneo ya *reserve* anaharibu mazingira lakini magunia ya mikaa yanayoondoka kila siku katika maeneo yetu ni mengi sana. Naomba Serikali imwangalie sasa mfugaji, akitengewa maeneo mazuri, nina uhakika hatutakuwa na migogoro hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi katika Jimbo la Igalula tuna maeneo ambayo tulishatoa mapendekezo tuwaongezee wafugaji kilometa tano ili waweze kufanya shughuli zao za ufugaji. Mheshimiwa Waziri, sisi katika Jimbo letu hatuna migogoro lakini kama hatutatengeneza mipango mizuri ya wafugaji wetu migogoro itakuja na Waziri ndiyo atakuwa amesababisha migogoro hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Tizeba, tunamwambia mambo mengi hayafanyiki, lakini niombe Wizara ya Fedha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngwali, umekubali kunipa dakika tano, si ndiyo? Haya, endelea.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuendeleza pale ambapo pameachwa na Mbunge wa Mkinga, Mheshimiwa Dunstan Kitandula juzi Jumamosi alipokuwa akichangia. Niseme tu kwamba Mheshimiwa Dunstan Kitandula alikuwa ni Makamu Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara katika msimu uliopita ikiongozwa na Mwenyekiti makini, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili tu na zote zitahusu mambo ya uvuvi. Nilipochukua kitabu hiki nilikuwa nikiangalia kwenye *cover* ya kwanza hapa nikaona hii *eco culture,* nilipoiona nikaona mambo mazuri, nikafungua ndani hakuna kitu kabisa, niseme ukweli. Unapozungumzia *eco culture* huwezi kuzungumzia kutengeneza bwawa fulani ambapo mabwawa yenyewe yametengenezwa na wananchi, lakini unazungumzia dhana pana sana ambayo ni lazima Serikali iwe imejipanga katika kuhakikisha kwamba hiyo *eco culture (*ufugaji wa samaki) ambao sasa hivi karibu nusu ya watu duniani wanakula samaki wa kufuga, inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uwe na *eco culture* lazima uwe na *fishing habours* ambazo hutuna. Katika bajeti ya mwaka 2016/2017, ametenga shilingi milioni 500 pesa za ndani kwa ajili ya utafiti pamoja na shilingi milioni 24 za nje kwa ajili ya utafiti. Hebu tukitoka Waziri nitampa *clip*, Kenya wametenga bilioni 6.6 kwenye *eco culture* sasa lazima uwe na hizo *fishing ports* ambazo zitakuwa na *dry dock,* kutakuwa

kuna maji ya kutosha, kutakuwa na *facilities* zote, ndiyo unaweza kufanya jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia inatakiwa uwe na *fisheries laboratory,* hakuna *lab* zozote za kukagua hao samaki kama wana viwango au hawana. Inatakiwa kuwe na *fish market,* soko la nje na la ndani la kuuza samaki hao lakini pia ahamasishe walaji wa samaki kwa sababu kiwango cha kimataifa sasa hivi cha ulaji wa samaki, kila mtu anatakiwa ale kilo 20 kwa mwaka, Tanzania tunakula nusu yake, tunakula kilo nane kwa mwaka. Kwa hiyo, lazima fedha hizo zitengwe kwa ajili ya kuhamasisha watu wale samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia unatakiwa uwe na ile *fish landing site.* Sehemu ambayo utaweka hizi *eco culture* zako, ufugaji wa samaki ambayo imefanyiwa uchunguzi wa kutosha lakini na mazingira lazima yawe yameandaliwa, sijui kama Sekta ya Mazingira wana *study* yoyote waliyotoa juu ya suala hilo la ufugaji wa samaki. Vilevile unatakiwa uwe na viwanda vya kuchakata hao samaki, huna. Unatakiwa uwe na *cold chain facilities* pamoja na *ice plant,* huna. Sasa hao samaki jamani wana mipango gani, watuoneshe hiyo mipango ambayo kweli wanayo kwa ajili ya huo ufugaji wa samaki. Hamna mipango yoyote na haimo humu, humu wameandika tu, wamekaa na wataalam kaandikiwa Waziri, wame-*copy* sijui mahali gani, wameweka, hakuna kitu, hiki hapa kitabu hakuna chochote ndani yake, hiyo ilikuwa hoja yangu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kuu inahusu uvuvi katika Bahari Kuu. Uvuvi katika Bahari Kuu, hicho nacho ni kichekesho cha mwaka. Kwanza nataka kujua, wametoa leseni ngapi kwa mwaka huu na meli ngapi zilizokuja kuvua katika Bahari Kuu na meli ngapi zilizokamatwa lakini na mapato. Nataka kujua katika Bahari Kuu mwaka 2016/2017 wamepata kiasi gani? Nilikuwa nikizungumza na Zanzibar Makao Makuu juu ya suala la mapato wakaniambia na ni uhakika, vinginevyo itakuwa wamefanya tofauti hawakuwaambia wenzenu wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2015/2016 fedha zilizopatikana katika uvuvi wa Bahari Kuu ilikuwa ni Dola za Kimarekani milioni 2.9 lakini mapato 2016/2017 yameshuka mpaka dola laki 6.9, mapato yameshuka. Watuambie kwa nini mapato yakashuka kwa kiwango hicho, ni kwa nini vinginevyo watakuwa wanafanya tofauti, Zanzibar hawajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu tatizo lenyewe hizo pesa zinagawiwa katika mafungu matatu; *50 percent* inakwenda kwenye mamlaka, asilimia 30 inakwenda kwa Jamhuri ya Muungano na asilimia 20 inakwenda Zanzibar. Sasa ukizigawa hizo pesa, dola 600,000 maana yake Mamlaka zinakwenda kama dola 300,000, ukija ukigawa *30 percent* maana yake zinakwenda kama dola 100,000 na kidogo Jamhuri ya Muungano, Zanzibar zinakwenda dola 60,000. Sasa niulize, jamani ni kweli wako *serious?* Mapato ya Bahari Kuu nchi inapata dola 100,000, sawasawa na msimamizi wa ghala la unga la Bakhresa? Nchi inapata dola 100,000 mapato ya Bahari Kuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sasa walipoona hilo hawaliwezi, wakaja tena na jambo la ajabu, wakaja kubadilisha *regulations.* Wanasema wanataka kubadilisha *regulations* kwenye sehemu za kodi lakini tuzungumzie kuhusu *bycatch,* tuzungumze pia na mabaharia. Hizo *regulations* ambazo wamebadilisha, wanataka sasa kwamba wale wavuvi wanaovua Bahari Kuu, zile meli zikishapata samaki wale *bycatch* eti ichukue ije iwauzie katika nchi husika. Sasa mtu anavua katika Bahari Kuu mbali huko aje na meli mpaka ufukweni ambapo hiyo bandari yenyewe huna kwanza lakini na hiyo gharama ya mafuta na mambo mengine atazipata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu uvuvi wa tuna ni uvuvi wa ndoano kwa hiyo haiwezekani. Halafu utajuaje kwamba wamepata *bycatch* wangapi, wala huna utafiti, wewe unaona meli ikiingia inakwenda kuvua utajuaje sasa, huwezi kujua. Kwanza nataka kujua ni meli ngapi zilizovua safari hii? Hizo meli zenyewe za kuvua hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unakwenda mbio, nizungumzie suala zima la meli za uvuvi. Tanzania imesajili meli za nje ambazo zinapeperusha Bendera ya Tanzania 407, 407 ukizitia pale Dar es Salaam pote pale baharini zikipeperusha Bendera ya Tanzania huwezi kuona kitu. Katika hizo meli 407, Waziri hajui meli za uvuvi zilizosajiliwa ni ngapi au Waziri atuambie meli za uvuvi zilizosajiliwa ambazo zinazopeperusha Bendera ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo yenyewe haikusajili Jamhuri ya Muungano wala Zanzibar haikusajili imesajiliwa na Kampuni ya *Feltex* iliyopo Dubai, kwa hiyo hajui. Pia hajui ana mabaharia wangapi anasema sasa, katika hizo kanuni wanazobadilisha wataingiza mabaharia katika meli ambazo zitakuja kuvua, nani unampa leseni halafu unamwekea masharti, haiwezekani. Hata hizo kanuni mnazozibadilisha ni kiini macho tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watafanya vilevile kama lilivyokuwa zao la ngozi, zao hilo tuliweka *20 percent* kodi kusafirisha nje, halafu tukaweka *40 percent* kodi kusafirisha nje, lakini viwanda hakuna. Mwisho mwaka 2012 tukaweka kodi asilimia 90 ambayo ngozi ikawa inasafirishwa kwa njia ya magendo kwa sababu hata ukiiacha hapa inaoza. Sasa ndiyo hilo wanalofanya wao, wataweka kodi kubwa, wataweka sheria nyingi, mapato hayo wanayoyapata, hiyo 100,000 watakuwa hawapati, hilo ndilo tatizo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisema asilimia 90 kama ya ngozi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, muda ndiyo huo. Tunaendelea na Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia dakika hizi mbili, tatu za mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ya kwangu ni ushauri. Kwanza napenda ni-*declare interest* kwamba katika fani ambazo nimezisomea ni pamoja na hii fani ya uvuvi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishauri Serikali yangu, nimshauri Mheshimiwa Rais na kwa kusema ukweli, Mheshimiwa Rais wetu nia yake ni njema sana. Nataka nimwambie kwamba kuna mapato makubwa sana kwenye uvuvi wa Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa dunia nzima inahamia kwenye jambo linaitwa *blue economy.* Naomba niitolee mfano Kisiwa kidogo cha Maldives ambacho kina wavuvi 8,139, sisi tuna wavuvi wadogo wadogo 203,000. Maldives ina vyombo vilivyosajiliwa vya kufanya uvuvi ambao wao wanategemea *spicies* moja tu ya samaki aina ya tuna, mwenzangu Mheshimiwa Ngwali ametoka kusema hapa, tena amesema kwa kufoka kwelikweli, sisi tuna vyombo vilivyosajiliwa vya maji baridi na maji chumvi zaidi ya 59,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ikiwekeza katika uvuvi, hasa huu wa Bahari Kuu ambao hatujautumia vyema mpaka hivi leo, nataka nikuhakikishie kwamba tutapata kipato kikubwa sana na inaweza ikawa ni sababu ya kuinua uchumi wetu na ajira za watu wetu kwa kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Mheshimiwa Rais katika mwaka mmoja huu na nusu amenunua ndege za kutosha na anaendelea kutuboreshea, tunajenga *SGR,* tunajenga *flyovers*, namwambia Mheshimiwa Dkt. Tizeba mwambie Rais wetu anunue meli ya uvuvi wa kisasa, wa kibiashara. Meli ambayo itachakata na itafanya na mambo mengine yote, utaona namna ambavyo *GDP* inayopatikana kutokana na uvuvi, Wabunge wote humu tutakuja kushuhudia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni huo, najua kwa kufanya hivyo, sisi watu wa Mkuranga tutapata sasa

matrekta tunayoyalilia. Maana Wilaya nzima ya Mkuranga haina trekta la Serikali hata moja, tuna matrekta 22 katika vijiji 125, yote ni ya watu na yote ni mabovu. Sasa katika uchumi wa namna hii tutapataje lakini tukienda katika *blue economy,* sisi tumesoma pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mwalimu wangu, Mheshimiwa Dkt. Sware yule pale na wapo Walimu wangu wengine wengi kule, akina Dkt. Tamatama Rashid na wengineo, hawajatumika ipasavyo katika *blue economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Mheshimiwa Dkt. Tizeba na kaka yangu Mheshimiwa Olenasha, mwambieni Mheshimiwa Rais tununue meli ya uvuvi hata moja tu ya Serikali, mtaona namna ambavyo uchumi wa nchi hii utakavyopanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii niliyopata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, ni ushauri tu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mchana ndiyo tunaishia hapo lakini niseme hivi, tumefanya vizuri lakini sio vizuri sana, bado tuna wachangiaji wengi. Kwa mchana, kwa sababu tuna dakika 40 tu nitacheza kidogo na utaratibu, dakika tanotano tu *no negotiation on it,.*

Mchana tutaanza na Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Maria Kangoye halafu tutakwenda kwenye upande wa CHADEMA, hao ndio wa kwanza. Nazitunza hizi karatasi ili kutenda haki. Mimi Meza sipendi sana kuingiliwaingiliwa. Wa CHADEMA watakaofuata watakuwa ni Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mheshimiwa Joyce Sokombi na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, hawa wamekubaliana dakika tanotano.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Naomba niwatangazie kwamba yamefanyika mabadiliko madogo kwenye ratiba ya Mkutano huu wa Bajeti unaoendelea kuanzia tarehe 25 Mei, 2017 hadi tarehe 2 Juni, 2017 kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi itawasilisha bajeti yake tarehe 25-26 Mei, 2017 badala ya tarehe 27-29 Mei, 2017 kama ilivyokuwa mwanzoni.

(ii) Wizara ya Nishati na Madini itawasilisha bajeti yake tarehe 29-30 Mei, 2017 badala ya tarehe 25-26 Mei, 2017 kama ilivyokuwa mwanzoni.

(iii) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itawasilisha bajeti yake tarehe 31 Mei, 2017 badala ya tarehe 30 Mei, 2017 kama ilivyokuwa mwanzoni.

(iv) Wizara ya Fedha na Mipango itawasilisha bajeti yake tarehe 1- 2 Juni, 2017 badala ya tarehe 31 Mei - 1 Juni, 2017.

Waheshimiwa Wabunge, ratiba mpya inayoonesha mabadiliko hayo itasambazwa kwenu hivi punde.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji, nilikuwa nimewataja wachangiaji wetu wa mwanzo Mheshimiwa Shally Raymond akifuatiwa na Mkeshimiwa Sikudhani Chikambo na Mheshimiwa Moshi Kakoso lakini dakika tano tano Waheshimiwa Wabunge naelewa muda, sina jinsi. Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Zaidi kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na sote tuko hapa tunazungumzia maendeleo ya nchi yetu. Sina budi pia kumpongeza Waziri

wa Wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa hotuba nzuri waliyotupatia. Shukurani zangu ziende kwa Mheshimiwa Rais kwa kuondoa tozo mbalimbali ambazo zilikuwa ni kero kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo kuna mambo manne ambayo ni muhimu, ardhi, unyevu, pembejeo na pia inabidi sasa nguvu kazi iwepo na nguvu kazi ni sisi. Nguvu kazi hiyo ipo katika matabaka mengi lakini nitazungumzia lile la chini ambalo ni wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo wadogo nchi hii wanajitahidi sana sana na wengi hapa ni watoto wa wakulima. Tumeona na tumekuwa kwenye kilimo lakini kuna kero ambayo haijawahi kupata ufumbuzi, ni kero ya masoko ya bidhaa zao na nitatoa mfano wa zao moja tu zao la mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu analima mahindi yake ili auze apate hela akafanye shughuli ambayo anataka yeye kulipa ada au kujenga nyumba na mengineyo, lakini siyo wakati wote ndiyo anataka hayo mahindi yafikie mpaka yakomae yakauke. Kwa mfano, mtu anategemea mvua mbili ikimpendeza Mungu, kuna vuli na masika. Wakati wa vuli anaweza akalima mahindi akaamua kuuza mahindi mabichi na mahindi mabichi haya ni mazuri. Katika hekari moja yanapatikana mahindi mabichi kama 45,000 mahindi haya akiuza hindi moja moja Sh.100 anapata Sh.4,500,000 lakini akilingoja hindi hili likakauka akaja kuuza anaweza akapata magunia 15 na labda akawa tu amepata Sh.700,500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililo hapa ni jinsi gani mtu huyu anakereka anapozuiwa kuuza mahindi mabichi. Wengi wenu hapa Waheshimiwa ni wateja au ni watu ambao wanafurahia mahindi wakati wanaelekea Dar es Salaam pale Dumila, Morogoro. Naiomba hii Wizara iwaache wakulima wauze mahindi yao pale ambapo wako tayari. Kwa nini nasema hivi? Wanaambiwa wasiuze, wanawekewa

doria na mageti mengi sana halafu unamnyima nguvu kwa sababu yeye anafanya kazi ili aweze kupata kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka hapo kwenye masoko baada ya ombi hilo ambalo najua watalifikiria Mheshimiwa Dkt. Tizeba yeye ni mtu mwenye uelewa mkubwa anaweza akaliwekea mikakati, naomba sasa nirudi pale kwenye kitabu chake kwenye ule ukurasa wake wa 14 na ule wa 110 anapozungumzia mitamba. Watu wengi ni wafugaji na baadhi ni *zero grazing.* Mifugo ninayoisikia inazungumziwa humu ndani ni yale makundi makubwa ya ng'ombe ya kuswaga. Mimi natoka eneo ambalo halina eneo kubwa, tunafuga ng'ombe mmoja, wawili lakini tunafuga kisayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri hii mitamba sasa tupatiwe kule Kilimanjaro tuweze kufuga kisasa. Mitamba hii ikishakuwepo ndani ya nyumba inatupatia mbolea, mbolea hii ndiyo inakuwa kwa ajili ya migomba na kahawa. Hiyo inakuwa kama mgonjwa na uji, migomba mizuri isipopata samadi haiendi. Kwa hiyo, naomba awamu hiyo inayokuja au popote anapoweza kunisaidia niweze kuwapelekea wale wanawake wangu wa Kilimanjaro wafuge kisasa na pia tupate maziwa tutakayopeleka kwenye viwanda, maziwa toshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nienda haraka haraka kwenye ufugaji wa nyuki. Mimi mpaka sasa hivi ukiniuliza nyuki ziko kwenye Misitu au Kilimo sijui lakini naomba leo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa na nyuki hao utawaona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Maria Kangoye wajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii ya mimi kuungana na wachangiaji wenzangu katika kuchangia Wizara hii ya Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema. Sambamba na kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba sana nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujali muda naomba niende moja kwa moja ukurasa wa 22. Katika ukurasa huu Wizara imeendelea kuhimiza matumizi bora ya mfumo wa stakabadhi ghalani. Naomba nimpongeze sana Waziri na naweza nikasema kwamba Waziri Mheshimiwa Dkt. Tizeba amekuja na mguu mzuri kwenye Wizara hii kwa sababu miongoni mwa watu ambao wamenufaika na mfumo huu wa stakabadhi ghalani ni sisi wakulima wa korosho wa Mkoa wa Ruvuma na hususani wa Wilaya ya Tunduru na Namtumbo tumefaidika sana kupitia mfumo huu wa stakabadhi ghalani na ni imani yangu kwamba kupitia mfumo huu utawezesha sana kuwasaidia wakulima wa korosho katika maeneo yote ambayo tunalima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa rahisi kuukubali mfumo huu kwa sababu kumbukumbu zangu zinaonesha mwaka 2011/2012 wakulima wa korosho Wilayani Tunduru na maeneo mengine tulitumia mfumo huu lakini mpaka hivi tunavyozungumza wakulima wale hawakupata pesa zao bado wanadai. Kwa hiyo, haikuwa rahisi kuukubali mfumo huu kutokana na hizo changamoto ambazo zimejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kwa nafasi ya pekee sana naomba sana nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na watendaji wake kwa hakika walijitahidi sana kuelimisha wananchi hatimaye waliendelea kuelewa mfumo huu na hivi sasa tunavyozungumza naomba niseme kwamba umeleta tija sana kwa wananchi wetu na mimi ni miongoni mwa waumini wa mfumo huu nitaendelea kuhamasisha kama kiongozi kuhakikisha mfumo huu unaendelea kuleta tija kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tulikuwa na kikao cha wadau, kupitia kile kikao cha wadau kumetolewa tamko la kugawa *sulphur* bure. Ni jambo jema na ni jambo lenye tija lakini naomba Waziri alete mchanganuo na vigezo ambavyo vitatumika katika kutoa *sulphur.* Kwa kuwa jambo hili lina tija lisije likaleta migogoro baadaye. Hivi tunavyozungumza wako wakulima kwenye mashamba yao wanatumia kuanzia mifuko 10, 20 na zaidi sasa tulipotangaza *sulphur* bure inawezekana watu wakabweteka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Wizara inayohusika ikatoa mwongozo mapema kujua vigezo ambavyo vitatumika katika kutoa hiyo *sulphur.* Niliomba nisisitize hili na nilisisitize sana kwa sababu linagusa wananchi. Kama hiyo haitoshi naendelea kusisitiza kwa sababu wako wafanyabiashara ambao wamekuwa wakileta *sulphur* kutoka nje ya nchi kuwauzia wakulima wetu sasa wasije wakabweteka kwa kuamini kwamba Serikali sasa itatoa *sulphur* bure na wale wasilete *sulphur* matokeo yake tena badala ya kuimarisha zao la korosho tukaliletea tena matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha basi ni vizuri aeleze ili wananchi wale ajue kwamba mfumo na vigezo vitakavyotumika katika kutoa *sulphur* bure. Ni jambo jema, binafsi napongeza Serikali yangu na kwa kuwa Serikali hii ikitamka inatekeleza naamini itatekeleza lakini ni vizuri iweke mchanganuo watu wajue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la tozo. Binafsi naomba nipongeze sana. Tunapozungumzia hizi tozo moja kwa moja zilikuwa zinagusa wakulima wetu. Tunapopunguza hizi tozo maana yake tunapunguza mzigo kwa wakulima wetu, naipongeza Serikali na naomba niendelee kusema kwamba hata kama kuna tozo zile zingine ambazo zinaleta ukakasi kwa wananchi wetu basi waziondoe ili mazao yetu haya yaendelee kuwa na faida, kwa mazao yote kwenye korosho, kahawa na mazao mengine yote. Kama kuna tozo zile ambazo zinaleta kero kwa wananchi wetu basi ziondolewe ili kuleta faida ya kilimo bora kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la uvuvi. Kwenye eneo hili la uvuvi naomba nizungumzie Wilaya ya Nyasa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Kakoso na Mheshimiwa Maria Kangoye ajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote, niipongeze sana Serikali kwa kuja na mfumo mpya wa uagizaji mbolea. Eneo hili nawapongeza sana kwa sababu ndiyo eneo ambalo litawasaidia sana wakulima wa nchi hii ili kuepukana na mfumo uliokuwepo zamani uliokuwa unawanufaisha wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niiombe Serikali isirudi nyuma na nimwombe Waziri, najua anafanya kazi ambayo itakuwa ngumu sana, wapo watu ambao walikuwa wananufaika na biashara hii kwa hiyo ni vizuri wakajipanga wasirudi nyuma. Naamini kuleta mbolea kwa pamoja litapunguza gharama kubwa sana ya bei ya pembejeo na

pale ambapo atakuwa amekwama zaidi tutahitaji sana kumsaidia ili tuweze kusonga mbele na kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili nashauri, hata zile mbolea za *NPK, KANI* na *SA* zina uwezekano kabisa wa kuweza kuisimamia Serikali ikaweza kuagiza mbolea hizi, upo uwezekano. Naamini tu tukifanya jitihada za pamoja wakishirikisha na wadau wataweza kusaidia zoezi hili likakamilika na likawasaidia wananchi wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la tozo ambalo limeletwa na Serikali. Tunaipongeza sana Serikali imetengeneza mazingira mazuri ya kuboresha mazao karibu yote kwa kupunguza zile tozo ambazo zilikuwa ni kero kwa wakulima wetu. Kuna maeneo ambayo zipo tozo zimeelekezwa hasa kwenye vyama vya ushirika, ni vyema wakaziangalia kwa undani zaidi tozo hizo kwani kuna baadhi ya maeneo wanaweza wakaviua vyama vya ushirika, vyama vya ushirika vinategemea sana tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa umahiri alionao Waziri atawashirikisha wadau kabla ya utekelezaji ili waangalie vile vyama visije vikafa kwa sababu ukiua vyama vya ushirika havina nafasi ya kuweza kushindana na makampuni. Vyama vya ushirika pekee ndivyo ambavyo vikiungana vina nafasi ya kuweza kutoa ushindani kwa haya makampuni ambayo yananufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zipo tozo ambazo zimeonesha wazi kwamba zinayasaidia makampuni ili yapunguze gharama sasa naomba Waziri aangalie tozo zile. Tunaweza tukatoa hizi tozo zikawasaidia makampuni moja kwa moja bila kwenda kwa mkulima. Ni vyema wakaangalia na wakachambua zile tozo mbalimbali ili zingine ziwarudie wananchi na kufanya zao liweze kuwa na bei nzuri kuliko tukitoa tu nafuu ni ya kuyabeba sana makampuni. Niombe

sana hili waliangalie na naamini wataalam waliopo watasaidia kuchambua zile tozo ili ziweze kusaidia wananchi kama Serikali ilivyokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye sekta ya uvuvi, kwangu kuna Ziwa Tanganyika ambalo kimsingi bado sekta hii haijafanya kazi vizuri sana. Tunaiomba Serikali iwasaidie wale wavuvi wa wadogo wadogo iwape mazingira ambayo yatawawezesha kufanya shughuli zao za uvuvi bila kupata shida. Ni vizuri tukaangalia vile vikundi vya wavuvi vikasaidiwa na Serikali ili viweze kutengeneza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie Mkoa wa Katavi hasa Wilaya yangu ya Tanganyika tulileta maombi maalum ya kulima zao la pamba. Tayari wakulima walishafanya jitihada zao, wameonesha nia njema na nimshukuru alinipa ushirikiano na kuagiza wataalam wakaenda kuangalia jitihada ambazo zimefanywa kule. Kwa hiyo, nina imani eneo hilo tunahitaji kibali tu kwa msimu ujao ili wakulima wale waliojipanga waweze kulima lile zao liwasaidie na kuongeza kipato kwani watakaponufaika kwenye eneo hili litawasaidia sana kwa Serikali na wananchi kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado kuna dakika moja, naomba niongelee sana miradi ya uwamgiliaji. Nchi yetu ili iweze kwenda inahitaji sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Maria Kangoye atafuatiwa na Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nianze kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba nzuri yenye malengo ya kuinua uchumi wa nchi yetu kupitia kilimo, uvuvi na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Kama tunavyofahamu kilimo kimeajiri takribani asilimia 75 ya wananchi lakini kimeweza kuzalisha chakula *almost* asilimia 100 ambacho kinatumiwa na wananchi wa nchi yetu hii na kuzalisha malighafi nyingi kwa ajili ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo bado Serikali imeendelea kutenga fedha kidogo kwa ajili ya Wizara hii ya Kilimo tena kinyume kabisa na Azimio la Maputo ambalo linahitaji Serikali kutenga asilimia 10 ya bajeti yake kwa ajili ya kilimo. Ni wakati sasa wa Serikali kuhakikisha kwamba inalifanyia kazi azimio hili kama kweli tunataka kuijenga Tanzania, hatutaweza kuijenga bila kuendeleza sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze sasa kuchangia changamoto za masuala ya Wizara hii ndani ya Mkoa wangu wa Mwanza, nitajikita sana katika masuala ya uvuvi. Kumekuwa na malalamiko mengi kwa miaka mingi kutoka kwa wavuvi ambao wanavua katika Ziwa Victoria na wapo baadhi ya wenzangu ambao tayari wameshatangulia wameliongelea hili lakini jinsi lilivyo nyeti suala hili na mimi nitaendelea kuliongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wote mnavyofahamu kuwa mimi ni mwakilishi wa vijana, tena ninayetokana na Mkoa wa Mwanza, ambapo vijana wengi wamejiajiri na kuajiriwa katika sekta ya uvuvi. Hata pale ambapo kunatokea na migomo mbalimbali ya uvuvi lazima vijana hawa wanaathirika kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, uvuvi katika Ziwa Viktoria una manufaa makubwa kwa wakazi wa Kanda ya Ziwa na Taifa kwa ujumla kwa sababu kuna mlolongo wa wafanyabiashara wengi ambao wananufaika kutokana na uvuvi huo. Wapo akinamama ambao wanakaanga na kuuza samaki katika vijiwe mbalimbali; wapo ambao vijana ambao wameajiriwa katika viwanda vya samaki na katika mialo ya samaki; wapo wafanyabishara wanaosafirisha

samaki ndani na nje ya nchi; wapo watu ambao kazi yao ni kusafisha tu samaki hawa; wapo wafanyabiashara pia ambao wamenufaika kwa namna mbalimbali kutokana na uvuvi huu wa Ziwa Viktoria na pia wapo mamilioni ya Watanzania wanaotegemea kupata kitoweo kutoka katika ziwa hilo na kupata virutubisho kwa ajili ya kujenga afya yao. Hao ni baadhi tu ya wanufaika wa uvuvi wa Ziwa Viktoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, unapotengeneza mazingira magumu kwa mvuvi wa Ziwa Viktoria ujue ni namna gani unavyoathiri uchumi wa nchi. Wavuvi hawa hawa wamekuwa wakishirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama katika kuwabaini wale ambao wanavua kwa njia haramu. Hivyo basi wana haki ya kusikilizwa mahitaji yao kwa sababu yamekuwa ni ya muda mrefu na naamini kabisa pale Serikali itakapoamua inaweza kuyatatua matatizo haya na yakafika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hawa mara nyingi wamekuwa wakiomba kuruhusiwa kuuza samaki tofauti na bondo. Mabondo yamekuwa ni gharama kuliko hata mnofu wa sangara. Leo hii mvuvi analazimika kuuza samaki pamoja na bondo lake ina maana yule anayenunua ndiyo ananufaika zaidi, wakati wao ndio wanaotoa jasho. Niombe Serikali iweze kuliangalia suala hili, nafahamu ina wataalam wengi ambao wanaweza wakakaa wakamshauri Waziri pamoja na Naibu wake wapate kuliangalia hili na namna gani wavuvi hawa wanaweza kunufaika kutokana na hayo mabondo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mara nyingi wamekuwa wakiomba kuondolewa vikwazo vya kuuza samaki mbichi mzima katika masoko ya nje ya nchi. Wapo wavuvi wakubwa na wadogo, lakini wapo wale ambao wanaweza kusindikika na kupaki, ifike wakati sasa Serikali ione...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Julius Laizer na Mheshimiwa Joseph Mkundi ajiandae.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii iliyopo mbele yetu ambayo kimsingi wote tunakubaliana kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Nataka nihoji kwa sababu katika mijadala mingi tumekuwa na hoja inayozungumzwa kwamba Serikali ina dhamira njema ya kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuhoji kwamba dhamira ya kweli ya Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi katika suala la kilimo na mifugo ipo wapi katika bajeti hii? Hivi dhamira ya kweli ya Serikali ni ya kutoa asimilia tatu ya bajeti yake kwa ajili ya sekta ambayo ni Uti wa Mgongo wa Watanzania? Tunataka Serikali ituambie kama asilimia 80 au 70 ya Watanzania ni wakulima na wafugaji, dhamira ya Serikali katika kuwasaidia wakulima na wafugaji hawa iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshangaa katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri huku wameweka ng’ombe huku mbele na samaki, huku nyuma wameweka kilimo ambacho kinaonesha mazao ya wananchi. Wao wamechangia nini, kwa nini wanajisifu kwa kitu ambacho hawachangii chochote katika kuwanufaisha Watanzania? Nini mmechangia katika mifugo wanaiweka huku wanaona imenawiri sana, nini wanachangia katika kilimo hiki wanachoona mazao yamenawiri sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Wizara ituambie hizi picha walizotumia kwenye kitabu hiki *copy right* yake iko wapi wakati hawachangii chochote, wanatenga bilioni 100 lakini mnapeleka bilioni tatu. Dhamira yao haiwasuti,

wanachukua picha ya ng'ombe zetu wanaweka kwenye kitabu chao lakini Wizara hii hawachangii chochote katika kusaidia maisha ya wananchi, hatukubaliani nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili tunataka dhamira ya Serikali katika hili ionekane katika matendo ya kweli, kama dhamira haionekani katika matendo dhamira hiyo imekufa. Katika hili dhamira imekufa kwa sababu hakuna chochote ambacho Wizara imefanya, nchi hii inaongoza kwa mito na maziwa lakini hakuna hata mradi mmoja wa mfano Wizara imeanzisha kwa ajili ya kuonyesha kilimo cha mfano kwa Watanzania. Sasa wanajisifu nini kama Wizara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wizara hii inaendelea kukubaliana na utekaji na uuzaji wa mifugo ya wafugaji ambao peke yake katika Wizara hii ndiyo mifugo inauzwa hata bila ya hukumu ya mahakama. Ni mahali ambapo Wizara ya Maliasili inanyanyuka inauza ng'ombe inavyotaka. Ni wapi umeona kwenye nchi hii mali za watu zinataifishwa bila mahakama kutoa hukumu, Wizara imenyamaza. Wizara hii haioneshi ni namna gani inawasaidia wafugaji kuondokana na matatizo yanayowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi mnasema ni uti wa mgongo lakini wameitenga Wizara ya Maji na Mifugo katika bajeti hii hapa. Nataka nishauri Serikali, suala la maji kwa maana ya umwagiliaji lihamishwe kutoka Wizara ya Maji lipelekwe kwenye Wizara ya Kilimo na Mifugo kwa sababu huwezi kuendesha kilimo wala mifugo bila kuwa na maji ya uhakika. Tusipofanya hivyo, tutaona bajeti ya Wizara ya Maji inakuwa kubwa lakini Wizara hii ya Mifugo na Kilimo haitakuwa na chochote na wao hawatatekeleza miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapata kigugumizi gani kuhamisha suala la umwagiliaji ikapeleka kwenye Wizara inayohusika na kilimo ili angalau tuwe na miradi michache kwenye Ziwa Tanganyika, Ziwa Viktoria ili angalau tuwe na miradi michache tunayosema kama nchi tumeweza kuzalisha. Ni nchi pekee tuna maziwa makubwa lakini

kiangazi cha miezi miwili tu, mitatu nchi tunalia njaa halafu tunasema kwamba tufanye kazi, kazi ipi ambayo tunafanya kama Serikali haisaidii wananchi wake kuondokana na matatizo tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka niishauri Serikali, kumekuwa na tatizo la muda mrefu kati ya wafugaji na wanyamapori lakini wameanzisha na zoezi la kuweka ng'ombe chapa. Ili waweze kufanikisha zoezi hili ni muhimu kuweka miundombinu ya maji katika maeneo ya wafugaji. Kama hawajaweka miundombinu mifugo itahama tu na kama itahama wataishia kutunyanyasa na kutunyang'anya mifugo yetu yote. Nataka niwaambie hawatakuwa wamewasaidia wafugaji ambao wameonekana kama kundi ambalo halina haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba hili suala la kuweka ng'ombe chapa lisimame mpaka Serikali itakaposema ni kwa namna gani imeboresha mazingira katika maeneo haya ambayo wanataka mifugo iwepo. Huwezi kuniambia nichunge ng'ombe mahali ambapo hakuna maji. Bahati nzuri Naibu Waziri naye ni mfugaji, hivi anavyosema aweke chapa ng'ombe kule Ngorongoro wakati hajaweka masuala ya maji katika eneo hilo anategemea wale wapiga kura wake waende wapi? Nataka yeye mwenyewe awe mfano kwa kuisaidia Serikali kuona kwamba hawezi kutenga eneo la mifugo bila kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma za maji na majosho katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho, kwa nini sekta ya mifugo haina ruzuku.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Sokombi ajiandae.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza niunge mkono wale wote walioonesha *concern* ya bajeti ndogo ya Wizara hii ya Kilimo. Tukizingatia umuhimu wa kilimo na namna tunavyoelekea kwenye uchumi wa viwanda kwenye nchi yetu, sekta ya kilimo ni muhimu sana kwa ajili ya uzalishaji wa mali ghafi lakini ajira na kutengeneza kipato kwa wananchi wetu ili waweze kununua bidhaa zitakazozalishwa na viwanda hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunapofikiria kuingia kwenye uchumi wa viwanda ni muhimu sana tukaimarisha kilimo chetu kuwa kilimo cha kisasa zaidi na hasa kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunaweza kuwekeza vizuri kwenye kilimo cha umwagiliaji kama tutazingatia rasilimali tulizonazo kwenye maeneo yenye *resources* kama maji, kwa mfano kwenye maeneo ya Ziwa Viktoria hususani eneo la Ukerewe kidogo inaleta shida kwenye eneo kama Ukerewe ambalo limezungukwa na maji wananchi wa Ukerewe kulalamika kutokuwa na chakula cha kutosha. Tuna maeneo ya kutosha ambayo Serikali inaweza kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji tukazalisha chakula cha kutosha tukaweza kukabiliana na hali tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nitake tu kujua kuna Mradi wa Kilimo wa Umwagiliaji kwenye Bonde la Miyogwezi na Bugolola. Kwenye bonde la Miyogwezi iliwekezwa zaidi ya shilingi milioni 600 na Serikali lakini pesa ile imewekwa pale ule mradi haukuendelea, lakini kama Serikali ingeweka mkazo ikaweka pesa nyingine ya kutosha mradi ule ukaanza kufanya kazi, kusingekuwa na tatizo la chakula kwenye eneo la Ukerewe, inawezekana wangeweza kutoa chakula zaidi nje ya eneo la Ukerewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kufanya vizuri kama hatuwekezi kwenye utafiti kwenye eneo la kilimo. Ni vizuri sana tukawekeza kiasi cha kutosha cha pesa kwenye utafiti, kutambua kwamba changamoto zinazokabili maeneo yetu hususani kwenye udongo tulionao ni zipi, ni

mbegu zipi tunaweza kutumia ili tuweze kutoa mazao ya kutosha yanayoweza kutusaidia kuhimili changamoto tulizonazo za chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni uvuvi. Uvuvi kwenye eneo la Ziwa Viktoria ni muhimu sana na kimsingi kama Taifa uvuvi unachangia sehemu kubwa sana ya pato la wananchi wetu. Kwenye maeneo ya ziwa kwa mfano Ziwa Viktoria, sehemu kubwa ya vijana kwenye Mikoa ya Kanda ya Ziwa wanapata riziki yao na kuchangia kwenye uchumi wa nchi hii kupitia ziwa hili lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana kwenye sekta ya uvuvi hususani kwenye Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kutoka kwenye Wizara ni kwa nini wavuvi wetu hawafikiriwi sana kupata mikopo. Kuna Benki ya Wakulima, ni namna gani inawasaidia wavuvi? Kwa sababu wavuvi hawa kama watapata mikopo, itawawezesha kufanya shughuli zao katika mazingira mazuri na kuweza kutengeneza ajira nyingi zaidi lakini sioni kama benki hii ina msaada kwa wavuvi wetu. Hata taasisi nyingine za kifedha ni namna gani wavuvi hawa wanaweza kupata mikopo kupitia rasilimali walizonazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya sana katika mazingira yalivyo sasa wavuvi hawawezi hata kutumia rasilimali walizonazo kama dhamana kuweza kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha. Niiombe Serikali ione umuhimu wa kuwajengea mazingira mazuri wavuvi wetu kupata mikopo ili watengeneze mitaji yao kuwa imara zaidi na kuzalisha ajira nyingi lakini na kutengeneza uzalishaji mkubwa wa mazao ya ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto nyingi sana ambazo ningependa Serikali iweze kuzifanyia kazi. Nashukuru kwamba Serikali imeanza kuona matatizo ya tozo zilizopo kwa wavuvi lakini bado kuna tatizo kubwa la tozo nyingi kwa wavuvi wetu. Niombe Serikali iendelee kulifanyia kazi, kwa mfano, kuna tozo za *SUMATRA*, leseni za uvuvi na tozo za kupaki.

Ningeomba Wizara inieleze hivi inakuwaje mimi ninayemiliki gari naweza kuchukua leseni na bado nikafanya shughuli zangu na gari langu kwenye maeneo yote Tanzania nzima lakini mvuvi anapokuwa na leseni ya uvuvi akitoka Halmashauri moja kwenda nyingine analipa tena leseni nyingine ya uvuvi, akitoka Halmashauri hiyo akienda Halmashauri analipa tena leseni ya uvuvi ni kwa nini kuwa na matatizo haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mazingira ya uvuvi yanabadilika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mkundi. Tunaendelea na Mheshimiwa Sokombi, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Khadija Aboud wajiandae.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii nami nichangie Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Jambo la kwanza naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sekta kubwa ya ajira hapa nchini kwetu maana inaajiri takribani asilimia 70 ya Watanzania. Wizara hii hii ndiyo yenye kauli mbiu nyingi tulianza na kauli mbiu ya Baba wa Taifa ya Siasa ni Kilimo, ikaja Kilimo cha Kufa na Kupona cha Mheshimiwa Alhaji Ali Hassan Mwinyi, ikaja Kilimo Kwanza cha Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema siasa ni kilimo maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba kilimo kinagusa maisha ya kila mwananchi, kilimo kinagusa maisha ya kila Mtanzania lakini kilimo hiki hakijamkomboa Mtanzania huyu. Kwa mfano, katika Mkoa wa Mara, enzi za zamani nilipokuwa naenda kijijini kwetu Kabulabula wazee walikuwa wanalima sana pamba na ilikuwa inastawi kwa asilimia kubwa sana na ndiyo maana Mkoa wa Mara ulikuwa una

viwanda vingi sana na mazao mengine kama mihogo na viazi vilikuwa vinashamiri sana, lakini sasa hivi wakulima hawa wanahangaika kutokana na uhaba wa mazao haya hayapati rutuba na hayakui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze hizi mbegu wanazozileta sasa hivi ni mbegu za aina gani, maana hazikui na zao la pamba limekufa katika Mkoa wa Mara halistawi tena. Mazao ya mihogo zao hili limekufa ni tofauti kabisa maana unapopanda mihogo inapokaa kidogo tu inapata ugonjwa wa ukungu, sasa sielewi hii mihogo inapopata ukungu tatizo ni kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mara ni Mkoa ambao ulikuwa unategemea kwa kiasi kikubwa kilimo lakini kilimo hiki kinasuasua. Naomba Waziri atakapokuja atueleze ni mbadala wa mbegu zitakazoletwa katika Mkoa wa Mara ili watakapokuwa wanalima kama ni mazao ya pamba, mihogo na viazi vistawi kama vilivyokuwa vinaota zamani. Kwa sababu sasa hivi mkulima akipanda mbegu ya pamba kama ni heka tano, matokeo ya lile zao uvunaji wake ni kama heka moja tu. Tunaona ni namna gani zao la pamba linavyodidimia kutokana na uhaba au ubovu wa mbegu ambazo si stahili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Aboud ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kuweza kuchangia Wizara hii ya Kilimo. Nimesimama kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kila mtu hapa anafahamu Mkoa wa Mbeya ni mkoa ambao unaweza ukalisha nchi hii vizuri lakini bado nashangaa kwa nini Serikali haitaki kuwekeza zaidi katika mkoa huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda hasa kwa kuchambua Mkoa wa Mbeya nitazungumzia Wilaya ya Kyela. Wilaya ya Kyela ina mambo mengi ambayo yanaweza kulisaidia Taifa hili. Tunafahamu Ziwa Nyasa linatoa samaki wa aina nyingi ambapo kama tukiwekeza katika lile ziwa tunaweza tukasafirisha samaki katika nchi yetu wenyewe lakini katika soko la Afrika Mashariki. Tunafahamu Kyela kunapatikana *cocoa*, Mheshimiwa Waziri anapokuja kuhitimisha hotuba yake atuambie ni nguvu gani amewekeza katika zao la *cocoa*. Tunajua *cocoa* inanunulika sana katika soko la dunia lakini mwananchi wa Kyela amefaidikaje na zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye mpunga, Wabunge mnafahamu kuna mahali mpaka tunadanganywa mpunga wa Kyela, kwa nini tusiwekeze katika mpunga huu kama unapendwa na una soko zuri kuweza kusaidia wale wakulima wadogo wadogo ambao pia wengi wao ni wanawake tukaweza tukapata zao hilo na faida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua hii Benki ya Kilimo kwa nini isiende kusaidia wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Wananchi wanapolima tatizo kubwa tunaona ni mitaji, twende mahali tuachane na kilimo cha jembe, tunahitaji kilimo cha kibiashara ili kuweza kumkwamua mwananchi katika kujiendeleza maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Benki ya Kilimo, najua ipo Dar es Salaam sijui kama ina matawi, kama ina matawi hayafanyi kazi, ukienda huko kwetu Rugwe, Kyela, Mbarali hakuna mwananchi anayeijua na wala hata kupata maelezo ya benki hii ikaweza kuwasaidia hawa wananchi. Naomba Wizara ichukue juhudi za makusudi kusaidia wanawake na wananchi wa Mkoa wa Mbeya waweze kujua maana ya kuwa na Benki ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia pembejeo. Pembejeo imekuwa ni tatizo kubwa sana katika Mkoa wa Mbeya. Kwanza haziji kwa wakati, pili nyingi ni feki,

hata hatujaelewa Serikali imechukua hatua gani kwa wale walioleta pembejeo zisizofaa. Naomba kwa bajeti ya mwaka huu pembejeo zifike kwa wakati na zilizo bora kwa sababu hata Wabunge wenzangu wamelalamika mazao hayatoki mengi ni kwa sababu mbegu hizi si bora na hata hizi mbolea zinazokuja si sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Wizara isimamie na ituambie inafanyaje na kama inaweza ikabadilisha mtindo ambao unatumika sasa wa ugawaji wa pembejeo kwa sababu wachache wananufaika na wakulima wanaingia kwenye nafasi ambayo haziwafikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia suala la chai, nimezungumza mara nyingi katika Bunge lako Tukufu nikilalamika juu ya wakulima wa chai wadogo wanavyolalamika chai isivyowasaidia wao kama wakulima. Ni watu wachache sana wananufaika na zao la chai, mwananchi wa kawaida chai bado iko chini wakati chai inauzwa bei nzuri soko la dunia lakini sisi wenyewe Tanzania tunahitaji kunywa chai kwa nini chai isimnufaishe mkulima wa Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia mazao, Mbeya ina mazao mengi sana. Sisi sote tunafahamu unapotaka kupata karoti unapata Mbeya, unapata viazi lakini linakuja tatizo kwenye soko, bei ya mkulima ni ndogo anayefaidika ni mtu wa katikati ambaye ni dalali. Tunawezaje kusaidia wakulima wakauza mazao yao kwa bei ambayo ni nzuri. Mwananchi wa kawaida anahangaika kulima mwisho wa siku anauza gunia la viazi Sh.25,000, Sh.20,000 au Sh.30,000 lakini ukija Dar es Salam gunia hilo hilo linauzwa kwa Sh.150,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inamsaidiaje mwananchi huyu aweze kuuza kwa bei kubwa na tunajua kabisa mpaka sasa kuna watu wanatoka Kenya wanakuja huku kwenye masoko yetu na mashamba yetu bado

wananunua kwa bei ndogo. Tunahitaji wateja waje lakini Serikali inawabanaje wanunue kwa bei inayomnufaisha mkulima wa kawaida?

Tunapozungumzia kilimo tunahitaji kuwekeza kwenye kilimo kweli kweli wala si katika maneno. Tunapozungumzia mpunga, tumezungumzia mpunga wa Kyela ulivyo mzuri lakini tuna Mbarali, Mbarali kuna shamba kubwa sana la mpunga lakini je Serikali imewasaidiaje wale wakulima wa Mbarali, imesaidiaje wale wakulima....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Aboud na Mheshimiwa Fredy Mwakibete ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Naanza na *NFRA*. Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo hayatabiriki naomba sasa hii *NFRA* iongezewe nguvu, iongezewe fedha ili kwanza iweze kununua mazao ya kutosha na kwa wakati na kwa bei muafaka. Pili iongezewe fedha ili tuweze kuhifadhi mazao yetu kwa njia za kisasa zaidi na tuepukane na ile kuhifadhi katika maghala twende kisasa zaidi ambapo mazao yetu yatakaa kwa muda mrefu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu ukulima na ufugaji unaohifadhi mazingira. Nashauri Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Maji hawa wafugaji ambao wana mifugo mingi wahamasishwe na wapewe elimu ya kuhifadhi maji ya mvua kwa ajili ya mifugo yao huko wanakoishi. Katika ukulima nashauri Serikali ihimize zaidi hasa wale wanunuzi wakubwa mfano wa tumbaku, waje na yale majiko ya kisasa ya kukaushia tumbaku ili kuepusha ukataji wa miti yetu kiholela ambayo inatumika kukaushia tumbaku. Naomba yale majiko ya tumbaku yapewe hamasa zaidi ili yatumike tumbaku yetu ikaushwe kwa majiko ambayo hayahitaji kukata miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza uvuvi wa bahari kuu kwa Serikali kuamua kwa makusudi kujenga au kuendeleza gati namba sita na gati namba tatu ya kule Zanzibar kwa ajili ya kupokea na kuhifadhi samaki wa bahari kuu. Naomba hili Serikali ilitilie mkazo, hizo bandari zimalizike kwa haraka ili nchi yetu iweze kupata mapato ya fedha za kigeni na ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba Serikali yetu ina dhamira ya dhati kabisa katika kumsaidia mkulima na mvuvi wa Tanzania. Kwa maana hiyo kwa makusudi imeondoa tozo mbalimbali na kodi mbalimbali zitakazomsaidia mvuvi na mkulima. Dhamira nyingine ya dhati ni kuweka ununuzi wa pamoja wa mbolea, hizi zote ni mojawapo ya dhamira za dhati za kuwasaidia wakulima wetu na mvuvi ili waondokane na tabu ndogo ndogo zinazowakabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na naipongeza Wizara kwa marekebisho ya baadhi ya kanuni za mamlaka katika uvuvi wa bahari kuu. Naomba Kanuni hizi zitumike kwa haraka ipasavyo ili ziweze kutuletea mapato katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongeza kwenye Benki ya Kilimo, nashauri benki hii iongezewe mtaji ili iweze kusaidia wananchi kulima ikiwemo kuhamasisha vikundi vidogo vidogo vya vijana na wanawake kuwapa mkopo ili Wizara ya Kilimo itoe utaalam wa ukulima na utengenezaji wa mbegu bora ili wananchi wetu wapate mbegu bora ambazo zitaendana na soko, uchumi wa kati na uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Fredy Mwakibete na Mheshimiwa Bashe ajiandae.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Wizara hii ndiyo utii wa mgongo wa nchi yetu ya Tanzania lakini niwashukuru sana na kuwapongeza Mawaziri wote wawili mara nyingi sana nikiwa na changamoto huwa nawaona, Naibu Waziri amekuwa akinisaidia na Waziri amekuwa akinisaidia, kwa hiyo nawapongeza sana. Niwapongeze kipekee zaidi baada ya kutoa tozo katika mazao mbalimbali ambazo wakulima ilikuwa ni shida na changamoto kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri mchache kwa Serikali hasa tukianza na Jimbo langu la Busokelo ambako mara nyingi sana tunazalisha lita za maziwa zaidi ya 30,000,000 kwa mwaka lakini yanaharibika kabla hayajafika kiwandani kwa sababu hatuna kiwanda katika Halmashauri ya Busokelo. Tumejitahidi kujenga lakini tumeshindwa, tunaomba Serikali iweze kutusaidia katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu tunazalisha pia ama tunalima viazi mviringo, viazi vitamu, ndizi kwa wingi, mpunga na mazao mengine mbalimbali na hayo yote yanashindwa kufika sokoni kwa sababu ya miundombinu ambayo haiko rafiki kwetu. Kwa hiyo, tunaomba kama itawezekana kuanzishwa kwa viwanda vidogo vidogo katika maeneo yale kwa kuwa ninyi watu wa kilimo ndio wenyewe kwa sababu ninyi ndio mnaosimamia sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tozo ambazo zimetolewa hasa katika zao la chai. Zao la chai sisi ni wakulima wakubwa katika nchi hii ya Tanzania katika Wilaya ya Rungwe. Kuna hii tozo ambayo inaitwa gharama za uendeshaji wa vyama vya wakulima nafikiri kwa *typing error* imeandikwa ni Sh.5 lakini tozo hii ni Sh.9.50, ningeishauri Serikali isiiondoe kwa sababu kwanza hivi vyama ni vichanga na Serikali inahubiri habari ya ushirika. Sasa wakishawaondolea hawa maana yake watatawanyika kabisa hawatakuwa na

nguvu yoyote ya kuweza kusimama na kulisimamia zao hili la chai, kuna kodi nyingi ambazo ningeshauri huko ndiko wangeweza kuondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, zao la *cocoa* pia tunalima kule lakini hapa sijaona hata kidogo kutamkwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Naomba pia walizingatie kwa sababu ni muhimu na linaingiza fedha nyingi za kigeni kwa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pembejeo limekuwa likizungumzwa lakini nipongeze Serikali kwa sababu tumeamua kwamba ziletwe kwa *bulk procurement*. Wazo langu na ombi langu kwa Serikali kwamba katika nchi ya Tanzania kila sehemu tunazalisha ila kwa bahati mbaya majira yanatofautiana. Kwa hiyo, hata kama watanunua hizo pembejeo basi ziende kwa majira husika katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la TEHAMA na kilimo. TEHAMA na kilimo kwa nchi ambazo zimekomboka limekuwa ni msaada mkubwa sana katika nchi hizo. Hii TEHAMA itumike vizuri katika kuendeleza mazao mbalimbali nchini si kilimo tu hata uvuvi lakini pamoja na shughuli zingine zozote za kibinadamu zinazomwingizia kipato. TEHAMA inatumika namna gani? Kama sasa hivi tukijenga *data center* itapunguza *gap* kati ya watafiti wanaofanya tafiti pamoja na mkulima kwa sababu mtafiti mara nyingi anafanya tafiti lakini zile tafiti haziwasaidii wale wakulima wadogo wala wavuvi, wala wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia TEHAMA maana yake watakuwa wanapata *SMS direct* kutoka *data center* hiyo kwenda kwa mkulima kama watakuwa na simu za mkononi tu inatosha kabisa. Kupitia TEHAMA pia tutapunguza majanga mbalimbali kwa kutoa taarifa kwa jamii mapema. Kwa mfano, mwaka jana tulikuwa na changamoto kubwa ya ukame, kama wakulima wa maeneo mengi wangepata taarifa kwamba kuna changamoto za

ukame zinakuja kupitia simu za kiganjani mikononi mwao tusingekuwa na shida ya chakula katika maeneo tofauti tofauti katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu TEHAMA itasaidia zaidi kutafuta masoko. Kama Serikali itakuwa inasaidia kutafuta masoko dunia halafu wanatuma *massage* moja tu kwa wakulima fulani labda wa zao la pamba, chai, kahawa na mazao mengine maana yake itasaidia wale wapate taarifa mapema kuliko vile ambavyo kila mkulima mmoja mmoja anajitafutia soko lake pale anapoona yeye inafaa. Kwa hiyo, tukiwekeza katika TEHAMA najua na nina hakika kwamba wakulima wetu hawatakuwa kama walivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mchango wangu huu kidogo, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa muda. Kwanza sina shaka na dhamira na uwezo wa Mheshimiwa Dkt. Tizeba hata kidogo ila nina mashaka na dhamira na *focus* ya Wizara ya Fedha ambayo asilimia 65 ya Watanzania wanaishi katika sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi lakini *development budget* tuliyopeleka kwenye kilimo ni asilimia tatu na kwenye mifugo ni asilimia nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mkononi ninayo barua aliwahi kuiandika Mheshimiwa Rais Magufuli akimuandikia wakati huo Waziri wa Fedha, Ndugu Mustapha Mkulo mwaka 2009 na nitamkabidhi kaka yangu, nitaomba wahudumu wampelekee Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Rais Magufuli wakati huo akiwa Waziri wa Mifugo alitaja changamoto saba zinazokabili sekta ndogo ya maziwa katika nchi hii. Mpaka leo zile changamoto ziko hai, unaona ni namna gani Serikalini kuna tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mifugo kwa maana ya sekta ya ngozi, katika nchi ya Ethopia asilimia 47 ya *GDP* ya Ethiopia inachangiwa na sekta ya mifugo na sekta ya kahawa. Sisi ni wa pili na ningeomba niweke kumbukumbu sawa humu Bungeni tunasema watatu Sudan imeshagawanyika sasa hivi nchi ya pili Afrika kwa mifugo mingi ni Tanzania. Hata hivyo, hawa wafugaji tunawasaidiaje? Nataka nikupe mifano namna gani Serikali inawafilisi wafugaji wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Ngara katika hii operesheni ya kufukuza wafugaji, zaidi ya ng'ombe 2,047 za wafugaji ambao walinyang'anywa mifugo yao zimefilisiwa leo ni watu maskini. Waziri kwenye kitabu anazungumzia mauzo ya *hay,* yale majani yale yanayofungwa ya thamani ya Sh.55,000,000. Ukipiga hesabu ni sawasawa na *hay* 20,000, *are we serious? Hay* 20,000 ni chakula cha ng'ombe kwenye shamba la mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani yetu ya Uchaguzi hii hapa, ukurasa wa 14 na 15 unazungumzia namna gani tutaweza kuongeza uzalishaji wa mifugo bora kwa wafugaji. Ilani yetu ya Uchaguzi imeweka *target* ya kupeleka mitamba 10,000 kwa wafugaji wetu. Waziri anazungumzia mitamba 500 kwa mwaka, Ilani inazungumzia mitamba 10,000. Mabwawa kwa mwaka katika kipindi cha 2015-2020, Ilani yetu inazungumzia kuchimba mabwawa 2000 mpaka sasa bajeti ya mwaka jana na ya mwaka huu hakuna fedha za mabwawa. H*ow can we help this country? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali, hatuwezi kufikia dhamira ya *industrialization* kama hatutowekeza kwenye kilimo na ufugaji katika nchi hii. *GDP* yetu ni Dola bilioni 52, bilioni 15 inatoka katika sekta ya *Agro* lakini hatuwekezi yaani sekta inayotuingizia bilioni 15 tunapeleka *only three percent of our budget*. Hii inasikitisha sana na inaenda *against our promises* kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri akija hapa atueleze, leo tumbaku inaporomoka na ninavyoongea hivi leo gulio la tumbaku limezuiliwa Tabora, ame-*project* mwenyewe kwamba mwaka huu 2017/2018 yaani Serikali kabisa inapanga kwamba zao la tumbaku litashuka, wana mpango gani kwa hawa wakulima watakaopata umaskini kutokana na zao kushuka na ni namna gani umaskini wao unakuwa *compensated* kwa mazao mengine, hakuna mpango. Waziri amefanya kazi kubwa ya kufuta tozo ambayo itatusaidia bei yetu kuwa *competitive* kwenye soko la dunia, jambo jema lakini kama hatuwekezi kwenye *production* hizo tozo zote anazofuta kaka yangu Mheshimiwa Tizeba hazitakuwa na manufaa yoyote yale kwa wananchi wetu wala uchumi wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mungu kwa wema na rehema zake nyingi katika maisha yetu. Nakushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya sekta hii muhimu sana kwa ustawi na mustakabali mzuri wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa William Olenasha, Katibu Mkuu na watendaji na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kusimamia sera, sheria na utendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sekta ambayo ikisimamiwa vizuri itainua uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa sana kama takwimu zinavyoonyesha. Naipongeza Serikali kwa kuja na mapendekezo mazuri ya kuboresha sekta

zinazosimamiwa na Wizara hii. Hii inalenga moja kwa moja kuongeza mali ghafi muhimu za viwanda mbalimbali nchini kwetu hususan vijijini na wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali ni kukaa kwa pamoja kuweka mikakati inayojengana (*complementary)* ili kuhakikisha malengo ya uzalishali, tija na ubora vinafikiwa kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Nnazungumzia Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Viwanda, Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Nishati na Madini. Hii itawezesha kuhakikisha kuwa lengo letu kuu la kufikia uchumi wa kati na wa viwanda linafikiwa kwa ufanisi, gharama ndogo na matokeo makubwa kwa kuanzia na maeneo ya kimkakati yaliyoainishwa yote yawekewe huduma ya miundombinu muhimu ili yawe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba inaonesha kuwa sekta ya kilimo inachangia asilimia 29.1 ya pato la Taifa, ajira asilimia 65 na chakula kwa asilimia 100. Basi Serikali ione umuhimu wa kutoa kipaumbele kwenye sekta hii kwa kuwavutia vijana wengi zaidi kuingia katika sekta kwa njia zifuatazo:-

(i) Kuanzisha vikosi vya uzalishaji vya vijana kila kata nchini na kuainisha aina ya uzalishaji unaofaa kila eneo, ufugaji wa mifugo ya kawaida mikubwa kwa midogo, samaki kwa mabwawa, nyuki na kilimo cha aina mbalimbali;

(ii) Kuwapatia mafunzo ya taaluma ya kufanya shughuli hizi na mafunzo ya ujasiriamali;

(iii) Kuwezesha kujisajili kama kampuni au ushirika wa vijana na kuwaunganisha na vyombo vya kifedha kwa kupata mitaji; na

(iv) Vikundi viwe chini ya Halmashauri na Afisa Kilimo, Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Misitu na Afisa Mifugo. Wote wawasimamie vijana hawa na kuhakikisha wanaendelea na miradi yao hadi kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo maeneo na shughuli za masoko yatengwe na kuwekewa miundombinu mizuri ya kuuza mazao hayo na vijana wawezeshwe kuanzisha viwanda vidogo na biashara ndogo za mazao wanayozalisha. Hii itawafanya vijana wengi kubaki vijijini kulima, kufuga, kusindika, kufanya biashara na kuacha kwenda kunyanyasika mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kuona jinsi Wizara hii inashirikiana moja kwa moja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwenye kilimo cha umwagiliaji. Hali kadhalika tuone miundombinu ya barabara na reli na umeme vinaendelezwa kwenye maeneo haya ya uimarishaji wa sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe, hususan Wilaya ya Ileje ambayo iko kwenye Programu ya Bonde la Mto Songwe ina eneo kubwa sana la takriban hekari 6,428 ambalo linafaa sana kwa kilimo cha mazao ya nafaka mbalimbali, ufugaji wa samaki, mifugo na mbogamboga na matunda. Licha ya maji ya Mto Songwe, Wilaya ya Ileje inapata mvua nyingi kila mwaka na ina rutuba ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali iingize eneo la Bonde la Mto Songwe lililoko Ileje ili lipangiwe mkakati mzuri wa kuliendeleza kwenye mazao ya kilimo cha biashara, kwa mfano, kahawa, ufuta, alizeti, pareto, karanga, mpunga, matunda, mboga mboga pamoja na ufugaji wa samaki wa mabwawa, kuku, ng'ombe wa maziwa na wa nyama, nguruwe, mbuzi, kondoo na nyuki. Hii iendane na wazo la hapa juu la kuwawezesha vijana kwenye vikosi vya uzalishaji itainua ajira sana, mapato ya vijana wenyewe, Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ileje ni wilaya ya mpakani mwa Tanzania na Malawi na kwa kiasi Zambia lakini vilevile ni jirani sana na Wilaya ya Tunduma ambako biashara kubwa inafanywa na watu wa nchi za jirani hadi DRC Kongo. Halmashauri ya Ileje ilijenga soko kwa ajili ya mazao lakini *NFRA* wamekuwa wakitumia soko la Isangole kama maghala

yao. Tunaitaka Wizara kujenga maghala makubwa sana kwa nafaka na mazao mengine ya biashara kama kahawa, pareto, viungo mbalimbali kama iliki, pilipili manga, mdalasini, tangawizi, *cocoa* na kadhalika. Tunaiomba Wizara itupatie maghala ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu pia kuwa *SAGCOT* inahusisha Mkoa wa Songwe. Pia tunaitaka Serikali itufahamishe hadi sasa Songwe na hususan Ileje inaguswa vipi na mradi huu na ni katika maeneo yapi na hawa wahusika kwa eneo letu ni akina nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya kilimo chetu ni upatikanaji wa mvua za kutosha, mbegu bora na pembejeo. Tunaipongeza sana Serikali kwa kuja na pendekezo la kuboresha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo. Huu ni mfumo wa kimageuzi na utahakikisha wakulima wengi kupata pembejeo na kulima vizuri zaidi. Tutashukuru kuwa sasa pembejeo zitapatikana kwa wakati na kwa bei nafuu na kuondoa malalamiko ya muda mrefu na vilevile kuhakikisha wakulima wanazalisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atafute muda wa kutembelea Ileje yeye na maafisa/ wataalam wake waje kujionea wenyewe fursa nyingi zilizopo wilayani humo ili watuweke kipaumbele chini ya programu ya *SAGCOT* na mradi wa Bonde la Mto Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya na Iringa ni wakulima wakubwa wa *arabica coffee*, pareto, chai na viungo kwa kutaja machache. Japan wana soko kubwa la *gourmet coffee* na wanailipa bei nzuri. Wilaya hizi zina uwezo wa kuzalisha aina hii ya kahawa na kuiuza Japan. Tunaitaka Wizara ituunganishe na soko hilo lakini pia watupatie utaalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mnada wa kahawa ufanyike Songwe kwenye uzalishaji mkubwa wa kahawa na tunahitaji soko/viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja na niwapongeze kwa kazi nzuri pamoja na changamoto zote wanazokumbana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nishauri tu katika kuboresha sekta ya uvuvi ni vyema *season fishing* ikapewa kipaumbele, italeta tija sana katika sekta hii. Tuyatambue mazalia ya samaki na kisha tuweke programu maalum ya kutekeleza *season fishing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tutoe kipaumbele katika *cage fishing*. Tuwekeze kwa vijana ili ufugaji wa samaki ufanyike katika mfumo wa kuwa na *plot* ndani ya ziwa ama bahari kwa kuweka wigo katika maeneo yatakayowekezwa katika uvuvi kwa njia ya uvuvi wa wigo ziwani ama baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu ufugaji wa ng'ombe ni vyema wafugaji/wachungaji wakashauriwa kufuga ufugaji wa kitaalam na kuwaelekeza wafugaji wetu kufuga kitaalam ili wawe na tija katika ufugaji wao badala ya kuwa na ufugaji wa kuhamahama kitendo ambacho kinachangia sana katika kuleta migogoro ya wakulima na wafugaji.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kwanza kuhusu wakulima wa chai Rungwe. Kumekuwa na migogoro mingi sana kati ya wakulima wa chai Mkoa wa Mbeya, Wilaya ya Rungwe na wadau wa chai akiwemo *Mohamed Enterprises* na *WATCO* kwani bei ya chai ni ndogo sana na baadhi ya wakulima kujiondoa katika uuzaji wa chai katika viwanda vya Katumba na Busokelo kwa madai ya maslahi madogo na wakati huo huo Bodi kuzuia kuuza kwa chai na kampuni ya *Mohamed Enterprises* na kuzuia uhuru wa kibiashara ambapo mwisho wa siku mkulima ndiyo hunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili mazao kuuzwa kwa ujazo wa lumbesa. Naomba Wizara iweke mkazo na msisitizo

wa kusaidia wakulima wanapouza mazao kulazimishwa kujaza mazao katika mfumo wa lumbesa kwani wakulima hupata hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, naomba niongelee kuhusu pembejeo zisizo bora. Kumekuwa na malalamiko ya pembejeo zisizo na kiwango na kupelekea makusanyo duni na kuwapa hasara wakulima wetu hasa wa Mkoa wa Mbeya. Serikali ina mkakati gani wa kusaidia wakulima hawa na pia kuchukua hatua kwa wahalifu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, niongelee kuhusu bei ndogo za mazao. Wizara inasaidiaje wakulima wauze mazao yao kwa bei ya faida ambayo itasaidia kulipa gharama za kilimo walichowekeza na kudhibiti madalali wanaopata pesa nyingi kuliko wakulima wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, Kituo cha Kilimo Uyole. Kituo hiki ni muhimu sana kwa wakulima wa Nyanda za Juu Kusini kwani utaalam wao unahitajika lakini cha kushangaza pesa inayotengwa kwa shughuli za maendeleo haziwafikii kwa wakati na hata wakati mwingine kutofika kabisa na kukwamisha shughuli za kitafiti na kiutendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita ni kuhusu wakulima na wafugaji. Tunaomba ufumbuzi wa kudumu juu ya wakulima na wafugaji utafutwe ili kupunguza/kuondoa ugomvi kati ya jamii hizi.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea suala la vinyungu. Niombe Serikali ione namna ya kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Njombe ambao wanategemea vinyungu, bila vinyungu Njombe watapata umaskini. Serikali itoe mbadala wa vinyungu maana wananchi hawana sehemu nyingine ya kulima, wakilima mashamba ya nchi kavu hawapati chochote pia maji ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

(i) Naishauri Serikali kuangalia upya kuhusu pembejeo kwa ajili ya kilimo kufika mapema kulingana na misimu na pia mbegu ziboreshwe;
(ii) Serikali ijitahidi kuwajali wagani tulionao kwa kuwapa vitendea kazi, usafiri wa kuwafikia wakulima wetu;

(iii) Nashauri Serikali itoe elimu ya ufungashaji ambayo imegharimu mazao yetu yanafungashwa Kenya na kusafirishwa hivyo kupata fedha nyingi kuliko wakulima;

(iv) Nashauri Serikali kuangallia jinsi dawa zinavyohifadhiwa kwani kuna nyingi ni sumu na zinaharibu afya za wananchi;

(v) Nishauri Serikali kuhakikisha wanashughulikia miundombinu ya kutoa mazao mashambani;

(vi) Nishauri Serikali kuelimisha wananchi juu ya uuzaji mazao siyo kuzuia tu kwani mwananchi anatakiwa kuuza ili kununua mahitaji mengine.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa namna inavyoendelea kufuta kodi, tozo, ushuru na ada ambazo zinaleta kero kwa wananchi hususan wafanyabiashara kama vile tozo ya afya ya kusafirisha mifugo nje ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifute tozo ya kusafirisha mifugo nje ya Mkoa katika Minada ya Upili, kwa mfano, Mnada wa Mhunze, Wilaya ya Kishapu, Serikali Kuu hukusanya tozo zote, ushuru Sh.5,000/= kwa ng'ombe na tozo ya kusafirisha ng'ombe nje ya Mkoa Sh.2,500/= jumla Sh.7,500/=, zote huchukuliwa na Serikali Kuu na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu haipati kiasi chochote cha fedha. Naomba *permit* ya Sh.2,500/= iondolewe ili kumpunguzia mzigo mfanyabiashara wa mifugo ile Sh.5,000/= inatosha kabisa Mkoa kugawana na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo kama uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu bado hakipewi uzito unaostahiki. Pesa zilizotengwa katika bajeti hazitoshi kukabili mahitaji yaliyopo, hata hivyo nashauri yafuatayo:-

(a) Utafiti ufanyike ili kujua matatizo katika ardhi na kwa maana hiyo ushauri ufanyike ni mbegu gani itumike kwenye eneo husika kulingana na utafiti uliofanyika. Mfano, ardhi ya Visiwa vya Ukerewe inahitaji kufanyiwa utafiti na hatimaye lipatikane suluhisho la aina ya mbegu, mazao na kilimo kinachopaswa kufanyika.

(b) Ufanyike uwekezaji wa kutosha katika kilimo cha umwagiliaji hasa kutokana na mabadiliko ya tabianchi hali inayoathiri kilimo chetu kinachotegemea zaidi mvua. Mfano, eneo linalozungukwa na maji kama Ukerewe ingepaswa kuwa wazalishaji wakubwa wa chakula iwapo tu Serikali itawekeza katika kilimo cha umwagiliaji katika visiwa hivyo. Kuna mabonde makubwa ya Bugorola na Miyogwezi ambapo Serikali imewekeza zaidi ya shilingi millioni 700, lakini mradi huo umetelekezwa. Naomba kujua Serikali ina mpango gani na miradi ya umwagiliaji wa Miyogwezi?

(c) Zitolewe ajira kwa Maafisa Ugani wengi na wasambazwe kwenye maeneo mbalimbali ili kutoa ushauri kwa wakulima wetu na hivyo kuongeza tija katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli za uvuvi zinatoa ajira kubwa kwa wananchi wengi katika nchi hii lakini kuna changamoto nyingi sana na hivyo naomba kushauri yafuatayo:-

(a) Sheria Na. 22 ya mwaka 2003 ipitiwe upya na ufanyike utafiti wa kina kwa kushirikisha wadau hasa wavuvi wenyewe ili tuwe na sheria nzuri na rafiki kulingana na

mazingira. Mfano, kuzuia nyavu '*piece* 3' kunahamasisha wavuvi wa sangara kuvua kina kifupi cha maji na hivyo kuharibu mazalia ya samaki. Pia nyavu za *mm10* kwa nyavu za dagaa ni kuwanyima fursa wavuvi hasa katika Ziwa Victoria ambapo ni vigumu kupata dagaa *size* hiyo.

(b) Wavuvi wamekuwa wanavamiwa na kujeruhiwa au kuuawa wanapokuwa wanafanya shughuli zao za uvuvi katika ziwa. Nashauri Serikali iweke mfumo thabiti wa kiulinzi ili wavuvi hawa wafanye shughuli zao kwa usalama.

(c) Bado tozo ni nyingi sana katika sekta hii zinazowakabili wavuvi na hivyo Serikali ipunguze tozo hizi ili wavuvi wetu wafanye shughuli zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hatua ya kuondoa ada ya usafiri kwa mitumbwi midogo.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kupunguza kodi mbalimbali na kuanzisha utaratibu wa *bulk procurement* ili kupunguza bei za pembejeo na hasa mbolea, lakini tunaomba isije ikatokea kama mwaka jana bei zilitangazwa lakini ikawa hakuna utekelezaji wowote. Mfumo wa vocha unakiua chama na Serikali mambo yafuatayo ni muhimu kupewa uzito unaostahili:-

(i) Kukuza kilimo; naamini kuwa kilimo kilichopo kwa sasa ni kilimo kidogo cha kupata chakula tu, nchi haiwezi kuendelea kwa kilimo hiki lazima yaanzishwe mashamba makubwa ya kibiashara ambayo yatatoa ajira rasmi kwa watu wengi, yatazalisha kwa tija na kutumia mbegu bora na zana za kisasa yaani *commercial farming*. Bila kufanya hivyo, tutaendelea kuimba bila mafanikio makubwa, hili linawezekana kama ilivyokuwa siku za nyuma.

(ii) Kufufua kilimo cha kahawa. Kwa miaka mingi zao la kahawa lilikuwa ni kitovu cha mazao ya biashara.

Hata hivyo, zao hili limeporomoka sana kiuzalishaji nchini. Lazima mkakati wa kulifufua zao hili uandaliwe haraka iwezekanavyo.

Sambamba na hilo, Chama cha Wadau wa Kahawa kiliunda *TACRI* kwa ajili ya kufanya utafiti wa zao la kahawa. Taasisi hii ilipewa majengo na maeneo yaliyokuwa chini ya Serikali. Hata hivyo, hivi sasa taasisi hii inakabiliwa na changamoto kadhaa. Hivyo, ili kuendeleza utafiti, napendekeza Serikali iichukue taasisi hii na kuifanya kama wakala wa Serikali ili kuongeza ufanisi na tija katika utafiti wa zao la kahawa. Zao hili ni muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi wetu.

(iii) Suala la Benki ya Kilimo; Benki hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo. Ni vizuri kufungua matawi katika mikoa yenye kilimo sana ili kuwakopesha wakulima wengi, suala hili ni muhimu sana.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pili, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa uongozi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2013/2014 ilipitisha bajeti ya kuwapelekea huduma za mifugo (miundombinu) kama majosho, malambo na visima virefu. Pia mwaka 2015 wataalam wa Wizarani walitembelea Kata ya Ruvu na maeneo ya kujenga miundombinu hiyo. Je, miradi hiyo itakamilika lini na tutegemee miradi hiyo itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga tumeanzisha utaratibu wa kuhamasisha wakulima kila Wilaya kulima kilimo cha mihogo ambacho kitasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Tunaiomba Serikali itusaidie kuboresha Chuo cha Utafiti Mlingano ili kiweze kupata fedha, wataalam na vifaa kwa ajili ya kusaidia wakulima kulima kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Muheza na Lushoto ni maarufu kwa kilimo cha matunda, mbogamboga na viungo, mfano, machungwa, ma-*apple*, maembe, mdalasini, hiliki, pilipili manga na pilipili mtama. Pamoja na wakulima kujitahidi lakini kumekuwa na tatizo kubwa la magonjwa ya mimea na dawa zimekuwa bei ghali kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kuwasaidia wakulima kwa kupunguza gharama za upatikanaji wa dawa za kuulia wadudu ili wakulima walime kilimo chenye tija? Je, Serikali iko tayari kuwasaidia wakulima hawa kupata masoko ya uhakika kwa kuwa hadi sasa wakulima wa matunda hasa machungwa wanategemea walanguzi kutoka Kenya, kitu ambacho kinasababisha wakulima kutokuwa na maamuzi juu ya bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mkonge. Moja ya mikoa ambayo inalima mkonge kwa wingi ni Mkoa wa Tanga na karibu kila wilaya ina shamba au mashamba ya mkonge lakini cha kushangaza mashamba mengi yamegeuka mapori na mengine yamekufa. Serikali haioni kuacha hili zao kupotea ni kuwakosesha wananchi ajira na kipato? Je, Serikali iko tayari kuwanyang'anya wawekezaji na kuwapatia wananchi ambao wako tayari kufufua mashamba hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya samaki. Mkoa wa Tanga umejaliwa kuwa na bandari ambapo wavuvi na wananchi wanaozunguka au waliokaribu wanapata ajira lakini pia wanapata chakula. Wavuvi wamekuwa wakipata usumbufu wa kodi, ukosefu wa masoko ya uhakika na kupelekea kuuza samaki kwa bei ya hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la bei linatokana pia na ukosefu wa viwanda vya samaki, hili limekuwa tatizo la muda mrefu. Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki ili wavuvi wawe na uhakika wa kipato?

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii muhimu ina changamoto nyingi sana ikilinganishwa na mikakati inayoendana na utatuaji wake. Hii ipo dhahiri kabisa ukiangalia umuhimu wake unaopewa na Serikali Kuu kupitia *budget allocation* na upatikanaji fedha husika kwa shughuli mbalimbali inayohusu sekta hii. Changamoto hizi zinajulikana ila hazipewi *attention* inayotakiwa kama:-

(i) Vitendea kazi/vifaa/teknolojia za kilimo, uvuvi na ufugaji asilimia kubwa ya wananchi hutumia vifaa kale kama majembe na mashoka katika *century* hii;

(ii) Tegemezi ya kilimo cha mvua;

(iii) Mfumo wa masoko ulio una upungufu mwingi na uliopitwa na wakati. Mfano, hatuna ama hakuna *reliable, efficient market data* na *information;*

(iv) Maeneo mengi hakuna kabisa/ipo katika hali hafifu ya *adequate production and post-harvest technologies*;

(v) Pembejeo za kilimo; utengenezaji, upatikanaji na usambazaji wa mbolea, mbegu ni hafifu na hauzingatii *microclimate* ya maeneo husika, ucheleweshwaji, *low quality;*

*(vi) Extension officers;* kuna upungufu mkubwa. Hawa ni kiungo muhimu katika kusaidia wakulima, wavuvi na wafugaji kwa ajili ya kuelimisha na *consultation* kuipa umuhimu kupitia *budget, research,* Maafisa Ugani kutahakikisha kupatikana kwa chakula *(food security)* katika nchi yetu;

(vii) Kuimarisha Taasisi za Utafiti mfano, *TAFIRI* na *TAWIRI*. Bila kuwa na takwimu siyo rahisi kufanya maamuzi. Taasisi hizi inabidi kupewa kipaumbele kwa kuhakikisha zinatengewa bajeti mahsusi kwa ajili ya tafiti, kukusanya *data* na kuajiri watafiti;

(viii) Sekta ya uvuvi; Serikali iangalie sekta hii kwa jicho la pekee ni eneo lenye *potential* kubwa sana katika kuimarisha uchumi wa wananchi na nchi kwa ujumla wake. Sekta inahitaji kuimarisha *research and data collection,* kuwa na bandari ya uvuvi, kudhibiti uvuvi haramu, kuimarisha *Deep Sea Fishing Authority (monitoring, licensing e.t.c)*;

(ix) Wizara inahitaji kuwa *strengthened* kupitia *budget allocation/ release of funds* ili iweze kusimamia sera yake. Kiwango cha bajeti inayokuwa *allocated* inaenda kinyume na maazimio ya Malabo. Kwa kipindi cha takribani miaka 10 Serikali imekuwa ikitenga chini ya asilimia mbili ya bajeti ya Taifa. Hata fedha hizi zinazotengwa kwa asilimia kubwa zimekuwa zikitolewa chini ya asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huu ni dhahiri Tanzania haitakaa ibadilike katika kukuza uchumi wake. Wizara inatakiwa kuja na mipango mikakati katika kuhakikisha sekta hizi muhimu (kilimo, mifugo na uvuvi) zinatuvusha kutoka katika umasikini.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri Dkt. Tizeba, Naibu Waziri Mheshimiwa Olenasha, Watendaji wote wa Wizara kwa kutuletea bajeti yao ili tuweze kuipitisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kuongelea kuhusu bima ya kilimo. Ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kuwapatia elimu wananchi ili waweze kuweka bima kwa ajili ya kilimo? Kwa sababu kilimo chetu nchini kimekuwa hali ya hewa haitabiriki na pia Serikali haijaweza kuwa na uwezo wa kutoa pesa ya kutosha kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji. Tulipotembelea nchi ya China tulijifunza mengi yanayohusu kilimo mojawapo ni kuwaelimisha wananchi kuwa na Mashirika ya Bima ya Kilimo ili pia itawasaidia hata kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Benki ya Kilimo. Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha Benki ya Kilimo nchini ambayo ilikuwa ndiyo kilio chetu na tukiamini ndiyo

mkombozi kwa wakulima ambao ndiyo walio wengi. Ni kwa nini benki hii Makao Makuu yasiwekwe Dodoma ambako ndiyo katikati ya mikoa yote iwe rahisi na kuweza kufikika kirahisi? Vilevile ni kwa nini benki hii isiweze kufunguliwa madirisha katika mikoa na wilaya ili kuwatendea haki wakulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kilimo cha umwagiliaji. Mkoa wa Iringa una eneo linaweza kumwagiliwa lenye jumla ya hekta 54,446, kati ya hekta hizo zinazomwagiliwa kwa sasa ni hekta 25,575 sawa na asilimia 47 ya eneo lote. Mazao makuu yanayolimwa kwa skimu za umwagiliaji ni pamoja na mpunga, mahindi, nyanya, vitunguu, mbogamboga na matunda. Mkoa wetu una jumla ya skimu za umwagiliaji 48 katika mchanganuo ufuatao; Iringa 32, Kilolo tisa (9), Mufindi tano (5) na Manispaa ya Iringa mbili (2).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii miradi ya Manispaa ya Iringa ni miradi ya muda mrefu sana, Serikali imekuwa haitoi pesa kwa ajili ya miradi hii na tunategemea miradi hii ingeweza kusaidia vijana wetu hawa wa mjini waweze kujiajiri kupitia kilimo. Je, Serikali inatumia vigezo gani kutoa pesa kwa miradi hii ya kilimo cha umwagiliaji? Pia baadhi ya miradi ya umwagiliaji maji kutokamilika vyema na mingine haihitaji ukarabati wenye gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za jumla katika kilimo katika Mkoa wetu wa Iringa ni kama zifuatazo:-

(a) Mtawanyiko mbaya wa mvua/ukame unaochangiwa na mabadiliko ya tabianchi;

(b) Uhaba wa mikopo yenye riba nafuu na isiyohitaji dhamana kubwa kwa kuwa wakulima wengi hukosa vitu vya kuwekea dhamana;

(c) Kuendelea kupungua kwa rutuba katika udongo suala linalosababisha wakulima wengi kuwa na mahitaji ya matumizi makubwa ya mbolea;

(d) Bei kubwa ya pembejeo za kilimo hasa mbolea na mbegu bora kunakosababisha wakulima gharama za uzalishaji wa mazao ya kilimo kuongezeka mara kwa mara;

(e) Magonjwa ya mimea hasa nyanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inasaidiaje changamoto hizo kwa sababu asilimia 75 ya wananchi wa Iringa ni wakulima na ndiyo wanaochangia pato la mkoa.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja. Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kuhakikisha mapinduzi makubwa kwenye uchumi wa viwanda yanapatikana lakini tutafanikiwa tu iwapo tutakuwa na mikakati thabiti ya kulima kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali bado kuna changamoto nyingi ambazo hazina budi kupatiwa ufumbuzi wa haraka ili kuyafikia malengo ya uchumi wa viwanda. Tukilima kilimo cha kisasa tutapata malighafi za kutosha, tutapata chakula cha kutosha na kuweza kuuza mazao ya biashara ndani na nje ya nchi na tatizo la njaa nchini litageuka kuwa historia**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya wakazi wa Mkoa wa Singida wanajishughulisha na kilimo na ndiyo ajira kubwa kwa vijana na wanawake. Hulima mahindi, mtama, mihogo, uwele, viazi vitamu kama mazao ya chakula na mazao ya biashara ni alizeti, vitunguu, pamba, ufuta na choroko lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo:-

(i) Pembejeo zisizokuwa na viwango;

(ii) Bei kubwa ya pembejeo na zana za kilimo;

(iii) Uhaba wa wataalam na mashamba darasa ambayo husababisha uzalishaji kuwa mdogo;

(iv) Ukosefu wa mitaji na mikopo kwa wakulima;

(v) Ruzuku ndogo ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi zilizotajwa hapo juu zinakatisha tamaa vijana na wanawake wengi ambao wana hamasa kubwa ya kujikita katika kilimo cha kisasa lakini wanashindwa kufanya hivyo na kukimbilia mijini wakidhani huko ndiko kwenye maisha bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa Ugani ndiyo watu muhimu wa kuwapa mbinu bora za kilimo na hasa wakulima waliopo vijijini lakini Mkoa wa Singida una uhaba mkubwa wa maafisa hawa. Kwa Wilaya ya Iramba wako 79 wakati mahitaji ni 324; Wilaya ya Singida Vijijini mahitaji ni 188 lakini waliopo ni 45; Wilaya ya Mkalama mahitaji ni 185 na waliopo ni 38 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya uwepo wa Maafisa hawa wachache lakini nao wanakabiliwa na ukosefu wa vitendea kazi kama vile pikipiki na hivyo kushindwa kuwafikia wakulima wengi huko vijijini. Ni vyema Serikali ikaangalia jambo hili kwa kina kwa kuongeza Maafisa Ugani wa kutosha katika Halmashauri zetu kwa kuwa maafisa hawa ni kiungo muhimu katika kuyafikia maendeleo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze masikitiko yangu juu ya mgao mdogo wa ruzuku ya pembejeo kwa Mkoa wa Singida kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ambapo Serikali ilitupa tani 20 za mbegu ya mahindi na tani 100 za mbolea ya kupandia/kukuzia ambayo ni sawa na asilimia 0.29 ya mbolea kwa mahitaji ya mkoa mzima. Hiki ni kidogo sana kwa mkoa kwani mahitaji yetu ni kuanzia tani 33,000 hadi tani 40,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida ni miongoni mwa mikoa inayolima mazao ya mafuta, kwa Mikoa ya Pwani ni nazi, kwa Mkoa wa Kigoma ni mawese, kwa Singida na Dodoma ni alizeti lakini Serikali haijalitaja zao hili kama zao la kimkakati ili tija iweze kuonekana na

hata mpango wa *SPDA II* haujatilia mkazo zao hili. Kwa msimu uliopita, takribani tani 58,000 ziliuzwa nchini Congo ambazo ziliingiza zaidi ya shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo zao hili litatiliwa mkazo, uzalishaji utaweza kuongezeka lakini wakulima hawa wa alizeti wamesahaulika, wengi hawana mbinu mpya bado wanatumia mbinu za zamani ambazo husababisha uzalishaji mdogo hata viwanda vilivyopo vya kuchakata alizeti havina viwango vyenye ubora wa kutosha. Iwapo Serikali itaviendeleza viwanda hivi vitaweza kuzalisha mafuta mengi yenye ubora wa kuweza kuuzwa ndani na nje ya nchi. Ifike wakati sasa Serikali iwatazame wakulima wa zao la alizeti kwa kuwapa mbegu bora za *F1,* utaalam wa kilimo cha kisasa na ruzuku ya pembejeo ili kukiboresha kilimo hiki cha alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni mfumo wa manunuzi wa pamoja wa pembejeo *(bulk procurement).* Naipongeza Serikali kwa kubuni mfumo huu kwani utamaliza matatizo yaliyopo katika mfumo wetu wa sasa. Wakulima wetu wameteseka sana kwa kulanguliwa na kuuziwa pembejeo zisizo na viwango kama ilivyotokea msimu uliopita wakulima wa pamba Singida walipata hasara kubwa. Hapa naishauri Serikali kuangalia mambo matatu kwa kina ili kufanikisha mfumo huu. Moja, ni udhibiti wa bei, ubora wa pembejeo na mahitaji kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri Serikali kujikita katika kilimo cha umwagiliaji na hasa katika Mkoa wa Singida ili wananchi wa mkoa huu waweze kulima kwa msimu wa mwaka mzima kwa kuwa jiografia yake ni mkoa wenye ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake.

**MHE. PROSPER J. MBENA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya kiongozi wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada kubwa ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka huu wa 2016/ 2017, haukuwa mzuri hasa bajeti ya maendeleo kutokana na fedha kidogo zilizotolewa na Hazina ambazo ni asilimia 3.31 tu ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Naishauri Serikali yetu ihakikishe fedha zote za maendeleo zinazoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii zitolewe kwa wakati ili tulete mabadiliko makubwa ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya bajeti ya Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi haikueleza kwa namna gani Serikali itamaliza migogoro ya wafugaji na wakulima. Jimbo langu la Morogoro Kusini limekumbwa kwa kiasi kikubwa sana na migogoro ya wafugaji na wakulima na wananchi wanaathirika, wapo waliopoteza maisha yao, waliopata ulemavu na waliopata umaskini. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi haijasema Serikali imejipanga vipi kuitafutia ufumbuzi wa kudumu wa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufugaji wa sasa wa ng'ombe kwa utaratibu wa kuchunga mashambani hauna tija. Wizara ijipange kufanikisha ufugaji wa kisasa wa *zero grazing.* Nchi za Botswana na Namibia zinaweza kuwa mfano mzuri wa kuigwa, tujipange na sisi kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo katika bajeti hii bado hakijapewa umuhimu unaostahili kwa kuzingatia rasimali zinazotengwa, kilimo cha trekta na umwagiliaji ndicho kitakacholeta mapinduzi ya kilimo nchini. Kwenye bajeti hii, mikopo ya kununua trekta ni kidogo mno. Mfuko wa Taifa wa Pembejeo umepanga kutoa mikopo ya matrekta 71 tu kwa nchi nzima, kiasi hiki ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali lazima ijenge miundombinu ya kilimo, barabara, trekta nyingi za kutosha, vifaa vya umwagiliaji pia Serikali ihakikishe mbegu bora na mbolea ya kutosha inapatikana kwa wakati. Kwa upande wa Jimbo la Morogoro Kusini tunayo maeneo mazuri sana ya kilimo cha trekta na umwagiliaji mfano eneo la Kongwa, Kilengezi, Selembala, Magogoni, Lundi, Dutumi na Kisaki ni maeneo makubwa yanayolima mahindi, mpunga, ufuta, mihogo, viazi na kadhalika. Tunaomba Serikali ituwezeshe wakulima wetu wapate mikopo ya nyezo hizo za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa upande wake itengeneze barabara za kwenda mashambani ili zipitike muda wote wananchi watalima sana. Taarifa ya Serikali kuwa zao la muhogo limepata soko China ni habari njema kwetu, tunaomba kufahamu utaratibu utakaotumika na chombo gani kinachosimamia hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeeleza dhamira yake ya kuifanya nchi ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Hivyo, nashauri Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi itengeneze mpango wa uzalishaji wa mazao yatakayoingia katika viwanda vitakavyojengwa nchini kuandaa upatikanaji wa *raw materials* za viwandani mfano miwa kwa viwanda vya sukari, matunda kwa viwanda vya juisi na vinywaji baridi na kadhalika. Mashamba ya mazao haya yatakuwa makubwa na ni vema kuanza kuandaliwa vinginevyo viwanda vyetu vitajengwa hakuna *raw materials*. Kwenye uzalishaji huu, matumizi ya sayansi na teknolojia uongezeke ili tupate mazao mengi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, sekta ya uvuvi bado kuimarika tunahitaji mapato yaongezeke mara dufu. Nashauri tuingie ubia na makampuni ya nje yenye meli kubwa za uvuvi kwenye uvuvi wa bahari kuu badala ya utaratibu wa sasa wa kutoa leseni kwa makampuni hayo ya nje kutoka China, Hispania, Seychelles, Taiwan, Ufaransa na Mauritania. Serikali haipati mapato ya kutosha kwa utaratibu huu kuliko kama tungeingia nao ubia. Msumbiji wanafanya hivyo na

wamekuwa na mapato mazuri. Wanayo matatizo mengi ya jinsi walivyotumia fedha zao kununulia meli za uvuvi lakini hiyo ni tofauti na mpango wa ubia ninaoushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Vinyungu na Mita 60 Kutoka kwenye Vyanzo vya Maji. Suala hili nalipeleka kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuwa linagusa kilimo moja kwa moja japo usimamizi wa sheria ya mita 60 inasimamiwa na watu wa mazingira kupitia *NEMC*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha vinyungu kwa lugha nyepesi tunaweza kusema ni kilimo cha mabondeni. Sasa tafsiri hii ya mita 60 kutoka vyanzo vya maji au kingo za mito ni tofauti sana na kilimo cha vinyungu. Vinyungu (Iringa na Njombe) au masebula (Kigoma, Katavi, Rukwa na Kagera) ni kilimo cha muda mrefu ambacho ni sawa na asilimia 50 ya maisha ya wananchi wanaoishi kwa kutegemea vinyungu miaka nenda miaka rudi na hakijawahi kuathiri mtiririko wa maji; na ndiyo maana mpaka leo ni mikoa hiyo pekee ambayo vyanzo vya maji vimeendelea kuwepo. Wananchi wanaheshimu vyanzo vya maji, wanatunza maji tena kwa njia ya asili; hivyo vinyungu si tatizo wala chanzo cha kuvuruga vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari; Mkoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, na Ruvuma/Rukwa imeendelea kuwa kimbilio la chakula miaka yote kwa sababu pamoja na mashamba ya kawaida vinyungu vimekuwa na mchango wa zaidi ya asilimia 40 ya chakula katika mikoa hiyo kuanzia mahindi, viazi na mazao ya mbogamboga kwa hiyo kuibuka na kusema tunazuia kilimo cha vivyungu maana yake tunaandaa mazingira ya kuleta njaa kwenye maeneo hayo. Jambo hili litazamwe upya na maamuzi yanayohusu kilimo cha vivyungu, wananchi na sisi viongozi wao tushirikishwe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Suala la Mbolea. Ukweli ni kuwa mfumo wa ruzuku ulinufaisha watu *at*

*individual level* wakiwemo wafanyabiashara na baadhi ya watendaji wa Serikali. Uamuzi wa kuagiza kwa mkupuo *(bulk)* utasaidia. Angalizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Haitakuwa na maana ikiwa mbolea itachelewa kuwafikia wakulima wa mbolea vijijini. Kwa mfano kwetu Iringa msimu unaanza Oktoba kuandaa mashamba na kufikia Novemba tarehe 15 wanakuwa wameshapanda bila kujali mvua zipo au hazipo, mbegu hutangulia ardhini. Sasa katika hali hiyo ni vyema mbolea iwafikie mapema Oktoba

(b) Kuhusu upatikanaji, jambo hili ni kubwa sana na mtego kwa Serikali hasa kama upatikanaji na usambazaji utakuwa duni. Ushauri wangu, maandalizi kwa kila msimu yafanywe mapema

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasiasa *VS* Ushirika. Serikali imedhamiria sana kutusaidia kupitia ushirika na hasa *SACCOS.* Baadhi ya maeneo Halmashauri zimeshapokea fedha kwa ajili ya *SACCOS* za vijana na hata zile milioni 50 kwa kila kijiji, matarajio ni kuwa zitapitia ushirika na *SACCOS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, pamoja na uwepo wa Sheria bado wanasiasa *directly or indirectly* wanajihusisha kwenye *SACCOS* na ushirika na wengine ni viongozi. Hili ni bomu mbele ya safari kwa sababu linaweza kuibua chuki, upendeleo na baadaye kuvuruga ushirika na *SACCOS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri. Pamoja na uwepo wa sheria ni vizuri Wizara ikasimamia utekelezaji wa sheria na kupitia TAMISEMI mwongozo/waraka ukatolewa kuwaeleza Mamlaka za Mikoa (Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri) kuwa wanasiasa hawaruhusiwi kuwa sehemu ya ushirika/*SACCOS* ili kuepusha migongano na hatari ya kuvuruga ushirika/*SACCOS,* naomba kuwasilisha.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri na watumishi wote wa Wizara kwa hotuba ya Wizara yao ambayo inaonesha mwelekeo wa kutatua changamoto za wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii bila kilimo cha kisasa, chenye kutumia mbolea na zana za kisasa, bado ndoto ya kuzalisha mazao mengi haitafanikiwa. Niipongeze Wizara, katika hotuba hii inaonesha mwelekeo wa kuleta ukombozi kwa mkulima, kwa mfano uagizaji wa mbolea kwa pamoja *(bulk).* Eneo hili lilisababisha wananchi wengi kushindwa kuzalisha mazao yenye tija kwa sababu mbolea ilikuwa juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri awe makini sana katika mpango huu, kwamba wale watakaopewa majukumu haya wawe watu makini na wazalendo wa dhati kwa sababu bado baadhi yao wanaweza kutumia nafasi hiyo vibaya. Kwa kuwa mpango huu ni mpya changamoto nyingi zitajitokeza, naomba tu uwekwe utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia na ambalo naona Wizara haijalipa uzito ni kilimo cha umwagiliaji kwani yapo maeneo mengi nchini yanapata mvua za kutosha na yana mabonde mengi ambapo yangetumika vizuri nchi hii isingepata tatizo la njaa. Mvua zinanyesha maeneo mengi na maji yote yanaishia baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano katika Jimbo la Kilindi, Kata za Kilwa, Kilindi Asilia, Masagulu, Kibirashi pamoja na Mgera. Maeneo yote haya yana mabonde ambapo hata kwa shughuli za kilimo cha mbogamboga kingefaa pia. Tatizo Wizara haina mpango mkakati ili kuwasaidia wananchi kwa kutoa elimu, zana na hata mikopo ambayo ingeweza kusaidia katika kuboresha maisha yao kwa shughuli za kilimo.

Niombe Wizara hii, pamoja na mipango yake mizuri, wakati umefika Benki ya Kilimo isaidie sasa wananchi wakulima wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni eneo la Mkoa wa Tanga na maeneo mengine ambayo yana fursa za kulima mazao ya matunda. Mkoa wa Tanga ni miongoni mwa mikoa michache nchini ambayo inazalisha matunda lakini uzalishaji wake umekuwa hauna faida kwa sababu wanachopata, kwa maana ya bei, ni ndogo kwa sababu tu Wizara haina utaratibu mzuri wa kuwatafutia soko la uhakika wananchi hawa. Nishukuru, pengine kwa mpango wa Serikali wa kujenga tena viwanda, unaweza kurudisha tena imani na uchumi wa wananchi wetu. Niombe Serikali kupitia Wizara hii iwaangalie wananchi kutoka kwenye maeneo yenye fursa za kilimo kama ilivyo Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia migogoro ya wakulima na wafugaji; je, zoezi la Wizara tatu au nne la kutaka kutatua migogoro ya wananchi wetu limefikia wapi? Nchi hii inawahitaji wakulima na wafugaji, hivi kwa nini jamii hizi mbili hazipatani? Tatizo ni upimaji wa maeneo; hivyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri ashirikiane na TAMISEMI na Wizara ya Ardhi kuhakikisha maeneo ya kilimo yanatengwa na ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajitokeza mara kwa mara wafugaji wanaingiza mifugo kwenye mashamba ya wakulima lakini tatizo lingine la wakulima kupanua maeneo ya kulima kwenye maeneo ya wafugaji, tatizo hili halitakwisha kama Serikali haitapima maeneo ya ufugaji na kilimo, huu ndio mwarobaini pekee. Kwa mfano maeneo ya Wilaya ya Kilindi, Rufiji na Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi na vilivyomo. Nikushukuru wewe kwa nafasi hii

uliyonipatia ili na mimi nichangie, ingawa kwa muhtasari, katika Wizara hii muhimu sana kwangu kwa sababu imenilea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizobarikiwa na rasilimali muhimu za bahari, maziwa na mito. Tanzania Bara tunao mwambao wa bahari wenye kilometa 750 ambapo Unguja na Pemba wanazo kilometa 675. Maeneo haya ni muhimu kwa Taifa letu kwa sababu yana samaki wengi wa kila aina pamoja na vivutio vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa na ni bahati mbaya sana Serikali imeshindwa kudhibiti eneo hili na chanzo hiki cha utajiri. Eneo hili muhimu linakumbwa na changamoto mbalimbali ambazo zinarejesha nyuma na kuvunja moyo wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto zinazokabili eneo hili la utajiri wetu ni pamoja na wavuvi haramu; (wavuvi wanaotumia mabomu, wavuvi wanaotumia nyavu zenye matundu madogo na wengine wanatumia gesi). Changamoto zote nilizotaja hapo juu ni baadhi tu lakini zote ni hatari sana. Kwa mfano, uvuvi wa kutumia mabomu unaharibu mazingira vibaya sana, unaharibu mazalia ya samaki (matumbawe), mapengo ya mikoko pamoja na kuharibu maji ya bahari; wanaua samaki wengi wadogo wadogo pamoja na kuharibu mazalia mpaka mayai ya samaki, hakuna kinachobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya nyavu zenye matundu madogo vile vile ni hatari kwa sababu hazibakishi zinavua mpaka samaki ambao hawafai hata kwa kula, hivyo inakaribiana na bomu, gesi pamoja na wanaotumia kemikali; athari zake zinafanana ingawa uvuvi wa kutumia kemikali na gesi ni hatari zaidi kwa sababu ni sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangazie kidogo katika wizi wa kimataifa katika Bahari Kuu kwa meli za kigeni. Pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali lakini bado tatizo hili lipo na ni hasara kwa Taifa. Meli za kigeni bado zinafanya magendo katika bahari yetu na kuangamiza uchumi wa nchi

yetu. Wataalam wanasema uvuvi haramu unalikosesha Taifa letu kila mwaka asilimia 80 ya mapato ambayo yanapatikana katika sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia uvuvi huu haramu unawakosesha mapato wavuvi wadogo wadogo wapatao 40,000 ambao wanashindwa kupata samaki wa kutosha. Udhibiti wa Bahari Kuu bado ni dhaifu na ndiyo maana wahalifu wanaendelea na uhalifu kila siku ambao unatukosesha zaidi ya dola milioni 220 kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tulipokamata Meli ya *MFV TAWARIQ* 2009 kuna meli gani nyingine ambayo imekamatwa? Takribani miaka saba (7) mpaka nane (8) hivi sasa. Je, Mheshimiwa Waziri hivi ndiyo tuseme hakuna meli zinazovua katika bahari yetu? Nishauri, ni lazima sasa Serikali iwekeze katika Bahari Kuu kwa maslahi ya Taifa na watu wake.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kuangalia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakulima Wadogo; Tanzania ni nchi ya wakulima na wafanyakazi lakini sekta hii ya kilimo inachukua asilimia 65.5 ya wakulima kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa nne wa hotuba yake. Kwa maana hiyo, ajira hii kwa Taifa ni kubwa sana na kuna haja ya Serikali kupitia Wizara yake kufikiria hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wadogo wadogo wana juhudi kubwa za kilimo na kwa kiasi fulani wanazalisha sana. Tatizo mazao ya wakulima yanaharibika na kuoza kwa kukosa soko. Mazao kama mahindi, maembe, nyanya, mananasi; matunda haya yanapotea kila mwaka na hivyo wakulima hawa wanapata hasara kubwa na kupoteza nguvu zao. Kwa sababu hiyo ni lazima kuwepo na soko la wakulima wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Ardhi; wakulima wengi sana wanatumia ardhi kinyume na mahitaji ya mazao yanayotakiwa. Ardhi ambayo inafaa kuotesha kunde wanaotesha mananasi na vinginevyo. Hivyo, ushauri wangu ni kwamba kuwe na utafiti kuhusu zao gani lioteshwe katika ardhi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utunzaji Mbaya wa Chakula; ni jambo la kusikitisha sana kuona wakulima wakizuiliwa kuuza mahindi yao nje na matokeo yake yakanunuliwa na Serikali na kuhifadhiwa *NFRA,* tani 13.583 yenye thamani ya Sh.6,793,310,000/=. Mahindi haya yaliharibika na yamesababisha hasara kubwa kwa Serikali. Hata hivyo, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi akizungumza na waandishi wa habari alisema anatarajia kuwa mahindi hayo hayakuharibika. Je, ni hatua gani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi alichukua dhidi ya uzembe huu uliosababisha hasara kubwa kwa Serikali? (kwa kupoteza Sh.6.793,310,000/=)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Migogoro ya Wakulima na Wafugaji; kwa taarifa tunazo hekari milioni 88.6 za nchi kavu. Hekari milioni 60 ni mbuga zinazomfaa mfugaji. Mbuga hizi zina uwezo wa kulisha mifugo milioni 20 *(livestock unit),* zilizopo ni 17.1 milioni. *Unit* tulizonazo ni 20, kwa maana hiyo Serikali ina uwezo mkubwa wa kuondoa mzozo/mgogoro huu. Kwa hiyo zitumiwe hizo *units* milioni 17.1 kutoka *units* milioni 20 kutatua mgogoro huu wa wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi wa Bahari Kuu; meli za uvuvi wa Bahari Kuu zinatolewa leseni *dollar* 50,000 na kuruhusiwa kuvua samaki idadi yoyote na wale wa ziada wanatupwa. Mheshimiwa Waziri analijua hili, lakini agizo lake la samaki wa ziada waletwe nchini ni kwa sheria gani? Huu ni upotevu wa makusudi wa mazao ya bahari kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kuwe na sheria maalum kwa idadi ya uvuvi wa samaki wa Bahari Kuu na

kuwe na sheria inayowataka wavuvi kuwapeleka samaki wa ziada nchini kinyume na angazo la Waziri pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na Kiti chako, napenda kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho wakulima hawajalipwa; kutokana na taarifa za TAKUKURU mwaka 2015/2016 wakulima wa Mkoa wa Mtwara wa zao la korosho hawajalipwa bilioni thelathini na vyama vya msingi. Hali hii imekuwa inawavunja nguvu sana wakulima kwa kuwa Serikali ilijigamba kwa kiasi kikubwa kuwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unamsaidia mkulima. Hata hivyo, pamoja na wizi wote huu kwa wakulima wanyonge, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malipo ya Korosho 2016 Mtwara Mkindani; Mtwara Mjini kuna *AMCOS* mbili, moja ya Naliendele na nyingine ya Mikindani. Wananchi wameniambia wamepeleka korosho zao kwenye vyama hivi vya msingi lakini cha ajabu;

(a) Baadhi yao mpaka sasa hawajalipwa.

(b) Kuna minada mine ambayo ilifanyika mfululizo lakini vyama hivi vimelipwa minada ya tatu na nne (ya mwisho na kuacha ya kwanza ambayo ilikuwa na bei kubwa).

(c) Korosho kuuza kwenye mnada Sh.4,000/= lakini wananchi wamelipwa Sh.3,100/= (elfu tatu na mia moja) tu au chini ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakulima hawa walipwe pesa zao haraka iwezekanavyo na wahusika wote wachukuliwe hatua stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pembejeo ya Salfa *(sulfur)*. Naomba sana Serikali inunue pembejeo na kugawa bure kama ilivyoahidi. Kuna wakulima ambao wanahitaji salfa ya maji ambayo wanadai ni nzuri kuliko ya unga, hivyo, wasikilizwe wakulima hawa juu ya salfa hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uvuvi Mtwara. Mtwara kuna Bahari ya Hindi yenye samaki wengi sana. Naomba Wizara ijenge viwanda vya samaki kama ilivyo Mwanza. Viwanda vya samaki vikijengwa itasaidia watu wetu kupata ajira na kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zana za Kisasa za Uvuvi; Wizara hii kazi zake ni pamoja na kuhakikisha inawasaidia Watanzania wavuvi waweze kuvua uvuvi wa kisasa. Naomba Wizara itenge pesa ya kutosha ili kununua zana za uvuvi, mfano boti za kisasa na mashine za boti hasa kwa wavuvi wa Mikindani, Misete na Kianga ambako wanavua uvuvi ambao hauna tija kwa sababu hawana vifaa vya kisasa. Serikali itenge pesa za kutosha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Cooperate Social Responsibility.* Wizara kwa mwaka 2016/2017 imekusanya pesa nyingi sana za mapato ya korosho, lakini jambo la ajabu hivi vyama vya msingi havina mchango wowote kwenye kusaidia jamii. Hakuna shule hata moja kupitia fedha nyingi zinazokusanywa katika korosho, Bodi ipo, vyama vya ushirika vipo wanakusanya pesa nyingi sana, kwa nini hawasaidii katika elimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara itoe miongozo ili pesa za korosho Kusini zitumike kuinua kiwango cha elimu Kusini. Serikali inakusanya pesa nyingi kwenye korosho kuliko zao lolote lile nchini, vyama vya ushirika vya korosho viwe vinasaidia elimu kwa lazima Mtwara.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Charles Tizeba pamoja na Naibu wake Mheshimiwa William Tate Olenasha kwa kazi

nzuri katika Wizara hii. Naomba pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara Eng. Mathew Mtigumwe pamoja na timu ya watendaji wa Wizara hii kwa jitihada zao. Hata hivyo ninayo machache:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Katibu Mkuu kwa hatua alizochukua za kuhakikisha kuwa wakulima wangu wa kahawa wanalipwa. Pili, tunapongeza Wizara kwa kuweka kipaumbee katika zao la korosho na hivyo kutoa ruzuku katika pembejeo za madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Nyasa ni wakulima wa kahawa na uvuvi. Kwa upande wa wakulima Serikali imekuwa ikiwapa *support* ya kuwajengea maghala na pembejeo za mbolea (ruzuku).

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa wavuvi mazingira yao ya uvuvi ni duni sana. Mialo imekuwa na vibanda duni na hata mitumbwi yao ni duni. Wavuvi hulazimika kumwaga dagaa ziwani wakati wa mvua kwani hawana *drying shed.* Serikali ina mpango gani wa kuwainua kundi hilo kwa kurekebisha mazingira yao ya biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la samaki wanaoitwa vituwi, wavuvi wa nyasa wanasikitika kuwazuia kuvua samaki hao kwa kutumia nyavu za saizi ndogo, wao wanadai kuwa samaki hao hawakui. Naomba ufanyike utafiti juu ya suala hilo. Nitanyimwa Ubunge kwa ajili ya vituwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zao la mihogo; Wilaya ya Nyasa Kata ya Kihagare bado ina mihogo ya asili (Gomela) ambayo ina ladha nzuri sana. Baada ya kuleta mbegu za kisasa wakulima wengi walihamasika kwa mbegu mpya, lakini katika kuchemsha ladha ya mbegu mpya haina uzuri kama gomela. Matokeo yake Gomela imesababisha utamaduni wa wizi. Ukipanda Gomela iwe katikati, pembeni, vyovyote vile ikikua lazima iibiwe. Mimi pia niliibiwa. Naomba Wizara ifuatilie mbegu hiyo ili isipotee, ni mbegu nzuri sana na inaweza kufaa zaidi hasa kwa kitafunwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ruzuku za injini za boti, utaratibu ukoje? Kwa nini zisitengwe fedha za kuleta maboti ya mbegu ili kuwasaidia wavuvi kununua yakiwa jirani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kuwaomba kutembelea Jimbo langu la Nyasa. Nawatakia kazi njema.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha hotuba hii na kuiwasilisha kwa utaalam mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikopo ya Pembejeo; napenda kuipongeza Serikali yetu kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo wakulima wetu. Wakulima wetu ni wa kipato cha chini sana (maskini), hivyo ni nyema kuwapatia mikopo hii. Naiomba Serikali izidishe jitihada ya kuwapatia mikopo na kuwawekea mazingira rafiki wakulima wetu ili waweze kufikia malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Uvuvi; sekta ya uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi na wananchi wetu. Hivyo ni vyema Serikali yetu ikachukua juhudi za makusudi katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwaendeleza wavuvi wadogo, kuwapatia elimu na kuwapatia vifaa vya kisasa. Serikali ni lazima ichukue na iwe na mpango maalum wa kuwaendeleza na kuwapatia elimu wavuvi wadogo. Wavuvi wetu wanajitahidi sana lakini bado hawana mwelekeo, bado wanafanya kazi ya uvuvi kwa mazoea. Ni vyema Serikali iwapatie elimu na miongozo juu ya kujiendeleza. Aidha, Serikali iwapatie vifaa vya kisasa vya uvuvi. Hivi sasa vifaa ambavyo wavuvi wetu wanavitumia bado ni vya kizamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kupata nafasi hii ili nitoe mawazo yangu katika Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara hii iangalie suala la maji upande wa mifugo yetu. Tunaishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria ambao utatoka Solwa – Tinde – Nzega – Igunga – Tabora na maeneo mengine. Naomba Wizara itambue kwamba matumizi ya maji si kwa binadamu tu, ni nyema wakajenga mabirika kwa ajili ya kunyweshea mifugo yetu ili tatizo la maji lipungue au liishe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Kilimo izingatie mradi wa umwagiliaji wa Kijiji cha Ishololo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Serikali imetumia fedha nyingi katika mradi huu lakini hauna tija kwa kuwa ndani ya mwaka mmoja tuta lilishabomoka na hivyo kufanya bwawa hilo kutokuhifadhi maji kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo mkandarasi aliyefanya kazi hiyo ameacha mashimo mengi katika eneo hilo la bwawa na kuonekana kama uchafu na ni hatari kwa watoto wadogo hata watu wazima pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa mambo yote. Pili, nakushukuru wewe binafsi kwa umahiri wa kazi yako ya hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza mchango wangu juu ya suala zima la uvuvi. Uvuvi hapa Tanzania ni sekta ambayo ikiwekezwa vizuri inaweza ikatoa mchango mkubwa sana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebarikiwa kwa kuwa na eneo kubwa la bahari, mito, maziwa na eneo kubwa la mabwawa ambayo maeneo hayo yamesheheni rasilimali kubwa ya samaki na mazao mengine ya baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahari ni kama shamba lililosheheni samaki wengi wa kutosha, shamba ambalo halihitaji mbolea, madawa wala halihitaji pembejeo ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahari yetu ni shamba linalotaka kuvunwa tu na mazao yake ni muhimu na ni bidhaa unayoweza kuuza duniani popote. Kwa fursa hii tuliyoipata kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwa na bahari kubwa yenye samaki wengi hatukuwa na sababu yoyote kuwa soko la kununua samaki kutoka nchi nyingine. Hata hivyo, ni ukweli usiopingika kwamba Tanzania kweli ni soko la nchi nyingine kama Afrika ya Kusini, China na nchi nyingine kwa kununua samaki na kutumika hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa samaki baharini ni pamoja na kuwepo dhamira ya makusudi ya Serikali ya kuweka miundombinu ya kisasa na ya uhakika. Nipende kusema kwamba katika eneo hili Serikali haijaonesha utayari kwa kuifanya sekta ya uvuvi kuwa mchangiaji mkubwa kwenye pato la Taifa. Hii ni kwa sababu hatuoni juhudi kubwa ya Serikali kutayarisha miundombinu sahihi ya kumudu uvuvi kama vile zana za kisasa zenye uwezo mkubwa wa kuvua bahari kuu, lakini pia ujenzi wa bahari ya uvuvi, vyuo vya uvuvi vitakavyotoa wahitimu wenye uwezo mkubwa lakini pia uwepo wa viwanda ili samaki wakivuliwa waweze kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la sekta ya uvuvi kama Serikali itachukulia umuhimu wa kipekee ndio mwarobaini utakaolisaidia Taifa kuongeza mapato na kutoka katika hatua hii na kulisogeza Taifa mbele katika nyanja mbalimbali. Sekta hii ikipewa fursa pia itaweza kutoa fursa nyingi za ajira kwa Watanzania na kutoa unafuu wa maisha kwa kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iitendee haki neema ya uvuvi na kuitendea haki neema hii ya bahari tuliyonayo tunaweza kuondokana na umaskini wa kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kiujumla wake. Namwomba Mheshimiwa Waziri japo kwa uchache atupe maelezo ya kina kuhusu uvuvi, Serikali imejipangaje?

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwake Mheshimiwa Waziri Charles Tizeba na Naibu Waziri Mheshimiwa William Olenasha kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na timu yao, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara. Hotuba yao ni nzuri na imejitosheleza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji lishe bora kwa wananchi wote wa Tanzania. Ni muhimu tuwahakikishie upatikanaji wa mboga na matunda kwa mwaka mzima kwa bei nafuu. Wizara ianzishe *Drip Irrigation* kila Wilaya kwa kutumia visima virefu. Kilimo hiki pamoja na kuboresha lishe ya jamii kitasadia kuongeza kipato hasa kwa makundi ya wanawake na vijana. Pia kitaongeza ukuaji wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zitembelewe na ukaguzi ufanyike kuhusiana na tozo kubwa wanazotozwa wavuvi. Yapo malalamiko ya kwamba wavuvi kule Mtwara wanalipa dola 500 kwa kila kilo moja ya samaki wanaovuliwa kutoka Msumbiji na hivyo kupelekea hasara kwani bei ya kuuzia huwa ni ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana kwa usimamizi mzuri wa zao la korosho. Kwa msimu huu umakini uongezeke katika ugawaji wa pembejeo kwa wakati na udhibiti wa kangomba. Kutokana na bei nzuri ya korosho ya mwaka uliopita wakulima wengi sasa wanaomba mfumo wa stakabadhi ghalani kwa mazao mengine kama mbaazi. Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha mfumo huu kwa mazao mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na ninaitakia Wizara kila la heri.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Tumbi kimesahaulika kwa ukarabati wa majengo, upungufu wa wakufunzi, mashamba darasa kutengewa fedha za kutosha. Mashamba darasa hayo yanatumika kwa kufundishia kwa vitendo; madai ya watumishi yalipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zao la tumbaku, natoa pongezi kwa kutatua tatizo la wakulima wa zao hilo kutoka Chama Kikuu cha Ushirika cha *WETCU.* Niombe Serikali kuhakikisha madai ya wakulima ambao walipunjwa na wanunuzi ili walipwe haki zao. Pembejeo zipelekwe kwa wakati, watumishi wanaodai haki zao *WETCU* walipwe kwani ni ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya Kilimo, nashauri benki hiyo tufunguliwe dirisha Tabora ili wakulima waweze kukopeshwa. Wakulima wakopeshwe matrekta ili wapunguze umaskini kwa kulima kilimo cha kisasa. Wakulima watafutiwe masoko ya uhakika kwa mazao yao. Tuombe benki iweze kusaidia wakulima wadogo wadogo hasa wanawake, wafugaji pamoja na wavuna asali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kupunguza zaidi idadi za tozo hususani kwenye zao la tumbaku ili bei ya uuzaji ipande. Kiongozi wa Ushirika angalau awe kidato cha nne, kwani kukosa elimu kwa viongozi kunachangia kuibiwa kwa fedha za wakulima. Pia mizani ya kupimia tumbaku (uzito wa kilo) iwe inakaguliwa mara kwa mara, masoko ya tumbaku yasicheleweshwe kwani kuchelewa kununua kunapunguza uzito, ndio ujanja wa wanunuzi na mawakala wao. Tuwasaidie wakulima wetu kama azma ya Serikali ya Awamu ya Tano.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wa Wizara hii, Dkt. Charles Tizeba pamoja na

Mheshimiwa William Olenasha pamoja na Makatibu wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze moja kwa moja kutoa mchango wangu katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ambayo ni Wizara nyeti inayotegemewa na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera tumebarikiwa kwa kuwa na ardhi nzuri yenye rutuba na hali ya hewa nzuri yenye mvua za kutosha. Mkoa wa Kagera kilimo kimekuwa cha kusuasua kutokana na changamoto mbalimbali ikiwemo teknolojia duni pamoja na pembejeo kutokufika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoani kumekuwa na miundombinu mibovu ya kusafirisha mazao kutoka shambani hadi kwenye masoko. Naomba Wizara husika iweze kuwasiliana na Wizara ya Uchukuzi ili waweze kutuwekea miundombinu mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa ya mimea kwa mazao ya chakula yamekuwa yakiongezeka sana. Katika mkoa wa Kagera zao la mgomba linalolimwa na kutegemewa na wananchi wa Mkoa huo linashambuliwa na ugonjwa wa mnyauko ambao unatutesa sana kwa sababu ndizi ndicho chakula kikuu kwa mkoa wetu. Hivyo naomba Serikali itusaidie kutokomeza ugonjwa huo ili wananchi wa Mkoa wa Kagera waweze kunufaika na zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wangu wa Kagera umebarikiwa kwa kuwa na mazao ya biashara kama vile kahawa na miwa. Kwenye zao la kahawa tuna changamoto ya masoko kiasi kwamba inasababisha wananchi kwenda kutafuta soko nchi jirani. Naiomba Serikali iweze kutatua changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa miwa napenda kuishauri Serikali kuweka mashamba darasa kwa

wakulima wadogo wadogo ili waweze kuungana na wakulima wakubwa na hivyo waweze kupata utaalamu wa kulima kisasa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kama Serikali na Wizara ya Kilimo wakiweza kuutumia Mkoa wa Kagera nina uhakika unaweza kuzalisha sukari ya kutosha nchini kwetu na kuuza nje ya nchi. Mawakala wa pembejeo za kilimo mpaka sasa wameendelea kupigwa dana dana kwa kutolipwa fedha zao. Tukumbuke mawakala wengi walichukua fedha za mikopo kwenye benki na sehemu nyingine kama dhamana hali iliyosababisha wengine kupigiwa minada nyumba zao na hivyo kusababisha wengine kupoteza maisha kwa ajili ya *pressure (blood pressure).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawakala wote nchi nzima wanaidai Wizara ya Kilimo shilingi bilioni 64.4 ambapo Wizara inawapiga dana dana na hawajui hatima ya deni lao, japo Wizara ya Kilimo inasema bado ina hakiki uhalali wa deni hilo. Basi ni vyema Serikali ikaanza kuwalipa wale iliyojiridhisha kuwa wanastahili kulipwa na wale ambao bado hawajajiridhisha Wizara iangalie namna ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usalama kwa wavuvi haupo vizuri wakiwa ziwani au baharini, wanatekwa na majambazi, wananyang'anywa samaki na wengine kupoteza maisha. Ninaomba Wizara waweke doria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi wasitozwe leseni zaidi ya mara mbili na kwa kweli ninaomba Wizara iwaangalie kwa jicho la huruma hawa wavuvi wanaoingiza nyavu ambazo hazifai. Itawasaidia wavuvi kupata nyavu zinazokubalika, za kiwango kuliko kuchukua mbovu ambazo zinawaletea hasara zikishachomwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kipekee kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri na watendaji wote kwa kutimiza ahadi ya kuondoa kodi/tozo ambazo zilikuwa zinamdidimiza mkulima. Mheshimiwa Rais wetu kila anapoahidi lazima atekeleze, namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu, tunapoongelea Tanzania ya viwanda na kwenda kwenye uchumi wa kati lazima tuwekeze nguvu yetu kwenye kilimo cha kisasa, kilimo kilichofanyiwa utafiti, kilimo chenye kumuwezesha mkulima kupata mbegu bora, kilimo ambacho kitamuwezesha Mtanzania kupata soko la uhakika lazima tuweke miundombinu wezeshi kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu Watanzania zaidi ya asilimia 65 ni wakulima. Pamoja na hayo ukweli ni kwamba sekta hii imesahaulika kabisa hasa hasa maeneo ya vijijini ambako wakulima wamekata tamaa. Kilimo ndio uchumi wa Taifa, ninaamini tukiwekeza nguvu yetu kwenye kilimo Taifa letu litainuka kwa muda mfupi. Taifa letu limejaliwa maji mengi sana yaliyo ardhini lakini pia tuna vipindi vingi vya mvua, karibu nchi nzima tunapata mvua ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali kwa kodi na tozo mbalimbali zilizoondolewa kwenye mazao. Hata hivyo bado zipo kodi nyingine ambazo hazijaondolewa. Niombe Serikali kuziondoa ili mkulima aweze kufaidi bei nzuri za mazao. Pia niiombe Serikali kutoa bei elekezi kwa kila zao kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishauri Serikali kujifunza katika mataifa mengine ambayo mataifa hayo ni

yenye ukame, lakini mataifa hayo yametumia kilimo cha umwagiliaji ambacho kimeinua mataifa hayo yamepaa sana kiuchumi kupitia sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee ufugaji, kama tunataka kuondoa migogoro mingi ya wakulima na wafugaji lazima tuhakikishe tunalinda maeneo ambayo yalitengwa kwa ajili ya wafugaji na wakulima ili wananchi wetu wasiendelee kuuana na kuondoa chuki kati yao ambayo inaendelea kukua na kuleta matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea hili kwa sababu maeneo mengi yaliyotengwa yamevamiwa na watu, Serikali ipo na inaiona migogoro hii ambayo mpaka leo hii ni mikubwa. Nasema haya nikiwa na ushahidi, kwenye Jimbo langu Serikali ilitenga maeneo ya wafugaji, yakatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na kupewa GN. 620 ya mwaka 1987, lakini maeneo hayo yamevamiwa na matajiri na kuzungushia uzio na tayari wamepatiwa hatimiliki ya miaka 99, Serikali imekaa kimya wafugaji wanateseka hawana maeneo ya kufugia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri kulifuatilia jambo hili ambalo limeleta mgogoro mkubwa Jimboni kwangu. Pia nataka kujua eneo ambalo lilitangazwa na Serikali na kupewa *GN* linawezaje kubadilishwa matumizi bila tangazo lingine la kubadilisha tangazo la kwanza? Tusipomaliza migogoro hii italeta matatizo makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimwia Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii kwa muda mrefu inabadili matamko kuhusu kilimo, lakini hakuna tamko hata moja lililofanikiwa katika kuboresha kilimo na kuleta matokeo chanya. Kwa mfano pamoja na Serikali kusema Mkoa wa

Morogoro ni ghala la chakula, lakini ukifuatilia kwenye mkoa huo hakuna jitihada za makusudi za kuufanya mkoa huo kuwa ghala la chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kumaliza tatizo la wakulima na wafugaji, kuboresha upatikanaji wa pembejeo, kuajiri wagani hasa Jimbo la Mlimba ambapo hali ya wataalam wa kilimo na mifugo ngazi za kata hakuna. Kwa hali hii kilimo kitakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la mchele Serikali kwa miaka yote hamumtendei haki mkulima wa mpunga na kumuacha mkulima kutokuwa na soko la uhakika na kumuongezea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itilie mkazo uanzishaji wa mabwawa ya samaki ili kuboresha maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo, mifugo na uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta hizi zimeendelea kutoa mchango mkubwa ikiwemo kuwa chanzo cha kipato kwa asilimia 65 ya Watanzania, kuhakikisha usalama wa chakula, kuchangia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 28 na mauzo ya nje kwa zaidi ya asilimia 24. Ingawa sekta hizi ni muhimu sana lakini zina changamoto nyingi sana ambazo zinaathiri ukuaji wake; changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

(i) Utengaji na utoaji mdogo wa fedha za bajeti ya maendeleo.

(ii) Wataalam wa utafiti kuwa wachache ama kukosekana.

(iii) Miundombinu duni kwa mfano utoaji wa taarifa za tahadhari na upungufu wa viwanda vya bidhaa zake.

(iv) Athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa mfano kuongezeka kwa ukame, magonjwa ya mimea na mifugo, mvua zisizotabirika na mashamba kuingiliwa na maji ya chumvi na kuathiri mazao na vyanzo vya maji baridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka 2017/2018 si wakuridhisha japo kwamba sekta hizi hutoa mchango mkubwa sana kwa Taifa. Takwimu zinaonesha kwamaba wastani wa bajeti ya Wizara kwa sekta hizo ni asilimia 2.2 kwa kipindi hicho tu ya Bajeti ya Taifa ambacho ni kiwango kidogo sana ukilinganisha na lengo la kufikia asilimia 10 kama Serikali ilivyoridhia katika Azimo la Malabo kwa kipindi cha mikaka mitano ya mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kwa Wizara hii ni kuwa haijapewa kipaumbele cha kuridhisha katika Bajeti ya Serikali japokuwa vimeendelea kutoa mchango mkubwa kwa Taifa ukizingatia kwamba tunakwenda kwa kasi ya Tanzania ya viwanda. Pia mabadiliko ya tabianchi yameendelea kuathiri maendeleo ya sekta hizi na Taifa, jambo ambalo pia limesisitizwa na Waziri wa Fedha na Mipando kwenye Bunge mwezi Machi 2017; kwa hiyo napendekeza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kuwe na utengenezaji wa bajeti halisi na utoaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kwa kuwa wastani wa utoaji wa fedha kwa sekta hizi ni chini ya asilimia 60. Hivyo naishauri Serikali ifanye marejeo katika utaratibu wa utengaji wa fedha za bajeti ili kufuata uhalisia wa makusanyo yake japo kwa Mheshimiwa Rais ameonesha jitihada kubwa ya kupunguza rushwa na matumizi yasiyo ya lazima na tija kwa raia lakini utoaji wa fedha wa bajeti uwe wa kutosha na kwa wakati, kwa hiyo, Serikali inahitajika.

Mheshimiwa Mwenyeki, pia kuongeza jitihada na kuweka mikakati mahususi na kabambe ya upataji wa mapato ya nje ya vyanzo vya kodi. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa Bunge Machi mwaka huu

inaonesha kuwa vyanzo vingine vya mapato kutofanya vizuri ukilinganisha na vyanzo vya kodi. Hii inajumuisha misaada ya wahisani, mapato ya Serikali za Mitaa na mauzo ya nje, pia uwekezaji mzuri wa misaada ya wahisani na mikopo tunayopata ili kupunguza na kuacha kabisa uteegemezi huo kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza utengaji wa bajeti ya maendeleo kutoka vyanzo vya ndani kwa mwaka 2016/2017. Vyanzo vya ndani vilichangia kwa asilimia 26 tu ya Bajeti ya Wizara ambapo mwaka 2017/2018 inategemewa kupanda mpaka kufikia asilimia 40 ya makusanyo ya mapato kwa vyanzo vya ndani kutokana na sekta husika kuboreshwa na kuwa za kisasa zaidi. Hii inajumuisha matumizi ya pembejeo na zana bora za kilimo, kuwekeza katika miundombinu bora ya kilimo, mifugo na uvuvi na kuboresha tafiti. Haya yakifanyika yatasaidia kufikia na kuvuka malengo ya ukusanyaji wa maduhuli kwa Wizara ambayo bado yapo chini kwa mwaka 2016/2017 ambapo lengo lilikuwa ni kukusanya kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni nne kiwango ambacho ni kidogo sana ukilinganisha na uwezo wa sekta hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi kupewa kipaumbele, yaani ni kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika bajeti ya Wizara na sekretalieti za mitaa. Ninatambua jitihada zilizofanywa na Wizara hii kuhuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango yao, hata hivyo bado hicho hakijafanyika vizuri katika bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukizingatia masuala ya kijinsia, yaani ni kuandaa na kutoa taarifa za kibajeti zenye mchanganyiko na mchanganuo wa kijinsia. Taarifa hizi za mchanganuo zitasaidia zaidi katika mipango na maamuzi katika sekta hizo ambazo zinachangiwa zaidi na wanawake. Hivyo basi mahitaji maalum yatatambuliwa na kuwekewa mikakati mizuri na imara ya utekelezaji. Vilevile kuboresha mkakati wa kuwasaidia wakulima wanawake wadogo wadogo. Hivyo Wizara na Serikali kiujumla inahitaji kupitia upya na kuboresha utekelezaji wa kuwasaidia wakulima

wanawake na wakulima wadogo wadogo ili waje na mrengo wa kijinsia na hivyo kuwasaidia ikiwemo katika upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuajiri Maafiasa Ugani wa kutosha, hii itaongeza uwezo wa Serikali kutoa elimu ya ugavi kwa sekta hizo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi. Hivyo agizo la kusitisha ajira zikiwemo za maafisa ugani lisitishwe, Wizara iombe kibali mara moja cha kutoa ajira kwa mamlaka husika, na pia suala hili liwekwe katika bajeti za Halmashauri zote zenye uhitaji ili kufanikisha utekelezaji wake. Pia kuboresha uwezo wa maafisa waliopo ili kuendana na mabadiliko ya taaluma na teknolojia kwa kupewa mafunzo rasmi ya vyuoni, semina elekezi na pia ziara ya mafunzo kwa maeneo mengine ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ya viwanda haitakuwepo kama kilimo hakitapewa kipaumbele na kuzitumia sekta hizi vizuri na kuziboresha na kuziwekea bajeti ya kutosha na kufika kwa wakati kwa maslahi ya umma na Taifa hili kwa ujumla wake. Vilevile kuweza kuithamini kauli yetu ya kuwa kilimo ni uti wa mgongo na kilimo kwanza yenye Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kuchangia. Naunga mkono hoja ya hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani katika kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia Waziri Kivuli, Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na Kamati ya Kilimo katika maoni na ushauri ilioutoa katika kitabu chake ukurasa wa tatu. Inashangaza kuona wafadhili wanatoa fedha nyingi kufadhili kilimo kuliko Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ili tuendelee tunahitaji mambo manne; moja, ardhi – kilimo, ujenzi, ufugaji, viwanda, barabara na kadhalika; pili, watu – wakulima, wafanyakazi

na wafanyabiashara; tatu, siasa safi - kwa kuwa haipo; nne, uongozi bora – hakuna sababu. Uongo na mipango isiyotekelezeka. *If you fail to plan, you plan to fail.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tupo hapa kwa kuwa *plans* zetu zote tume-*fail* na tunapeleka mambo kisiasa ili kuvutia wapiga kura. Asilimia 75 ya Watanzania ni wakulima. Wizara hii ni nyeti na ni uti wa mgongo wa Taifa letu, inachangia 29% ya pato la Taifa letu na inatoa ajira 75% ya watu wetu. Kwa masikitiko makubwa, bajeti iliyotengwa ni 3.0%. *It is the shame,* hapa Serikali inafanya utani na kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa katika bajeti; wafadhili 78%, fedha zetu 21%. Fedha zilizotengwa katika bajeti, shilingi bilioni nne mifugo, shilingi bilioni mbili uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkanganyiko/ ugumu katika taasisi za fedha; wakulima ni wachangiaji na wazalishaji wakubwa katika uchumi wa Taifa letu, lakini ndio wanadharauliwa mno na Serikali haina *mission* wala *vision.* Wakulima katika benki wamewekewa masharti magumu, pamoja na kuwa na hatimiliki za ardhi, nyumba na vyombo vya moto. *CRDB (Co-operative and Rural Development Bank)* enzi za Mwalimu *(by definition)* ilikuwa ndiyo benki yao wakulima. Je, leo *CRDB* ni ya wakulima? Ni ya wafanyabiashara na wawekezaji. Yamewekwa mazingira na dhana kuwa wakulima hawakopesheki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni kizungumkuti, Tanzania haijaamua kutoa kipaumbele katika kilimo *(first priority)* kwa kuwa kilimo kinaendeshwa kisanii kwa matambo na misamiati mingi na siasa kibao:-

(i) kilimo cha kufa na kupona;

(ii) kilimo cha ujamaa na kujitegemea;

(iii) kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu;

(iv) kilimo cha bega kwa bega; na

(v) kilimo kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa misamiati hii ndiyo tutavuna mahindi, mpunga, viazi, mtama, ngano, alizeti, pamba na karafuu? Serikali ijipange na tusiwe wababaishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tumbaku na soko la nje, kilogramu 32,000 ni sawa na *3.2 tonnes* iliyouzwa Uturuki kutoka Tanzania. Nchi nyingine wanaolima tumbaku wameuza tumbaku kilogramu 939,000,000, Uturuki *(Europe).* Hii inadhihirisha namna gani Serikali haiko *serious* katika mambo ya kiuchumi tofauti na nchi za jirani, *Mozambique,* Rwanda, Kenya, Uganda, na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanga na zao la mihogo na matunda. Tanga ni wazalishaji wakubwa wa mihogo hususan katika maeneo ya vijijini. Mfano, maeneo ya Kirare, Mapojoni, Pongwe, Kisimatui, Marungu, Mkembe, Mpirani, Mabokweni, Putini, Bwagamoyo na kadhalika. Mihogo ya Tanga ni mihogo bora, mitamu na haina sumu ukilinganisha na mihogo ya maeneo mengi katika Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mihogo ya Tanga haina soko la uhakika ndani na nje ya Tanzania. Siku za karibuni China walitoa tangazo *(tender)* kwa kutaka zao la muhogo katika mitandao/*media.* Je, Serikali ya Tanzania, Mheshimiwa Waziri anatuambie? Wamelifuatilia soko hilo vipi? Wamefikia hatua gani ya majadiliano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu uvuvi na siasa za Tanzania. Norway ni nchi tajiri na mfadhili mkubwa katika miradi mingi ya kimaendeleo Tanzania na Afrika nzima. Utajiri wao unatokana na uvuvi ambao wameamua kuwekeza, kutafiti na kushughulika kikamilifu. Tanzania tunazo *1,400 cubic kilometres (Indian Ocean)* kutoka Jasini – Mkinga – Tanga hadi Msimbati – Mtwara; ni bahari tupu na kuna samaki wa kila aina. Humo *Indian Ocean* kuna gesi pia, lakini

Watanzania *(Coastal zone are very poor people),* ndio maskini wa kutupwa. Badala ya Serikali kuwasaidia, vyombo na nyavu zao zinachomwa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba Serikali ithamini watu wa Ukanda wa Pwani katika Mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Unguja, Pemba na Mafia kwa kutafuta wawekezaji *(investors)* wa viwanda vya kusindika samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijengwe vyuo vya uvuvi kwa ajili ya elimu ya uvuvi wa kisasa. *If you fail to plan, you plan to fail.* Jambo lolote likifanywa kitaalam (kielimu) linakuwa na manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvuvi *(registration fees 20,000 under 20mt boat);* Serikali iondoe tozo/kodi ambazo ni kero kwa wavuvi. Tukiachilia mbali kodi iliyoondolewa kwa vyombo vyenye urefu chini ya mita 20, lakini bado Halmashauri inatoza tozo na Serikali Kuu inatoza tozo ya leseni kwa kila baharia. Leseni alipe nahodha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, katika vyombo vingine kama *bus*, anaulizwa leseni dereva na siyo *conductor* wala *turn boy?* Kwani wavuvi ni wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika meli meli/*ferry boat* anahojiwa *captain* tu. Kwa nini wavuvi wanatozwa leseni? Samaki wao wanatozwa ushuru na vyombo vyao *registration fees* na kodi ya mapato *(revenue).* Matrekta hayana kodi, lakini mashua zina kodi kubwa. Badala ya kukamata vyombo na nyavu za wavuvi wadogo na kuzichoma (hasara), wazuie utengenezaji wa nyavu ndogo katika viwanda vyetu na iache kuchukua kodi na itoe vipimo vya nyavu *(size)* zinazohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba kwa kuwa mara kwa mara wakati wa kaskazi ajali nyingi hutokea, hivyo Serikali iwe na *Rescue Team Department* isaidie kuokoa ajali zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mifugo, kuna usafirishaji katili, wanyama wengi wanateswa/kufa katika usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna gharama kubwa za dawa kwa ajili ya kilimo na mifugo. Wanyama hawatendewi haki Tanzania kwa sababu hakuna chama cha kutetea haki zao. Wanyama kama ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku wanasafirishwa katika vyombo vidogo na wanabanana na kuumia hadi kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Wizara iliangalie suala hili kwa umakini kwa kuwa hata wanyama wetu wanakosa soko bora kwa kuwa nyama yao huwa na dosari.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara kuboresha mnada wa Pugu ambao unaitwa mnada wa kimataifa ili kufanana na jina lenyewe kwa kupeleka maji na kuboresha barabara inayoenda mnadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna mnada wa kimataifa Pugu, bado hakuna machinjio ya kisasa ila kuna machinjio ya mtu binafsi Mazizini, Ukonga, lakini katika kata ya Zingiziwa Ukonga kuna eneo la wazi la kujenga machinjio ya kisasa na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango mzuri lakini fedha inayotengwa kwenye Wizara ni ndogo mara zote na wakati wote fedha ya ndani ni ndogo zaidi. Fedha ya nje ni kubwa kidogo. Vilevile fedha inayopatikana kwenye bajeti zinazotengwa ni fedha kidogo sana na mara nyingine fedha

ya nje inatolewa nyingi kidogo kuliko ya ndani. Maana yake ni kwamba kama Taifa tunaiacha sekta muhimu kuipa umuhimu wake, tunategemea wafadhili ambao wangependa kuona uchumi wetu hautengemai ili tubaki tegemezi kwa kila jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa kama ni mazoea kuwa kila mwaka pembejeo huwafikia wakulima kwa kuchelewa. Je, ni matarajio yapi yanayokusudiwa kuleta mapinduzi ya kilimo kwa utaratibu huu? Naomba Serikali itusaidie namna ya kumaliza kabisa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa yapo makampuni yanayojitangaza kuzalisha na kusambaza mbegu na dawa mbalimbali za kilimo, mengi yanakuwa *fake* na hakuna hatua zinachukuliwa hasa kwa dawa za kuua wadudu na palizi (kuuwa magugu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Kuboresha Kilimo *(ASDP)* inayokuwa na malengo ya kuongeza tija kwa mkulima, kuongeza uzalishaji ili kuhuisha viwanda, kuwezesha mkulima wa chini, kuongeza kipato na kuongeza thamani ya mazao ili wakulima na kilimo kwa ujumla kiwe ni kazi yenye kuleta manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iratibu katika mpango huu kuboresha barabara katika maeneo ya uzalishaji katika Jimbo la Nkasi Kusini. Barabara zifuatazo ni muhimu kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo, nazo ni barabara ya Milundikwa – Kisu - Malongwe ni muhimu kwa kilimo Jimboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kasu – Katani – Myula ni muhimu sana kwa maendeleo ya kilimo Wilayani. Vilevile barabara ya Nkomo II – Kipende, nayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nkasi Kusini tuna mabonde mawili yanayofaa kwa umwagiliaji, nayo ni Bonde la Kate lenye hekta 1,500 na Bonde la Namansi lenye ukubwa wa

hekta 440. Mabonde yote yameombewa fedha na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi lakini bado kupata fedha ya kuanza kujenga miundombinu ya kumwagilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ranchi ya Karambo ina ukubwa wa hekta za eneo 23,000 lina ng'ombe 710 tu, kondoo 215, farasi nane, uwezo wake ni ng'ombe 7,000. *Under-utilized.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *please* Serikali iongeze mtaji.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima na kuweza leo kuandika mchango wangu kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni sekta muhimu sana katika nchi yetu japo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake anasema kilimo kinaajiri asilimia 65.5 ya Watanzania wote. Jambo hili siyo kweli kwani Watanzania wengi wako vijijini na wanategemea kilimo kwa uchumi wao. Hivyo, kilimo huajiri zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania, lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba sekta hii haijapewa umuhimu unaostahili, ndiyo maana Wizara hii imetengewa fedha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa katika sekta ya kilimo ni uhaba wa masoko ya uhakika na bei ya mazao husika. Hamasa pekee ya kukuza kilimo ni bei nzuri ya mazao na soko la uhakika. Vilevile miundombinu ya barabara ni muhimu sana katika kukuza kilimo nchini, kwani kuna mazao kama vile viazi, nyanya na matunda yanashindwa kulifikia soko kwa kukosa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la ufuta kwa sasa linalimwa katika maeneo mengi katika nchi yetu. Hivyo ni wakati sasa Bodi ya Mazao Mchanganyiko ikatazamwa upya na ikiwezekana zao la ufuta likaundiwa bodi yake ili kuwapatia tija wakulima kwani hadi sasa tatizo kubwa la

ufuta ni uhakika wa masoko hasa kwenye mikoa ya Kusini (Lindi na Mtwara).

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali ingetilia mkazo sana ili mazao haya yasindikwe nchini badala ya kuendelea kuuza mazao ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgao wa chakula cha njaa ni bora ukazingatia mahitaji na kufuata jiografia ya nchi yetu. Mfano, Mkoa wa Lindi tunakuwa na uhaba mkubwa wa chakula kati ya miezi ya Desemba hadi Aprili. Hivyo, kuwapelekea chakula mwezi Mei ni sawa, kwani kipindi hiki huwa ni cha mavuno kwa wakulima wengi na shida ya chakula huwa imeisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwa mgao wa chakula cha msaada, mgao wa pembejeo za kilimo ni lazima uendane na mazingira halisi, kwani vipindi vya msimu wa mvua haulingani nchi nzima. Mfano, kwa Mkoa wa Lindi, mazao ya nafaka hupandwa mwezi Desemba hadi Januari na kwa zao la korosho uwekaji wa dawa huanza kati ya mwezi Mei hadi Julai. Hivyo, pembejeo ya zao la korosho zinatakiwa kuwafikia wakulima kati ya mwezi Machi na Aprili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta inayotegemewa zaidi katika usindikaji kwa mazao ya kilimo ni sekta binafsi, lakini Serikali haijaonesha dhamira thabiti ya utekelezaji wa jambo hili. Wawekezaji wengi wanashindwa kufanya hivyo, kwani gharama za uzalishaji hapa nchini ni kubwa sana na hii inatokana na wingi wa mamlaka zinazosimamia jambo hili. Kwa mfano, *TFDA, TBS, OSHA, EWURA* na kadhalika. Kodi ni nyingi sana hapa nchini, punguzeni kodi kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia njema ya kuwa na Vyama vya Ushirika nchini haijatusaidia sana, kwani elimu juu ya ushirika haijatosha, hivyo kupelekea Vyama vya Ushirika kuwa mzigo wa wakulima nchini. Vyama vingi vya ushirika badala ya kukuza masoko ili kusaidia wanachama wao, wenyewe ndiyo vimekuwa kikwazo kwa ustawi wa wakulima, ushindani wa kibiashara katika masoko ya

wakulima hakuwapi tija viongozi wa ushirika, hivyo wao huwakumbatia wanunuzi wachache kwa manufaa yao binafsi na siyo ushirika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Liwale tumepata mwekezaji wa zao la alizeti na yuko tayari kujenga kiwanda na uchujaji, lakini hadi leo mwekezaji huyu bado anazungushwa kupata ardhi. Japo Halmashauri ya Liwale ilishampatia ardhi ya kutosha, lakini Kamishna wa Ardhi bado anakuwa na kigugumizi katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wana-Liwale tunaomba mwekezaji huyu apatiwe ardhi ili Liwale tuweze kukuza ajira na uchumi wa Halmashauri yetu.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii ya kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kufuta kodi zenye kero kwa wakulima na wavuvi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kero kubwa ya taasisi ya Serikali ya Hifadhi ya Bahari Mafia (HIBAMA) kwenye mgao wa maduhuli yatokanayo na watalii wanaoingia katika maeneo ya hifadhi, Halmashauri ya Mafia inapata asilimia 10 ya pato halisi, yaani baada ya kutoa gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza asilimia 10 ni kiwango kidogo sana ukizingatia mzigo unaobebeshwa na Halmashauri kwenye kuendesha shughuli za afya, elimu na miundombinu. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri yeye ndiye mwenye kutengeneza kanuni, kwa kipekee tunamwomba sasa aridhie ombi letu la kubadili kanuni ili kiwango hiki kiongezwe kutoka asilimia 10 mpaka kufikia asilimia 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni hili la pato halisi *(net income),* baada ya kutoa gharama zote za uendeshaji za

hifadhi ya bahari zikiwemo semina, safari, likizo na malipo ya ziada, baada ya saa za kazi ibaki zile gharama za kukusanya mapato tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni uwekezaji unaofanywa na hifadhi ya bahari katika visiwa vya Shungimbili, Mbarakuni na Nyororo. Kimsingi sisi watu wa Mafia hatupingi mwekezaji, bali namna ya uwekezaji na mchakato mzima ndiyo unaacha maswali mengi bila majibu. Kitendo cha kutowashirikisha wananchi hakikubaliki hata kidogo. Ni ushauri wetu kwamba suala la mwekezaji liachwe kwenye ngazi ya Halmashauri kutoka hifadhi ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ongezeko la vijiji vya eneo la hifadhi ya bahari. Hifadhi ilianza na vijiji vinne tu, lakini leo imeongezeka mpaka kufikia vijiji 13 na Wilaya ya Mafia ina jumla ya vijiji 23. Ukweli huo zaidi ya nusu ya vijiji ipo chini ya himaya ya hifadhi ya bahari na sasa wananchi wanakatazwa hata kulima mbali ya kuvua. Kilio chetu ni kwa nini mchakato wa kuongeza vijiji vya eneo la hifadhi haikushirikisha wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ubinafsishaji wa kisiwa cha Nyororo na Mbarakuni usitishwe mara moja kwa maslahi ya Taifa hili ili kasa waweze kupata maeneo ya kutagia mayai yao, kuokoa kiumbe huyo asipotee katika sura ya nchi yetu.

Mheshimiwa Waziri, Meneja Mkuu wa Hifadhi ya Bahari awajibishwe kwa kosa la kuuza kisiwa cha Shungimbili kinyume na utaartibu wa kushirikisha wananchi na mwekezaji kujenga bila ya kuwa na kibali cha ujenzi *(building permit).* Vilevile huyu Meneja Mkuu alimwongopea Mheshimiwa Waziri alipofanya ziara ya kiserikali Mafia kuwa Halmashauri ya Mafia haidai hifadhi fedha za maduhuli, lakini baada ya Waziri Mkuu kuondoka, Hifadhi ya Bahari walilipa Halmashauri shilingi milioni 44. Kitendo hiki cha kumdanganya kiongozi mkubwa huyu mbele ya Mkuu wa Wilaya ni kitendo cha utovu wa nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara 106 katika ukurasa wa 68 wa hotuba inayozungumzia mazao yanayozalisha mafuta ya kula, Mkoa wa Kigoma ni mzalishaji mkubwa wa mawese na uzalishaji wake unaweza kusaidia nchi kupunguza uagizaji kutoka nje. Mkoa wa Kigoma umeandaa mkakati wa kuendeleza zao la michikichi na kupitishwa na *RCC* ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali Kuu ishirikiane na Halmashauri za Serikali za Mitaa Mkoa wa Kigoma ili kuwezesha utekelezaji wa mkakati huu. Tunategemea kuwa wakulima wadogo 100,000 wenye hekta moja kila mmoja watahusika na uzalishaji wa mawese na hivyo kukuza viwanda mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba zao la mawese lisisahaulike, ni ukombozi kwa Mkoa wa Kigoma. Kuna fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya mazao ya mafuta ya kule. Wizara ishirikiane na Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma kufanikisha hili. Manispaa ya Kigoma Ujiji inaomba msaada wa kununua miche milioni moja ili kuweza kupanda kwenye msimu huu wa kilimo kuanzia Novemba. Tunaomba Wizara ishirikiane na sisi kufanikisha mradi huu wenye ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi ya jamii kwa wakulima, naishauri Serikali kupanga sera na baadaye sheria itakayowezesha wakulima kuwa na hifadhi ya jamii. Nimeona mafanikio ya wakulima *scheme* ya *NSSF.* Hata hivyo, tunaweza kuwa na wakulima wengi zaidi kwenye hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutungie sheria suala hili ili mafao kwa wakulima yawe ya kisheria. Fao la bei itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa mkulima. Hifadhi ya jamii inaendelea na kuwepo kwa fao la bei.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa uchumi wa Watanzania wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango wangu wa mdomo, niko hapa katika kuongeza mchango wangu huo wa awali nilioutoa kwa kuchangia kwa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa viwanda nchini na kutokana na umuhimu wa ajira na fedha za kigeni na ushindani uliopo katika soko la kimataifa, naomba kuishauri Serikali kama ifuatavyo kwa kuongezea katika ule mchango wa mdomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kukutana na wawekezaji wa ndani wa kubangua korosho haraka iwezekanavyo ili kutambua matatizo wanayowakabili husussan kushindwa kupata malighafi, kushindwa kubangua korosho kutokana na uwezo wa viwanda vyao na wengine kufunga na kuhamia nchi za jirani kama Msumbiji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa kuwa tunayo makampuni ya ndani kama vile *ETG, Sunshine Group, Hyseas, MECT* na hata yale yaliyofungwa kama vile *Olam (T) Ltd., Buko Agro Focus, Micronix, Premier Cashew, Lindi Farmer* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukutana nao, Serikali itabaini wana matatizo gani na aina ya msaada gani wanahitaji kutoka Serikali ili Serikali ije na mipango, sera na mikakati ya kuweza kubangua korosho zetu ndani ya nchi ili kuongeza thamani ya korosho zetu, kutengeneza thamani ya korosho zetu, kutengeneza ajira kwa vijana wetu na kuongeza mapato ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naishauri Serikali kuwapa kipaumbele wawekezaji wa ndani wa kuchakata mazao ya kilimo husussan wabanguaji wa korosho katika mnada wa Stakabadhi Ghalani kwa kuwa unaweza kushindana na wabanguaji wa nje na wafanyabiashara wa korosho ghafi kwenda nje, sababu mataifa ya nje wanatoa ruzuku kwa wafanyabiashara hao na gharama za uendeshaji ziko chini katika nchi ya India, Brazil na Vietnam na

kusababisha korosho inayobanguliwa nchini kuwa na gharama kubwa na kusababisha kuwa na bei ya juu katika soko la kimataifa na kukosa ushindani wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba Serikali itoe kipaumbele kwa wawekezaji wa ndani kupata korosho katika minada ya mwanzo ili kupata korosho bora ambazo zina viwango vikubwa vya ubora kabla ya zile korosho za mwanzo zinazoathiriwa na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuongeza *export* toka asilimia 15 mpaka asilimia 20 na hili ongezeko kwenda kuwapa ruzuku wabanguaji wa ndani na kuvutia wawekezaji wengi zaidi na kutengeneza ajira na kuongeza thamani ya bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na sababu za kihistoria na kwa sababu za ushindani wa soko la korosho katika soko la dunia, naishauri Serikali kutokujiingiza tena katika biashara ya kubangua korosho. Kama tulivyojenga viwanda 11 mwishoni mwa miaka ya 1970 vya kubangua lakini tulishindwa na kuua kabisa zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu suala hapa siyo kubangua tu korosho, suala la msingi ni soko la kuuzia korosho zilizobanguliwa katika soko la dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lengo mojawapo la kubinafsisha na kupata mbinu na masoko ya kimataifa, soko la kimataifa lina ushindani mkubwa kwa kuwa walaji wanataka au wanapenda kununua kutokana na *brand* na jina la makampuni waliyoyazoea. Sasa wasiwasi wangu tutawekeza lakini tunashindwa kuuza katika masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba baada ya kuwekeza kama Serikali, ni bora kuwapa ruzuku na vivutio wawekezaji wa kubangua korosho nchini ili kupunguza gharama za uzalishaji ili kuweza kushindana na kwa kuwa

wengi wana masoko katika masoko ya kimataifa, itakuwa ni rahisi kushindana kuliko Serikali au Bodi ambayo haina wateja kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na siyo kwa umuhimu, nataka kupata kauli ya Serikali kuhusu ununuzi wa ufuta mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa sababu tarehe 9 Mei, 2017 Mkuu wa Mkoa wa Lindi katika kikao cha wadau wa zao la ufuta alitoa tamko la soko la ununuzi wa ufuta msimu wa mwaka 2017/2018, utakuwa wa Stakabadhi Ghalani. Pia tarehe 17 Mei, 2017 Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Kilwa ambalo ni sehemu ya Mkoa wa Lindi limekaa na kutoa tamko nalo kuwa mwaka huu soko la ufuta litakuwa ni soko huria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hizo ni kauli kutoka kwa viongozi wa Serikali halali, Serikali Kuu na Serikali ya Halmashauri ambazo zimeleta mkanganyiko mkubwa kwa wakulima na wafanyabiashara, ukizingatia msimu uko karibu kuanza na makampuni yameshaajiri wafanyakazi, mawakala na kuchukua maghala ya kukusanyia ufuta na kusababisha taharuki kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufunga hoja yake, aje atuambie nini kauli ya Serikali kuhusu mfumo wa ununuzi wa ufuta mwaka huu, utakuwa ni mfumo upi? Wa soko huria au stakabadhi ghalani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo

wamekuwa wakizifanya. Umuhimu wa kilimo hauna maelezo, kwani unachangia asilimia 29.1 ya pato la Taifa na kuleta ajira kwa asilimia 65.5 kutokana na asilimia kubwa hususan vijijini kujishughulisha na kilimo. Aidha, napongeza kodi/tozo ambazo zimeondolewa, hiyo itawapa afueni kubwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana na kushangaa kutokana na fedha za maendeleo kupelekwa kidogo mno, yaani asilimia 3.31 ya fedha zilizoidhinishwa. Naomba tuweke umuhimu na kuhakikisha fedha hizo zinapelekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga tunalima mazao mengi ya biashara kama katani, nazi, korosho machungwa, viungo na kadhalika; lakini pamoja na Serikali kufuta hati za mashamba ya mkonge Wilayani Muheza, bado Wizara haijaonesha juhudi za kufufua zao la katani na kulifanya kuongeza pato la Taifa kama zamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi zinaendelea kufanyika kwa Maafisa Kilimo kuendelea kutoa elimu Wilayani Muheza, namna bora ya kulima machungwa, minazi na viungo vya chai na kadhalika wakati tunaendelea na mihogo kutafuta wawekezaji wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana na ulimaji wa korosho ambapo Serikali imewapa wakulima pembejeo bure, jambo ambalo litaongeza ari ya kulima kwa bidii. Tunaomba Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho afanye mipango ya kutuletea mbegu Wilayani Muheza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifikirie namna ya kutoa mbegu na mbolea bure kwa baadhi ya mazao, hii itawaongezea motisha wakulima. Kwa mfano, kuna wakati nchi ya Malawi ilifanya hivyo na walivuna mahindi mengi sana na kuongeza pato lao la Taifa. Aidha, nchini Zimbabwe pia waliwahi kuwakopesha wakulima zana za kilimo na wakaongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ubora wa mazao, pia Wizara inabidi isaidie sana wakulima. Ubora wa mazao yetu ukilinganisha na nchi nyingine kwa baadhi ya mazao, bado tunahitaji wataalam wetu walifanyie kazi. Kwa mfano, zao la pamba tunakosa kupata bei nzuri kutokana na ubora na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo cha Mlingano cha Utafiti kinakufa, kwani Chuo hicho hakipelekewi fedha kabisa na mambo mengi yako ovyo. Tunaomba wapelekewe fedha chuo hicho kifufuke. Muheza tunafuga sana ng'ombe. Kiwanda cha *Tanga Fresh* kinategemea sana maziwa kutoka kwa wafugaji wa Muheza, namshauri Mheshimiwa Waziri atutumie wataalam wake wawasaidie wafugaji hawa kuongeza maziwa kitaalam na pia namna ya kuwapatia mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umwagiliaji bado tupo nyuma sana. Inabidi tufanye kazi tuweze kuwa na mashamba makubwa na ya kisasa. Tutumie zana za kileo za umwagiliaji. Tukitaka kuwa na kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda, ni vizuri Mawaziri husika kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara kama Waziri wa Kilimo, Ardhi, Maji, Nishati, Umeme na Fedha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo ni uti wa mgongo, pia Tanzania tunategemea sana kilimo katika maisha ya kila siku. Naomba Serikali iwezeshe tuwe na viwanda vya kusindika vyakula, viwanda vya nyama, viwanda vya samaki, matunda, juisi na viwanda vya maziwa ya ng'ombe. Tukiwa na viwanda, vijana wetu watapata ajira katika viwanda hivyo. Kwa hiyo, kuwa na viwanda vinavyotumia nafaka ya kilimo tunaweza kuendelea na kukuza uchumi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba Serikali ipeleke mbolea kwa wakulima kwa muda unaotakiwa. Jimbo la Mufindi wakulima wanaanza kulima kuanzia mwezi wa Tisa hadi mwezi wa 11. Muda huo ndiyo mbolea inatakiwa kwa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupanga bei ya mbolea ambayo mkulima mdogo anaweza kumudu kununua kwa bei ya chini. Pia naomba Serikali ilipe madeni ya Wakala wa Mbolea. Wapo watu ambao wanaidai Serikali kwa sababu walikopa kwenye mabenki ili kuongeza mitaji yao, basi naomba Serikali iwalipe hao mawakala wa mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba Serikali ipeleke matrekta ili kulima kilimo cha kisasa. Matrekta yatasaidia sana kukuza kilimo katika nchi yetu. Pia iwepo mikopo ya pembejeo kwa wakulima wadogo wadogo. Kuwepo na vikundi vinavyojihusisha na kilimo, uvuvi na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kilimo ni uti wa mgongo. Katika nchi yetu asilimia 75 tunategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo ni muhimu ila inakabiliwa na changamoto nyingi ambazo zinaathiri ukuaji wake. Kwanza, ni utoaji mdogo wa fedha za bajeti ya maendeleo, upungufu mkubwa wa Maafisa Ugani, wataalam wa utafiti na upungufu wa kuchakata bidhaa zake. Kubadilika kwa tabianchi inaathiri kilimo kama vile kupata ukame, mimea kupata ugonjwa, mvua zisizotabirika, mashamba kupoteza ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwaangalie wakulima wadogo wadogo kwa kuinua juu mazao yao. Wakulima wanapata hasara kutokana na mazao yao kukosa soko la uhakika. Leo utaona mazao mengi yanaharibika, mfano, mananasi, embe, machungwa, nyanya na pesheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawarudisha nyuma wakulima na kumrudisha kwenye umaskini kwa sababu itambidi lazima auze mazao yake kwa hasara. Je, Serikali ina mkakati gani wa kumwinua mkulima ili aweze kurudisha angalau hasara ya nguvu zake (mbolea).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uvuvi ambao unainua pato la nchi yetu kwa biashara na pia kuwainua wananchi kimapato katika maisha ya kila siku. Pia samaki ni chakula chetu na kila mtu anahitaji kula samaki ili kupata *protein* nyingi na kujenga afya yake. Sekta hii imemezwa na Sekta ya Viwanda. Tunahitaji tupate viwanda vingi vya kusindika samaki ili kupata tija zaidi. Viwanda vyetu vilivyokufa vinahitaji vifufuliwe na vifanye kazi. Samaki wapo wengi, tutakula na wengine tutainua biashara kwa ukubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji viwanda katika Ukanda wa Pwani kwa mfano Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mtwara Mafia, Zanzibar na Pemba. Samaki hawa wakivuliwa na kusindikwa, wengi watapata ajira na Serikali itapata kodi mbalimbali na itainua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya tatu Afrika kwa kuwa na mifugo mingi ukilinganisha na nchi kama Ethiopia na Botswana. Pia ng'ombe hutoa maziwa mengi lakini tunashindwa kusindika. Tunahitaji kujenga viwanda vingi tukamwinue mfugaji na pia tukainua uchumi wa nchi yetu kwa kusafirisha maziwa ya kopo tuachane na kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina haja ya kuwapa elimu kubwa wafugaji kuhusu kuitunza ngozi na kuzikausha vizuri ili apate bei nzuri ili apate kujua tija ya kazi yake. Mfano, Ethiopia inafaidika kupata dola milioni 186 kwa mwaka 2016 kwa uzalishaji wa biashara ya ngozi pekee. Je, Serikali yetu inaingiza shilingi ngapi kwa mwaka kwa biashara ya ngozi pekee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango wangu, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa maandishi Wizara hii muhimu kwa mustakabali wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *importation* ya mbegu za kilimo, kwa nini tunaendelea kuruhusu makampuni makubwa kama *Panner SIDCO* ambayo *hurb* zao zipo nje ziendelee kushika kasi katika soko la mbegu? Serikali lazima ifikirie kuwezesha makampuni ya ndani na wakulima wetu kupitia Vyuo vya Utafiti kama Ilonga, *ASA*, kuwasadia wakulima kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakika wa chakula unaenda sambamba na uhakika wa mbegu. Lazima Taifa lijitafakari na kutenga bajeti ya kudumu kuwezesha makampuni ya ndani kuyajengea uwezo wa kutengeneza mbegu hasa zinazoendana na hali ya hewa ya mazingira tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako malalamiko ya wananchi juu ya mfumo wa *NFRA* na hii inatokana na urasimu wa Viongozi wa Vyama vya Ushirika ambao wanatumia mfumo huu kuwapa fursa wafanyabiashara wa mazao kuuza mazao badala ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Maafisa Kilimo katika ngazi za Kata watumike kusaidia kuwatambua wakulima na kuwawezesha kupata fursa badala ya sasa hivi ilivyo kwa mfumo huu kwa nje unaonekana kuwasaidia wakulima, lakini wengine wanaumizwa na urasimu huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mbegu feki masokoni; mamlaka zinazohusika kwa nini zinashindwa kufanya kazi? Wakulima wananunua mbegu madukani hawana utalaam wa mbegu, lakini hakuna hatua za dhati za kuwakamata, kukagua maduka ya pembejeo za kilimo

na mifugo ili kubaini mbegu feki na mbegu zilizoisha muda wake wa matumizi. Mfano, viuatilifu holela vinavyoingia madukani kwa njia ya panya, mfano Mkoani Mbeya na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji katika mikoa mbalimbali ikiwemo Mkoa wa Morogoro katika Wilaya ya Kilosa, Mvomero, Kilombero na Wilaya ya Morogoro Vijijini. Serikali, Wizara ya Ardhi isaidie kufuta mashamba pori yasiyoendelezwa kwa miaka mingi. Mfano, Mvomero na Kilosa, Serikali ichukue hatua kubadilisha matumizi ya mashamba hayo. Mfano, *NAFCO* Kilosa yagawiwe kwa wakulima na wafugaji ambao migogoro yao inatokana na uhaba wa maeneo ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlundikano wa kodi au ushuru wa mazao kwa wakulima mfano, soko la mazao Kibaigwa. Ni kilio cha wakulima wengi wa Mikoa ya jirani na Morogoro; Kiteto na Dodoma ambao wanashindwa kupeleka mazao yao kutokana na ushuru wa mazao wa kila kituo cha kizuizi cha ushuru wa mazao. Ushuru huu ukiondolewa, utawasaidia wakulima kuacha kuuza mazao yakiwa mashambani na badala yake ushuru huu watozwe wafanyabiashara. Vinginevyo, wakulima wataendelea kuuza mazao yakiwa shambani na kwa lumbesa.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii. Kwa kuwa nilichangia kwa kuongea kuna baadhi ya masuala ambayo sikuweza kuongea kutokana na muda. Naomba kuyachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na *NGO* nyingi zinazofanya kazi zinazofanana katika eneo moja, hii huwachanganya wakulima kutokana na *duplication* ya kazi. Aidha, kuna baadhi ya wakulima wanaamini *NGO* zipo kwa ajili ya kufuja fedha. Mfano, kuna *NGO* zinafanya kazi eneo la Iringa Vijijini, ni budi Serikali ikawapa ushauri *NGO's* wafanye mipango kwanza ili kujua *NGO* ipi inafanya kazi

katika eneo lipi? Aidha, *NGOs* zinapoenda kuomba kibali cha kufanya kazi ni budi Halmashauri wakatoa ushauri, yale maeneo yaliyofikiwa na *NGO* yasipelekewe huduma na *NGO* hizo badala yake wawape maeneo mapya katika kutekeleza miradi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Extension Officers* wapo wachache, hawana msemaji wa fani, kwani wakipelekwa katika maeneo ya Vijiji/*Ward*/Wilaya hawapati mafunzo ya mara kwa mara yanayoendana na teknolojia ya kisasa. Aidha, ukosefu wa vitendea kazi ni kikwazo kikubwa katika utekelezaji majukumu ya Mabibi Shamba na Mabwana Shamba. Vifaa mfano magari, pikipiki na ukosefu wa mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wadudu waharibifu hasa katika Kanda ya Kati, ndege waharibifu aina ya Kwelea Kwelea. Nashauri Serikali ifanye utaratibu wa kununua ndege yake ya kunyunyuzia dawa ili pindi inapotokea ndege waharibifu dawa ziweze kunyunyiziwa kwa muda sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Idara ya Mifugo ukurasa wa 106 wa hotuba umebainisha kupungua kwa uzalishaji wa maziwa. Nashauri Serikali ibaini maeneo na kugawa mashamba kwa wafugaji na wapate utaalam wa kupanda majani kwa ajili ya chakula cha mifugo. Aidha, ni budi Serikali ikapata idadi kamili ya wananchi ambao ni wafugaji wadogo wadogo nchini ili kubaini nao wanazalisha maziwa kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado suala la unywaji maziwa shuleni upo katika kiwango kidogo, ni budi wadau mbalimbali wakashirikishwa ili waweze kusaidia suala la utoaji maziwa kwa watoto shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, pongezi za kipekee ziwaendee kwa namna wanavyosimamia tasnia ya korosho tangu waingie Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo, kwanza ni pembejeo za korosho. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kutoa pembejeo za ruzuku kwa asilimia 100. Matarajio yangu ni kuwa pembejeo hizi zitakuwa motisha kwa wakulima wa korosho na hivyo kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama ilivyokuwa inafanyika huko nyuma pembejeo hizi hazitoshelezi mahitaji ya pembejeo kwa wakulima wa korosho. Wakulima watalazimika kununua zingine kwa bei ya soko ili kukidhi mahitaji yao. Kiasi hiki nacho kisiachwe hivi kuwe na utaratibu wa manunuzi kama itakavyofanywa kwenye mbolea. Tusipofanya hivyo mkulima atapata pembejeo kiasi ya ruzuku na nyingi kununua kwa bei ya juu, hivyo atailaumu Serikali kwa utaratibu huu badala ya kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utendaji kazi wa Maafisa Ushirika. Kumekuwa na malalamiko mengi juu ya utendaji kazi wa Maafisa Ushirika hususan katika tasnia ya korosho. Maafisa hawa baadhi yao hushirikiana na viongozi wasio waadilifu wa vyama vya ushirika ili kufanya ubadhirifu kwa fedha za wakulima. Naishauri Serikali kupitia Tume ya Ushirika na Wizara kufuatilia utendaji kazi wa Maafisa hawa ili wale ambao siyo waadilifu wachukuliwe hatua ya kinidhamu kusafisha uozo uliopo katika kada hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mihogo. Mikoa ya Mtwara na Lindi, inazalisha kiasi kikubwa cha mihogo lakini wakulima wanakata tamaa kwa sababu ya bei ndogo ya zao hili sokoni. Naishauri Serikali kutumia fursa iliyopatikana hivi karibuni ya kuingiza muhogo wetu nchini China kwa kusimamia vizuri taratibu za soko la zao hili ili mkulima apate bei ya juu itakayomshawishi kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dosari zilizojitokeza katika mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu 2016/2017; msimu wa mwaka huu, 2016/2017 kulikuwa na mafanikio makubwa ya marekebisho ya mfumo huu. Hata hivyo, kuna dosari zifuatazo:-

(i) Kuchelewa malipo kwa wakulima na hivyo kuleta manung'uniko yasiyo ya lazima;

(ii) Wakulima kulipwa fedha tofauti na bei iliyouzwa kwenye mnada, kama korosho zilizouzwa kwa kilogramu Sh.3,800, wakulima wanalipwa Sh.3,400 bila maelezo yoyote; na

(iii) Wanunuzi kupanga bei hivyo bei mnadani kushuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ifanyie kazi dosari hizi ili kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani.

**MHE. JUMANNE K. KISHIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na Wabunge wote waliochangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda nitaongelea suala la upungufu wa chakula kwa baadhi ya wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Ukweli baadhi ya chakula kilichopo kwenye maghala na mashine za kukoboa mpunga ni chakula cha watu binafsi ambao wengi ni wakulima waliopata mavuno mengi mwaka jana, ambao ni kama asilimia15 ya wananchi hao wa vijijini na wakulima hawa ama hawataki kuuza kwa hofu ya njaa au wanasubiri bei zaidi isiyojulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu chakula hiki mpaka leo ni kingi sana kama kingekuwa cha Serikali lakini ni cha watu binafsi, kwa hiyo huenda hata takwimu zikatofautiana kadri muda unavyoenda. Itakumbukwa hata

wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Wilayani Kahama nilimwomba awaruhusu wauze mchele wao nje maana soko la ndani lisingeweza kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna asilimia 25 ya wananchi ambao wanategemea kuuza mifugo yao ili wanunue chakula, lakini bei ya mifugo haipo kupelekea kurudi na mifugo yao toka minadani au magulioni bila kuuza na kuongeza hofu kubwa ya maisha kwa wananchi hawa hasa ikizingatiwa wanakabiliwa na ukame pia kwa ajili ya malisho na maji kwa ajili ya wao na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya wananchi ambao wakiwemo watoto, wazee, wajane na watu wenye ulemavu mbalimbali na watu ambao ni maskini kabisa kundi hili ndilo linahitaji msaada wa dharura. Ni ukweli watu hawa walipata mavuno mwaka 2015/2016 lakini baada ya ukame wa mwezi wa Novemba – Desemba na Januari kuwa mkubwa ikapelekea mavuno machache na viwavi jeshi vikala kidogo kilichokuwepo kuwapelekea kupitia kipindi kigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa historia na jiografia ya maeneo haya hakuna sehemu yoyote wanaweza kupata pesa ili waweze kununua chakula hata cha bei nafuu, hawana mifugo, hawana ndugu wa mjini ambao wanaweza kuwasaidia na hakuna hata sehemu ya kufanya kibarua ili waweze kupata pesa wanunue chakula, ikizingatiwa watakuwa kwenye njaa kuanza Juni – Januari ambapo kama hali ya hewa itabadilika katika maeneo haya ambayo ni karibu miezi saba mpaka nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri anapofanya majumuisho yake aje na jibu sahihi ili Wabunge wanaotoka maeneo haya yaliyoathirika na ukame tuwe na majibu sahihi kwa watu wetu, vinginevyo nitakamata shilingi ya bajeti.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate orodha ya wawekezaji wenye vitalu vya kufuga ng'ombe katika ranchi ya Misenyi. Nitashukuru sana nikipata orodha yao ikibainisha na uraia wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko taarifa kwamba wafugaji wengi wanaofuga ng'ombe Misenyi ranchi haijulikani wanakouza ng'ombe wao. Je, Serikali inazo taarifa kuhusiana na jambo hili? Kwa mwaka ng'ombe wangapi wanauzwa Misenyi ranchi na nani ni wanunuzi wakuu? Pia je, Serikali inatumia shilingi ngapi kupambana na magonjwa yanayosumbua ng'ombe katika ranchi ya Misenyi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ufugaji wa samaki Ziwa Victoria unazinufaisha sana nchi jirani isipokuwa Tanzania. Kwa upande wa Tanzania mfugaji wa samaki akitaka kufuga samaki Ziwa Victoria anatakiwa kufanya nini? Hapa Tanzania kwa hivi sasa tunao wafugaji wangapi wa samaki katika Ziwa Victoria? Je, kuna samaki ambao hivi sasa wamepotea au kutoendelea kupatikana katika Ziwa Victoria? Samaki hao kama wapo ni aina gani? Tanzania tuna mpango gani wa kuhakikisha chakula cha samaki cha viwandani kinapatikana kwa gharama nafuu na je Tanzania tuna viwanda vingapi vinavyozalisha chakula cha samaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipongeze Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi hasa kwa Waziri na timu yake yote kwa hotuba yao nzuri ambayo imejaa matumaini makubwa ya Watanzania hasa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Wizara kwa kupunguza tozo hasa kwenye zao la kahawa. Serikali kutoa tozo 17 siyo kitu cha mchezo. Sambamba na hayo, Wilaya ya Lushoto inalima kahawa na kutoa tani zaidi

ya 300 kipindi cha nyuma, lakini sasa hivi ni tani 40 tu ndiyo zinazopatikana. Hii yote ni kulitupa kabisa zao la kahawa ambalo linaipatia Serikali pesa za kigeni na zao hili Wilaya ya Lushoto limeonekana ni zao ambalo linalimwa na wazee tu na siyo vijana, yote hayo ni kutowawekea vijana miundombinu mizuri na kuhamasisha kupenda kahawa na zaidi vijana kukimbilia mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo Idara ya Kilimo ilikuwa inapanda miche ambayo walikuwa wanaipata au kununua *TACRI N39*, miche hii inakaa muda wa miaka mitatu inazaa na kila mbuni wa mbegu hii unatoka kilo tatu lakini Idara ilishindwa kutokana na ukosefu wa fedha. Kwa hiyo, niishauri Serikali yangu itoe tamko katika Halmashauri zile pesa za kahawa wanazotoza ushuru wazirudishe zinunue miche ile ili kuokoa zao la kahawa linalokufa katika Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kutenganisha Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji pamoja na Wizara ya Ujenzi. Kule Lushoto kuna mvua nyingi zinazoendelea kunyesha na zimeleta madhara makubwa na kuharibu miundombinu ya barabara pamoja na madaraja kuvunjika. Hivyo, kusababisha mpaka sasa hivi ninavyoandika mchango wangu huu mazao ya wakulima yanaozea shambani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo niishauri Serikali yangu itoe pesa za dharura ili kwenda kutengeneza barabara zile ili wananchi wasiendelee kupata hasara ya mazao yao maana ukitegemea Halmashauri zetu hazina pesa za kutengeneza barabara zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo kuna barabara ya mchepuo ya kuanzia Dochi – Ngulwi hadi Mombo barabara ile niliisemea sana kuwa iwe mbadala lakini mpaka leo hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na kama ingetengenezwa kusingekuwa na upatikanaji wa hasara ya mazao ya wakulima. Kwa hiyo, niiombe Serikali yangu itengeneze barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakulima wa chai Mponde, takribani miaka minne sasa kiwanda kile cha chai kimefungwa, kwenye hotuba inaonesha kiwanda kile kimepewa mfuko wa jamii *(LAPF)* lakini mpaka sasa mfuko huo umefika mara moja tu kuona kiwanda kile. Kwa heshima na taadhima naiomba Serikali yangu hasa Waziri wa Kilimo aende Lushoto eneo la Mponde ili akaone wakulima wanavyonyanyasika na chai yao. Wakulima wale wamefikia kula mlo mmoja kwa siku na kushindwa kulipa mpaka bili za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha mbogamboga; kilimo hiki kimetupwa pembeni kabisa wakati kilimo hiki ndicho kinachochangia mapato makubwa katika Halmashauri. Naishauri Serikali yangu iwaandalie wakulima hawa miundombinu ili waweze kulima kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, mvua hizi zinazoendelea kunyesha kungejengwa mabwawa yangenufaisha wakulima wetu na kulima kilimo chenye uhakika na chenye tija kuliko ilivyo sasa, mvua zinaendelea kuharibu miundombinu ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niishauri Serikali yangu ifufue kiwanda cha mbolea Tanga ili kuwezesha mbolea kupatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu. Naishauri Serikali yangu ipeleke Benki ya Wakulima Mikoani hadi Wilayani kwa sababu huko ndiko kwenye wakulima au wahitaji kuliko Benki hiyo kuwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo. Kilimo kwangu mimi ni Wizara mama kwani wazazi wangu walionipa maisha haya wamenilea na kunisomesha kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wote wa Tanzania kuanzia vitongoji hadi Taifa na Watanzania wote kwa ujumla tunapaswa kujiuliza swali hili, ni Tanzania ipi tunayoitamani? Jibu sahihi ni Tanzania yenye nguvu ya kiuchumi. Ili Tanzania

ifikie kuwa Taifa la uchumi wa kati na Tanzania ya viwanda ni lazima na muhimu kupanua wigo katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya leo ya Wizara ya Kilimo, nitaongelea suala moja tu nalo ni zao la tangawizi. Nianze kwa kuuliza swali ambalo nitalijibu sawia. Tangawizi ni zao gani? Ni zao ambalo ni jamii ya viungo *(spices).* Pili, tangawizi ni malighafi ya kutengeneza madawa ya binadamu, vipodozi, vinywaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea tangawizi kiulimwengu, Afrika na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiulimwengu; ukisoma vitabu vya zao la tangawizi ulimwenguni utaona kwamba mataifa tano bora yanayoongoza ulimwenguni kwa kulima zao la tangawizi ni India, China, Nepal, Nigeria, Thailand. Nchi hizi tano bora kwa kilimo cha tangawizi zimeweza kujiboresha kiuchumi kupitia zao hili la kilimo. India inalima asilimia 34.6 ya tangawizi yote inayolimwa duniani, inaongoza kwa kulima tangawizi na pia inaongoza kwa kuitumia. China inalima asilimia 19.1, Nepal inalima asilimia 10.1, Nigeria inalima asilimia 7.8, Thailand inalima asilimia 7.8. Nchi nyingine zinazojitahidi ni Indonesia, Bangladesh, Japan, Cameroon na Taiwan hizi zinaingia kwenye kumi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiishie hapo nchi tano ulimwenguni zinazoongoza kwa ku-*export* tangawizi aidha ikiwa mbichi *(raw ginger)* au ikiwa imesindikwa, kwa takwimu hizi za mwaka 2015 China inaongoza kwa ku-*export* asilimia 39.9 ya tangawizi yote iliyouzwa duniani, India inashika nafasi ya pili kwa ku-*export* asilimia 14.5 japo inaongoza kwa kulima tangawizi duniani lakini inaongoza kwa kutumia tangawizi pia. Nigeria inashika nafasi ya tatu kwa ku-*export* tangawizi duniani na ina-*export* asilimia tisa ya tangawizi inayofika kwenye soko la duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa unyenyekevu mkubwa, kwa moyo uliopondeka nitoe shukrani zangu za dhati kwa wafuatao:-

Bodi ya Wadhamini wa *LAPF* na Mkurugenzi wa *LAPF* kwa kumuunga mkono Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli katika jitihada zake za kuijenga Tanzania mpya ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *LAPF* wameingia ubia na kiwanda cha kusindika tangawizi cha Miamba Same Mashariki kupitia kampuni yake ya *Mamba Ginger Company Limited. LAPF* kuingia ubia na kiwanda cha kusindika tangawizi kuna yatokanayo yafuatayo:-

(i) Walima tangawizi wa Wilaya ya Same na Tanzania nzima watapata soko la uhakika la kuuza tangawizi yao.

(ii) Ni dhahiri kwamba kilimo cha tangawizi Tanzania kitapanuka na haswa kama Serikali itajali kujenga miundombinu endelevu kwa wakulima tangawizi.

(iii) Ni dhahiri kwamba tangawizi sasa tutaingia kwenye biashara ya uhakika ya kuuza tangawizi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika na haya ninayoyasema kwamba walima tangawizi wa Tanzania wanapata taabu sana inapofikia kwenye kupata soko la zao kwa walanguzi ambao wanawapangia bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangawizi inastawi sana Same Mashariki na mpaka sasa hivi ninapoandika hotuba hii ardhi ya Same Mashariki ililimika tangawizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tunayo mikoa yenye ardhi nzuri sana yenye rutuba kama ile ya Nigeria. Mvua ya kutosha, *climate condition* nzuri; mito isiyokauka. Mikoa hiyo kwa uchache wake niitaje ni pamoja na Ruvuma, Mbeya, Iringa, Rukwa, Kigoma, Arusha na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangawizi sasa hivi imeonesha mwamko wa Watanzania kuanza kulima zao la tangawizi. Napata simu nyingi sana kutoka Kigoma

wananchi wakinipa simu kuhusu wapi wanauza zao lao la tangawizi. Songea vijijini Jimbo la Madaba wananchi wameanza kilimo cha tangawizi tangu mwaka 2012. Mimi nahamasisha sana kilimo cha tangawizi nami nikiri kwamba nimewekeza katika kilimo cha tangawizi na nimeanza na ekari 20 nalima tangawizi Madaba, Songea Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naisihi sana Serikali ifanye kila jitihada kuliangalia zao hili la tangawizi kwani iwapo Serikali itajihusisha kikamilifu tutakuwa tunatengeneza zao litakaloweza kutuingizia fedha za kigeni. Leo hii nchi ya Nigeria inachangia asilimia tisa ya tangawizi yote inayouzwa kwenye soko la dunia na matumizi ya tangawizi kiulimwengu yamepanda kwa asilimia takriban asilimia 7.5

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia sekta hii ambayo ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, ukizingatia zaidi ya Watanzania asilimia 80 ni wakulima na wafugaji na ukizingatia kauli mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kilimo chenye tija hatutapata malighafi kwa ajili ya viwanda bila kuboresha sekta ya mifugo hakuna njia tutakuwa na viwanda vya kuchakata nyama, ngozi, kwato, pembe na kutoa bidhaa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni sekta ya uvuvi, Tanzania ni kati ya nchi iliyojaliwa maziwa, bahari, mito na mabwawa ambayo tukiwekeza basi uchumi wa nchi yetu utakuwa ni wenye tija. Kama nchi tunahitaji kuwekeza kwenye uvuvi wa kisasa, kuna teknolojia za ku-*fence* maeneo muhimu kwenye ziwa au bahari ambapo baada ya muda huwezi vuna samaki wengi na kuweza kuwachakata na kutoa mazao mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie *issue* ya mnada wa Magena ambao ulifungwa bila sababu za msingi zaidi ya kisiasa. Nashukuru niliweza kuuliza swali humu ndani ambalo lilisababisha aliyekuwa Waziri

Mheshimiwa Mwigulu Nchemba pamoja na Watendaji wake wa Wizara waliweza kufika Tarime na tukawa na vikao pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama ambapo baadaye tulienda eneo la mnada na wakaongea na wananchi na kuwaahidi kuwa ule mnada utafunguliwa, maana hauhitaji gharama kuufungua, miundombinu yote ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni takriban mwaka sasa tunaomba ule mnada ufunguliwe ili kuokoa pato la bure linalopotea kwa njia za panya ambapo ng'ombe wengi hupelekwa ng'ambo ya pili upande wa Kenya kwa maelfu. Tulikumbushana kuwa mnada wa Butiama/Kinesi uwepo lakini ule ambao upo mpakani ni wa muhimu sana, utatoa ajira nyingi kwa wananchi wa Tarime na hivyo kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wakati wa kuhitimisha niweze kupata jibu la hili, yale maazimio walioelezwa wananchi juu ya ufunguzi wa ule mnada yatatimia, wananchi wana imani na Serikali ya Awamu ya Tano, watatimiza hayo ya kukuza uchumi wa viwanda kwa kufungua ajira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu ni kuhusiana na Chuo cha Kilimo kilichopo Tarime *(Tarime Extensions Centre)* kimetelekezwa kabisa wakati ni chuo ambacho kama Serikali ingewekeza tungekuwa tunatoa si tu wataalam bali Mabwana Shamba wengi ambao wangeweza kutembelea na kutoa elimu juu ya kilimo cha kisasa na ukizingatia Wilaya ya Tarime ina udongo ambao unastawi mahindi, ndizi, mihogo, mtama, alizeti, tikitimaji, ulezi, viazi vitamu, viazi mbatata, kahawa, chai zao linalochipukia, vitunguu na kadhalika. Tukiwekeza vema kwenye kilimo chenye tija Tarime tutakuza uchumi imara na viwanda vingi vitajengwa kwa ajili ya kusindika mazao haya na kuongeza thamani, viwanda vya *biscuits* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali ione ni muhimu wakafanya tafiti za kina juu ya zao la bangi na kuona kama inaweza kuwa zao la biashara kwani kuna

nchi hununua na kutengeneza bidhaa zinazotumika hospitalini. Pia hivi karibuni tuliona ndugu Keluch wa nchini Kenya aliweza tumia *marijuana* (mirungi) na kugeuza toka dawa ya kulevya na kutengeneza vinywaji mbalimbali kama *wines* (mvinyo), *juice,* maziwa ya mtindi *(yoghurt)* na kadhalika. Hivyo wataalam wa madawa ya kulevya pamoja na chakula na wale wa dawa za binadamu wafanye tafiti ya kina ili kuona madhara ambayo kama zao hili likiwa *processed* hayana *direct effect,* maana hili ni moja ya zao lenye uchumi mkubwa kuliko hata tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusiana na zao la kahawa na kushuka kwa bei ya kahawa jambo ambalo linakatisha tamaa wakulima. Vilevile usimamizi juu ya kilimo cha miwa huko Jimbo la Tarime Vijijini.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu imeonesha namna gani ya kuboresha na kutatua kero zilizopo katika Wizara hii hususan wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya wakulima na wafugaji ni migogoro inayosababishwa na Serikali kwa wafugaji. Naomba Serikali itatue kero na mapigano yanayoendelea katika makundi haya mawili. Serikali ina uwezo kabisa wa kutatua migogoro hii? Nini kifanyike? Serikali itenge maeneo maalum kwa wafugaji na wawe wanalipia maeneo hayo. Wakulima wapewe maeneo rasmi ili kuondoa vita hii kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isifanye siasa na makundi haya mawili. Tutabaki na Tanzania ambayo ni jangwa, wakati huo huo njaa kwa sababu kila eneo wakulima/wafugaji watafanya shughuli zao bila kujali utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Serikali isifanye siasa kwa kuongea tu bila utekelezaji. Ihakiki maeneo ili wafugaji wasiingilie mashamba na kuharibu mazao ya wakulima lakini pia wakulima nao Serikali ikipanga eneo la malisho basi wakulima wasilime kila eneo ili kutatua hii migogoro ya mapigano na vita kati ya makundi mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi – Wilaya ya Tanganyika na Mlele ni moja ya maeneo yaliyopita katika migogoro mingi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *Operation* tokomeza ujangili, *operation* kuondoa wavamizi wa maeneo ya wakulima na wafugaji. Kata ya Kabage Wilaya ya Tanganyika, Mwampuli, Chemalendi, Mgimoto, wafugaji waliondolewa na Serikali kwa kupigwa, akinamama kubakwa na Askari wa Wanyamapori, wakaibiwa pesa zao, kuibiwa mali zao madukani. Je, hili lilikuwa lengo la Serikali kuwanyanyasa wananchi katika Kata ya Isengule, maeneo ya Lyamgoloka kuchomewa nyumba na Askari hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka leo Serikali haijawahi kuwafidia wananchi waliokumbwa na kadhia hii. Walipwe fidia, Askari waliohusika kufanya vitendo hivi wapo na wanatembea kifua mbele huku wafugaji wakifilisika katika Taifa lao. Wananchi wakielezwa mipaka yao nadhani migogoro itapungua kuhusu utunzaji mazingira, kuhusu mipaka yao katika kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya wafugaji, wafugaji wanapigwa risasi, ng'ombe wanaibiwa na hawa Askari. Je, Serikali ina lengo la kuwamaliza wafugaji, kwani ni dhambi mtu kuwa na mifugo mingi, Serikali iweke mkakati wa viwanda ili kupunguza migogoro hii wafugaji, visindike nyama na masoko yapatikane wananchi/wafugaji wakipata faida katika masoko kelele zitapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katavi na Vyama vya Ushirika. Katika hotuba hii nimeona Katavi kuna vyama vya msingi vya ushirika 14, wakati Mikoa mingine viko zaidi ya elfu moja. Je, hamuoni Katavi hamuwatendei haki? Katika vyama vya msingi ushirika vilivyopo pia kuna wizi wa waziwazi kwa wakulima wa tumbaku, zaidi ya milioni 600 zimeliwa na Viongozi Nsimbo- Katavi.

**MHE. PROF. ANNA K. TIBAIJUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Nampongeza Waziri na timu yake kwa hotuba na bajeti nzuri. Kwa kuzingatia

umuhimu wa sekta hii kwa wapiga kura wangu ambao huko Muleba Kusini ni ama wakulima ama wafugaji ama wavuvi, nitachangia vitu muhimu katika sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo huko Muleba Serikali ni kama imetusahau, hatuna wala hatuoni jitihada za Serikali kuwaendeleza wakulima wa kahawa na wakulima wa migomba, maharage, mihogo, viazi vitamu na kadhalika. Nasema hivi nikiwa pia shahidi kwani nami ni mkulima. Sijamwona bwana shamba wa Wilaya akipita kuangalia hali ya mazao. Rais wetu mpendwa ameelekeza msema kweli ni mpenzi wa Mungu. Sijui tatizo la hawa Mabwana Shamba ofisi na Mabwana Shamba mashamba, Mheshimiwa Waziri anatusaidiaje na je, tatizo lao ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri awasikilize nao wamweleze tatizo lao, wakulima hatuna msaada sana wa Ofisi ya Kilimo Wilayani. Haigawi pembejeo, haitoi utaalam, haitutembelei kujua tatizo ni nini. Serikali, tena ya Awamu ya Tano itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wanahitaji ardhi, lakini watu wameongezeka na ardhi inazidi kupungua kwa uwingi wetu na uwingi wa mifugo. Kwa hiyo, *land pressure,* uhaba wa ardhi hivi sasa ni mojawapo ya matatizo yanayoikabili nchi hii. Juhudi za Rais wetu kuendeleza viwanda zitasaidia kupunguza *land pressure* kwani vijana watapata ajira viwandani, kwa sasa viwanda bado, pamoja na hatua nzuri za uhamasishaji zinazoendelea. Kwa hiyo, vijana wanahitaji kupewa ardhi, ili wajiajiri katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itueleze ina mpango gani kuorodhesha vijana wote wasio na ardhi waume kwa wake ili wapewe ardhi na kujiajiri katika kilimo. Kuwaacha wazazi peke yao ndiyo wahangaike kuwapatia vijana wao ardhi kuanzisha mashamba ya kisasa haitasaidia. Mheshimiwa Waziri anatambua bila kilimo cha kisasa ikiwa ni pamoja na umwagiliaji viwanda vitashindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna viwanda bila malighafi na malighafi inatokana na kilimo. Naomba Serikali na Waziri anapohitimisha anieleze mpango wa kuwapatia ardhi vijana wa Kata za Muleba ambazo ni Kushasha, Ijumbi, Nshamba, Biinabo, Ikondo na Kibanga, Bereza na Muleba kuhamishwa na kupewa mashamba ukanda wa Ziwa Burigi. Naomba Mheshimiwa Waziri jambo hili alichukue na kulifanyia kazi. Vijana katika Kata hizi wana haki ya kuhamia Mjini kwani hawana pa kwenda, hawajakataa kulima ni *landless*, hawajawezeshwa, tunaomba *youth resettlement program* ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake Muleba hatumiliki mashamba ya migomba au vibanja, ni mali za ukoo kwa kawaida, lakini wanawake tuna jukumu la kulima mfano mahindi, maharage, karanga, kwenye *grass lands* au nyeya. Sasa uhaba wa ardhi umefanya mashamba ya migomba pamoja na miti kupanuliwa hadi kwenye hizo nyeya, matokeo yake wanawake uchumi wao na lishe vinakosekana kwenye familia kwa kukosa mikunde, *legumes,* ambayo inatoa protini, isitoshe zile sehemu ndogo zilizobaki wanapolima na mifugo nayo haina sehemu za malisho. Mheshimiwa Waziri naomba atueleze ana utaratibu gani kuwapatia wafugaji maeneo ya kuendeleza ufugaji wa kisasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji hawana maeneo, wapo kwenye mapori ya akiba siyo kwa kupenda, bali kuepuka migogoro na wakulima. Nasikitika kutamka bayana kwani Serikali na hasa ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba, jambo hili ama hajaonekana kulielewa au anaamini propaganda za wanaonufaika kwa kudai rushwa kutoka kwa wafugaji katika mapori ya akiba kwamba, mifugo ni ya Wanyarwanda na Waganda huko Kagera. Naomba Serikali ilete taarifa zake katika jambo hili katika uwazi ili ukweli ambao Rais anahimiza ujulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtandao muovu unaoeneza propaganda hizi na wananchi tuko tayari kueleza ukweli. Tanzania ya viwanda haiwezi kushamiri bila

kupunguza eneo la hifadhi kutoka asilimia 28 ya sasa na kugawa kiasi cha kutosha kwa wafugaji ili wapewe hati ya ardhi kukopesheka na kuanzishwa *small scale ranching association.* Hakuna njia nyingine, kupora mali za wafugaji kwa kutaifisha mifugo yao bila kutuonesha hiyo mifugo imenunuliwa na nani na imehamishwa kwenda wapi baada ya kunadiwa huko porini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutuhadaa, kusababisha umaskini badala ya kuuondoa. Kuswaga mifugo kutoka mapori ya akiba kuzingatie agizo la Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa Wakuu wa Mikoa kwamba, wabaini maeneo ya ufugaji kabla ya zoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, wavuvi wasisumbuliwe na nyavu ndogo wakati hawahusiki na viwanda vinavyozitengeneza na kuziingiza nchini. Ziwa Victoria ni hazina ambayo haijapewa kipaumbele. Mheshimiwa Waziri anajua usalama wa wavuvi hautoshi, majambazi yanapora na kuua. Serikali inaombwa kuendelea kutumia vyombo vyake katika eneo hilo. Aidha, utaalam wa ufugaji wa samaki katika ziwa lenyewe bila kuathiri mazingira ni jambo ambalo litahitaji utafiti wa Serikali kuonesha njia kama sehemu ya kuendeleza viwanda vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wote kwa pamoja kwa uchapakazi wake katika kuhakikisha Wizara hii nyeti yenye kuwagusa wananchi kwenye masuala ya kilimo, uvuvi na ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuzungumzia suala la tumbaku. Tumbaku ni zao linaloingizia sana kipato Taifa letu, ukizingatia hata wanunuzi hununua na pesa ya kigeni yaani dola, lakini tumekuwa na tatizo kubwa na *middleman* wanaokaa katikati ya mkulima na mnunuzi, hawa wamekuwa wakisababisha wakulima kupata bei za chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika. Tunaomba Wizara iimarishe vyama vya ushirika vya kilimo na mazao. Nashauri pia, sambamba na hili nizungumzie pia mikopo ya pembejeo. Sote tunatambua vyama vya ushirika wa mazao kama vile, mazao ya tumbaku, pamba, korosho, kahawa, michikichi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua jitihada za Serikali za kuanzisha Benki ya Kilimo. Kwa nini sasa Serikali isione umuhimu wa kuweka matawi kwenye Kanda zote nchini ili basi wakulima wetu huko Majimboni waweze kupata fursa ya kukopa na kuendeleza mashamba yao. Uimarishaji wa mazao baada ya mavuno na kuongeza upatikanaji wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie kuhusu uvuvi. Zao la uvuvi ni zao ambalo likifanyiwa kazi na kuwekewa mkakati wa kuwakopesha wavuvi zana za uvuvi kama maboti, mashine, nyavu za kisasa na kadhalika, lingeingizia Taifa letu kipato kikubwa. Mfano, nimeona ukurasa wa 18 Mheshimiwa Waziri kaonesha idadi ya samaki waliopo kwenye Ziwa ya Victoria, tani 2,451,296 Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna tani zote hizi tungeweka mikakati ya makusudi ya kuvua samaki hawa na kuuza nje ya nchi tungepata kipato kikubwa cha Taifa, lakini nijuavyo mimi idadi hii ya samaki waliopo Ziwa Tanganyika ya 295,000 siyo ya kweli. Tuombe Serikali ifanye utafiti wa kina wa kujua idadi kamili na siyo kubuni tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko nyuma walikuja watafiti kutoka China na walifanya utafiti na kugundua Ziwa Tanganyika lina samaki wengi na lina aina ya samaki zaidi ya 250. Iweje leo utafiti uoneshe idadi hiyo ya 290,000. Tuombe utafiti ufanyike na kumbukumbu stahiki ziwekwe kwa faida ya nchi na faida ya vizazi vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie zao la uvuvi kwenye tozo. Wavuvi wamekuwa wakitozwa tozo kubwa

na nyingi, tuiombe Wizara ione namna ya kutoa maelekezo (Waraka) kwenye Halmashauri zetu ambako Maafisa Uvuvi ndiyo wako huko. Tuombe pia, Wizara iangalie zao la michikichi, zao hili lina faida kubwa na Kigoma ndiyo mkoa unaoongoza kulima zao hili. Zao hili lina faida kubwa, zao hili linatoa mafuta ya mawese *(palm oil)* na mbegu zake zinatoa mafuta ya Korea na pia linatoa sabuni za miche na sabuni za maji. Naamini utafiti ukifanyika wanaweza kupata faida nyingine nyingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Waziri aone namna ya kutoa miche bora ya michikichi ya muda mfupi wa miaka mitatu kwa bei nafuu kwani bei wanayouziwa wakulima, mche mmoja Sh.5,000/=. Eka moja inahitajika miche 50, swali ni wakulima wangapi wana uwezo wa kununua miche hiyo bora? Kuna ulazima wa kupata ruzuku ya miche hii ili wakulima wang'oe miche ya zamani na kupanda miche bora inayokua kwa miaka mitatu kama wenzetu wa zao la korosho wanavyoweza kupanda miche bora ya muda mfupi na leo zao la korosho limeingizia wakulima pato kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie migogoro ya wakulima na wafugaji kwenye Jimbo langu la Kigoma Kusini, Wilaya ya Uvinza. Mheshimiwa Waziri Wilaya ya Uvinza tunavyo vitalu vingi sana kwenye ranchi ya Uvinza. Vitalu hivi vingegawiwa kwa wafugaji wa Uvinza au wenyeji wa Uvinza, lakini cha ajabu vitalu vyote vimegawiwa kwa wageni toka mikoa mingine wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu hivi karibuni aliwahi kutoa tamko vitalu vyote kwenye ranchi viangaliwe na vigawiwe kwa wenyeji wa maeneo hayo ili kupunguza migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri akija kuhitimisha aniambie waliopewa vitalu kwenye ranchi ya Uvinza na je, kuna vitalu vilivyobaki ili basi mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Uvinza nijue na mwisho Waziri atakuwa tayari kunipa majina ya wamiliki waliogawiwa hivyo vitalu na maeneo yaliyobaki ili basi niweze kushauri jinsi ya kuvigawa vilivyobaki ili kupunguza migogoro ukanda wa reli na ukanda wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yale yote niliyoyochangia pale uliponipa nafasi zipo baadhi ya changamoto za uvuvi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kodi za samaki na dagaa mipakani ni kubwa sana, naiomba Serikali kuliangalia hili suala kwa ukaribu ili kunusuru gharama kubwa zinazoelekezwa kwa mvuvi. Lipo suala la Sheria ya Uvuvi ya mwaka 1973 ambayo ilitungwa kabla hata samaki aina ya sangara hawajapandikizwa katika Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba sheria hii aiendani na uvuvi wa kisasa, pamoja na yote nyavu hizi za inchi saba bado hazikidhi mahitaji ya uvuvi katika kina kirefu ambapo zimekuwa zikichukuliwa na mawimbi mazito pamoja na makundi ya samaki aina ya sangara. Hii ni kwa sababu nyavu hizo zinakua nyepesi. Hivyo basi, naiomba Serikali kutumia wataalam wake kuweza kutatua tatizo hili ili malalamiko haya yafike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mawaziri na watachangia kwa dakika tatu tatu tu. Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji dakika tatu, Mheshimiwa January Makamba dakika tatu, Mheshimiwa Simbachawene dakika tatu.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi uliyonipa. Kwanza naomba nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii nyeti kwa manufaa ya Watanzania kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba hii, kwa kweli inatoa mwelekeo mzuri wa kutufikisha mahali ambapo

tutakuwa kwanza tuna chakula cha kutosha, lakini pia tutaendeleza uchumi wa viwanda ambapo sehemu kubwa itategemea kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi wanavyochangia na wameishauri Serikali kwamba ni vizuri tuwe na mkakati wa kutosha wa kuinua kilimo cha umwagiliaji. Ni kweli nakubaliana nalo na ni kweli kwamba asilimia zaidi 75 ya kilimo chetu tunategemea mvua na kilimo cha mvua kwa kweli siyo endelevu, kama mvua hakuna maana yake hakuna kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa vyovyote vile lazima tuweke mkakati na ndiyo maana tayari tumeanzisha Tume ya Umwagiliaji ambayo ndiyo itakayosimamia eneo hili la umwagiliaji. Tumeona tuwe na Tume ili wawe na nguvu zaidi kuliko kufanya kama idara ya Serikali. Kwa hiyo, Tume tunayo na sasa hivi wanaandaa mpango kabambe wa umwagiliaji katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye bajeti yangu kwamba tuna hekta 29,000,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Bahati nzuri tumepata msaada kutoka shirika la *JICA* ambalo limetufadhili kuandaa mpango ule, sasa hivi tunafanya manunuzi ya kupata Mhandisi Mshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu katika kuendeleza sekta ya kilimo tumekuwa na miradi midogo midogo ya kusaidia wakulima wadogo wadogo, kila Halmashauri imekuwa na miradi lakini kwa sehemu kubwa miradi hii haijawa endelevu. Kwa hiyo, sasa tunataka tufanye mkakati wa kuhakikisha kwamba miradi hii ya umwagiliaji ambayo iko kwenye Halmashauri zetu inakuwa endelevu kwa kuipa nguvu kupitia hii Tume ya Umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi kubwa na ya muhimu kwanza maji kama ambavyo wanavyosema ni muhimu kwa binadamu lakini ni muhimu kwa mifugo yetu na ni muhimu kwa kilimo. Kwa hiyo, tutajenga mabwawa na mabwawa haya haya ndiyo tutakayoyatumia tupate maji

ya umwagiliaji ili tuweze kuinua kilimo chetu na tuwe na uhakika wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kwa hiyo, hii ndiyo kazi kubwa ambayo tunakwenda kufanya, hatutaweza kuendeleza kilimo kwa kutegemea mvua. Kwa hali ya tabia ya nchi inavyoonekana sasa mvua imekuwa inapungua kila mwaka kwa hiyo tukitegemea mvua kilimo chetu kitakuwa si endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa January Makamba na Mheshimiwa Simbachawene ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ataongea Naibu Waziri kwa niaba yangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwa muda mfupi uliopo napenda niongelee suala la vinyungu ambalo limezungumziwa sana na Waheshimiwa Wabunge hapa ndani lakini vilevile wakati tunazungumzia hotuba ya Maji na Umwagiliaji nilitolea ufafanuzi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba, suala hili ni la kisheria ambapo linalindwa na Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 pamoja na Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi ya mwaka 2007, vyote hivi ni katika kulinda vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwa Waheshimiwa Wabunge ni kwamba sisi kama Serikali hatujazuia vinyungu nje ya mita 60 lakini kama nilivyosema

kwamba tutakwenda kuyaona maeneo hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza ili tuone yameguswa vipi na tuone hatua za kuchukua. Kwa hiyo, ahadi itabaki ile ile ya kwenda kuyaona maeneo hayo ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyalalamikia na Serikali itachukua hatua katika jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa dhidi ya Taasisi za Muungano yaani za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokushirikiana katika kufanya utafiti. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Taasisi zetu za Muungano na zisizokuwa za Muungano zinashirikiana vizuri sana hasa katika hili suala la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Benki Kuu imefanya utafiti mwingi sana Zanzibar, zaidi ya tafiti 13 katika mazao mbalimbali mazao ya mpunga, mchele, minazi, karafuu na ripoti yake kukabidhiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na inayafanyia kazi na inanufaika vizuri sana na tafiti hizi ambazo zinafanywa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSTECH* ndiyo mratibu mkubwa wa tafiti za kisayansi pamoja na hizi za kilimo na imekuwa ikitoa fedha katika Taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na zile za Zanzibar kwa mfano *SUZA* pamoja na *IMS* kwa maana ya *Institute of Marine Science* na tafiti zake zimekuwa zikileta tija kubwa sana. *COSTECH* wameweza kutoa zaidi ya bilioni tatu kwa ajili ya ku-*facilitate* tafiti nyingi ambazo zimefanyika Zanzibar na zimeleta tija kubwa sana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Simbachawene dakika tatu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza kabisa, niseme tu kwamba maoni mengi yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge na kwa sababu Wizara ya TAMISEMI inafanya kazi kwa karibu na Wizara hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, tutashirikiana kuhakikisha kwamba yale yote yanayohusu TAMISEMI tunayashughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili eneo ambalo limeguswa sana ni tozo na ushuru kwenye Mamalaka za Serikali za Mitaa kupitia Sheria ya Fedha, Sura Na.290 ambayo imebainisha vyanzo mbalimbali ambavyo vinatoka kwenye kilimo na vingine kwenye biashara, lakini hapa nitazungumza kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema ukweli ni kweli kabisa na Mheshimiwa Rais amesisitiza sana kwamba tufanyie kazi eneo hili la kodi kwa maana ya ushuru na tozo mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kwamba haziendi kutozwa kwa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya majukumu makubwa ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kuhakikisha kwamba tunajenga uwezo na kujenga mazingira ya wananchi wetu ili kuweza kujitegemea na kuishi maisha bora. Watu hawa wanapojitegemea hivyo, kazi ya Serikali ni kujenga mazingira wezeshi, kuwafanya watu hawa waweze kumiliki lakini pia kuendesha biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua mambo yafuatayo katika utafiti na ndiyo maana baadaye nitasema nini tunafanya, kwamba kuna *problem* ya *double taxation* yaani kodi zinatolewa mara mbili katika jambo moja. Pia kuna kodi kufanana, kwa mfano, mahali ambapo unatozwa *service levy* haupaswi tena kutozwa *produce cess,* kwa hiyo, hizi unakuta kule zinakuwa zinatozwa zote kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumegundua kwamba kuna tozo hutozwa kwenye mitaji yaani tozo inatozwa kwa kupiga hesabu ya mtaji badala ya faida. Pia kuna tozo za ushuru usiozingatia mazingira ya uzalishaji, haya yote tumeyafanyia kazi na *AG* ataleta hapa mabadiliko ya sheria ambayo sisi kwa upande wa TAMISEMI tumeshamaliza tumepitia sheria zote, tumeangalia zile tozo zote, tunadhani nyingine zinahitaji kuletwa hapa ili tubadilishe sheria zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tulitunga hapa sheria ambayo inatoza *service levy* hata kwa *non corporate entity,* yaani mtu ana kibiashara cha *saloon* unamtoza *service levy 0.3%* ya *turn over,* huu ni unyonyaji, haiwezekani! Hii ilikuwa inatozwa kwa *corporate entity* tu, kampuni kubwa ndiyo inatozwa lakini sio mtu ana *saloon* ya mtaji wa shilingi milioni tano unamtoza *service levy*, hii siyo sawasawa. Kwa hiyo, marekebisho hayo yote tutayazingatia na maandalizi ya sheria yako tayari, tutaleta hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa William Tate Olenasha, Naibu Waziri Kilimo, Mifugo na Uvuvi, unazo dakika 20 katika kusafisha njia ya mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo nikiwa na afya njema. Niwahi mapema kabisa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kujibu na kutoa maelezo ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, naomba kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuongoza nchi yetu kwa busara na hekima ambayo imeendelea kuleta amani, utulivu na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Eng. Charles John Tizeba, Mbunge wa Buchosa kwa kunishirikisha kwa karibu sana katika majukumu ya kuongoza Wizara hii nyeti ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Vilevile napenda kuwashukuru sana Makatibu Wakuu wa Wizara yetu, Eng. Mathew Mtigumwe, Dkt. Yohana Budeba na Dkt. Mary Mashingo, Wakuu wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ushirikiano wa hali ya juu wanaonipa katika kazi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Ngorongoro kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa Jimboni na mara nyingine wamekuwa wavumilivu pale ambapo shughuli za kitaifa zinanifanya nisiwepo Jimboni mara kwa mara. Mwisho lakini sio kwa umuhimu, namshukuru sana kwa dhati kabisa mke wangu mpendwa Asha Mlekwa na watoto wangu wapendwa. Wao wamekuwa sehemu kubwa sana ya mafanikio yangu kwa kunipa nguvu na faraja katika shughuli zangu za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi, sasa nianze kuchangia moja kwa moja hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mapema kabisa niseme kwamba zimetolewa hoja nyingi sana na sitaweza kujibu kila hoja lakini vilevile itaniwia vigumu kuwataja Wabunge mmoja mmoja kwa majina. Niseme tu kwamba tunathamini sana michango yao na tutaendelea kuifanyia kazi, hatutaweza kuyajibu yote hapa, lakini niwaahidi Waheshimiwa Wabunge kwamba tutaleta majibu ya hoja zote ambazo wametoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kwa hoja ambayo imezungumziwa sana na Waheshimiwa

Wabunge wengi na hii inahusu umuhimu wa sekta ya mifugo hapa nchini. Michango ya Waheshimiwa Wabunge ilielekea katika sehemu kubwa kuonyesha kwamba Serikali haitoi kipaumbele katika sekta ya mifugo na wala haitambui kwamba ni sekta muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano haiwezi kamwe kuitenga na kuiweka nyuma sekta ya mifugo. Sekta ya mifugo ina umuhimu sana katika usalama wa chakula, uchumi na ajira ya watu wetu. Sekta ya mifugo inatoa ajira kwa kaya zipatazo milioni 4.4 ambayo ni karibu asilimia 50 ya kaya milioni tisa zilizopo hapa nchini na vilevile sekta ya mifugo inachangia asilimia 7.7 ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inajulikana kuwa zipo baadhi ya nchi zinazoagiza mazao ya mifugo kwa asilimia 100 endapo nchi yetu ikiingia kwenye kundi hilo, ingetumia jumla ya shilingi trilioni 17.8 kwa mwaka ambayo ni sawasawa na asilimia 60 ya bajeti ya mwaka 2016/2017 kwa ajili ya kuagiza mazao ya mifugo. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za ulaji yaani *consumption data* ya mwaka 2016/2017. Kwa maana hiyo, hata pale kunapokuwepo na watu wanaosema sekta ya mifugo haichangii katika pato la Taifa, ni vizuri kuangalia kwamba tungeweza kupata hasara gani kama tusingekuwa na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile bei ya mazao ya mifugo ingekuwa kubwa sana na wananchi wa kawaida wasingemudu kutumia mazao hayo kama tusingekuwa na mifugo. Kwa hiyo, sekta ya mifugo ni muhimu sana na Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa sekta hii, lakini jitihada mbalimbali lazima ziendelee kufanyika ili kuendelea kuboresha sekta hiyo na iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inachukua hatua kadhaa kwa kutambua umuhimu wa sekta ya mifugo ili kuongeza mchango wake kwa Taifa. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mipango

mbalimbali ya kuendeleza sekta hiyo ikiwa ni pamoja na Mpango Kabambe wa Sekta ya Mifugo *(Livestock Master Plan)* ambao unatekelezwa kupitia *ASDP II.* Vilevile mradi wa uendelezaji wa uhamilishaji; mradi wa kuendeleza tasnia ya maziwa wa Afrika Mashariki; mradi wa kuendeleza nyanda za malisho; mradi wa kuboresha ambali za kuku; mradi wa kuboresha ambali za ng'ombe na maziwa na mradi wa kuimarisha lishe wa kaya kupitia ufugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kupitia mkopo wa riba nafuu wa dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Ushirikiano wa Kiuchumi wa Serikali ya Korea umepanga kukamilisha ujenzi wa machinjio ya Ruvu na hii itaendana na ujenzi wa viwanda vingine vya kusindika ngozi, kutengeneza bidhaa za ngozi na viatu. Vilevile itaboresha Ranchi ya Ruvu kuwa ya mfano; kukarabati na kuweka mizani katika minada 164 nchini kote; kuweka mfumo wa kidigitali wa kuunganisha wafugaji, wasindikaji na wafanyabiashara wa ndani na nje na vilevile mradi huu utajenga mtandao wa wasambazaji wa nyama Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge walitumia muda sana kuijadili, ni suala la migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Migogoro ya matumizi ya ardhi inayohusisha wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi imeendelea kuwepo hapa nchini kwa muda mrefu. Juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali inawezekana hazijaweza kumaliza tatizo hili na hii ni kutokana na ukweli kwamba migogoro hii huhusisha sekta zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo, Serikali ya Awamu ya Tano iliamua kuunda timu ya wataalam kutoka sekta zinazohusika na ardhi ili kuhakikisha kwamba masuala ya kila sekta yanaangaliwa kwa pamoja. Tayari kama tulivyoweza kuonesha wakati wa hotuba ya bajeti yetu, ripoti ile tumeshaipata na inafanyiwa kazi ili iweze sasa kwenda kwenye Baraza la Mawaziri na hatimaye utekelezaji wa

mapendekezo uweze kufanyika. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira kazi iliyofanyika ni kubwa na tunaamini mapendekezo yale yatatusaidia sana kuondokana na tatizo la migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vizuri kueleza kwamba changamoto tuliyonayo katika sekta ya mifugo ni zaidi tu ya migogoro ya ardhi, mifugo mingi tuliyonayo nchini iko kwenye maeneo yanayopata mvua kidogo kwa mwaka ambayo kwa kiwango kikubwa yameathiriwa na madhara yatokanayo na mabadiliko tabia ya nchi hususani ukame ambao umeacha maeneo haya yakiwa hayana nyasi zinazofaa kwa malisho ikiwemo kuongezeka kwa majani yenye sumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wakaendelea kufahamu kwamba hata maeneo ambayo ardhi ya wafugaji bado inapatikana kwa kiwango kile kile, lakini ubora wa ile ardhi kwa malisho umepungua sana na ndiyo maana lazima tufikirie tu zaidi ya migogoro. Hali hii imesababisha wafugaji kuhitaji maeneo makubwa zaidi ya kawaida na wakati mwingine hulazimika kuhamia maeneo yenye unafuu na upatikanaji wa malisho na maji na hivyo imekuwa chanzo cha migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro pia imesababishwa na ongezeko la watu, mifugo na shughuli za kijamii na kiuchumi ambazo zinafanyika kwenye ardhi hivyo kusababisha mgongano wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na hali ya nyanda za malisho kuendelea kupungua na malisho nayo kuwa duni Wizara imeanza mpango wa kuboresha nyanda za malisho kwa kupanda mbegu za nyasi zinazoweza kukabiliana na hali ya ukame hasa katika maeneo yaliyoathirika. Kwa hiyo, Wizara inazihamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo Waheshimiwa Wabunge nyie wote ni Madiwani, kuandaa mipango itakayowashirikisha wafugaji

katika kuunga mkono juhudi za Wizara kwa kutenga maeneo ya wafugaji pamoja na kuboresha malisho na kuweka miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwasisitiza wafugaji wetu kubadilisha aina ya ufugaji ili waendane na mabadiliko ya tabia ya nchi. Katika enzi hizi ambapo mvua na nyasi zimepungua ni lazima nazo tabia zetu za ufugaji zibadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo Waheshimiwa Wabunge wameizungumzia sana ni kuhusiana na suala la upigaji wa chapa. Zoezi la upigaji wa chapa linatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na.12 ya mwaka 2010. Utekelezaji wa sheria hii unaendelea nchi nzima na tunafahamu kwamba kuna changamoto ambazo zinaendelea kutokea. Wizara ilibidi isitishe kwanza zoezi hilo ili kutoa fursa kwa Wizara na wadau wengine kujipanga upya na hususani kutoa hamasa na elimu ili wadau waweze kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja ambayo imetokea karibuni ni kuhusu bei na gharama ya kufanya zoezi hilo. Wafugaji wanalalamika nchi nzima kwamba bei imekuwa kubwa lakini niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba utaratibu ambao unatakiwa ufuatwe ni kwamba Halmashauri inayotaka kupiga chapa mifugo ni lazima ijadiliane na wafugaji na wadau wengine kuhusu gharama. Kwa hiyo, ni marufuku Halmashauri au Mkurugenzi mwenyewe kujiamulia bei ya kupiga chapa bila kuwashirikisha wafugaji na wadau wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tatizo la elimu limekuwa kubwa na ndiyo maana Wizara ilielekeza kwamba kabla Halmashauri haijafanya zoezi la chapa ya mifugo ni muhimu kutoa elimu kwa wafugaji na wadau wengine. Nalo hili ni sharti ambalo tumeliweka na tunaomba Halmashauri zote zizingatie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunatambua kwamba suala la upigaji wa chapa linahusiana vilevile na ubora ngozi, tumetoa maelekezo ya namna ya kupiga chapa ambapo haitaathiri ubora wa ngozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nalo limevuta hisia ya Waheshimiwa wengi ni suala la maendeleo ya ushirika nchini. Serikali inapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa itaendelea kusimamia maelekezo ya kisera na Sheria ya Vyama vya Ushirika, Na. 6 ya mwaka 2013 ili kupata maendeleo endelevu ya ushirika nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaendelea kushirikiana na Wizara ya kisekta kuwahamasisha wananchi kote nchini kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika wa aina mbalimbali kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi mkubwa sana wa baadhi ya tozo ambazo tunapendekeza kufutwa kwamba zitaua ushirika nchini na hususani vyama vya msingi. Tunafahamu kwamba ni kweli kabisa ushuru ni chanzo kikuu cha mapato ya vyama vya ushirika katika kusaidia uendeshaji wake lakini nataka nitumie fursa hii niwatoe wasiwasi Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara imebadilisha mfumo wa upatikanaji wa fedha hizo ambazo awali zilikuwa zikichukuliwa moja kwa moja kulingana na mjengeko wa bei wa mazao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu tunaopendekeza sasa ni kwamba bodi za vyama zinatakiwa kuomba fedha hizo za uendeshaji kupitia mikutano mikuu ya wanachama ambao wataidhinisha kutokana na hali halisi ya uzalishaji katika makisio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kimsingi ushuru ule wa kuendesha vyama vya ushirika utakuwepo lakini siyo kwa mpango wa sasa ambapo tunaweka kiwango kimoja katika nchi nzima, ni lazima mahitaji ya chama kimoja kimoja

yajadiliwe na kuombewa ruhusa ili hizo fedha ziweze kupatikana. Kwa hiyo, kimsingi Waheshimiwa Wabunge ninachosema tunajali suala hili kwa sababu vyama vya ushirika ndiyo hasa vinaendesha maendeleo ya mazao kwa hiyo siyo kwamba vyama vya ushirika vitakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walitoa hoja kuhusu kupatiwa ruhusa ya baadhi ya vyama vikuu ambavyo vimeonekana vikubwa viweze kugawanywa. Mfano uliotolewa ulikuwa ni chama cha *TANEKU*. Tunachosema kulingana na sheria lakini vilevile kulingana na Katiba, uhuru wa kujumuika ni pamoja na uhuru wa kutotaka kujumuika kwa mtu au taasisi ambayo inapenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama chochote cha ushirika ambacho kinataka kuchukua hatua za kujigawanya ni sharti wazo hilo na maamuzi yafanyike katika mikutano ya kisheria hasa mikutano mikuu lakini baadaye wakishafanya kwa sababu Wizara na hasa Tume ndiyo inayosimamia Sheria ya Ushirika, ni lazima vitu vingine viangaliwe ikiwa ni pamoja na kuangalia kwamba ushirika unaendelea kuwa imara lakini vilevile kuangalia *economic viability.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wananchi na wanachama wa *TANEKU* wanakusudia kugawa chama cha *TANEKU* wao wakae kwenye mikutano yao halafu baada ya hapo walete mapendekezo Wizarani na sisi tutaangalia kama kweli masharti mengine wameweza kukidhi ikiwa ni pamoja na kuangalia isije ikasababisha migogoro zaidi kwa sababu kuna maeneo ambayo tumegawanya vyama lakini migogoro ikatokea hususani wakati wa kugawanya mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachosisitiza tu ni kwamba tunachoangalia sana siyo utitiri wa vyama, sio uwingi, lakini ni ubora na uwezo wa kujiendesha kama taasisi ambazo zina demokrasia lakini ambazo zinaweza kujimudu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ningependa kuzungumzia suala la uwekezaji katika maeneo tengefu ya Shungimbili, Mbarakuni na Nyororo kwa sababu ya muda nitazungumzia kuhusu kisiwa cha Shungimbili. Hoja ilitolewa kwamba kisiwa cha Shungimbili kimeuzwa, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba hakuna ukiukwaji wowote wa utaratibu uliofanyika katika uwekezaji katika kisiwa cha Shungimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hifadhi ya bahari na maeneo tengefu haijawahi kupora maeneo na kuyauza, shughuli zinazofanyika katika maeneo tengefu ni zile zinazokubalika kwa mujibu wa sheria ambazo ni mafunzo, utafiti na utalii ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya utalii ambayo ni rafiki kwa mazingira, hicho ndio kilichotokea Shungimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wasiwasi wa wananchi wa Mafia kwamba kisiwa kimeuzwa ni kwa sababu mwenye hoteli amegeuza jina akaita *Thanda Island* na hivyo akaona kwamba imeuzwa mpaka imebatizwa jina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari kuna maelekezo kutoka Wizara ni kwamba mwekezaji abadilishe jina kutoka *Thanda Island* lirudi kuwa Shungimbili. Haiwezekana kisiwa ambacho cha watu wa Pemba kwa miaka yote wanafahamu kwa jina la Shungimbili halafu leo hii Mwekezaji anakuja anabadilisha jina analotaka yeye, tumetoa amri kwamba ni lazima jina lirudi kama ilivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa tu kumhakikishia Mbunge wa Mafia kwamba taratibu zinaendelea, lakini vilevile Halmashauri ya Mafia imekuwa ikinufaika na uwekezaji uliofanyika hapo, changamoto zingine ambazo zipo tutaendelea kujadiliana na Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi na Halmashauri ya Mafia ili kuendelea kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, machache, nashukuru sana na niombe kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa mchango wako mzuri. Sasa namwita mtoa hoja Dkt. Tizeba Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi unazo dakika arobaini.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha tena kukutana jioni hii tukiwa na afya njema thabiti kabisa, ili tujadili yale ambayo yamezungumzwa kwa kipindi cha takribani siku tatu wakati Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakijadili mapendekezo ya mapato na matumizi ya Wizara yetu ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utangulizi nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, Wajumbe wote wa Kamati yetu, vilevile nimshukuru Mheshimiwa Cecilia Paresso Mbunge wa Viti maalum aliyewasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa niaba ya Msemaji Rasmi wa Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi Dkt. Emmaculate Sware. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru Wabunge wote waliochangia katika hoja hii ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na kwa kutambua umuhimu mkubwa wa hoja hii Wabunge wengi wamejitokeza kuchangia, kutoa maoni na ushauri hali ambayo binafsi imenipa faraja kubwa kwani michango hiyo itasaidia katika utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza sekta ya kilimo mifugo na uvuvi na ni ushahidi tosha kwamba kilimo mifugo na uvuvi ni sekta muhimu kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Wabunge takribani 134 wamechangia kwa kauli na maandishi wakati tukijadili makadirio ya matumizi ya Wizara yangu. Kati ya hao

Wabunge 87 walichangia kwa kauli na Wabunge 47 kwa maandishi. Kwa hali hiyo Wabunge hawa ni wengi sana na hivyo kwa dakika hizi arobaini sidhani kama naweza kuwataja wote na kujibu hoja ya kila mmoja, haitakuwa rahisi kwangu kufanya hivyo na kwa hivyo ntajitahidi kujibu kwa ujumla mambo makubwa yaliyojitokeza katika michango hii. Napenda pia niwahakikishie kwamba Waheshimiwa Wabunge yote mliyojadili mliyochangia, mliyohoji tutajitahidi kuyajibu kwa maandishi na kuwapatia kabla hatujamaliza mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa uniruhusu nijibu baadhi ya hoja zilizojitokeza katika mjadala wa hotuba kama ifuatavyo; Nitaanza na hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji halafu nitazungumzia machache yaliyojitokeza katika hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge karibu wote waliochangia wamezungumzia jambo hili la bajeti ndogo ya Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi. bajeti ya Sekta hii haiko yote katika Wizara yangu ili labda ndio nianze kwanza nalo ili tuelewane vizuri Waheshimiwa Wabunge, bajeti kubwa iko maeneo mengine nje ya hii Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara mtambuka zinazojihusisha na mambo ya kilimo kubwa kabisa ya kwanza ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kule mipango yote karibia ya utekelezaji wa shughuli za kilimo inafanyikia TAMISEMI katika Halmashauri zetu Waheshimiwa Wabunge, Wizara inajihusisha zaidi na sera na miongozo ya Kitaifa, lakini utekelezaji unafanyika kule kwenye *grassroot* ambako haya mambo yanasimamiwa na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ziko Wizara zingine kwa mfano Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano, hawa nao wanafanya kazi ambazo zinahusu kilimo ingawa sio moja kwa moja. Kwa hivyo, ukilichukulia katika ujumla huo mpana utaona kwamba sekta hizi tatu kilimo mifugo na uvuvi siyo kwamba zimepata

bajeti ndogo kihivyo isipokuwa tu ile inayoonekana katika Wizara yetu ya Kilimo ndiyo kwa mtazamo unaweza ukaona kwamba ni bajeti kidogo. Halmashauri jumla ya bajeti yake inayohusu sekta hizi tatu ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili zipo taasisi zetu karibia 11 ama 12 ambazo zinakusanya maduhuli ni taasisi za umma na zinajihusisha na mambo haya haya ya kilimo, mifugo na uvuvi ambazo maduhuli yale hayaji katika bajeti kuu ya Serikali wana-*retain* na kutumia moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchache, niseme tu hizi taasisi hizi zinakusanya na kutumia katika sekta za kilimo jumla ya shilingi karibia bilioni 260. Hizi ukiziongeza katika ile bajeti ya kwetu ya moja kwa moja kwa sababu ni taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, ukiziongeza hizi utaona kwamba kutoka kwenye karibu 400 ile tunakwenda kwenye 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu kuna fedha nyingi ambayo inaingia katika miradi ya kilimo, mifugo na uvuvi nje kabisa ya utaratibu wa bajeti ya Serikali. Ziko taasisi nyingi za wabia wetu wa maendeleo ambao wanachangia sana katika kilimo lakini siyo kupitia mfumo wa bajeti ya Serikali. Hata hivyo, jambo la kuzingatia tu ni kwamba hawa wote hawa ushiriki wao katika miradi mbalimbali wanayoiendesha unakuwa na baraka za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *approach* tu ndiyo ina-*differ*, kule kwenye afya wana *basket* wanayochangia, kwa hivyo zinaonekana zimepitia kwenye mfumo wetu wa bajeti wa Serikali, lakini kwenye kilimo wanakwenda wame-*opt* kwenda na kwa sababu wana *complement* kazi inayofanywa na Serikali hatuna sababu ya kufinyana nao. Kwa hivyo, tunawaacha watekeleze hayo majukumu ambayo *otherwise* ingebidi Serikali itenge bajeti hapa kwenda kufanya hayo majukumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo tu, katika mwaka 2015/2016, kwa ujumla wadau wetu wa

maendeleo walichangia trilioni moja na bilioni 730 katika kilimo *direct*, wakati bajeti yetu ya Serikali kwa ujumla ilikuwa trilioni 1.001, wenzetu wakachangia trilioni 1.73; ukizijumlisha hizi ni karibia trilioni 2.7, ni fedha nyingi kuliko Wizara nyingine yoyote iliyopata mchango wa namna hiyo katika bajeti ya mwaka uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka tu kusema kwa maneno haya ni kwamba fedha inayokuwa *directed* kwenye kilimo ni nyingi, katika mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao mpaka hapa ninapozungumza leo *commitment* za fedha hizi zinaendelea kutoka, lakini mpaka ninavyozungumza sasa hivi fedha kutoka kwa wadau wetu wengine nje ya mfumo wa bajeti wamesha-*disburse* karibu bilioni 400. Kwa hivyo, hizi ni fedha ambazo zimeingia kwenye kilimo kupitia *programs* mbalimbali ambazo wadau wetu tunashirikiana nao katika kukuza na kuimarisha kilimo chetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tusipate wasiwasi kwamba kilimo kinakuwa *under funded* na kadhalika. Nasema kilimo ni kipaumbele hakuna asiyejua na mmesema vizuri hapa kwamba bila kilimo viwanda na nini vitakuwa tabu sana ku-*achieve, yes* itakuwa vigumu sana ku-*achieve!* Hata hivyo, hata ukiwa na *priority* maana yake ni kwamba utakataa misaada, utakataa ziada eti kwa sababu jambo hilo unaloshughulikia wewe kwako ni kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo. Taifa la Israel kipaumbele namba moja chao ni usalama, *security of that country is priority number one*, ulinzi bajeti yao ya ulinzi pamoja na kwamba ndiyo *concern,* ndiyo *priority number one* Taifa la Israel, bajeti yao ya ulinzi wanapata msaada kutoka Marekani. Mwaka jana tu wamepata msaada wa bilioni 38 dola wakati wao bajeti yao ya ndani ilikuwa imetenga bilioni 4.6. Hata hivyo, hiyo haimaanishi kwamba wameondokana na kufanya suala la ulinzi kuwa kipaumbele namba moja. Kwa hivyo, hata sisi wakati tuna bajeti tunaangalia pia kwamba wenzetu wanaotuunga mkono

katika kilimo *commitment* yao ni kiasi gani ili tuweze kufanya *rational distribution* ya *resource* tuliyonayo ya ndani. Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge hili suala lisitusumbue sana kwamba kwa nini asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nielezee hapa asilimia tatu ambayo inasemwa kwamba kwa mwaka mzima bajeti ya Fungu 43 iliyotolewa ni asilimia 3.8. Ni kweli mpaka tunaandika hivi vitabu pesa iliyokuwa imetolea ni shilingi bilioni kama 3.4 ambayo ukiipigia hesabu inakuwa asilimia tatu, lakini ni asilimia tatu yaa shilingi bilioni 101 ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya mradi mmoja tu, mradi wa kujenga vihenge *(silos)* na hivi tunavyozungumza majadiliano *almost* yamekamilika na Serikali ya Poland ambako hizi fedha sasa zitapatikana dola karibu milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa hivyo vihenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, huenda wakati Waziri wa fedha anakuja kusoma bajeti yake hapa *performance* ya hiyo miradi ya maendeleo kwenye bajeti *commitment* ya Serikali inaweza kuwa imeshafika kwenye asilimia 98. Ndugu zangu ile asilimia tatu inayoonekana kwa sababu tusingesema uwongo, mchakato ulikuwa haujakamilika, lakini tuna hakika sasa kila lililohitajika ili tukamilishe upatikanaji wa hizo fedha kutoka Serikali ya Poland tumekwishafanya, zitapatikana, vihenge vitajengwa na kwa hivyo utekelezaji wa bajeti yetu ya maendeleo utakuwa umekwenda kwenye asilimia kubwa sana kuliko inavyoonekana kwenye maandishi yetu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa hisia ni hili suala la tozo tulizoziondoa. Nimesikitika kweli jana kuona baada ya kelele zote za wananchi wa nchi hii kuhusu tozo, kero zinazowasababishia kutonufaika na jitihada zao, baadhi ya wenzetu hapa ndani wamesimama wakibeza eti kwamba hili tulilolifanya ni jambo baya halina manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siyo msemaji mzuri

sana wa *exchange* hizi za mambo ya humu ndani, lakini itoshe tu kusema kwamba mambo ambayo ni *serious* kama haya tunatakiwa kuacha hizi *politics* za ajabu. Hapa tunazungumzia maisha na *well being* ya Watanzania. Watu wanalalamika anapeleka ng'ombe mnadani hajauza, anatozwa kodi ya makanyagio, halafu sisi tukae tuache kodi ya hivyo eti kwa sababu kuna mtu hapa anadhani kwamba tuko tunatafuta sifa, hatutafuti sifa! Sisi tunashughulikia matatizo ya wananchi, matatizo ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia mdogo wangu Mheshimiwa David Silinde asubuhi hapa, anasema kodi hizi zimewalenga *middle men* hazijawalenga wakulima, hivi Tanzania hizi kodi tunaziweka kwa ubaguzi? Hizi kodi zinawaathiri wote katika mnyororo wa thamani, kodi hizi zinamuathiri kila mmoja kwenye mnyororo wa thamani. Mkulima akilima kama hakuna mnunuzi kilimo chake hakina manufaa, mnunuzi akiwapo bila mkulima, uchuuzi wake hauna manufaa, wote wanategemeana. Kama watu wana mazao lakini hakuna msindikaji, mazao yale yatapoteza thamani. Kwa hivyo, tulichokifanya tumeangalia mnyororo mzima wa thamani na namna hizi kodi zinavyowa-*affect* mmoja mmoja kwenye mnyororo huo wa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuondosha kwa hizi kodi hakukulenga kundi moja tu la Watanzania, kumelenga Watanzania wote ambao wanakuwa *affected* na hizi kodi, wafanyabiashara, wakulima wasindikaji na wengine. Nitatoa mfano mdogo ili tuwe na ufahamu unaofanana. Kwenye tumbaku au tuseme kwenye mbegu ili mfanyabiashara mzalishaji wa mbegu aweze kuzalisha mbegu alitakiwa kuwa na mtaji wa tozo tu wa milioni 60, dola 20,000 kwa ajili ya kusajiliwa kama mzalishaji wa mbegu na dola 10,000 za kusajili mbegu anayotaka kuzalisha hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu ni mfanyabiashara anazalisha mbegu auze kwa wakulima, ukimuachia hii kodi ibaki maana yake mbegu atakayozalisha lazima aweke ndani yake hizi gharama. Akiweka ndani yake hizi gharama bei ya mbegu inapanda, bei ya mbegu ikipanda

anayeathirika na kushindwa kuinunua ni mkulima. Kwa hivyo, tunalazimika kuondoa hizo kodi kwa yule ili *finally* mkulima apate mbegu kwa bei rahisi aongeze uzalishaji, akiongeza uzalishaji Halmashauri zetu zinatoza *cess* na tunapanga mipango mingine ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu ndugu zangu siyo kwamba watu walilala wakaamka usingizini wakaanza kufuta moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba. Ndiyo maana kodi ambazo tumeona zina uhusiano wa moja kwa moja na kuongeza uzalishaji, kusimamia mazao yaendelee kuwepo na kadhalika hizo hatujazigusa, tumeziacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine mdogo, kwamba tumeondoa eti kodi ya vifungashio vya korosho, kwa hivyo hili jambo litawanufaisha wanaoingiza magunia yale ndani. Jamani wanaoingiza hayo magunia ni Vyama vya Msingi vya Wakulima, korosho ikitoka kule kwenye *primary societies* haiendi kwenye malori kama mchanga imebebwa, inawekwa kwenye hivyo vifungashio inaingizwa kwenye ghala na hapo kila mtu ndiyo anajua, hiii ya kwangu, hii ya nani na nani *by weight and everything.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoondoa hii tozo maana yake ni kwamba hawa wakulima waliokuwa wanalazimika kulipa kodi kwa ajili ya magunia yale sasa hawatalipa hiyo hela inabaki kwao. Nilikuwa napiga hesabu, kwa hilo moja tu la tozo ya magunia *saving* itakayokuwepo kwa wakulima wa korosho msimu unaokuja, bilioni 11. Sasa hizi siyo hela ndogo zikibaki kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, tumeondoa *VAT* kwenye mashudu ya pamba. Mtu anaweza akadhani kwamba tumewasaidia *ginner's* siyo kweli! *Ginners* hawa katika mjengeko wa bei wanayonunua pamba kwa wakulima wanaweka mle ile *VAT* kama *cost.* Kwa hivyo, bei ya pamba kama ilikuwa iwe Sh.1,100/= kwa kilo moja wanaondoa shilingi karibu mia moja wanasema hii tutarudisha Serikalini kama kodi. Sasa hivi tunachofanya hiyo ikiondoka maana yake hiyo mia moja itabaki kwa mkulima,

itamjengea uwezo wa kulima zaidi, itamjengea uwezo wa kununua dawa na uwezo wa kufanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo niombe jamani ndugu zangu, haya mambo *serious* namna hii, tusi-*relate* nayo kimzaha mzaha kama tulivyoona wenzetu wanajaribu kufanya hapa ndani. Nawashukuru sana wote ambao mmetuunga mkono kwenye hili jambo, tutakuwa makini, tutaangalia *impact* yake. Haya ni mambo siyo *static,* tutaangalia *impact* yake katika tasnia nzima, yale yatakayohitaji *adjustment* tutafanya *adjustment. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la ununuzi wa pamoja, uingizaji wa pamoja wa mbolea. Nashukuru sana kwamba Bunge limetuunga mkono Serikali katika hili jambo nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Maangalizo yenu yote kabisa tumeyachukua, yako maangalizo ambayo mmeyasema ni ya msingi tumeyachukua. Tutahakikisha wakati tunatekeleza hili jambo tunakuwa makini na hayo maeneo ambayo mmetupa angalizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni la kuhujumiwa kwa sababu wako ambao watapoteza katika huu mchakato na kwa hivyo kama watakuwa wanapoteza wakipata uwezekano wa kuzuia tusifanikiwe watajaribu na tumeona *attempt* ilikuwepo na wote ninyi ni mashahidi. Kwa hivyo hayo maeneo ya hivyo tutakuwa makini nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe wasiwasi wakulima wa nchi hii kwamba *fall back position* sijui niisemeje kwa Kiswahili. Kwamba jambo hili likipata tatizo lolote kwa mfano, namna ya kufikisha mbolea kwa wananchi kwa wakati kwa msimu huu tunayo. Nawaomba sana ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge mtu asidhani kwamba tunakwenda kwenye jambo *blindly* kwamba ikitokea *something unforeseen* basi sisi ndiyo tutakuwa tumeporomoka hatujui la kufanya, wakulima wamekosa mbolea na kadhalika, hapana! *Fallback position* ipo, siyo jambo la mjadala wa hapa ndani, lakini naomba tu muamini kwamba *fallback position* ipo.

Mheshimiwa Mweyekiti, ndiyo maana tumeanza kwa uangalifu na aina mbili tu za mbolea. Tumeanza na aina mbili kwa makusudi kabisa, sio kwa bahati mbaya, kwa makusudi! Kwamba uwezekano wa kuli-*perfect* hil jambo asilimia 100 tunasema *who knows!* Kitu chochote kinaweza kutokea huko tunakoagiza na nini, sasa tunafanyaje; kwa hivyo tumejiwekea na sisi hizo tahadhari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kwa ruhusa yako kuwaonya hao ambao wanajaribu kutuvuta shati. Sisi dhamira yetu ni kuhakikisha gharama za uzalishaji katika kilimo zinashuka, watu hawaoni faida ya kulima kwa sababu *margins* zinakuwa ndogo sana, mtu anahangaika na tumbaku miezi tisa faida anayokuja kupata *two, three percent.* Sasa hiki tunachokifanya tunahangaika angalau hiyo faida iongezeke basi kutoka kwenye hizo *three percent* ifike angalau kwenye *ten, fifteen percent.* Tutalisimamia kwelikweli hili jambo. Kanuni hizi ziko *strict* kweli kweli, mtu yeyote akiingia hapo katikati atakiona cha mtema kuni. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahamasishe Watanzania kwamba kilimo sasa hivi kitalipa. Wale ambao wamekuwa wanadhani kwamba kilimo hakitalipa, nataka niwaambie leo kwamba kilimo kitalipa, awe ni mkulima, awe ni mfanyakazi wa kuajiriwa, ardhi Tanzania ipo, hebu twende tulime. Tukilima kwanza unakuwa umejihakikishia kama ni umelima mazao ya chakula utakuwa na chakula chako mwenyewe hulazimiki kwenda sokoni, kama utakuwa ni mkulima utapata chakula chako lakini utalazimika kupeleka ziada sokoni. Kwa hivyo tunashusha, tunapunguza hizi gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uki-*combine measure* hii ya *bulk purchase* ya pamoja na hizi tozo na kodi mbalimbali ambazo tunaondoa kwenye pembejeo kwa vyovyote vile mbolea itashuka bei na huenda katika bajeti yetu hii hapa tunayoomba iko fedha ambayo tumeiomba Bunge lituidhinishie kwa ajili ya ruzuku ya pembejeo. Tukifanya vizuri mwaka huu katika huu mfumo yawezekana kabisa mwaka kesho Serikali ikaja hapa bila maombi ya ruzuku kwenye

pembejeo kwa sababu pembejeo itakuwa sasa ni rahisi inapatikana na kila Mtanzania anaweza kumudu kununua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni mbegu. Ni kweli kwamba utoshelevu wetu wa mbegu inayozalishwa hapa nchini bado uko chini, tuko asilimia 35 ya mahitaji. Hili jambo niliongelee kwa kujibu pia hoja ya kwamba hatuweki malengo yanayopimika katika mipango yetu. Jamani, tunayo mipango ya muda wa kati na muda mrefu, mipango ya muda wa kati tunaitekeleza kupitia bajeti za mwaka mmoja mmoja halafu *finally* tunakuwa na mpango wa muda mrefu wa miaka mitano au kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuondokane na hali hii ya udhaifu wa upatikanaji wa mbegu bora hapa nchini kulikuwa na tatizo kubwa sana la kisheria. Utaratibu tuliokuwa nao ulikuwa haumwezeshi mzalishaji wa mbegu kuzalisha hapa nchini aina nyingi za mbegu kwa tija au akapata faida mwisho wa siku. Faida hiyo ilikuwa inamezwa katika sheria na kanuni tulizokuwa nazo. Kwa hivyo, hatua ya kwanza siyo kuanzisha mashamba, hatua ya kwanza lazima iwe ku-*adress* tatizo linalozaa mengine *(root cause).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tumeanza na hilo, tumeanza na kurekebisha sheria na kanuni za mbegu ili sasa tukishaweka mazingira mazuri kwa wazalishaji waingie kwenye uzalishaji kwa sababu suala la uzalishaji yeyote atakayeona sasa hiyo fursa iko nzuri kwake anaingia kwenye uzalishaji. Tutoke kwenye huu mtindo ambao mbegu inazalishwa Kenya, Zambia tunakuja kuuziwa Watanzania kama vile sisi hatuna ardhi hapa ya kuzalisha mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tumeanza na sheria. Tumefuta tozo za ovyo ovyo zilizokuwako kwenye uzalishaji wa mbegu, tumepunguza masharti ya muda na mlolongo ule tumeu-*short circuit* wa kupata vibali ili mtu uanze uzalishaji wa mbegu. Kwa hivyo, kwa *combination*

ya hizi *measures,* tuna hakika mwaka kesho tutaona *investment* zaidi kwenye suala la uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko mbegu moja imepigiwa kelele hapa ndani, naomba na yenyewe niitolee ufafanuzi, mbegu ya pamba *UK91* ni ya tangu mwaka 1991, leo ina miaka 26 imepitwa na wakati, imechoka na mimi nasema ni kweli. Yaani aliye-*observe* namna hiyo ame-*observe* vizuri kabisa UK91 ni mbegu ya zamani, uzalishaji wake umeshuka chini lakini hata uhimilivu wa visumbufu wa hii mbegu sasa na wenyewe uko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana ndani ya Serikali na tumeweka proramu ambayo tumeanza kuitekeleza mwaka huu na tumejiwekea lengo, wale wanaosema hatuweki malengo, tunaweka! Tumejiwekea lengo kwamba inapofika msimu wa kilimo wa 2019 tutakuwa na utoshelevu wa mbegu mpya aina ya *UKM08* kwa nchi nzima. Hatutakubali tena mkulima yeyote wa pamba Tanzania apande pamba ya *UK*91.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu peke yake tumepanda *hectares* 80,000 katika Wilaya tatu, Wilaya ya Igunga, Wilaya ya Nzega na Wilaya ya Meatu. Tumepanda *hectares* 80,000 za *UKM08* na tuna-*control* isije ika-*mix* na *UK91* na tutapata kama tani 8,000 ya mbegu na baada ya hapo katika msimu unaofuata wa 2018 tukipanda mbegu ile tani 8,000 tutakwenda kwenye tani 14,000/15,000 ambayo ndiyo mahitaji ya nchi nzima kwenye aina hii ya mbegu ya *UKM08*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo ndugu zangu wakulima wa pamba naomba niwahakikishie tu kwamba, hili jambo tutalisimamia kikamilifu na mwaka 2018 wakulima wote wa pamba tunatarajia kabisa watakuwa na mbegu mpya ya *UKM*08. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wafanyabiashara wanajaribu kuingiza mbegu feki, dawa feki na kadhalika.

Jambo la kusema hapa kwa kifupi tu ni kwamba ni lazima tuimarishe usimamizi, haya mambo ya feki na nini, dawa yake ni usimamizi. Tunapoimarisha usimamizi maana yake hatutoi mwanya kwa mtu kuchomekea mbegu au dawa ambayo sio sahihi. Tumechukua hatua, *stern measures* kweli kweli kwa Watendaji wa Serikali ambao wamekuwa wana-*collude* na wafanyabiashara kuingiza mbegu na dawa mbaya ambazo zinawaathiri wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Maige akilalamikia wale waliopewa mbegu ya pamba miaka mitatau iliyopita wakapanda haikuota halafu mamlaka mbalimbali za Serikali zikaanza kutupiana mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo kwa sababu lina utaalam ndani yake huwezi kulirukia kusema kwamba ni *TOSK* au *TPRI* au ni nani waliotufanyia *foul* katika hili. Kwa hivyo, tutakapojiridhisha kwamba ni nani hasa *culprit* katika hili tutamchukulia hatua tu. Hata kama uwezo wake wa kifedha utakuwa hauwezi kuwa-*compensate* wale wakulima lakini tutamfunga, tutamfanyia chochote ili iwe fundisho kwa wengine kwamba uki-*temper* na mambo ya wananchi Serikali ipo itakuona na itakuchukulia hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la uvuvi wa bahari kuu na mchango wa uvuvi kwa ujumla. Mheshimiwa Abdallah Ulega amesema kwa maneno mazuri sana kwamba *blue economy* Tanzania ni kama haipo, haipo kwa sababu tulikuwa na kanuni legelege. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka, alitumwa Mheshimiwa Mama Tibaijuka kwenda *UN* kwenda kuomba hiyo *EZ* tukafanikiwa kwenye hilo jambo, lakini tangu tupate hiyo *EZ* nchi kama nchi kwa mwaka tumekuwa tunaambulia shilingi bilioni sita. Huu udhaifu ulikuwa katika kanuni tulizotunga wenyewe. Nchi zote zinazofanya uvuvi wa bahari kuu, majirani zetu hawa wamekuwa wanatushangaa, hivi Tanzania hawa wakoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa nafanya majadiliano na kampuni kutoka *Spain* kampuni 29

zinazofanya uvuvi bahari kuu walikuja kuniona wanahoji hizi kanuni kwa nini ziko hivi. Siku hiyo tunafanya hayo mazungumzo, *South Africa* walikuwa *tempted* kumleta Waziri wao wa Uvuvi aje kusikiliza kama tuta-*yield/bow* kwenye hoja za hawa watu. Mimi nikamwambia wewe kaa tu huko, tuko imara, tunajua tulichokifanya. Tume-*research,* tumeangalia *best practice* ya wenzetu wanafanyaje na sisi tumeji-*peg* katika mambo ambayo yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali *by catch* siyo mali ya aliyevua, mvuvi anaomba *license* ya aina ya samaki, tunampa *license* ya kuvuna huyo jodari basi, akikamata samaki mwingine huyo hakuwa ameruhusiwa na wala hajakata *license* kuvuna yule na ile ni rasilimali ya Watanzania. Tunachosema kwenye Kanuni zetu, hiyo rasilimali uliyokamata ambayo siyo ya kwako ambayo tumekuruhusu kuvuna leta. Tunazungumza *modality* ya *compensation* ya mafuta na kadhalika, lakini tumeweka suala la uhakiki wa *volumes au tonnage* wanazovuna*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zamani mtu akivua samaki kule akishakata *license* ile dola 50,000 miezi sita, anavua kiasi chochote atakachopata sisi hatuambulii chochote. Tulichokomea ni hiyo dola 50,000. Sasa hivi tumesema hii nayo ni maliasili kama zingine, zitalipiwa pia mrabaha na kwa maana hiyo tutapeleka *observers* wetu, wakajue bwana huyu kavuna kiasi gani kwa hivyo mrabaha wetu kiasi gani. Katika hizo alizovuna kwenda nazo huko anakoenda sawa, zile zisizostahili ngapi tuletee hapa Watanzania wapate samaki kwa bei nafuu tuongeze lishe kwa watu wetu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna *multiply* effect kubwa sana. Meli zile zitakapoleta ile *by catch* watakuja kununua chakula, kuweka maji, wataweka mafuta, watalipia sijui nini. Kwa hivyo, uchumi utanufaika siyo kwa samaki tu lakini uchumi utanufaika hata kwa mambo mengine zaidi ya hao samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweka sharti la kuwa na Mabaharia Watanzania. *Activity* hii inafanyika ndani ya eneo letu la nchi, si ndiyo? Ni kama mtu aje aweke kiwanda hapa halafu asilimia 100 ya wafanyakazi ni watu wa nje tutakubaliana na jambo la hivyo? Kwa hivyo ile meli inapokuja kufanya *activity* ya mwaka mzima Tanzania, tunasema na Watanzania wa-*participate* lazima kuwe na *local content* Mheshimiwa Ngwali! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako vijana hapa wanasoma vyuo vyetu hapa wanamaliza halafu wanatushangaa tu, kwamba watu wanatoka huko watokao, China, Indonesia na Taiwan wanakuja wanafanya shughuli ya uvuvi hapa, Tanzania hakuna hata Baharia mmoja huko ndani, hakuna kila kitu tumewaacha wanasomba wanavyotaka, mimi nasema jamani niacheni jamani niacheni nishughulikie hili jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wakati akiwa Waziri wa Uvuvi alikamata tani 290 tu ya meli iliyokuwa inafanya uvuvi haramu pale. Tani ile 290 ilisambaa Magereza yote Dar es Salaam, Morogoro mpaka Tanga. Sasa kwa wastani hesabu na wataalam wetu wanasema, ukivua tani moja *at least* asilimia 20 ni *by catch,* wanakamata kule zaidi ya tani 20,000, tani elfu ngapi. Kwa hivyo, tunatarajia tu hata ile *by catch* itakuja hapa maelfu ya tani.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri muda wetu ndiyo huo.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, tunakushukuru. Katibu.

**NDG. RAMADHANI ABDALLAH ISSA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 43 – WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI**

Kif.1001 – *Administration and HR Mgt*......Sh. 6,631,658,700/=

**MWENYEKITI:** Wheshimiwa Wabunge, wote mmeangukia kwenye Kanuni 101(3) mshahara wa Waziri na baadaye mtalalamika, nina orodha ndefu sasa naanza na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, lakini hapa ni sera tu.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, habari yangu mimi itahusu udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Nimepitia ukurasa wa 57 wa bajeti ya Wizara husika, kuna ndege wanaitwa kwelea kwelea, ndege hawa wameleta madhara makubwa sana hasa kwa sisi wakulima wa mpunga na mtama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtakumbuka mwaka juzi tumehangaika sana kulikuwa na mlipuko mkubwa sana wa ndege hawa wamekula sana na walileta madhara makubwa, tatizo hapa ambalo nitahitaji maelezo ya Wizara sababu nimepitia kwenye kitabu sijaona *commitment* iliyoniridhisha. Tunapotaka kuwaangamiza ndege hawa tunahitaji ndege pamoja na sumu kwa ajili ya kunyunyiza

kuwaua hawa ndege, lakini hii *aeroplane* tunakodi kutoka Kenya na nchi zingine, nchi hii ni kubwa ndege tu ya kunyunyizia dawa, nini *commitment* ya Serikali katika jambo hili? Naomba maelezo ya kutosha kwa sababu kwelea kwelea hawa wanaleta madhara makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli suala la kwelea kwelea na wadudu wengine waharibifu wa mimea lipo na ni kubwa, kwa msimu huu wa kilimo tulikuwa na kesi kama tano za kwelea kwelea hapa nchini. Kwelea kwelea walionekana na walianza na kuharibu mazao Singida, maeneo ya Kondoa, maeneo ya Morogoro na maeneo mengine kule Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo tulichokifanya, kwamba nchi za Kanda hii ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika tunao ushirikiano chini ya *umbrella* ya Umoja wa Afrika wa namna ya kudhibiti na kushambulia hawa ndege waharibifu, kupitia *program* hiyo ya pamoja ambayo inaratibiwa na Umoja wa Afrika, nchi ikipata janga la hawa ndege inachofanya ni kuwaarifu Addis Ababa na Addis Ababa wanaandaa utaratibu wa kuja kuteketeza hao ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi ni zile ada ambazo tunatakiwa kulipa kama nchi kwenye Umoja wetu wa *AU* ziwe zimelipwa, kwa hiyo mkiwa na kesi ya kwelea kwelea ni kupiga simu ndege inakuja inanyunyizia. Hatukodi ndege kutoka Kenya, ile ndege ni mali ya *AU* na ipo pale ku-*save* nchi zote wanakuwa ni *members* wa *AU* katika hii *zone* yetu ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtuka, ulikuwa unataka maelezo umeridhika.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Bado sijaridhika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa sasa aah! Haya tutaendelea kujifunza Kanuni. Endelea kwa kifupi tu.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa uzoefu ambao tumepata shida kubwa sana.

**MWENYEKITI:** Sema *straight* kwamba usiporidhika nitatoa shilingi lakini tangu mwanzo hukusema ndiyo taratibu zetu. Shabaha yako iwe ni moja kwa moja kama hutaridhika na maelezo ya Waziri.

**MHE. DANIEL E. MTUKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli na nina nia ya kutoa shilingi kwa sababu...

.

**WABUNGE FULANI:** Toa

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi, naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono.

**MWENYEKITI:** Sisi hatushughuliki na nia. Mheshimiwa Daniel Mtuka umesikia maelezo ya Serikali sisi ni wanachama wa *AU*, ndege hii tungeliweza ikakaa Dar es Salaam lakini inakaa Nairobi na Ethiopia, tunapopata matatizo inaitwa inakuja kufanya shughuli hiyo hatulipi chochote, sasa unataka Waziri afanye nini?

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kutokana na uzoefu nilionao, ucheleweshaji unakuwa ni mkubwa sana, mpaka hiyo ndege ifike yaani mazao yameshakwisha. Naomba nitoe hoja ili wenzangu waniunge mkono katika kujadili jambo hili. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hujaungwa mkono, wachache mno. Tunaendelea Mheshimiwa Abdallah Ulega na Mheshimiwa Jumaa Aweso ajiandae.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

nakushukuru sana kwa kupata fursa hii. Kwa kuwa, katika mchango wangu wa dakika tatu uliponipa nafasi nilizungumzia juu ya kuona namna ya kuongeza pato la Taifa letu kwa kupitia bahari yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapo katika maelezo yake wakati anahitimisha hoja ameeleza kwamba tumuachie suala hili la uvuvi kwa sababu jambo lililokuwa kubwa ni kanuni. Nataka nimwambie tu, pamoja na kutaka kuongeza bajeti yetu kupitia pato la *blue economy* bado ukitazama bajeti hii ya Serikali eneo la uvuvi ni kiasi kidogo mno. Pesa iliyopangwa kutoka katika mapato yetu ya ndani ni shilingi bilioni mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi ni sehemu ya watu maskini sana katika nchi hii, bado ningependa nimsikie Waziri juu ya mkakati tulio nao na hasa nimemshauri tunataka tuongeze mapato yetu, tunaishauri Serikali na kumshauri Rais wetu, tununue meli kwa ajili ya shughuli hii ya uvuvi. Nataka nimsikie Waziri anasemaje anyambulishe zaidi maelezo yake.

**MWENYEKITI**: Ahsante muda wako ndiyo huo.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo nitatoa shilingi

**MWENYEKITI:** Umeshtuka eeh! haya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Mheshimiwa Ulega amenisikiliza vizuri hapa nilivyosema, kwamba udhaifu tuliokuwa nao haukuwa nje ya kanuni tulizotunga wenyewe. Kanuni tulizokuwa nazo ndizo zilikuwa dhaifu ambazo zilikuwa zinasababisha watu waje wafanye shamba la bibi huko baharini, sasa tulicho kifanya tumebadili hizo kanuni zifanane na wenzetu wanaonufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulega huyu amekwenda Maldives kujionea mwenyewe wenzetu

wanachofanya makusudi tulifanya hivyo Serikali, ili wenzetu Wabunge wakishaona hatua tunazofanya watatuunga mkono katika hili jambo. Kwa kweli nina hakika aliyoyaona kule ndiyo aliyokuwa anayasema leo. Uwekezaji katika hili jambo unaweza kufanywa na Serikali lakini kama fursa itaonekana inavutia tunachotarajia ni kuona wawekezaji wa ndani wakiingia kwenye hili jambo, siyo lazima kila kitu kinachojenga uchumi kifanywe na Serikali. Tumetengeneza masharti haya ili wawekezaji wa ndani na hao wanaotoka nje wote watakachokifanya Taifa linufaike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napiga hesabu leo tunapata bilioni sita kutokana na uvuvi wa Bahari Kuu lakini tukitekeleza na *application* za *license* zinaendelea kutolewa tukitekeleza hili tu, tuliloliweka kwenye kanuni kwa ukamilifu, makadirio yetu tutafika kwenye bilioni 80 mpaka 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ya msingi mengine ambayo yanatakiwa kufanywa pamoja na ujenzi wa hiyo bandari ya samaki, ni jambo ambalo wengi wanasema mbona hamjajipanga sawa sawa, sisi tunasema tumejipanga kwa kuanzia na hizo gati Namba sita pale Dar es Salaam na gati Namba tatu.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ulega lakini ukifika kwenye hatua ile nataka tu niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge asije akajisikia vibaya Mheshimiwa Daniel Mtuka, ninaposema iungwe mkono hoja ni Wabunge zaidi ya 10.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli ameeleza Mheshimiwa Waziri lakini najenga hoja kwa kusema kwanza naomba hili jambo tulijadili. Kwa hivyo, naichukua shilingi yake Mheshimiwa Waziri, tuwaruhusu wenzangu tuweze kulijadili jambo hili la uvuvi, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. COSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Imeungwa mkono, tuwachukue majina, Kanyasu, Haonga, Waheshimiwa hebu tuwe na *displine* kidogo, ilikuwa ni kuunga mkono hatua ya kwanza, wanaotaka kuchangia hoja ndiyo hao tunawataka sasa. Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Dau, Keissy na wewe upo haya, Mheshimiwa Dkt. Immaculate Semesi, Kanyasu, Mheshimiwa Ngwali lakini Mheshimiwa Ngwali umenielewa mimi ulichonifanyia kwenye meza haya, lakini Waheshimiwa muda haya Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaanza na Mheshimiwa Kitandula ndiyo mwenyewe naelewa haya. Tunaanza na Dkt. Emmaculate.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Abdallah Ulega kwa kusisitizia kwamba tuna mali kwenye bahari yetu, tuna mali kwenye maziwa na mito yetu ambayo hatuitumii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Ulega ni kwamba tufunguke na tufungue macho yetu tuone *potential* tuliyo nayo kwenye uvuvi. Mimi nitajikita kwenye uvuvi wa bahari kuu. Unaposema kwamba *private sector* inaweza ikachukua hiyo fursa lakini hiyo fursa hakuna miundombinu ya kukufanya wewe uende baharini. Mfano ni kwamba wale wavuvi wetu wa sasa hivi wanatumia hii bahari fupi kwa kutumia vifaa ambavyo vimepitwa na wakati, wenzetu wanakomba mali yetu kwenye bahari kuu, sasa anasema Mheshimiwa Ulega tuamke nchi yetu tunaweza kuiendesha uchumi wetu kwa kutumia uvuvi peke yake, akatoa tu mfano mdogo wa Maldives na kuna nchi nyingi Norway, Wajapani, nchi za Asia zinaishi kwa uvuvi na hiyo rasilimali tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaacha rasilimali yetu inaibiwa wakati tuna uwezo wa kuamka na kujikita kwenye shughuli ya uvuvi.....

**MWENYEKITI:** Dkt. ahsante sana. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ulega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina maziwa ina mito, ina bahari ni aibu kuagiza samaki kutoka nje, wakati tuna samaki wa kutosha na kuweza kuuza nje. Mfano Ziwa Tanganyika tu samaki wake wanaharibika unaweza kuuza nchi nzima na zikaenda nchi za nje, sasa Serikali ifanyie mkazo uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tozo kwenye uvuvi katika Ziwa Tanganyika Mheshimiwa Waziri haukupunguza hata senti tano, tumelalamika kila mara hapa. *License* tuna Halmashauri sita; ukikata Halmashauri ya Kalambo huwezi kwenda kuvua Halmashauri ya Mpanda, wala Halmashauri ya Nkasi huwezi unavulia pale pale Mzee. Mtumbwi *license* wakiwa wavuvi 10, kila mvuvi awe na *license* mbona kwenye gari siyo namna hiyo. Wavuvi bado wanagandamizwa nchi hii watainuka vipi, hakuna watu maskini katika nchi hii kama wavuvi, ni watu dhalili kabisa katika nchi hii, hawana uwezo kwa sababu wanagandamizwa na kodi za ajabu na ushuru wa ajabu ajabu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ulega kwamba uwekezaji kwa kweli uwekezaji katika Wizara hii hasa kuhakikisha kwamba tunajaribu kulinda wavuvi wakubwa kwenye bahari kuu ni mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa ipo kwenye upande wa Ziwa Victoria. Wakati nachangia nilimueleza Mheshimiwa Waziri kuhusu matumizi mabaya ya sheria ya kukamata nyavu. Mheshimiwa Waziri anajua kwamba kule Ziwa Victoria samaki ambao ni sangara wanasemekana wamekwisha, miaka michache iliyopita ilikua ni zao la pili

kwa *forex.* Serikali haijawahi kufanya uwekezaji wa aina yoyote, *reproductive capacity* ya sangara mmoja anachukua *maturity* ya miaka mitatu kutengeneza *offspring* milioni tisa, lakini Serikali ingeweza kutengeneza mazingira ya kuwa inazalisha hawa *offspring* na kuwamwaga ziwani kwenye maeneo ambayo yametengwa wakaondokana kabisa na tatizo la kuonekana sasa hivi sangara mpaka kwa ajili ya mboga wanakosekana kwa sababu Serikali inachokifanya ni kupambana na wavuvi badala ya kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naunga sana hoja ya Mheshimiwa Ulega Serikali iwekeze kwenye uvuvi...

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru ninasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ulega. Katika maelezo yake Mheshimiwa Waziri anasema wanazipitia kanuni, sasa atupe *timeframe* na commitment hizi kanuni zitakuwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoevu wangu binafsi, unaonesha Mheshimiwa Waziri huyu toka anaingia *day one* katika ofisi aliniahidi mimi atabadilisha kanuni za Hifadhi ya Bahari ya Mafia mpaka leo hata nukta hajaibadilisha. Sasa hapa leo atuambie hizo kanuni ambazo anasema atazibadilisha, anazibadilisha *by when?* Aseme hapa hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Mheshimiwa Ulega amesema vizuri tu hapa, Serikali mtanunua lini Meli ya Uvuvi wa Bahari Kuu? Kama kweli kuna faida kwa nini sasa tunakaribisha watu waje, kwa nini tusivue wenyewe? Tujibu na suala la meli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, ingawa yeye siyo Waziri wa Maliasili. Mheshimiwa Ngwali umeondoa haya. Mheshimiwa Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Labda nijaribu kuzungumza taratibu labda litaeleweka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *blue economy,* unazungumzia Uvuvi wa Bahari Kuu, vilevile unazungumzia ufugaji wa samaki. Ulimwenguni sasa zaidi ya asilimia 50 ya samaki wanaoliwa duniani wanatokana na ufugaji wa samaki. Naomba sana, hebu tujielekeze kwenye ufugaji wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukichukua asilimia moja tu ya pato lililopatikana kwenye mapato ya uvuvi tukalipeleka kwenye ufugaji wa samaki unazungumzia takribani bilioni 14, tutakuwa tumepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya bajeti hii wameweka hata kwenye mirungi, wamepeleka pale bilioni moja kwa ajili ya ku-*support* mirungi. Sisi tunashindwa nini kwenye jambo hili ambalo... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kitandula. tunaanza upande wa Serikali, Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza niungane na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna *potential* kubwa sana kwenye sekta hii ya uvuvi ambayo wanaongelea. Nijikite tu sehemu aliyoisema Mheshimiwa Ulega kuhusu Serikali kununua meli ya uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wazo zuri la Mheshimiwa Ulega Serikali kwa maana ya Wizara

wanaendelea na utaratibu ambao utahusisha sehemu ya mkono wa Serikali, kwa maana ya taasisi zinazoweza kufanya biashara kama Mashirika ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na kile kilichokuwa kikifanya kazi hiyo siku za nyuma, hata kama kitarudi kwa jina tofauti. Katika utaratibu wa uendeshaji wa uchumi wa kisasa, ukiwa na vitu vingi sana ambavyo ni vikubwa na Serikali ikafanya yenyewe ujue una mazingira makubwa sana ya ku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana. Mheshimiwa Mpina.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoanza mwaka 2009/2010 mapato ya kutoka Bahari Kuu yalikuwa ni Dola za Marekani 700,000 peke yake, leo tuko Dola za Marekani 3,000,000 ambayo ni bilioni sita (6) fedha za Kitanzania, tumepiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri hapa ameelezea juu ya kuwezesha sheria zetu tumezifanyia marekebisho hapa Bungeni ya kuwezesha meli kubwa za uvuvi wa Bahari Kuu kutia nanga hapa nchini. Kigezo hicho kiliwafanya hata wawekezaji wetu wa ndani, ambao wangeweza kununua hizo meli za uvuvi wa bahari kuu wasifanye hilo zoezi kwa sababu hazina mahali pa kutia nanga zile meli, wangenunua zingetia nanga wapi?

Sasa leo tumefanya hatua ya kwanza tumekubali kwamba meli zile zitie nanga hapa, ni kwa kweli tulikuwa tunapoteza mapato mengi sana, nami nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge. Sasa kwa sababu meli zitatia nanga hapa kwetu tutaweza kuhakiki samaki wanaovuliwa na kuweza kujua mapato ambayo tutapata.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilitegemea Mjumbe wa

Kamati ya Spika ya Chenge *One* Mheshimiwa Zungu angesema lakini tuendelee. Mheshimiwa Stella Manyanya Injinia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge waweze kurudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Pia niseme, michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge Serikali kwa kweli hakuna ujanja wa kuikataa kutokana na ukweli ni kwamba wananchi wetu wengi ambao ni wavuvi bado maisha yao hayajawa mazuri. Kwa kuzingatia hilo ndiyo maana hata ikatungwa sheria ya kuona namna gani ufanyike utafiti. Kwa mfano, upande wa Zanzibar tayari kuna hata utafiti wa kuzalisha vifaranga vya kaa, hiyo yote ni kuonesha umuhimu wa *blue economy.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa suala hilo la meli Mheshimiwa Rais wakati huo kama mtakumbuka alikamata hata zile meli za wenzetu waliokuwa wanakuja kuvua. Sasa tumeshaona mfano kwa nini tusifikie huko? Kwa hiyo, tuipe muda Serikali lakini tuone kwamba hilo jambo ni la msingi na wote tunaliunga mkono ikiwemo na ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri una jambo la ziada au niende kwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi sina tofauti na wazo alilosema Mheshimiwa Ulega. Nakubaliana naye kabisa kwamba ukiwa na uwezo unafanya mwenyewe, lakini kama huna uwezo unamwacha mwenye uwezo afanye wewe unufaike. Ndiyo maana sera ni kukaribisha wawekezaji siyo kwamba kila kitu ambacho Serikali inaweza kufanya, basi ing'ang'anie ifanye. Nataka kusema jambo moja la faraja sana katika kumjibu Mheshimiwa Ulega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekwishaanza mpango na nimeona siyo mahali pake hapa kusemea mambo ambayo bado yanapikwa hayajaiva halafu wewe unaanza kusema, tuko katika hatua nzuri tu, Serikali pia itanunua meli zake za uvuvi. Sasa sikutaka ku-*jump the gun*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nakushukuru sana. Mheshimiwa Ulega baada ya maelezo hayo kweli ndugu yangu. Karibu.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hayo maneno ya mwisho ya mjukuu wangu Dkt. Tizeba yamenipa faraja. Sasa nataka nikuhakikishie shilingi yake ya kumfikisha kule Buchosa namrudishia. Naendelea kusisitiza kwamba meli hiyo inunuliwe na hii habari ya gati lazima tukubaliane kama alivyosema yeye mwenyewe nilikwenda Maldives na nimeona. Tusi-*complicate* mawazo yetu, magati ya mabilioni ya mapesa matokeo yake yanatupotezea hela nyingi sana, halafu matumizi yake ni madogo. Wenzetu wamefanya vitu *simple* na wamefanikiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Jumaa Aweso.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Juzi katika mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, nilitoa mchango kuhusu suala zima la kufufua zao la minazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda hii ya Pwani kwa maana ya kutoka kwa kaka yangu Kitandula, Mkinga mpaka Kusini uchumi wetu pamoja na visiwa vyote kwa maana ya Zanzibar na Mafia tulikuwa tukitegemea zao la nazi. Zao hili la nazi linakufa kwa kasi ya *4G* na hakuna mikakati yoyote thabiti ya Serikali katika kulifufua zao hili la nazi. Nataka *commitment* ya Serikali juu ya mikakati ya kulifufua zao hili la nazi, kama majibu yake hayakuniridhisha nitashika shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Maelezo Mheshimiwa Waziri, anataka ufafanuzi kabla hajakasirika. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe tu wasiwasi Mheshimiwa Aweso kwamba zao la nazi halina mkakati. Zao la nazi linao mkakati. Tulikuwa na utaratibu wa kuja kuwapitisha Wabunge katika *program* ya Maendeleo ya Kilimo awamu ya pili, bahati mbaya ratiba ikabana, lakini ndani ya *program* hiyo angeweza kuona jinsi mazao kadhaa yanavyowekewa mkakati wa namna ya kuyazalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunacho Chuo cha Utafiti wa Kilimo pale Mikocheni, moja ya eneo ambalo wanafanyia utafiti mkubwa kabisa ni zao la nazi za kuzaa kwa muda mfupi na mavuno mengi zaidi. Kwa hivyo, kwenye *ASDPII* katika ile miradi 56 ile tunayozungumzia yako mazao ambayo yamewekwa mahsusi na *program* za uendelezaji wake, nazi ni mojawapo.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Aweso.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakuwa umesikiliza kauli mbalimbali za Mheshimiwa Rais alikuwa anasema msema mkweli ni mpenzi wa Mwenyezi Mungu, mimi nataka kwenda peponi naomba niseme ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majibu ya Serikali kuhusu suala hili la mnazi wamesema wameshafanya tafiti miaka 25 mpaka sasa majibu hawajapata kama UKIMWI. Sasa naomba nitoe hoja kwa Waheshimiwa Wabunge waungane na mimi katika kulijadili suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Wanaotaka kuchangia sasa ndiyo wasimame tuwachukue majina,

Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mheshimiwa Amina Mollel wametosha. Nazi itaelezwa vizuri tu na hawa watatuwakilisha, tunaanza na Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi natoka Mkoa wa Lindi, Mkoa wa Lindi ndiyo Mkoa kwa sasa ambao unalima nazi nyingi kuliko Mkoa wowote nchi hii. Miongoni mwa vyanzo vyetu vikuu kabisa vya mapato katika Halmashauri zetu tunategemea ushuru wa nazi. Miaka ya hivi karibuni nazi imeanza kupotea kwa sababu ya minazi kufa, watu wa kawaida hatuelewi tatizo ni nini na wakulima hawajui tatizo ni nini?

Mheshimiwa Waziri, inawezekana Mheshimiwa Waziri hajui thamani ya nazi, lakini kwetu watu wa Pwani hatuwezi kula ubwabwa bila kuwa na nazi, thamani ya nazi ni kubwa sana kwetu. Sasa Mheshimiwa Waziri namwomba nazi inapotea, na nazi ikipotea wali hauliki, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nakuomba sana.......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bobali. Mheshimiwa Khadija Aboud wewe si unatoka Zenji?

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naungana na Mheshimiwa aliyejenga hoja hapa kwamba zao la nazi linapotea nchini na zao la nazi linahitaji kwa sasa tulipe kipaumbele kwa sababu zao la nazi halitumiki tu kama chakula, lakini zao la nazi kifuu ni thamani ya mapambo na nishati, mti wa mnazi ni mbao nzuri ya kutengeneza thamani zinavutia kwa watalii, makuti inatumika katika ujenzi na mapambo, tui linatumika katika chakula na mafuta mazuri ya kujipaka kungarisha ngozi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa kuna wimbi linaloingia la kuingiza nazi kutoka nje nazi ya unga kwa sababu ndani ya nchi kuna upungufu wa nazi. Nazi ni eneo moja la kupatia fedha za kigeni kwa sababu nazi inatumika dunia nzima. Tunaweza kupata fedha za kigeni kwa kutumia nazi, na vifaa vya nazi.......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana umeeleweka. Mheshimiwa Maryam Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi naunga hoja mkono. Sasa hivi miti ya minazi inakatwa ovyo sana. Kwa mfano, Bagamoyo ukiangalia sasa hivi mashamba yote yale ya minazi yameshakatwa. Sasa hivi tunapata nazi ambazo zinatoka nje ya nchi, hatujui ubora wake, hatujui viwango vyake viko vipi na ukiangalia sasa hivi kuna maradhi ya saratani, kuna maradhi ya moyo, kuna maradhi chungu nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali zao la nazi lipewe kipaumbele hasa kwa Mikoa ya Pwani, ukanda wote wa Bagamoyo, Zanzibar, Chalinze kila mahali palipokuwa panalimwa nazi yale mashamba yafufuliwe ya nazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mnaona nazi zinavyotuunganisha, Muungano. Sasa naongeza muda usiozidi nusu saa kwa mujibu wa Kanuni 104(1). Tunaendelea Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Aweso juu ya suala la nazi. Naomba tumweleze Mheshimiwa Waziri kwamba tunachosikitika hata kile kituo tunachosema pale Mikocheni yule *Researcher* Mkuu sasa hivi hayupo yupo kwenye *NGO* ya *CSDI*. Utafiti ule umekoma zaidi ya miaka saba au 10 nyuma. Bahati nzuri mimi nilikuwa ni

Meneja Utafiti wa mashamba ya utafiti kule Zanzibar, utafiti ule haupo. Kwa hiyo, tunataka Serikali hapa iji–*commit* itarudisha lini utafiti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa linaloathiri nazi ni mdudu ambaye anaathiri minazi ukanda wote huu wa Pwani na Zanzibar. Zanzibar ilikuwa ni sehemu ya kusafirisha nazi katika kila eneo la nchi hii, lakini leo Zanzibar tuna-*import* nazi, hali ni mbaya, Tanga, Bagamoyo na maeneo mengine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kama ulivyosema kwamba nazi imeunganisha Muungano, mimi nimeolewa Zanzibar, kwa hiyo naelewa umuhimu wa nazi. Nazi ni kiungo muhimu naungana na hoja ya Mheshimiwa Aweso. Niombe tu Serikali kwamba kwa sababu tayari imesema kuna vituo vinavyofanya utafiti kuangalia jinsi gani wanafanya utafiti ili angalau minazi iwe ya muda mfupi. Kwa sababu ni kweli kinachochangia ni minazi mingi tayari imeshakuwa mizee na inahitaji tuweze kupanda nazi nyingine kwa wingi. Kwa hiyo, Serikali tu itoe *commitment* ni kwa jinsi gani itakavyowasaidia wakulima wa nazi kuhakikisha kwamba wana-*supply* hiyo minazi ya muda mfupi ili basi zao hili liendelee kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jafo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hoja aliyozungumza Mheshimiwa Aweso unaona imegusa sana watu wa ukanda wa Pwani kwa sababu ni zao kubwa sana la uchumi katika ukanda huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kihistoria tulikuwa na *African*

*Tall* ni mbegu ambayo ilikuwa inatumika lakini katikati tulipata tatizo la *Lethal Decay* minazi mingi sana ukanda wa Pwani ikawa inaathirika na huu ugonjwa wa *Lethal Decay*. Mimi nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya Kilimo katika Bunge lililopita katika awamu ya kwanza. Kuna tatizo limejitokeza na ndiyo maana ukiangalia katika *Agriculture Development Strategic Plan II* imezungumzia mpango mkakati wa jinsi ya kuboresha zao la nazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hoja hizi na suala zima la msingi la nazi ningemwomba Mheshimiwa Aweso kwamba, kwa sababu kuna mpango huu wa Serikali, basi tuweze kumruhusu Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana shilingi yake iweze kurudi, kuhakikisha kwamba jambo hili sasa kwa sababu Waziri analibeba katika mpango huu wa kilimo katika agenda ya pili suala la nazi na Kamati yetu ya Bunge basi ilifanye kama ni jambo la kipaumbele hapo baadaye lakini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri una jambo la ziada.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tu niseme sio kwamba, sifahamu manufaa ya nazi. Ile habari aliyoisema Mheshimiwa Rehani ni nusu kweli na nusu siyo kweli kwa maana yule *Chief Researcher* ameondoka kweli, lakini siyo kwamba *research* imesimama kwa kipindi kirefu alivyosema, *research* inaendelea, wako watu pale wanafanya *research* ya nazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika kuona kwamba haya maradhi yanasababisha nazi kupungua, siyo Tanzania Bara peke yake lakini hata Visiwani tumeliwekea mkakati mahsusi ndani ya programu ya pili ya maendeleo ya kilimo. Nimwombe Mheshimiwa Aweso, tumekwishaweka programu ambayo inaanza kutekelezwa mwaka huu, maana yake kati ya sasa na tunapoanza kutekeleza programu

mwezi wa Saba siyo siku nyingi, nirudishie shilingi ili tuingie katika kuchapa kazi, minazi ianze tena upya ku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Aweso, baada ya maelezo hayo umeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge hebu sema neno.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Waziri, nami kwa roho safi tu narudisha shilingi. Kubwa pamoja na hilo nataka niwaongezee Waheshimiwa Wabunge pamoja na faida zilizotajwa pia ukitaka kuleta heshima kwenye ndoa tumia nazi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haloo! Sasa Mheshimiwa Aweso...Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitahitaji maelezo au *commitment* kutoka kwa Serikali, kupitia Waziri husika kwenye suala la sera kuhusu *research* na *development.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba basi utulivu tumsikilize mwenzetu, naelewa, Mheshimiwa Aweso nimekupa heshima sana lakini umemalizia kwa mambo ambayo siyapendi. Nataka utulivu sasa, naomba utulivu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Semesi endelea.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitahitaji maelezo kutoka kwa Waziri husika kuhusu sera au shughuli za *research* na *development.* Tanzania tumekuwa tukisuasua kwenye masuala ya tafiti kwenye kilimo, mifugo na uvuvi. Nataka tukumbushane kwamba, bila kuwa na tafiti, bila kuwa na *data* huwezi kufanya maamuzi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wameshaongelea hapa umuhimu wa *research,* tumeongelea kwenye nazi na maeneo mengine, hatuwezi kusonga mbele kimaendeleo kama hatutafanya tafiti, kwa sababu zile tafiti ndio zinatufungulia mwanga wa kuona kwamba tunapigaje hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nchi yetu imekuwa ikirudi nyuma badala ya kusonga mbele, hii iko dhahiri kwenye mambo ya kilimo, kwenye uvuvi, kwenye mifugo, sekta ambazo ndiyo maisha yetu. Tumeji-*commit* Watanzania na Nchi nyingine za Afrika kwenye *Maputo Declaration* 2013 kwamba, asilimia 10 ya bajeti yetu yote ya Serikali iende kwenye shughuli za kilimo. Asilimia moja ya *GDP* yetu iende kwenye tafiti kwa sababu tunajua umuhimu wake, lakini hii haijawahi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu ya kilimo tumeona namna ambavyo inashuka. Bajeti yetu ambayo inapelekwa kwenye tafiti ni sifuri! Tuna *Institutions* humu ndani, *TAFIRI* mambo ya uvuvi ina sifuri kwenye *research.* Hawa watu wa *TPRI* mambo ya *pesticides,* wana sifuri kwenye *research. TALIRI* ambayo inahusiana na mifugo ina sifuri kwenye *research.* Sasa tutatokaje hapa tulipo na tunaona dhahiri ambavyo tunarudi nyuma badala ya kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kutoa shilingi nisiporidhika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, si miezi mingi iliyopita Bunge lako Tukufu hapa lilipitisha sheria mbili zilizokuwa zinaanzisha taasisi za utafiti chini ya hii Wizara. Katika sheria hizo Waheshimiwa Wabunge kama mnakumbuka, viko vipengele ambavyo vilikuwa

vinaruhusu taasisi hizi kuzalisha au kuwa na *ventures* za kuziingizia vipato. Sambamba na ruhusa hiyo iliyotolewa kisheria ambayo zamani haikuwepo, bado vituo vya utafiti vyetu vya kilimo vinavyo njia mbadala za kupata fedha kwa ajili ya utafiti, nje ya bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kule kwenye korosho, korosho inakatwa *export levy; export levy* ile ikikatwa asilimia 15 ya ile *export levy* inapelekwa Naliendele kwa ajili ya utafiti wa korosho. Kule kwenye pamba kuna *CIDTF,* wale wanatoa fedha kwa mgawanyo ulioko kwenye kanuni ya zile pesa wanapeleka Ukirigulu kwa ajili ya utafiti wa pamba. Hivyo hivyo kwenye tumbaku, *TORITA* wanapata pesa kutokana na tozo kwenye tumbaku na hizi tozo Waheshimiwa Wabunge hatukuzigusa kihivyo kwa sababu ya kujua umuhimu wa utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na vyanzo hivi kuna kushindania pesa ambayo inatengwa na bajeti hapa ndani huko *COSTECH,* kwamba, watafiti, ambaye anaona hawezi kufanya utafiti kwenye *applied research* kule kama...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. maelezo mazuri na wewe ni *Researcher* mzuri, eeh.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba niseme sasa nitatoa shilingi na nitaomba niungwe mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kila *Institution* au siyo kila *research* inazaa na inapata pesa za kuweza kufanya kazi zake. Hii inaonesha kwamba hata hicho tulichokipitisha hakifanyi kazi, taasisi zina sifuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na naomba kuungwa mkono kwenye hoja yangu.

**MWENYEKITI:** Wamefika zaidi ya kumi. Sasa wanaotaka kuchangia na Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Frank, Mheshimiwa Devotha, Mheshimiwa Rehani, Mheshimiwa Kiula, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Mbogo, Mheshimiwa Nyongo. Ufuta pia upo, Mheshimiwa Ditopile, Mheshimiwa Shangazi. Sasa nakuja watatu; Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mpina. Tunaanza na Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nimesikiliza hoja ya Waziri kwamba fedha hazijatengwa kwenye bajeti kwa ajili ya utafiti kwa sababu kuna fedha kwenye hizo taasisi. Hii ni hoja ambayo haikubaliki hata kidogo na inathibitisha ambacho amekisema mtoa hoja kwamba, hakuna kipaumbele katika *research.* Bajeti ya Serikali ndiyo inayotakiwa ioneshe njia kwa taasisi nyingine zozote, kama hakuna fedha kwenye bajeti ya Serikali, unategemea hizo za tozo za kwenye taasisi husika hutapata fedha za kutosha za kufanya utafiti wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, wasikubali haya majibu mepesi ya namna hii. Fedha zitengwe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sware.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niseme kwamba, kama bajeti haitaonesha fedha za utafiti hiyo itakuwa siyo sawa. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, kuna baadhi ya mazao ambayo yanalimwa, katoa mfano wa tumbaku na mazao mengine kwamba, kuna baadhi ya tozo ambazo zinasababisha vituo vya utafiti vijiendeshe. Kuna uwezekano

mkubwa sana baadhi ya mazao yakakosa wateja na hili limetokea katika nchi hii, lakini kuna baadhi ya mazao pia uzalishaji wake ukawa ni mdogo sana. Tafsiri yake ni kwamba, hakutakuwa na utafiti katika mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni vizuri sana bajeti kwa kweli, ioneshe kabisa kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Frank Mwakajoka. Mheshimiwa Mariam Ditopile.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu Mheshimiwa Waziri alitilie maanani kwa sababu, wachangiaji wote waliposimama wameongea umuhimu wa tafiti. Tafiti bila *resources* haitawezekana. Mipango mmeweka, sheria za usimamizi tumepitisha, lakini bila nyenzo hakutafanyika chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tutoke hapa tulipo, ndiyo maana nimewaambia leo hii tuko milioni 50, baada ya miaka 10 lazima tutakuwa tumeongezeka, bila ya kufanya *research* tutajua kweli huko mbele tutakuwa vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uchungu na nchi yetu, tuna uchungu na kilimo, mifugo na uvuvi ndio maana tunasisitiza. Basi hata hizo hela ametwambia ana trilioni moja za kutoka Ulaya sijui wapi, naomba basi hata aziingize kwenye *research,* ukija mwakani tuone. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almasi Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii. Utafiti ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya jambo lolote. Tabora tuna Kituo cha Tumbi, lakini pia kuna vituo vingine vya

Naliendele kule Mtwara ni muhimu kuwepo utafiti ambao utakuwa na tija. Mashamba kama mashamba mfano haya ambayo yapo, kama hayana hela itakuwa vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali inafanya juhudi kubwa sana. Nilitembelea Tumbi nikaona kiasi gani hela zimewekwa pale, pia ni kweli wanatafuta hela wenyewe, vituo pia vinapata hela kutokana na mazao ambayo yanasimamiwa. Kwa hiyo, ningeomba shilingi hii irudishwe, lakini Serikali ichukue ushauri kwamba, kwa kweli ni muhimu sana kusimamia utafiti kwa sababu, utafiti ule ndiyo utakaoleta mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea viwanda, je, mazao yanayolimwa nchini yana uwezo wa ku-*feed* viwanda ambavyo tunategemea kuanzisha? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rehani Mtafiti mwingine.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nakushukuru kwa kunipa nafasi tena. Niseme kwa niaba ya Watafiti ambao wako Tanzania wakiwa wananitazama; hakuna nchi yoyote iliyofanikiwa duniani bila kuzingatia utafiti, hakuna! Sasa leo Tanzania tukiwa tunategemea utafiti kwa pesa za nje, tumechemsha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri lazima atuambie hapa, katika bajeti hii ni kiasi gani katika pesa zote utakazozipeleka za maendeleo kwenye utafiti zitakwenda shilingi ngapi? Tujue. Kwa sababu wamekaa pale Ukirigulu miaka 15 hawajatoa aina mpya za mbegu. Tunaendelea kutumia *M91* ambayo haijasaidia chochote, inaota vipara! Pamba imeshuka uzalishaji mpaka leo hakuna chochote! Tunahangaika watu wa Kigoma na Mchikichi wanaenda kununua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, utafiti kwa ujumla. Mheshimiwa yeye aliomba kwenye minazi, tunaendelea na Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatakiwa iangalie kwa makini kutoa *resources* kwenye upande wa *research and development.* Tukiangalia wenzetu wa Vietnam 1974 walifanya utafiti wakachukua zao la korosho na leo hii wanatushinda. Ninachoomba mwaka jana tulipitisha Sheria ya *Agricultural Research Institute Act* na *Fisheries Research Institute Act,* lakini Waziri hajajibu hapa hizi Bodi zimeshateuliwa zimeanza kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunachelewa katika maendeleo. Kwa hiyo, naunga mkono hoja ya mtoa hoja, Dkt. Sware kwamba *research* iwezeshwe na Serikali iji-*commit* hapa kiasi gani anaweka na lini zinawekwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami namuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Sware katika hoja yake ya suala la utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiviangalia vituo vingi vya utafiti viko hoi bin taabani. Kwa mfano, Kituo cha Ilonga kule Kilosa ni kituo kizuri sana kilichokuwa kikifanya kazi nzuri sana, lakini sasa hivi kituo kile kimebaki kufanya kazi kwa matakwa ya *donors* na siyo kwa *priority* ya Taifa. Ni kwa nini Serikali isiwe na bajeti ya kusaidia vituo hivi ambavyo tayari vina wataalam, watumike kwa ajili ya kusaidia kufanya tafiti ambazo zitawasaidia Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake wanafanya tafiti kwa kuangalia matakwa ya *donors* na baada ya tafiti *donors* wanachukua wanaenda ku-*implement* kwao. Kwa hivyo, nafikiri ni wakati wa Serikali kuangalia umuhimu sasa wa kutenga bajeti kwa ajili ya kusaidia vituo vyetu hivi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Kiula.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kukisoma hiki kitabu, ukiangalia ukurasa wa 32, ukiangalia ukurasa wa 141, ukurasa wa 187 utaona suala la utafiti limezungumziwa. Wote humu katika Bunge tunakubaliana kwamba, utafiti ni jambo muhimu. Pia, yako maeneo ambayo inabidi tuyaangalie, tunatakiwa kuangalia *resources* zilizopo tunazigawanya vipi kulingana na vipaumbele. Kwa hiyo, Wizara na kwa pesa ilizopewa kwa bajeti hii, hivi ndivyo vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, namwomba tu Mheshimiwa Sware arudishe hiyo shilingi tukizingatia ziko hatua ambazo zilishachukuliwa, sheria mbili zilizopitishwa. Pia suala la *dublication* ya *resources* ni muhimu sana. Viko vituo vingi vya utafiti ambavyo vilikuwa vinapata pesa kwenye maeneo mengine vinataka vipangiwe na huku pesa, hilo ni suala ambalo linatakiwa liangaliwe kwa ukaribu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Mheshimiwa Mbunge arudishe shilingi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi!

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru na naunga mkono hoja ya Dkt. Sware. Kama nilivyokuwa naongelea kwenye michango yangu kwamba, tuna tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi, hivyo ni lazima sasa wakulima wetu tuwape *comfort* kwa kufanya tafiti. Sasa bila tafiti kwa kweli, nchi hii tutakuwa tunaendelea kwa kilimo cha mazoea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Waziri aliyemtangulia alipoingia kwenye Wizara hiyo alianza kutembelea vituo vya utafiti pamoja na mashamba ya mbegu. Kwa hiyo, nimwombe na yeye, hebu achukue jitihada za makusudi, wananchi wanapata hasara, wanalima kwa mazoea wala hakuna tafiti zinazofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Naomba kuungana na wenzangu na Mheshimiwa Dkt. Sware hapa kwamba, lazima Serikali ioneshe *seriousness* kwenye *research.* Tunakwenda kwenye nchi ya viwanda, ni lazima tuinue uwezo wa kuvuna zaidi kuliko tunavyovuna sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri tu ukiangalia kwenye alizeti, mbegu ya alizeti inatoa mafuta asilimia 25 tu wakati wenzetu Kenya wanatoa asilimia 75. Ukienda kwenye pamba *CDTF* wanakusanya fedha, lakini pamba yetu uvunaji wetu ni uleule zaidi ya miaka 25 iliyopita. Tunaomba Serikali ioneshe *seriousness* kwenye masuala ya *research.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya changamoto ambazo tunazo za vipaumbele, lakini Serikali inajitahidi sana katika kuhakikisha kwamba kidogo kinachopatikana kinafanya kazi nzuri sana ya *research.* Kwa kweli, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana *Researchers* wa Taifa hili kwa sababu mambo ambayo wamefanyia *research* yanatuletea manufaa makubwa na tija kubwa sana katika Taifa mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu ndiyo huo aliousema Mheshimiwa Waziri hapa kwamba, fedha za utafiti kwa maana ya ruzuku ya Serikali ile asilimia moja ya *GDP*

hata kama haifiki, lakini ikitoka inaenda *COSTECH* na *COSTECH* ndiyo inazipelekea taasisi zingine za kiutafiti. Taasisi nyingine za Serikali zile za kiutafiti zinapopelekewa *OC* sababu ndiyo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpina. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianzie pale alipokuwa anaishia Mheshimiwa Mpina kwamba pamoja na Serikali Kuu ku-*support* taasisi mbalimbali za *research* na *think tank organization* na kwa ujumla wake kwa kuzipa *OC* kwa maana ya kulipa mishahara ya wafanyakazi na gharama za uendeshaji, hizi *think tank organization* mbalimbali zikiwemo taasisi za utafiti zinakusanya pia pesa kutokana na tozo, lakini pia pesa kutokana na mauzo ya bidhaa mbalimbali ambazo wanazalisha katika tafiti zao, kama kwenye mashamba ya mbegu na vitu vinginevyo. Vile vile wanaandika *proposals* kwa ajili kwa co*llaborators* mbalimbali wa Kimataifa na kushirikiana kwenye miradi ya Kikanda na ya Kimataifa, miradi hii inasaidia ku-*complement* lile fungu ambalo tunakuwa tumeshindwa kama Serikali......

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba hoja ya utafiti siyo hoja ambayo inapingwa na Serikali bali ni hoja ambayo Serikali imeweka jitihada kubwa sana kwenye kuipeleka mbele. Hivi tunavyoongea kama ambavyo Waziri wenye ajenda ametangulia kusema pana fedha ambazo zinatengwa

kupitia *OC* na ni utaratibu tu wa utengaji wa mafungu ambayo tunatumia kwenye bajeti unakwenda kwa watu ambao ni mahsusi kwa ajili ya tafiti hizo na wanafanya hizo tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza nikalisema nasi kama Wabunge tulihamasishe, bado kuna matatizo ya matumizi ya matokeo ya *research* pamoja na mbegu zilizotoka na *research,* watu wetu bado wanapenda zaidi kutumia vile walivyovizoea. Mbegu zikipatikana ni wagumu sana ku-*switch* kwenda kwenye mbegu ambazo zimetafitiwa na zikafanyiwa uvumbuzi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** .....hivyo nimwombe tu ndugu yangu arudishe shilingi Waziri aendelee nasi tuhamasishe.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Waziri una lingine au limetosheleza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kwamba Serikali haioni umuhimu wa *research,* ndiyo maana pamoja na kuanzisha hizo taasisi za utafiti mbalimbali kama tulivyoona kwenye uvuvi, kilimo na mifugo lakini bado Serikali inatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya watafiti hawa waendelee kufanya huu utafiti kama kazi yao ya kila siku na wanalipwa mshahara kwa kuendelea kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Fungu moja tu 43 wametengewa 18,387,000,000 kwa ajii ya utafiti. Sijakokotoa Mafungu mengine hapa, kwa hivyo suala la utafiti kutengewa fedha lipo, zinatengwa na ndiyo kazi yao ya kila siku. Hawa siyo watengenezaji wa miradi ya

maendeleo kwamba wanafanya miradi ya maendeleo *no*! Wao wanalipwa mishahara kwa ajili ya kazi ya kufanya utafiti na fedha Mheshimiwa Sware zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu sana kwamba kama tunazungumzia utafiti wa jambo mahsusi na litengewe fedha *then* hilo ni jambo la Mtafiti mwenyewe kuwasiliana na Wizara au nani ili utafiti ule ufanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pamoja na fedha hii ya Serikali ambayo inapitishwa katika bajeti hii bado wanapata fedha kutoka hivyo vyanzo vingine nilivyovitaja mwanzo. Hivyo nilivyovitaja ni ziada ya bajeti ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na nashukuru Waheshimiwa wote walioniunga mkono kwenye hoja yangu. Nitoe tu mfano, bado nashikilia shilingi yangu. Tuchukulie mfano wa *research* kama mbegu, huwezi kuvuna bila kupanda. Sasa hii *research* yetu lazima tupande ili tuvune.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi *so far* tuna-*fail* kwenye hii sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi inazidi kushuka, japokuwa mnasema kwamba mnatoa mishahara, mshahara siyo *research*. Unaponipa mimi mshahara nakaa ofisini napigwa *AC,* siyo kwenda *lab* au kwenda *field,* tunashuka na tumeji-*commit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nimeshikilia shilingi yangu sijaridhika lazima tupande mbegu ili tuvune.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Semesi.

**MHE. DKT. EMMACULATE S. SEMESI:** Naomba kutoa hoja.

**MWENYEKITI:** Hapana tumeshavuka huko.

**MHE. DKT. EMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanyaje?

**MWENYEKITI:** Kaa tu sasa.

**MHE. DKT. EMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Sasa ni uamuzi nawahoji sasa.

**MBUNGE FULANI:** Kura ya siri.

**MWENYEKITI:** Umesema kura ya siri?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Unafahamu utani unafaa saa fulani lakini siyo saa hizi.

Sasa nitawahoji kuhusu kukubali au kukataa hoja ya Mheshimiwa Sware.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Naamini wasioafiki wameshinda. Waheshimiwa Wabunge muda wetu umekwisha. Katibu.

**NDG. ASIA P. MINJA- KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea na utaratibu wa *guillotine*.

**FUNGU 43 - Kilimo**

Kif. 1001 - *Admn. and HR Mgt*.....................Sh. 6,631,658,700/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*...............Sh. 1,873,581,200/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*...................Sh. 1,644,310,400/=
Kif. 1004 - *Agriculture Training Institute*......Sh. 5,637,464,500/=
Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*.........................Sh. 496,220,500/=
Kif. 1006 - *Procurement Mgt. Unit*.................Sh. 740,337,200/=
Kif. 1007 - *Govt. Comm. Unit*........................Sh. 375,934,700/=

Kif. 1008 - *Legal Unit*...............................Sh. 441,687,000/=
Kif. 1009 - *Mgt. Info. Systems Unit* .................Sh. 504,092,200/=
Kif. 1010 - *Environment Mgt*.........................Sh. 381,213,200/=
Kif. 2001 - *Crop Development*..............Sh. 22,090,555,400/=
Kif. 2002 - *Agricultural Mechanization*..........Sh. 804,687,000/=
Kif. 2003 - *Agriculture Land use Planning and Management*.........Sh. 903,031,900/=
Kif. 2004 - *Plant Breeders Unit*..................Sh. 205,970,900/=
Kif. 2005 - *Irrigation and Tech. Services*..........Sh. 15,060,000/=
Kif. 3001 - *Research Development*.........Sh. 16,703,413,000/=
Kif. 5001 - *National Food Security*............Sh. 5,113,603,400/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64-Uvuvi**

Kif. 9001- *Fisheries Development*............Sh. 13,312,160,829/=
Kif. 9002 -*Aquaculture Development*........Sh. 1,480,485,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 99- Mifugo**

Kif. 1001- *Admn and HR Mgt*.................Sh. 3,307,126,285/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts*...........Sh. 1,197,020,112/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*..................Sh. 986,694,386/=
Kif. 1004 - *Livestock Research and Training Institute*.......................Sh. 5,898,485,240/=
Kif. 1005 - *Govt Comm. Unit*.....................Sh. 289,719,186/=
Kif. 1007 - *Internal Audit Unit*...................Sh. 347,495,606/=
Kif. 1008 - *Procurement Mgt Unit*..............Sh. 552,313,186/=
Kif. 1009 - *Legal Service Unit*...................Sh. 257,947,386/=
Kif. 1010 - *Inform. comm. & Technology*.....Sh. 396,771,686/=
Kif 7001 - *Veterinary Services*...............Sh. 8,470,898,936/=
Kif. 7005 - *Veterin. Council of Tanzania*.....Sh. 389,919,386/=
*Kif. 8001 - Animal Production*................Sh. 3,869,132,605/=
*Kif. 9001 - Fisheries Development division..................Sh. 0/=*
*Kif. 9002 - Aquaculture Development Division..........Sh. 0/=*

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24- Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kif.1001 - *Admn and HR Mgt Division*..........Sh. 3,096,327,656/=
Kif.1002 - *Finance and Accounts Unit*..........Sh. 107,044,000/=
Kif.1003 - *Planning Monit. & Evaluat. Unit*......Sh. 74,000,000/=
Kif.1004 -*Govt Comm. Unit*...........................Sh. 23,700,000/=
Kif.1005 -*Legal Service Unit*...........................Sh. 20,746,000/=
Kif.1006 -*Procurement Mgt. Unit* .................Sh. 30,000,000/=
Kif.1007- *Information Comm. Tech.*..............Sh. 35,000,000/=
Kif.1008 - *Internal Audit*..................................Sh. 28,040,000/=
Kif.1009 - *Research and Training Unit*............Sh. 25,320,000/=
Kif.4001- *Cooperative Promotion and Coordination Section*......................Sh. 138,164,584/=
Kif.4002 - *Cooper. Microfinance Section*........Sh. 25,940,000/=
Kif.4003 - *Regional Cooperative Officers* ......Sh. 172,960,000/=
Kif.4004 - *Coopererative Marketing and Investment Section*........................Sh. 24,580,000/=
Kif.4005 - *Registration Services Section*...........Sh. 23,880,000/=
Kif.4006 - *Inspection and Supervision Service Section*...........................Sh. 2,468,151,760/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Kilimo**

Kif.1003 - *Policy and Planning*...............Sh. 25,914,918,000/=
Kif.1004 - *Agriculture training Institute*......Sh. 5,023,639,000/=
Kif.1009 - *Manag. Inform. Systems Unit*..........Sh. 100,000,000/=
Kif.2001- *Crop Development*.................Sh. 31,233,068,300/=
Kif.2002 - *Agriculture Mechanization*...........Sh. 200,000,000/=
Kif.2003 - *Agriculture Land use Planning and Management*......Sh. 4,645,935,000/=
Kif.3001- *Research Development*.............Sh. 1,681,613,500/=
Kif.5001- *National Food Security*...........Sh. 81,453,826,200/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 64 – Uvuvi**

Kif.1009 - *Business development. Div.*.........Sh. 1,200,000,000/=
Kif.9002 - *Aquaculture Devpt*....................Sh. 800,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 99- Mifugo**

Kif.3001- *Policy and Planning*.......................Sh. 700,000,000/=
Kif.3004 - *Livestock Research & Train. Inst.*....Sh. 500,000,000/=
Kif.7001-*Veterinary Services*.........................Sh. 1,000,000,000/=
Kif.8001- *Animal Production*.....................Sh. 1,800,000,000/=
Kif.9001- *Fisheries Development Division*.....................Sh. 0/=
Kif.9002 - *Aquaculture Development*............................Sh. 0/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ASIA MINJA - KATIBU MEZANI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa hoja Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja imetolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio na Matumizi ya Serikali ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2017/2018 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Naibu Waziri wake pamoja na timu nzima ya Wizara hii muhimu. Nawapongeza pia ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya tangu siku ya Jumamosi hadi leo tunapohitimisha hoja hii. Mmesema mengi, Serikali imeyachukua yote. Jambo la msingi katika ushauri wenu ni hii idhini mliyoitoa kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara hii wakatumie fedha hizi. Mtawapima kwa kile ambacho watapata na jinsi watakavyokitumia.

Mheshimiwa Waziri amesema watakuwa wepesi kufanya *adjustment* katika maeneo ambayo yanahitaji *adjustment* haraka. Suala la *Blue Economy* tumeliongelea sana nadhani tulifikishe tamati, huu ni utajiri mkubwa sana kwa nchi hii. Mimi nimeshiriki kutoa mapendekezo kupitia Taarifa ya Spika ya Chenge *One*, kwa hiyo, umetoa matumaini sana kwa hayo uliyoyasema mwishoni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina matangazo, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Jumanne Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 2.10 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 23 Mei, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*